

**MWINGILIANOMATINI KATIKA USHAIRI WA MATHIAS MNYAMPALA**

**NA**

**KYAMBA ANNA NICHOLAUS**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI, IDARA YA KISWAHILI NA  
LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**2018**

## IKIRARI

### IKIRARI YA MTAHINIWA

Kazi hii ni yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine chochote. Hairuhusiwi kuiga, kunakili au kurudufisha sehemu yoyote bila ridhaa yangu mwenyewe au ya Chuo Kikuu cha Moi.

.....

.....

**Kyamba Anna Nicholaus**

Tarehe

**SASS/DPHIL/KIS/01/15**

### IKIRARI YA WASIMAMIZI

Tasnifu hii imeidhinishwa na wasimamizi wafuatao:

.....

.....

**Dkt. Magdaline N. Wafula**

Tarehe

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

.....

.....

**Dkt. Mosol Kandagor**

Tarehe

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

## SHUKURANI

Kwanza kabisa napenda kumshukuru kwa namna ya pekee Mwenyezi Mungu kwa kunilinda, kuniongoza na kunipa uwezo wa akili mpaka nikafika hapa nilipofika leo hii. Ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa kila mmoja aliyenipa ushirikiano wakati wote wa masomo yangu ya Uzamifu, uliofanikisha kukamilika kwa tamrini, utafiti na uandishi wa tasnifu hii. Ninakishukuru Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na uongozi wake kwa kukubali kufadhili masomo yangu ya Uzamifu nchini Kenya. Hakika hiki kilikuwa kipindi muhimu kwangu kwa kuwa niliweza kupata muda wa kutosha katika masomo yangu na kupata maarifa mbalimbali kuhusiana na taaluma yangu, utafiti na uandishi wa utafiti kwa ujumla.

Pili, nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Magdaline N. Wafula na Dkt. Mosol Kandagor kwa ushirikiano wao wa dhati. Ninawashukuru sana kwa dhati kwa kukubali kunisimamia, kuniongoza na kunitia moyo pale nilipokabiliana na mambo ya kunikatisha tamaa. Ninawaomba kwa Mwenyezi Mungu awalinde, awape afya njema na kuwaongezea ufanisi katika kazi zenu.

Tatu, ni kwa mume wangu mpenzi Bw. Ostack Renatus Mligo kwa upendo wake kwangu na kwa kunivumilia na kuniwezesha pale nilipokwama nikiwa masomoni. Nakushukuru kwa kuitunza familia yetu kwa muda wote niliokuwa masomoni. Asante sana na Mungu akubariki. Pia nawashukuru sana wanangu wapendwa Fransisco Ostack Mligo na Maria Ostack Mligo. Mlinivumilia sana kipindi chote nilichokuwa masomoni na mkakosa haki za mama kama watoto na niliwaacha peke yenu mkiwa wadogo sana. Nawapenda sana watoto wangu, Mungu azidi kuwalinda na kuwapa maisha marefu yenye baraka tele.

Ninawashukuru sana Maprofesa, Wahadhiri na Wakutubi kutoka katika Idara na Maktaba za Vyuo Vikuu mbalimbali vya umma nchini Tanzania na Kenya kwa kutoa msaada wenu wakati wa kukusanya data za utafiti wangu. Kwa upekee ninawashukuru wakutubi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania makao makuu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Moi pamoja na wakutubi wa Maktaba Kuu ya Taifa ya Tanzania. Kadhalika, ninawashukuru sana wanataaluma na wafanyakazi wote pamoja na wanafunzi wa Uzamili na Uzamifu wa Chuo Kikuu

cha Moi kwa ushirikiano wenu mlionionyesha kipindi chote cha masomo yangu. Hamkusita kunisaidia pale nilipohitaji msaada wenu.

Ninawashukuru sana wafanyakazi wa Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hasa wale wa Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji kwa ushirikiano walionionyesha wakati wote wa utafiti. Namshukuru pia Prof. Mugyabuso Mlinzi Mulokozi kwa mchango wake alionipa kuanzia kwenye mada na hata katika mahojiano kuhusiana na utafiti huu. Pia namshukuru sana Prof. Joshua Madumulla kwa ushirikiano alionionyesha wakati wa ukusanyaji wa data. Vilevile, namshukuru sana Dkt. Shani Omari kwa kunitia moyo na kunisaidia kuisoma tasnifu yangu na kunipa mawazo mbalimbali kuhusiana na utafiti huu. Mwenyezi Mungu awabariki wote na kuwapa afya njema.

Vilevile, shukurani zangu za dhati kwa familia yangu kwa ushirikiano wao wa hali na mali walionionyesha wakati wote nilipokuwa masomoni. Nawashukuru wazazi wangu Nicholas Kyamba na Eledina Mwanisawa na walezi wangu Richard Mwanisawa na mkewe Jenerosa Mwanisawa pamoja na ndugu na jamaa zangu wa karibu ambao kwa namna moja ama nyingine mlionyesha ushirikiano wenu kipindi chote nilichokuwa masomoni. Mwenyezi Mungu awabariki wote na kuwapa maisha marefu.

**TABARUKU**

Ninaitabaruku kazi hii kwa wanangu Fransisco Ostack Mligo na Maria Ostack Mligo;  
nawaachia mwenge huu wa elimu.

## IKISIRI

Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu kutokana na dhima yake katika jamii. Ukweli ni kuwa historia hiyo inatokana na watunzi ambao wamechangia maendeleo ya utanzu huu wa kifasihi. Wapo washairi wengi wa Kiswahili waliotunga mashairi katika nyakati tofauti lakini mchango wa kazi zao haujulikana kikamilifu katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Mmojawapo wa washairi waliosahaulika ni Mathias Mnyampala. Azma kuu ya utafiti huu ni kuchunguza na kuchambua ushairi wa Mathias Mnyampala kimwingilianomatini. Utafiti huu umelenga kuchunguza upekee wa tungo za kishairi za Mathias Mnyampala na kuzihakiki mbinu za kifani zilizotumika kuibua maudhui kwa kuzingatia muktadha wa utunzi wake kimwingilianomatini. Malengo ya utafiti huu ni mosi, kupambanua muktadha wa utunzi uliomsukuma mwandishi kutunga kazi teule za ushairi wa Kiswahili. Pili, kuhakiki mbinu za kifani zinavyotumika kuibua maudhui katika kazi teule za ushairi za Mathias Mnyampala. Tatu, kutathmini mchango wa kazi za ushairi za Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini. Mwingilianomatini ni nadharia iliyoasisiwa na Julia Kristeva miaka ya 1960. Nadharia hii inasisitiza kuwa hakuna matini asilia, bali uhai wa matini moja hutegemea matini nyingine tangulizi. Hivyo basi, matini za fasihi hutegemeana katika kukamilisha maana. Ni kwa msingi huu ndipo uhakiki wa mashairi ya Mathias Mnyampala yamechangianuliwa kimwingilianomatini. Kwa kutumia nadharia hii tumebaini kuwa kazi za Mnyampala zinaingiliana, zinakamilishana na kutegemeana na matini nyingine tangulizi. Utafiti huu ni wa maktabani na nyanjani. Kutoka maktabani, data ilikusanywa kutoka kazi teule zilizochapishwa ambazo ni: *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965) na *Ngonjera za UKUTA Na. 1* (1970). Kutokana na mahojiano ya watafitiwa nyanjani tulipata data kuhusu maisha na historia ya Mnyampala pamoja na miswada yake isiyochapishwa ifuatayo: *Hazina ya Washairi, Mahadhi ya Kiswahili na Mashairi ya Vidato*. Usampulishaji makusudi ulitumika kuteua kazi tatu zisizochapishwa na usampulishaji nasibu ulitumika kuchagua kazi tatu zilizochapishwa. Data zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kina yaliyohusisha udondozi na ufafanuzi wa mistari, beti na vifungu vya maneno. Uchambuzi huo unadhihirisha mwingilianomatini wa fasihi simulizi na tamaduni za kisasa katika mashairi ya Mathias Mnyampala. Utafiti huu unadhihirisha kuwepo kwa uhusiano mkubwa kati ya muktadha wa utunzi, mbinu za kifani na uibuaji wa maudhui ya kazi teule za Mathias Mnyampala. Matokeo ya utafiti ni kwamba, Mathias Mnyampala amechangia pakubwa katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Mojawapo ya mchango wake ni kuongozwa na Nadharia ya Kimapokeo katika utunzi wa mashairi yake. Wanamapokeo wanasisitiza upekee wa shairi la Kiswahili kimuundo hasa urari wa vina na mizani. Kwa kutumia nadharia hii, Mathias Mnyampala aliibua mbinu mpya za utunzi mfano mbinu ya mtiririko na msisitizo. Kupitia utafiti huu tumevumbua miswada, barua na nyaraka mbalimbali za kifasihi zilizotungwa na Mathias Mnyampala zenye mchango mkubwa katika ushairi, fasihi na Kiswahili kwa ujumla. Miswada hiyo ni malighafi ya tafiti za kifasihi na machapisho ya kitaaluma.

## ABSTRACT

Kiswahili Poetry has a rich history based on its functions in society. This rich history can be attributed to the composers of the poems and hence to the growth of this literary genre. Several Kiswahili poets exist and their contribution to Kiswahili poetry is well documented. However, one important figure seems to have escaped the attention of many literary critics in Kiswahili poetry. This is none other than Mathias Mnyampala. This study sets out to investigate and analyze the intertextuality of Mathias Mnyampala's poetry. The study focus on Mathias Mnyampala's poems by examining the stylistic devices deployed in transmitting themes generated in specific contexts. The objectives of this study were firstly, to expound the context that motivated the poet to compose the selected works. Secondly, to critique the literary techniques utilized to communicate the themes captured in Mathias Mnyampala's selected poems. And thirdly, to assess Mnyampala's literary contribution in the development of Kiswahili poetry. The study is guided by Intertextuality theory founded by Julia Kristeva in the 1960s. The theory emphasizes that there is no original text; instead the life of one text depends on other preceding texts. So, literary texts depend on and complement each other. It is on this background that Mathias Mnyampala's poems are analyzed intertextually. Based on intertextuality theory, it is realized that Mathias Mnyampala's works do interact with, are complementary to and depend on other preceding texts. This research is both library and field based. From the library we obtained the three published works namely: *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965) and *Ngonjera za UKUTA Na. 1* (1970). Through interviews we obtained data regarding the life and history of Mnyampala as well as his unpublished works which are: *Hazina ya Washairi*, *Mahadhi ya Kiswahili* and *Mashairi ya Vidato*. Data was analyzed and presented qualitatively by using a descriptive approach with quotations and clarifications of verses, stanzas, and paragraphs. The analysed data reveal the intertextuality of oral literature and modern culture as captured in Mathias Mnyampala's poems. This study demonstrates that there exists a strong relationship between the themes captured, the literary techniques deployed in Mathias Mnyampala's selected works and the context in which they were written. The findings attest to the fact that Mathias Mnyampala has immensely contributed to the development of Kiswahili Poetry. One major observation is that Mathias Mnyampala stands out as a propagator of the classical approach to Kiswahili poetry. This approach puts more emphasis on the unique structure of the Kiswahili poem. Based on this classical theoretical approach, Mnyampala came up with unique poetry trends namely: 'Mtiririko' and 'Msisitizo'. Through this study we have unearthed various literary manuscripts written by Mathias Mnyampala which significantly contribute to the wealth of Kiswahili poetry and Kiswahili literature as a whole. The manuscripts are a resource not only to future literary researchers but also academic publications.

## YALIYOMO

IKIRARI.....	ii
SHUKURANI.....	iii
TABARUKU.....	v
IKISIRI.....	vi
ABSTRACT.....	vii
YALIYOMO.....	viii
ORODHA YA PICHA.....	xii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xiii
ORODHA YA VIFUPISHO NA AKRONIMU.....	xiv
<b>SURA YA KWANZA.....</b>	<b>1</b>
<b>MISINGI YA UTAFITI.....</b>	<b>1</b>
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti.....	1
1.1.1 Historia ya Mathias Mnyampala.....	8
1.1.1.1 Mahali Alipozaliwa.....	8
1.1.1.2 Ndoa.....	9
1.1.1.3 Dini.....	10
1.1.1.4 Kazi.....	12
1.1.1.5 Ugonjwa na Kifo.....	14
1.1.1.6 Maandishi ya Mathias Mnyampala.....	18
1.2 Suala la Utafiti.....	20
1.3 Malengo ya Utafiti.....	21
1.4 Maswali ya Utafiti.....	21
1.5 Sababu za Kuteua Mada ya Utafiti.....	22
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	23
1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	24
1.8 Mbinu za Utafiti.....	25
1.8.1 Mkabala wa Utafiti.....	25
1.8.2 Eneo la Utafiti.....	25
1.8.3 Vyanzo vya Data.....	26
1.8.3.1 Upekuzi Maktabani.....	26
1.8.3.2 Utafiti Nyanjani.....	28
1.8.4 Sampuli na Usampulishaji wa Utafiti.....	29
1.8.5 Njia za Kukusanyia Data.....	31
1.8.5.1 Mahojiano.....	31



1.8.6 Vifaa vya Utafiti.....	33
1.8.6.1 Tarakilishi Pakatwa (Tarakilishi).....	33
1.8.6.2 Simu na Kinasa Sauti.....	33
1.9 Itikeli ya Utafiti.....	33
1.10 Uchanganuzi wa Data.....	34
1.11 Hitimisho.....	35
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>36</b>
<b>MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA.....</b>	<b>36</b>
2.0 Utangulizi.....	36
2.1 Mapitio ya Maandishi.....	36
2.1.1 Ushairi wa Kiswahili.....	36
2.1.2 Mukstadha katika Ushairi.....	42
2.1.3 Yaliyoandikwa kuhusu Tungo za Mathias Mnyampala.....	44
2.2 Misingi ya Nadharia.....	54
2.3 Hitimisho.....	59
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>60</b>
<b>ATHARI YA UKTADHA KATIKA MASHAIRI YA MATHIAS MNYAMPALA.....</b>	<b>60</b>
3.0 Utangulizi.....	60
3.1 Muhtasari wa kazi Teule za Mathias Mnyampala.....	61
3.1.1 <i>Diwani ya Mnyampala</i> (1965).....	61
3.1.2 <i>Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi</i> (1965).....	62
3.1.3 <i>Mashairi ya Vidato</i> (1966).....	63
3.1.4 <i>Hazina ya Washairi</i> (1966).....	65
3.1.5 <i>Mahadhi ya Kiswahili</i> (1967).....	65
3.1.6 <i>Ngonjera za UKUTA Na.1</i> (1970).....	67
3.2 Mukstadha wa Uandishi wa Kazi Teule za Mathias Mnyampala.....	68
3.2.1 Mukstadha wa Kijamii.....	68
3.2.1.1 Maingiliano ya Mila na Desturi za Kiafrika na Kigeni.....	69
3.2.1.2 Uzazi na Malezi.....	75
3.2.1.3 Kuathiriwa na Waandishi Wengine.....	78
3.2.1.4 Dini.....	80
3.2.1.5 Mapenzi na Ndoa.....	90
3.2.1.6 Kushamiri kwa Matumizi ya Lugha ya Kiswahili.....	94
3.2.2 Mukstadha wa Kisiasa.....	100
3.2.2.1 Harakati za Kupigania Uhuru na Kipindi cha Uhuru.....	101
3.2.2.2 Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.....	105
3.2.2.3 Muunganowa Tanganyika na Zanzibar.....	108

3.2.2.4 Mtunzi kuwa na Uhusiano wa Karibu na Wanasiasa.....	110
3.2.3 Mukstadha wa Kiuchumi.....	115
3.2.3.1 Uchumi wa Kisoshalisti.....	116
3.2.3.2 Utaifishaji wa Mali.....	119
3.2.3.3 Ujenzi wa Jamii Mpya.....	120
3.2.4 Mukstadha wa Kimwingilianomatini.....	122
3.3 Hitimisho.....	129
<b>SURA YA NNE.....</b>	<b>130</b>
<b>MBINU ZA KIFANI ZINAZOIBUA MAUDHUI KATIKA KAZI TEULE ZA</b>	
<b>MATHIAS MNYAMPALA.....</b>	<b>130</b>
4.0 Utangulizi.....	130
4.1 Mbinu za Kifani Zinazoibua Maudhui katika Kazi Teule za Ushairi wa Mathias	
Mnyampala.....	130
4.1.1 Taswira.....	131
4.1.2 Methali.....	159
4.1.3 Misemo.....	177
4.1.4 Ushairi-Drama.....	191
4.1.4.1 Wahusika.....	192
4.1.4.2 Hadhira.....	199
4.1.4.3 Jukwaa.....	202
4.1.4.4 Majibizano.....	204
4.1.5 Nyimbo.....	213
4.2 Hitimisho.....	224
<b>SURA YA TANO.....</b>	<b>226</b>
<b>MCHANGO WA MATHIAS MNYAMPALA KATIKA MAENDELEO YA</b>	
<b>USHAIRI WA KISWAHILI.....</b>	<b>226</b>
5.0 Utangulizi.....	226
5.1 Mtindo.....	226
5.1.1 Mtindo wa Mtiririko.....	227
5.1.2 Mtindo wa Msisitizo.....	229
5.1.3 Mtindo wa Majibizano.....	231
5.1.4 Mtindo wa Vidato.....	236
5.2 Muundo.....	240
5.3 Matumizi ya Lugha.....	243
5.3.1 Matumizi ya Taswira.....	247
5.3.2 Matumizi ya Methali.....	248
5.3.3 Mbinu ya Takriri.....	250

5.4 Kukusanya Mashairi ya Waandishi Mbalimbali.....	253
5.5 Kukuza Nadharia ya Ushairi wa Kiswahili.....	257
5.6 Kuingiza Maudhui ya Dini katika Ushairi wa Kiswahili.....	261
5.7 Hitimisho.....	265
<b>SURA YA SITA.....</b>	<b>266</b>
<b>MATOKEO, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....</b>	<b>266</b>
6.0 Utangulizi.....	266
6.1 Muhtasari wa Tasnifu.....	266
6.2 Matokeo ya Utafiti.....	268
6.3 Mahitimisho.....	272
6.3.1 Uhifadhi wa Kazi na Nyaraka za Mnyampala.....	273
6.4 Mapendekezo ya Mtafiti.....	274
6.5 Mapendekezo kuhusu Tafiti za Baadaye.....	276
MAREJELEO.....	278
VIAMBATISHO.....	289
Kiambatisho A: Mwongozo wa Mahojiano kwa Wahadhiri na Wanafunzi.....	289
Kiambatisho B: Mwongozo wa Mahojiano kwa Familia ya Mathias Mnyampala.....	290
Kiambatisho C: Kazi za Mathias Mnyampala ambazo Hazijachapishwa.....	291
Kiambatisho D: Mtindo wa Mashairi ya Mtiririko (uk. 5) katika Diwani Ya Mnyampala	292
Kiambatisho E: Mtindo wa Mashairi ya Msisitizo (uk. 121) katika <i>Diwani Ya Mnyampala</i>	293
Kiambatisho F: Mtindo wa Mashairi ya Vidato “Uaminifu” (uk. 1) katika Mswada wa	
<i>Mashairi Ya Vidato</i> .....	295
Kiambatisho G: Vibali vya Utafiti.....	296
Kiambatisho H: Picha Mbalimbali Zilizopigwa Nyanjani.....	309

**ORODHA YA PICHA**

Picha namba 1: Shairi la “Ndwele Sii Yaniuma.” .....	15
Picha namba 2: Shairi la “Taa Yangu Yafifia.” .....	16
Picha namba 3: Kaburi la Mathias Mnyampala.....	17
Picha namba 4: Barua iliyoandikwa na Mwalimu Julius Nyerere kumjibu Mnyampala. .....	112
Picha namba 5: Vifaa vinavyotumika kuhifadhi nyaraka za Mathias Mnyampala....	274

## **ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali Namba 1: Viongozi walioandika utangulizi/dibaji ya kazi za Mnyampala...111

**ORODHA YA VIFUPISHO NA AKRONIMU**

BAKITA	Baraza la Kiswahili Tanzania
Bw.	Bwana
Dkt.	Daktari
Prof.	Profesa
S.A.W	Salaia Alehu Wassalam (Rehema na Amani Zimshukie)
TANU	Tanganyika African National Union
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Taz.	Tazama
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
Uk.	Ukurasa
UKUTA	Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania

## **SURA YA KWANZA**

### **MISINGI YA UTAFITI**

#### **1.0 Utangulizi**

Sura hii inapambanua vipengele muhimu vya utafiti ili kuweka msingi wa sura zinazofuata. Vipengele vilivyoangaziwa ni usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti na hatimaye mbinu za utafiti.

#### **1.1 Usuli wa Suala la Utafiti**

Ushairi ni mojawapo wa tanzu kuu za fasihi ya Kiswahili. Sanaa ya ushairi imekuwepo na inaendelea kuwepo kadiri jamii ya mwanadamu itadumu. Wapo wataalamu mbalimbali waliochunguza ushairi wa Kiswahili kwa misingi mbalimbali na wengi wao wanaamini kwamba ushairi ulikuwepo tangu enzi za usimulizi (Chiraghdin, 1970; Ngogu na Chimerah, 1999; Wamitila, 2008 na Mulokozi, 2017). Wanaeleza kuwa chimbuko la asili la ushairi wa Kiswahili limetokana na nyimbo za jando, harus, kazi, matambiko na mengineyo. Aidha, ushairi wa Kiswahili ndio utanzu mkongwe sana katika fasihi ya Kiswahili. Utanzu huu chimbuko lake ni fasihi simulizi na baadaye fasihi andishi. Kimsingi utanzu huu wa fasihi ulianza kama fasihi simulizi, lakini kutokana na maendeleo ya hati za Kiarabu na baadaye Kirumi utanzu huu ukaanza kuandikwa katika maandishi.

Dhana ya ushairi inaelezwa kwa njia mbalimbali na wataalamu tofautitofauti. Kuna wale wanaoeleza maana ya ushairi kwa mtazamo wa kimapokeo na wengine katika mtazamo wa kisasa. Mfano wa wataalamu waliofafanua dhana ya ushairi kwa kufuata mtazamo wa kimapokeo ni: Abedi (1954), Robert (1958), Mnyampala (1965),

Mayoka (1977), Knappert (1974), Ramadhani (1974) na Chiraghdin na wenzake (1975). Abedi (1954:viii) anaeleza kuwa “ushairi au utenzi ni wimbo. Hivyo kama shairi haliimbiki halina maana.” Mawazo ya Abedi yanashabihiana na mawazo ya Shaaban Robert (1958:37) anayesema kuwa:

1. Ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi. Zaidi ya kuwa sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari. Mawazo, maono na fikra za ndani zinapoelekezwa kwa muhtasari wa ushairi huvuta moyo kwa namna ya ajabu.

Kadhalika, maelezo ya Abedi na Robert yanashabihiana na maelezo ya Mayoka (1977:3-5) ambaye anasema kuwa “ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama wimbo, tenzi na mashairi. Zaidi ya kuwa sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari.” Naye, Mnyampala (1965:vii) anasema kuwa:

2. Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Ndicho kitu kilicho bora sana katika maongozi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangiliwa kwa urari wa mizani na vina maalum kwa ushairi.

Kutokana na dondoo la Mnyampala, miongoni mwa sifa za ushairi wa Kiswahili ni matumizi ya lugha ya kishairi na maneno ya hekima akimaanisha kutumia lugha ya mkato, nzito yenye kunata na iliyopangwa kwa urari wa vina na mizani. Kwa ujumla, mawazo ya Mnyampala yanaafikiana na mawazo ya Amri Abedi na Shaaban Robert, kwa kuwa Mnyampala anasisitiza kuzingatia kanuni za ushairi, maana na dhima za ushairi. Wataalamu hawa wote wametoa maana ya ushairi kwa kuzingatia kanuni za ushairi zilizowekwa na wanamapokeo, ambazo zinafuata urari wa vina na mizani kama uti wa mgongo wa ushairi. Wanasisitiza arudhi au kanuni za ushairi katika kutunga mashairi ya Kiswahili.



Wanamapokeo wanadai kuwa ushairi wa Kiswahili ni taaluma iliyokamilika na sharti uwe na urari wa vina na mizani. Kwa hivyo lazima mashairi yanapotungwa yazingatie kanuni za tangu jadi zikitwazo arudhi, yaani urari wa vina na mizani (Walibora, 2007). Tofauti za mitazamo hiyo ndiyo iliyoibua utata ambao unaturudisha katika mgogoro wa ushairi wa miaka ya 1970. Misingi ya mgogoro huo ilikuwa maana ya ushairi kwa jumla na maana ya ushairi wa Kiswahili (Mulokozi na Kahigi, 1979). Mgogoro ulianza pale ambapo wanausasa Ebrahim Hussein, Euphrase Kezilahabi na Jared Angira walianza kuandika mashairi ya Kiswahili bila kufuata kanuni za ushairi wa Kiswahili zilizopendekezwa na wanamapokeo (Senkoro, 1995). Makali ya mgogoro huo yalipungua baada ya Nyerere (1976) kutoa mawazo kuwa wanausasa walistahili kuibuka, kwani taaluma huenda ikibadilika katika jamii, hivyo ilipasa mabadiliko hayo kutokea katika ushairi wa Kiswahili.

Wanausasa waliona kwamba kanuni au sheria zilizowekwa na washairi wa kimapokeo zilimnyima mtunzi uhuru wa kujieleza. Kwa hivyo walizikaidi kanuni za ushairi za wanamapokeo na kutunga mashairi yasiyozingatia kanuni hizo. Baadhi yao ni Kezilahabi (1973), Mulokozi na Kahigi (1979), Mulokozi (1989), Sanka (1994) na Shitemi (2010). Kezilahabi (1973:60) anafafanua maana ya ushairi kwamba:

3. Shairi ni tukio, hali au wazo ambalo limeonyeshwa kwetu kutokana na upangaji mzuri wa maneno fasaha yenye mizani kwa ufupi ili kuonyesha ukweli fulani wa maisha.

Kwa ujumla, maana hiyo iliyotolewa hapo ina upungufu kidogo, pale ambapo mwandishi anasema shairi lionyeshe ukweli fulani wa maisha. Kwa ujumla si kila shairi linaonyesha ukweli fulani wa maisha. Shairi linaweza kuonyesha kinyume cha ukweli wa maisha (taz. Senkoro, 1988). Wanausasa wengine waliofafanua maana ya ushairi ni Mulokozi na Kahigi (1979:25) ambao wameeleza kuwa:

4. Ushairi ni sanaa iliyopambanuliwa kwa sanaa maalum ya maneno fasaha na yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha au sitiari au ishara, katika usemi, maandishi, au mawazo, kufunza au kuelekeza tukio au hisi fulani, kuhusu maisha au mazingira ya binadamu, kwa njia inayogusa moyo.

Kwa hivyo, wataalamu hawa wanasisitiza kuwa ushairi unaweza kubadilika katika umbo lake kulingana na wakati, muktadha na jamii unamotokea. Aidha, kimaudhui ushairi unaweza kufunza na kutoa maonyo kutokana na wakati na mazingira ya jamii husika. Kwa maelezo hayo wanawakilisha dhana ya mwingilianomatini kuwa kuna mabadiliko yanayotokana na ushairi tangulizi. Kwa mujibu wa wanausasa, ushairi unaundwa na mambo makuu matatu ambayo ni muktadha, fani na maudhui (Mulokozi, 1989). Aidha mambo haya matatu huingiliana na kukamilisha katika kazi za ushairi na fasihi kwa ujumla. Katika fani, ni lazima kuangalia lugha, muundo, wahusika na mtindo. Maudhui hutokana na ufundi wa msanii katika matumizi ya fani, ambapo matumizi hayo yanaleta maana iliyokusudiwa. Maudhui mbalimbali huibuliwa ndani ya kazi husika kama vile, dhamira, migogoro, ujumbe, falsafa, msimamo na mtazamo.

Kwa upande wa muktadha, Mulokozi (2017) anaeleza kuwa, ni muhimu kuangalia mazingira yaliyozua shairi hilo. Mazingira hayo yanaweza kuwa ya kihistoria, kijiografia, kijamii na kiutendaji. Hivyo mazingira ndiyo yanayotupa muktadha wa shairi na mara nyingi ndiyo yanayotuwezesha kuelewa baadhi ya misemo, vidokezo, mafumbo na ishara anazozitumia mtunzi. Naye Sanka (1994) anaongezea kuwa ushairi umekuwa chombo muhimu katika kuhifadhi historia, falsafa na utamaduni wa jamii. Kwa upande wake Shitemi (2010:xix) anaeleza kuwa:

5. Ushairi ni sanaa ya lugha. Ni utanzu mojawapo wa fasihi ya Kiswahili sambamba na riwaya, hadithi fupi, tamthiliya na fasihi simulizi. Upekee wa shairi hutokana na jinsi ambavyo

lugha inatumika ili kudhihirisha upekee wa umbo na nafsi katika muktadha wa sajili na arudhi za kishairi. Licha ya upekee wa umbo na mtindo katika matumizi ya lugha, shairi huzingatia maudhui na mazingira bunia ya kijamii kadri zilizvyo tanzu nyingine za fasihi.

Ni bayana, dhana ya ushairi inaelezwa kwa njia tofauti na kila mtaalamu ametoa maana yake kutegemea mtazamo anaouchukua, uwe ni wa kimapokeo au wa kisasa. Hata hivyo kwa maoni yetu, ushairi ni utungo wa kifasihi kama zilizvyo tungo nyinginezo za kifasihi ambazo kifani hujipambanua kwa kuundwa na matumizi ya lugha kimantiki ambapo maneno hutumika kuwasilisha mambo mengi. Kimaudhui utungo wa ushairi unaweza kuhusu jambo lolote linalohusiana na tajiriba za watu wa jamii husika. Kutokana na fasili hizo, sanaa ya ushairi inaweza kuwasilishwa kwa namna mbili, namna ya kwanza ni ya masimulizi ya mdomo, na namna ya pili ni kwa njia ya maandishi. Pia, ushairi ni zao la jamii husika na hivyo huwa na sifa maalum kulingana na muktadha lengwa kwa jamii husika. Vilevile, ushairi kama zilizvyo kazi nyingine za kisanaa umesheheni tajiriba za wanajamii katika vipindi anuwai vya kihistoria na kuonyesha umuhimu wake katika jamii.

Hivyo, ushairi ni sanaa ambayo imetumiwa na wanadamu katika karne mbalimbali za maisha yao na inaendelea kutumika hadi leo. Wanadamu wamekuwa wakitumia ushairi kuelezea masuala ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii (Kitogo, 2002 na Omary, 2011). Hata hivyo sio rahisi kutenganisha masuala yanayozungumzwa katika ushairi na mambo yanayotendeka katika maisha ya mwanadamu ya kila siku. Katika ushairi, hali hizi zinasawiriwa vyema kupitia vipengele vya fani na maudhui kwa kuwa ni vipengele vinavyoingiliana na kukamilishana. Miongoni mwa tungo za kishairi ambazo zinasawiri masuala ya kijamii ni kama vile tungo za *Fumo Liyongo* (Mulokozi na Sengo, 2005). Mulokozi na Sengo wanasisitiza kuwa utungo huu

ulianza kama masimulizi ya shujaa wa kihistoria na baadaye ukafanywa kuwa utendi. Ndani ya utungo huu mna maudhui kama vile utamaduni wa jamii, ushujaa, falsafa na busara za mtunzi. Baada ya hapo, waliibuka washairi mbalimbali walioandika kazi mbalimbali zinazohusisha masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Baadhi ya washairi hao ni Muyaka bin Haji, Saadan Kandoro, Akilimali Snow White, Shaaban Robert, Mathias Mnyampala na Kaluta Amri Abedi (Kitogo, 2002 na Mulokozi, 2017).

Maendeleo ya sanaa ya ushairi wa Kiswahili imehusishwa siku nyingi na wataalamu mbalimbali kutokana na mchango wao kiutunzi au kiuhakiki. Baadhi ya wataalamu hao ni Fumo Liyongo, Muyaka bin Haji, Shaaban Robert na wengineo. Hawa wamehusishwa sana na tungo za ushairi katika vipindi maalum kulingana na mbinu za kifani na maudhui zinazojitokeza katika tungo zao. Jambo la kushangaza ni kwamba Mathias Mnyampala, licha ya kutunga tungo anuwai katika ushairi wa Kiswahili, hakuna utafiti wa kina unaopambanua umaarufu wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Kuna utata kuhusu mchango wa kazi za ushairi wa Mathias Mnyampala kutokana na mwingilianomatini wa mashairi yake na tungo za watunzi wengine pamoja na muktadha uliomzaa na kumkuza. Utata huo, ndio uliochochea ari ya kufanya utafiti kumhusu mtaalam huyu ili kubaini mchango wake katika maendeleo ya sanaa ya ushairi wa Kiswahili kimwingilianomatini.

Kuna maoni kinzani kuhusiana na mchango wa Mathias Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili. Wapo wanaodai kuwa kazi zake zina mchango mkubwa katika taaluma ya ushairi na fasihi ya Kiswahili. Wanaodai kuwa kazi za Mnyampala zina mchango mkubwa katika taaluma ya Kiswahili ni Abdulaziz (1969), Komba (1969), Mwangomango (1971), Williams (1974), Kihore (1978), na Gibbe (1978). Hawa

wanaeleza kuwa Mnyampala alitoa kijelezi cha tendi, alifufua ngonjera na ndiye mwanzilishi wa Chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania. Wataalamu wengine wanapinga kwa kudai kuwa hakuna jipya katika kazi zake na aliyoyaandika ni yale yaliyokuwa yakitokea katika jamii wakati huo. Ukinzani huu wa mawazo kuhusiana na kazi za Mnyampala ulichochea utafiti huu ili kuweka mwanga zaidi kuhusu kazi zake kwa kujikita katika mwingilianomatini wa kazi zake.

Wahakiki ambao hawatambui mchango wa kazi za Mnyampala ni Lambert (1966), Harries (1972), Ndulute (1985) na Frolova (2008). Wahakiki hawa wanaeleza kuwa Mathias Mnyampala ameandika diwani nyingi zenye mashairi mengi yanayohusu masuala ya kawaida na ya kila siku na kwamba Mnyampala anasisitiza fikra za kifalsafa zilizokuwepo wakati huo. Aidha, wanadai kwamba Mathias Mnyampala alishikilia kikaidi mno vina na mizani hadi kazi zake zikaathiriwa vibaya. Wanaeleza kuwa kwa kushikilia kanuni za ushairi, baadhi ya mashairi yake yalikuwa yameegemea zaidi katika sanaa kuliko uhalisia na kushindwa kufikisha ujumbe kwa sababu ya ugumu wa msamiati aliotumia. Hata hivyo madai haya hayakuhakikiwa kimwingilianomatini na hayathibitishwi kwa mifano mahususi.

Mawazo ya Harries, Ndulute na Frolova yanapingana na maoni ya Murusuri (2011), Makaka (2012), Masungwa (2012), Mgute (2012) Roy (2013) na Ponera (2015) wanaodai kuwa kazi za Mnyampala zina mchango mkubwa katika fasihi na ushairi wa Kiswahili. Murusuri (2011) amechunguza utamthiliya katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* (1970) na *Ngonjera za UKUTA Na. 2* (1971) za Mnyampala. Murusuri anaeleza kuwa kazi za Mnyampala zimeshamiri vyema vipengele vya utamthiliya na zina ubunifu wa kiwango cha juu pamoja na maudhui yenye kuleta mapinduzi kwa taifa lake.

Kutokana na ukinzani huo, ni dhahiri kwamba, kuna haja ya kufanya utafiti wa kina kuhusu nafasi na ujumi (fani, maudhui na muktadha) wa kazi za Mathias Mnyampala kimwingilianomatini. Kwa lengo la kuthibitisha au kukanusha hoja zilizotolewa na wahakiki hao. Roy (2013) ndiye anagusia kidogo tu mchango wa Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili pale anapoangazia namna tungo za Mnyampala zinapambanua maudhui ya ujenzi wa Taifa la Tanzania. Hivyo basi, kuna haja ya kufanya utafiti wa kina kuhusu kazi za ushairi zilizoandikwa na Mathias Mnyampala ili kutambua mwingilianomatini wa tungo zake pamoja na mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Kwa kuwa utafiti huu unamhusu msairi Mathias Mnyampala ni muhimu kutoa historia kumhusu ili kupata kiini cha utafiti huu.

### **1.1.1 Historia ya Mathias Mnyampala**

Katika kueleza historia ya Mnyampala tumeangalia vipengele vifuatavyo: mahali alipozaliwa, ndoa, msimamo wake kidini, kazi alizofanya Mnyampala, ugonjwa na kifo chake na hatimaye maandishi yake.

#### **1.1.1.1 Mahali Alipozaliwa**

Kwa mujibu wa data za utafiti zilizopatikana nyanjani, Mnyampala alizaliwa tarehe 18/11/1917 katika kitongoji cha Munhundya, kijiji cha Ihumwa manispaa ya Dodoma, mkoa wa Dodoma<sup>1</sup>, nchini Tanzania. Jina lake la utotoni na kabla ya ubatizo aliitwa Emnzehe. Baba yake aliitwa Mnyampala Machichimi na mama yake aliitwa Odina Mbogoni. Mbali na Mathias (Emnzehe)<sup>2</sup>, Odina alipata watoto wengine saba ambao ni Consolata (Majimbi), Andrea (Lesilwa), Anyesi (Majimbi), Fransis (Mamvula), Sostenes (Malejehe), Katarina (Mpelo) na Damiani (Madole). Baba yake alikuwa mhunzi, na kazi hii ilimletea utajiri wa mifugo. Hivyo wakati wa utoto wake na hata

<sup>1</sup> Dodoma ni makao makuu ya Tanzania.

<sup>2</sup>Majina yaliyoko kwenye mapano ni majina ya kilugha waliyopewa kabla ya kubatizwa.

baada ya kuoa mke wa kwanza, Mathias alifanya kazi ya kuchunga mifugo ya wazazi wake. Aidha, katika maisha ya utotoni Mathias Mnyampala hakuweza kupata elimu rasmi kwa vile alihitajika kuchunga mifugo ya baba yake ambaye hakuthamini elimu ya kisasa kwa kuwa hakujua umuhimu wa elimu hiyo. Vilevile, elimu rasmi kwake ilikuwa ngumu kwani shule zilikuwa chache na zilikuwa mbali na kwao.

#### **1.1.1.2 Ndoa**

Mathias Mnyampala aliozwa mke na wazazi wake mnamo mwaka 1931 kwa ng'ombe ishirini na watatu. Mke wa kwanza alikuwa Cecilia. Baadaye alioa wake wengine wawili ambao ni Mary na Magreth. Alijiunga na dini ya Kikristo na kuwa Mkatoliki mwaka 1933, mwalimu wake wa dini aliitwa Damiani na alibatizwa mwaka 1935. Mathias Mnyampala baadaye ilimlazimu kufunga ndoa na mke mmoja tu kati ya hao watatu. Hii ilitokana na taratibu zilizowekwa na dhehebu la Katoliki. Hivyo mwaka 1946 alifunga ndoa na Mary Mangwela huko Mlalo, wilaya ya Manyoni, mkoani Singida. Kila mke aliyemuoa alipata naye mtoto mmoja. Cecilia alimzaa Aloyce (Ngalya) ambaye sasa ni marehemu. Mary alimzaa Charles (Matonya), ambaye alifariki tarehe 03/01/2016. Naye, Magreth alimzaa Edward (Ndahani) ambaye leo hii anaishi Arusha. Mke huyu wa pili ndiye aliyeishi na Mathias mpaka wakati ule alipoaga dunia tarehe 8/6/1969. Mary angali anaishi katika nyumba waliyojenga na mume wake, Mtaa wa Mnyampala, Barabara ya Bahi, Nyumba Na. 6, akiwa na umri wa miaka 88 kwa sasa.

Mathias Mnyampala aliilea familia yake kwa kuzingatia misingi ya dini ya Kikristo. Kadhalika, alijitahidi kuwasomesha watoto wake ijapokuwa yeye binafsi hakubahatika kupata elimu rasmi wala hakuwa na cheti cha kuhitimu darasa lolote. Alijifunza kusoma na kuandika kwa kubahatisha huko Kinyambwa na katika misheni

ya Bihawana na misheni ya Bahi mkoa wa Dodoma. Hata hivyo, aliwasomesha watoto wake Charles na Edward katika elimu rasmi na walipohitimu mafunzo yao walijiriwa na Jeshi la Polisi kama Askari Polisi. Katika mahojiano niliyofanya na mkewe ilibainika kuwa Mathias Mnyampala alitumia muda wake wa mapumziko kucheza bao, kucheza ngoma ya asili ya Kigogo iitwayo Nindo, kuimba taarabu na kusimulia hadithi (visa) mbalimbali za jamii yake. Vilevile, alipenda kupiga kinanda (*harmonium*) na kutunga nyimbo za dini za kumsifu Mungu.

### **1.1.1.3 Dini**

Mathias Mnyampala alijiunga na dini ya Kikristo mwaka 1933 na kuwa Mkatoliki kama ilivyodokezwa awali na kushika imani ya dini hiyo kikamilifu. Katika maisha yake ya Ukristo, Mathias Mnyampala alikuwa mtu ambaye hakuwa na ubaguzi wa dini wala dhehebu licha yake kuwa muumini wa dhehebu la Kikatoliki. Mnyampala alishirikiana na waumini wa madhehebu tofautitofauti ya dini ya Kikristo na Kiislamu pasi na ubaguzi wowote. Vilevile, katika masuala ya utunzi aliweza kushirikiana na watunzi wa dini ya Kiislamu kwa umoja na ushirikiano kama inavyodhihirika katika *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi na Hazina ya Washairi*. Mnyampala aliweza kujifunza lugha ya Kiarabu ili aweze kujifunza *Kurani Tukufu* na hadithi za Mtume (S.A.W) na alifanikiwa sana kiasi cha kuitwa Sheikh<sup>3</sup>. Hadi wakati fulani Mnyampala aliitwa Sheikh kwa kuwa alikuwa anaweza vyema kusoma *Kurani Tukufu*<sup>4</sup>.

Mnyampala alishirikiana na viongozi mbalimbali wa dini na madhehebu tofauti. Kwa mfano, alikuwa rafiki mkubwa wa Kaluta Amri Abedi ambaye alikuwa Mwislamu.

<sup>3</sup>Maelezo hayo yalipatikana kupitia mahojiano baina ya watafitiwa na mtafiti, na mengine niliyapata katika maandishi yake hususani barua zake.

<sup>4</sup> Maelezo haya tuliyapata wakati wa mahojiano baina ya mtafiti na Mzee Hamsini Mubiru katika Msikiti wa Hamadiya Mnazi mmoja jijini Dar es Salaam tarehe 15/2/2017. Alinionyesha na sehemu ambayo walikuwa wanaghana mashairi yao katika ukumbi uliopo msikitini hapo.



Marehemu Rashid Mfaume Kawawa (Mwislamu), Hayati Julius Kambarage Nyerere (Mkatoliki) na Balozi Jobu Lusinde (Mwanglikana).

Vilevile, katika mswada wake wa *Mahadhi ya Kiswahili* katika dibaji yake iliyoandikwa mwaka 1967 anasema: “Nilikuwa na marafiki zangu akina Rashidi Mlewa, Iddi Hamisi na Mbabe Athumani.” Kwa hiyo, Mnyampala licha ya kuwa mkristo alikuwa na marafiki wengi wa dini ya Kiislamu aliohusiana nao katika kukuza ushairi. Aidha, Mnyampala aliruhusiwa kuingia misikitini, kama vile Msikiti wa Hamadiya<sup>5</sup> uliopo Mnazi Mmoja Dar es Salaam. Katika msikiti huo washairi mbalimbali walikutana na kughani mashairi yao<sup>6</sup>. Kwa ujumla, Mnyampala na washairi wengine wa kipindi hicho walikuwa hawana ubaguzi wa dini wala kabila. Walifanya kazi kwa ushirikiano. Tofauti na zama hizo, siku hizi kumeibuka ubaguzi wa dini miongoni mwa baadhi ya wanajamii.

Mnyampala ndiye Mkristo wa kwanza kuchaguliwa kuwa Hakimu wa Mahakama ya Waislamu. Kazi yake ilikuwa kusuluhisha na kuratibu masuala ya ndoa za Kiislamu katika mahakama ya Kadhi ya Kariakoo, Ilala ‘A’ mwaka 1967. Mnyampala alikuwa miongoni mwa wanajopo ambao walizunguka sehemu mbalimbali nchini Tanzania kuratibu masuala ya ndoa za Kiislamu<sup>7</sup>. Mnyampala aliwahi kuwa kiongozi katika chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi wa Tanzania (UKUTA). Katika uongozi wake Mnyampala aliweza kuwaunganisha washairi wote pasi na ubaguzi wowote wa dini wala kabila<sup>8</sup>.

<sup>5</sup>Taarifa hii ilitokana na mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na jamaa wa karibu na Mnyampala jijini Dar es Salaam, ambao ni Amiri Kaluta Amri Abedi (Mtoto wa Amri Abedi), Mudiru Hamsini na Said Manoro. Mahojiano hayo yalifanyika mwezi Julai, 2016

<sup>6</sup> Maelezo haya yanapatikana katika mahojiano yaliyofanywa na mtafiti na Mzee Hamsini katika Msikiti wa Hamadiyya, Mnazi mmoja Dar es Salaam, tarehe 15/07/2016.

<sup>7</sup> Maelezo haya yanapatikanakatika mahojiano yaliyofanyika baina ya Mtafiti na familia ya Mnyampala pamoja na marafiki na jamaa wa karibu na Mnyampala.

<sup>8</sup> Maelezo haya nimeyapata kutoka katika mahojiano niliyofanya na watafitiwa mfano Prof. Madumulla, Prof. Mulokozi, Mubiru Hamsini, Job Lusinde, Sulemani Kaniki na wengineo. Kadhalika katika Kihore (1978), Madumulla (2011) kwa kuwataja wachache.

#### 1.1.1.4 Kazi

Mathias alifanya kazi mbalimbali ndani na nje ya mkoa wa Dodoma. Hali hii ilimwezesha kuielewa vizuri jamii yake ya Wagogo na nchi yake ya Tanzania. Mnyampala alifanya kazi ya ualimu wa dini ya Kikristo na kuwafundisha watoto na watu wazima kusoma na kuandika katika kijiji cha Mzogole, mkoani Dodoma mwaka 1936. Mnyampala alikuwa karani wa kodi mwaka 1937 huko Kinyambwa, wilaya ya Manyoni mkoani Singida akiwa karani msaidizi na baadaye akahamia Hombolo mwaka 1941. Mwaka 1942 alikuwa karani msimamizi wa ukusanyaji kodi ya kichwa serikalini. Baadhi ya maeneo aliyofanyia kazi ni Usandawe, Matumbula, Buigiri, Msanga, Unyangwila, Itigi, Kivurumo, Jiwe la Singa na Itumbi mkoa wa Singida. Mwaka 1946 alikuwa mtafiti wa ndorobo maporini huko Shinyanga chini ya mradi wa “African Assistant Entomologist Laboratory.” Kazi yake ilikuwa kukamata ndorobo na kutambua jinsia yake. Kazi hii aliifanya kwa muda mfupi kwa sababu ya ugumu wake aliamua kuiacha na kuwa mkulima. Baadaye alikuwa mtunzaji wa stoo (Manyoni huko Singida) mwaka 1946. Pia alifanya kazi ya upigaji chapa (Ludewa huko Iringa na Dodoma) mwaka 1954.

Mnyampala pia aliajiriwa katika mradi wa kilimo cha karanga wilaya ya Kongwa, akawa mtunza muda, baadaye akawa karani na mkalimani. Kazi ya ukarani ilimpa nafasi kubwa sana ya kujifunza Kiingereza. Kutokana na ugumu wa kukaa kwenye mahema na vumbi la huko Kongwa, Mathias aliacha kazi huko Kongwa na aliamua kurudi Dodoma na kuwa karani wa kodi mwaka 1948. Mwaka 1952 alipata kazi ya ukarani wa baraza la watemi wote (Mamlaka ya Wenyeji) chini ya Mtemi Mazengo. Mwaka huohuo akapandishwa cheo na kuwa Katibu wa Mamlaka ya Wenyeji. Hapa alipata pia fursa ya kukutana na watemi mbalimbali wa Ugogo, na kuweza kujifunza mila na desturi za Wagogo kutoka kwa watemi na wazee wa Baraza. Ilikuwa katika

kipindi hiki ndipo alipoanza kujishughulisha na uandishi, na akawa miongoni mwa waanzilishi wa gazeti la *Wela*<sup>9</sup>. Gazeti hilo lilianzishwa Oktoba 1952 na Mnyampala alikuwa mhariri na kiongozi wa gazeti hili. Isitoshe, Mnyampala alikuwa mwanzilishi na kiongozi wa magazeti mbalimbali yaliyoandikwa kwa Kiswahili. Mfano gazeti la *Baragumu*<sup>10</sup> lililokuwa mkoani Dodoma na gazeti la Chama cha Washairi wa Kiswahili wilayani Mpanda lililojulikana kama *Sauti ya Washairi*. Kupitia magazeti hayo mashairi ya Kiswahili na makala mbalimbali yalichapishwa hali iliyochochea Kiswahili kuendelea kukua na kuenea kwa kasi nchini Tanzania. Kitabu chake cha *Historia, Mila na Desturi za Wagogo* (1954) kiliandikwa katika kipindi hiki.

Mnamo mwaka 1960 hadi 1962 alianza kazi ya uliwali katika mahakama ya mji wa Mpanda, mkoa wa Rukwa na baadaye mwaka 1963 hadi 1968 alishika kazi ya uhakimu (Mpanda, Dar es Salaam na Dodoma). Mnyampala alikuwa kiongozi wa mahakama ya Kadhi Ilala "A" Dar es Salaam 1966. Pia alikuwa Diwani wa Dodoma na mjumbe wa Halmashauri ya Ulimu na kamati ya mkoa wa Dodoma<sup>11</sup>. Komba (1969) anaeleza kuwa mwaka 1966 Mnyampala alikuwa mhadhiri wa muda mfupi wa Fasihi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kipindi hicho chuo kikuu kilijulikana kama The Institute of Adult Education, University College of Dar es Salaam. Komba anaongezea kuwa mojawapo ya kozi zilizofundishwa wakati huo ni "Mashairi ya Kiswahili." Wanafunzi walijifunza na kujadili mashairi ya Sayyid Abdala bin Ali Nassir, Muyaka bin Haji na ya Sheikh Amri Abedi<sup>12</sup>. Kadhalika, wanafunzi walijifunza namna ya kutunga mashairi kwa kuzingatia vina na mizani. Licha ya Mathias Mnyampala kuwa mhadhiri, pia alikuwa mjumbe wa kamati ya ushauri wa

<sup>9</sup> Neno la Kigogo lenye maana ya kumekucha.

<sup>10</sup> Gazeti hili lilikuwa linaendeshwa na Tanganyika Newspapers Ltd, Dar es Salaam.


<sup>11</sup> Taarifa hizi tulizipata katika mahojiano yaliyofanyika baina ya mtafiti na Mzee Sulemani Kaniki na Balozi Job Lusinde mjini Dodoma.

<sup>12</sup> Taarifa hizi zilizoelzwa na Komba tulizipata pia nyanyani katika nyaraka za Mnyampala zilizohifaziwa na mke wa Charles Mnyampala, zimeambatanishwa nyuma ya tasnifu hii. (Beatrice Laban Mhogolo)


Kiswahili ya Chuo cha Dar es Salaam. Mwaka 1967 alikuwa Karii<sup>13</sup> katika Mahakama Kuu ya Mwanzo Kariakoo, Dar es Salaam. Mwaka 1968 aliamishwa Dodoma ambako alifanya kazi mpaka akastaafu kutokana na maradhi.

### 1.1.1.5 Ugonjwa na Kifo

Mnyampala alianza kuugua ugonjwa wa ini mwaka 1966, na kuaga dunia mwaka 1969. Alipelekwa katika hospitali mbalimbali ikiwemo Muhimbili (Dar es Salaam) na Mvumi (Dodoma) na ndipo alipogundulika kuwa anasumbuliwa na ugonjwa wa ini. Ilikuwa katika kipindi hiki alipoamua kuacha kazi kutokana na udhaifu wa afya yake. Hata alipokuwa akiugua alijaribu kuandika mashairi kuelezea hali yake ya afya. Kuna mashairi mawili ambayo yanaeleza namna alivyoelekea mautini. Shairi la kwanza, ni lile lilolandiwa tarehe 7/3/1969 na kuliita “Ndwele Sii Yaniuma” ambalo ni lifuatalo:




<sup>13</sup> Kazi yake ilikuwa kutafsiri kazi za majaji zilizoandikwa kwa Kiswahili kwenda Kiingereza.



**Picha namba 1: Shairi la “Ndwele Sii Yaniuma” (tarehe 3/11/2016).**

Mathias Mnyampala pia aliandika shairi lingine wakati afya yake ilipokuwa ukingoni kabisa, kwani alishindwa hata kulimalizia, alikomea ubeti wa pili tu. Shairi hilo linaitwa “Taa Yangu Yafifia” na linasema hivi:

### TAA YANGU YAFIFIA



**Picha namba 2: Shairi la “Taa Yangu Yafifia” (tarehe 3/11/2016).**

Hati alioitumia katika uandishi wa mashairi hayo kwa mkono wake pasipo kuchapwa inadhihirisha udhaifu aliokuwa nao na ilifikia wakati akashindwa kumaliza shairi la pili na kumwambia mwanawe amsaidie kuandika wakati yeye akimtajia maneno<sup>14</sup>. Mashairi haya yanadhihirisha wazi jinsi Mathias Mnyampala aliipenda kazi yake ya utunzi wa mashairi na kuithamini. Kwa maneno yake anaonesha ni mtu aliyetambua umuhimu na thamani ya tasnia ya uandishi, lugha ya Kiswahili, jamii na utamaduni wake kwa ujumla. Baada ya jitihada za kuokoa maisha yake kushindikana, Mathias Mnyampala aliaga dunia tarehe 8/6/1969 na kuzikwa Dodoma mjini katika makaburi yaliyoko Barabara ya Bahi, Mtaa wa Mnyampala, kata ya Majengo. Picha ifuatayo inaonesha mandhari ya kaburi lake.

<sup>14</sup> Kwa mujibu wa maelezo ya mkewe Mathias Mnyampala na mkewe Charles Mnyampala nyanjani.



**Picha namba 3: Kaburi la Mathias Mnyampala<sup>15</sup> ( tarehe 11/11/2016).**

Picha hiyo ya kaburi lake inadhihirisha kuwa Mnyampala kweli ni jabali lililosahaulika sio tu katika uwanja wa taaluma bali hata katika jamii kwa ujumla. Mnyampala na waandishi wengine kama vile Shaaban Robert na waandishi wengine waliotangulia mbele za haki nao makaburi yao yapo katika mazingira yasiyoeleweka. Kwa kufanya utafiti huu katika kazi za ushairi wa Mathias Mnyampala tunakusudia kumuenzi Mathias Mnyampala kama mshairi maarufu katika historia ya ushairi wa Kiswahili.

#### **1.1.1.6 Maandishi ya Mathias Mnyampala**

Mathias aliandika maandishi mengi ya fasihi ambayo yanaweza kugawanywa katika mafungu makuu mawili: ushairi na nathari. Japo aliandika maandishi mengine ambayo yalihusu historia ya Ugogo na habari nyinginezo, tungo zake nyingi zilijikita

<sup>15</sup>Lilijengwa na Prof. Joshua Madumulla akishirikiana na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, mwaka 2011.

katika ushairi na nathari. Kwa upande wa ushairi ambako alibobea zaidi katika zama zake, alitambulika kwa lakabu ya “Penda Chako.” Kupitia lakabu hiyo tunatambua kuwa Mathias Mnyampala alikuwa mzalendo, mtamaduni na mwenye kuthamini nchi yake. Pia alitaka watu wathamini utamaduni wao kuliko wa kigeni. Kwa upande wa mashairi, alijishughulisha sana na mashairi ya utatu (tathilitha) na ya unne (tarbia), pamoja na tenzi. Madumulla (2011) anaeleza kuwa Mnyampala ndiye alianzisha mtindo wa mashairi ya msisitizo na mtiririko. Aidha, Mnyampala ndiye alifufua na kuvumisha ushairi wa majibizano na kuupatia jina la Kigogo la ngonjera<sup>16</sup>. Mathias alipoandika ‘ngonjera’ viongozi wa juu wa serikali waliguswa nazo sana hasa kwa jinsi yalivyotumika kutangaza, kuhimiza, kutetea na kueneza sera za chama tawala cha Tanganyika African National Union (TANU) pamoja na siasa za Azimio la Arusha.

Inasemekana kuwa, Mnyampala aliandika ushairi, nathari, hadithi fupi, insha na vitabu vya habari mbalimbali zinazohusu mila na desturi za Wagogo na nyinginezo. Baadhi ya tungo zake ni: *Diwani ya Mnyampala, Waadhi wa Ushairi, Azimio la Arusha na Maandiko Matakatifu, Diwani ya Lambert, Fasili Johari ya Mashairi, Hadithi za Wahenga Wetu: Kitabu cha Kwanza, Hadithi za Wahenga Wetu: Kitabu cha Pili, Hadithi za Wahenga Wetu: Kitabu cha Tatu, Hadithi za Wahenga Wetu: Kitabu cha Nne, Hazina ya Washairi, Historia ya Hayati Sheikh Kaluta Amri Abedi: 1924-1964, Historia ya Kiswahili, Historia ya Mtemi Mazengo, Historia, Mila na Desturi za Wagogo, Kisa cha Bahati na Wazazi Wake, Kisa cha Dume la Nyani na Hadithi Nyingine, Kisa cha Kazimba na Msichana, Kisa cha Mrina Asali na Wenzake Wawili, Kisa cha Ndezi na Binadamu: Kitabu cha Kwanza, Kisa cha Ndezi na Binadamu: Kitabu cha Pili, Kisa cha Ndezi na Binadamu: Kitabu cha Tatu, Kisa cha*

---

<sup>16</sup> Kwa maana yake twende pamoja; tushirikiane.



*Ndezi na Binadamu: Kitabu cha Nne, Kisa cha Tandala na Bibi Mtekamaji, Kito cha Hekima: Kitabu cha Kwanza, Kito cha Hekima: Kitabu cha Pili, Mahadhi ya Kiswahili, Maisha ni Kugharamia, Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi, Mashairi ya Vidato, Mbinu za Ujamaa, Methali za Kiswahili na Maneno yenye Hekima: Kitabu cha Kwanza, Methali za Kiswahili na Maneno yenye Hekima: Kitabu cha Pili, Ngonjera za UKUTA Na. 1, Ngonjera za UKUTA Na. 2, Sikilizeni Hekima: Methali na Mawaidha, Taaluma ya Kiswahili, Ufasaha wa Kiswahili, Ugogo na Ardhi Yake, Umoja ni Ngome Yetu, Utenzi wa Enjili, na Utenzi wa Zaburi.*

Licha ya jitihada yake kubwa ya kuandika tungo nyingi za kifasihi, mpaka sasa ni kumi na tisa (19) pekee zilizochapishwa. Kazi hizo ni: *Historia, Mila na Desturi za Wagogo wa Tanganyika (1954)*<sup>17</sup>, *Fasili Johari ya Mashairi (1959)*, *Kisa cha Mrina Asali na Wenzake Wawili (1961)*, *Utenzi wa Enjili (1963)*, *Utenzi wa Zaburi (1965)*, *Diwani ya Mnyampala (1965)*, *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi (1965)*, *Waadhi wa Ushairi (1965)*, *Taaluma ya Kiswahili (1966)*, *Kisa cha Bahati na Wazazi Wake (1967)*, *Sikilizeni Hekima: Methali na Mawaidha (1967)*, *Mbinu za Ujamaa (1968)*, *Ngonjera za UKUTA Na. 1 (1970)*, *Ngonjera za UKUTA Na. 2 (1971)*, *Diwani ya Lambert (1971)*, *Historia ya Kiswahili (1974)*, *Historia ya Hayati Sheikh Kaluta Amri Abedi: 1924-1964 (2011)*, *Maisha ni Kugharamia (2014)* na *Ugogo na Ardhi Yake (2014)*.

Baadhi ya vitabu vyake tangu vichapishwe miaka ya 1960 na 1970 havijawahi kuchapishwa tena na kwa sasa vinapatikana kwa nadra sana. Madumulla (2011) anadai kuwa Mnyampala kwa juhudi ya kuandika hapitani na waandishi wengine kama vile Shaaban Robert ambaye anatambuliwa na wengi kiasi cha kuitwa: “Baba wa Fasihi ya Kiswahili,” “Shakespeare wa Tanzania,” “Mhubiri Mimbarini” na lakabu

<sup>17</sup> Hiki ndicho kitabu chake cha kwanza kuchapishwa.

nyinginezo. Madumulla anasisitiza kuwa kwa hakika sifa alizopewa Shaaban Robert zinaweza pia kupewa Mathias Mnyampala. Aidha, wasanii hao waliishi kipindi kimoja, wakibadilishana mawazo na kufanya mambo mengi ya uendelezaji wa lugha ya Kiswahili na fasihi yake, hasa kupitia chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA). Hivyo vipengele vya fani na maudhui ya kazi zao huingilianana kukamilishana. Kutokana na maelezo ya Madumulla, tunaungana naye kuwa Mnyampala ni mtunzi maarufu ambaye anafaa kuenziwa katika tasnia ya ushairi, fasihi na Kiswahili kwa ujumla kutokana na mchango wake katika uandishi wa kazi mbalimbali.

## **1.2 Suala la Utafiti**

Mnyampala ni miongoni mwa watunzi ambao wamechangia pakubwa katika ushairi wa Kiswahili na fasihi yake. Umaarufu wake huenda ukawa kama ule wa akina Muyaka bin Haji na Shaaban Robert japo tahakiki za kifasihi zimeelekea kumpuuza. Maoni ya wataalam mbalimbali yanapingana kuhusu mchango wa Mathias Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili. Wapo wanaosema amechangia katika ushairi wa Kiswahili na wanaopinga. Isitoshe, tafiti chache zilizofanywa kuhusu kazi za ushairi wa Mathias Mnyampala hazijazingatia umuhimu wa mwingilianomatini wa muktadha wa utunzi katika kutathmini mchango wa tungo zake. Katika uhakiki wa kazi za msanii yeyote, muktadha wa utunzi ni muhimu kuzingatiwa kwani hakuna matini inayoibuka katika ombwe. Ni kutokana na hali hiyo ndipo tunapata mwanya wa utafiti kuchunguza upekee wa ushairi wa Mathias Mnyampala kimwingilianomatini. Upekee huu unachunguzwa kwa kuhakiki mbinu za kifani zinavyotumika kuibua maudhui kwa kuzingatiwa muktadha wa utunzi wake kimwingilianomatini. Kwa njia hii utafiti huu umeweza kutathmini mchango wa tungo za Mathias Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili kimwingilianomatini kwa

kuzingatia kazi teule zilizochapishwa na zisizochapishwa. Kazi hizo ni *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965), *Ngonjera za UKUTA Na. 1* (1970), *Hazina ya Washairi*, *Mashairi ya Vidato na Mahadhi ya Kiswahili*.

### **1.3 Malengo ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mwingilianomatini katika ushairi wa Mathias Mnyampala. Ili kulifikia lengo hili utafiti huu ulijikita kwenye malengo mahususi yafuatayo:

- i) Kupambanua muktadha wa utunzi uliomsukuma Mathias Mnyampala katika utunzi wa kazi zake za ushairi wa Kiswahili.
- ii) Kuhakiki mbinu za kifani zinavyotumika kuibua maudhui katika kazi teule za ushairi wa Mathias Mnyampala.
- iii) Kutathmini mchango wa kazi za ushairi za Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

### **1.4 Maswali ya Utafiti**

Maswali yafuatayo yanaongoza utafiti wetu:

- i) Ni muktadha upi umeathiri tungo teule za ushairi za Mathias Mnyampala?
- ii) Ni kwa njia gani mbinu za kifani zinatumiwa kuibua maudhui katika kazi teule za Mathias Mnyampala?
- iii) Je, mashairi ya Mathias Mnyampala yamechangia vipi maendeleo ya sanaa ya ushairi wa Kiswahili?

### **1.5 Sababu za Kuteua Mada ya Utafiti**

Mathias Mnyampala anajipambanua kama mtunzi wa kipekee kwa kuwa ni msanii wa kwanza wa Kikristo anayetoka bara (Dodoma) akilinganishwa na washairi wa enzi

zake. Wengi wa washairi wa enzi zake walitoka sehemu za pwani ama sehemu za bara ambazo zilitawaliwa na Waarabu. Baadhi ya washairi hao ni: Amri Abedi, Saadan Kandoro na Akilimali Snow White (Mulokozi na Sengo, 2005). Hata hivyo licha ya upekee wake, Mathias Mnyampala hajashughulikiwa kikamilifu na wahakiki wa fasihi ili kubaini mchango wa kazi zake kimwingilianomatini na kwa kuzingatia muktadha wake wa tungo zake anuwai zilizochapishwa na zisizochapishwa. Katika utafiti huu tumebaini kuwa kuna tahakiki chache zilizofanywa kuhusiana na kazi zake na hivyo kuna uhaba wa marejeleo muhimu kuhusiana na tungo za Mathias Mnyampala.

Kwa ujumla, mchango wa Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili haujaelezwa kikamilifu tukilinganisha na washairi wengine kwa mfano Muyaka bin Haji na Shaaban Robert (Hichens, 1940; Abdulaziz, 1979; Ohly, 1977; Senkoro, 1976; Khatib, 2011 na Ponera, 2014). Hizo ndizo sababu zilizotusukuma kumchagua Mathias Mnyampala ili kuchunguza kazi zake pamoja na kutambua mchango wake katika taaluma ya fasihi na Kiswahili kwa jumla. Mathias Mnyampala ni mwanafasihi mbobevu na mkomavu, lakini amesahaulika (Madumulla, 2011). Anaongezea kuwa Mathias Mnyampala ni 'Jabali Lililosahaulika'. Zaidi ya hayo Madumulla anadaiwa kuwa Mnyampala ni mtaalamu muhimu katika taaluma ya Kiswahili, hususani upande wa ushairi, fasihi, jamii ya Tanzania na Afrika Mashariki kwa jumla. Ni mtunzi aliyeandika kazi mbalimbali ambazo zimechapishwa na zisizochapishwa (Madumulla, 2011; Makaka, 2012 na Roy, 2013). Kwa hiyo imehalisi kufanya utafiti huu kuthibitisha madai hayo.

Kutokana na mawazo ya wahakiki hao, maswali tuliyojiuliza ni: Kwa nini Mathias Mnyampala aitwe Jabali Lililosahaulika? Mbona hajaangaziwa? Ujabali huo

unajitokezaje? Je, kazi ambazo hazijachapishwa zina umuhimu wowote kifani na kimaudhui? Aidha, wahakiki waliochambua kazi za Mathias hawajahusisha muktadha wa utunzi wa mwandishi pamoja na mwingilianomatini wa ushairi wa Mathias Mnyampala na watunzi wengine. Mazingira ya utunzi na uhusiano wake na mazingira ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kimwingilianomatini yanayochangia uelewa wa kazi za mtunzi na mchango wake kwa jamii. Utafiti huu unaangazia suala hili. Kwa ujumla, maudhui na fani hutegemea muktadha uliozaa kazi ya sanaa. Maswali hayo yanatokana na ukosefu wa utafiti wa kina kuhusu mchango wa Mnyampala katika taaluma ya Kiswahili, ushairi na jamii kwa ujumla. Haja ya kupata majibu kwa maswali hayo, ndiyo yaliyotufanya kuchunguza ushairi wa Mathias Mnyampala kimwingilianomatini ili kutathmini mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

### **1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu utakuwa rejeleo muhimu kuhusiana na muktadha wa utunzi na nafasi ya Mathias Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili. Aidha, utafiti huu unapambanua mchango wa Mnyampala (akiwa mshairi Mkristo anayetoka sehemu za bara) katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kimaudhui na kifani. Utafiti huu unabainisha mchango wa tungo za Mathias Mnyampala katika Kiswahili katika kukuza msamiati wa lugha, mitindo na miundo ya ushairi wa Kiswahili. Ni kichocheo kwa washairi chipukizi cha kusoma, kutunga na kuandika kazi mbalimbali za kisanaa kwa kuchota baadhi ya misamiati, mitindo na mbinu kutoka katika maandishi ya Mathias Mnyampala.

Kwa kuyachambua na kuyahakiki mashairi ya Mathias Mnyampala, utafiti huu utasaidia wasomaji na wanafunzi kupata hamu ya kuzisoma kazi zake na kuelewa

vyema mbinu za kifani na maudhui yaliyomo katika maandishi hayo. Vilevile, katika kufanya utafiti kuhusu mtaalam huyu tumebaini miswada mbalimbali inayohusu taaluma ya Kiswahili ambayo haijachapishwa. Inatarajiwa kuwa utafiti huu utachochea ari ya miswada hiyo kuchapishwa. Kwa njia hii, miswada hiyo itakuwa na manufaa kwa familia yake pamoja na wahakiki na watunzi wa kazi mbalimbali za Kiswahili, hususani ushairi na fasihi ya Kiswahili.

Utafiti huu ni muhimu kinadharia kwa sababu unapambanua ufaafu wa Nadharia ya Mwingilianomatini katika kuelezea uhusiano baina ya fani, maudhui na muktadha katika kutathmini mchango wa Mathias Mnyampala katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili. Aidha, nadharia hii imetusaidia kuona namna kazi za fasihi zinavyotegemeana, kushirikiana na kuhusiana katika kuleta maana ya kazi husika. Pia utafiti huu umeweka misingi imara kwa ajili ya tafiti nyingine katika kuchunguza maisha ya watunzi wengine na michango yao katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili na taaluma ya Kiswahili kwa ujumla. Utafiti huu utasaidia kurutubisha tahakiki za ushairi wa Kiswahili kwa kuangazia kunga za kifani na kimaudhui katika mashairi maalum ya Mathias Mnyampala.

### **1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Uchambuzi huu umehusisha kazi teule za ushairi ambazo zimechapishwa na zisizochapishwa. Kazi hizo ni: *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965), *Ngonjera za UKUTA Na. 1* (1970), *Hazina ya Washairi*, *Mashairi ya Vidato* na *Mahadhi ya Kiswahili*. Aidha, utafiti huu unachunguza muktadha wa uandishi kijamii, kisiasa, kiuchumi na kimwingilianomatini. Vilevile, tunachunguza mbinu za kifani zinavyotumika kuibua

maudhui katika kazi teule za Mathias Mnyampala na mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

## **1.8 Mbinu za Utafiti**

Katika kushughulikia mbinu za utafiti, tumefafanua mkabala wa utafiti, vyanzo vya data, mikakati ya uteuzi wa sampuli na usampulishaji, watafitiwa na kazi teule. Aidha, tumebainisha vifaa vya kukusanyia data na uwasilishaji pamoja na uchambuzi wa data uliofanyika na kufikia malengo ya utafiti huu.

### **1.8.1 Mkabala wa Utafiti**

Utafiti huu unatumia mkabala wa kitaamuli (kimaelezo au kisifa). Mkabala wa kitaamuli ni ule usio wa kitakwimu. Mara nyingi mkabala huu hutumika katika tafiti za sanaa na sayansi ya jamii. Aidha, mkabala wa kitaamuli hutumiwa na wanataaluma wa Kiafrika kwa sababu unawasaidia kupata welewa wa kina juu ya masuala ya kitamaduni, kisiasa na kiuchumi yanayoathiri jamii kwa ujumla. Huu ni mkabala unaolenga kufafanua data kwa maelezo tofauti na mkabala ule wa kiidadi unaotumia nambari ama takwimu katika ujengaji wa hoja. Kwa kuwa data za utafiti zinahusu sayansi ya kijamii, ni dhahiri kuwa mkabala huu umetufaa katika uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti huu kwa kutumia Nadharia ya Mwingilianomatini.

### **1.8.2 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika katika maeneo mbalimbali katika mkoa wa Dodoma na Dar es Salaam nchini Tanzania. Maeneo haya yamechaguliwa kimakusudi kwa sababu ni mojawapo ya maeneo ambayo Mathias Mnyampala aliwahi kuishi na kufanya kazi. Aidha, maeneo hayo ndiko wanakoishi jamaa na ndugu wa Mathias Mnyampala na hivyo ndiko kulifaa katika kupata data za kimsingi na fuatizi kutoka kwa watafitiwa. Kadhalika, tulienda Iringa kwa kuwa Prof. Madumulla alihamia huko kikazi.

### 1.8.3 Vyanzo vya Data

Utafiti huu ni wa maktabani na nyanjani. Ili kufanikisha malengo ya utafiti huu, mtafiti alikusanya data na taarifa muhimu kutoka maktabani na nyanjani kama ifuatavyo:

#### 1.8.3.1 Upekuzi Maktabani

Mtafiti alizuru maktaba mbalimbali kudurusu vitabu, tasnifu, majarida na maandishi mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu. Mtafiti alipata yaliyoandikwa kuhusu mada na marejeleo muhimu kuhusu utafiti huu. Katika upekuzi maktabani data zilizopatikana ni za msingi na za upili. Data za msingi zilipatikana katika kazi teule za mwandishi. Na data za upili tulizipata kupitia vitabu, tasnifu, majarida na maandishi mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu. Maktaba zilizohusika ni pamoja na maktaba za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Dodoma pamoja na maktaba ya Taifa na Makavazi ya TATAKI katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Nchini Kenya maktaba ya Margaret Thatcher katika Chuo Kikuu cha Moi ilitumika kikamilifu katika utafiti huu. Vitabu teule vimesomwa pamoja na maandishi na matini mbalimbali zilizohusiana na utafiti huu.

Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilituuliwa kwa vile ni chuo ambacho kina marejeleo na tafiti nyingi kuhusu wataalamu mbalimbali waliowahi kuandika, kutafiti na kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi, ukiwemo ushairi. Pia, Mathias Mnyampala alikuwa mhadhiri wa fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1966, akifunza utunzi wa mashairi (Komba, 1969). Wakati huo, chuo hicho kilijulikana kama “The Institute of Adult Education, University College, Dar es Salaam<sup>18</sup>. Vilevile, kwa sasa shahada ya kwanza hadi ya tatu hutolewa chuoni hapo

<sup>18</sup> Taarifa hizi pia zilipatikana kutokana na mahojiano yaliyofanyika baina ya mtafiti na jamaa wa karibu waliowahi kufanya kazi na Mnyampala. Tarehe 12/05/2017.



kwa Kiswahili. Hivyo ilikuwa vyema kujua wengine wamefanya nini kuhusu Mnyampala na kazi zake. Nayo maktaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma iliteuliwa kutokana na sababu kwamba chuo hicho ni cha kwanza nchini Tanzania kutoa shahada ya Awali ya Kiswahili. Na sasa Chuo Kikuu cha Dodoma kinatoa shahada ya B.A Kiswahili, M.A Kiswahili na Uzamifu katika Kiswahili. Pia, kuna kozi inayofundishwa katika ngazi ya M.A Kiswahili inayohusu wataalamu mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili akiwemo Mathias Mnyampala. Katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma tulipata tasnifu mbalimbali za kiwango cha uzamili zilizoandikwa kuhusiana na mada tunayoshughulikia.

Nchini Kenya maktaba ya Margaret Thatcher katika Chuo Kikuu cha Moi imetumika kutokana na ukweli kwamba ipo katika chuo ambacho mtafiti anasoma digrii yake. Aidha, ni chuo cha kwanza nchini Kenya na Afrika Mashariki kwa ujumla kutoa shahada ya Uzamifu ya kwanza ulimwenguni iliyoandikwa kwa Kiswahili. Hivyo, maktaba ya Chuo Kikuu cha Moi ilikuwa kitovu cha kujua wengine wamefanya nini kuhusiana na mada tunayoishughulikia. Pia, maktaba hii imetuwezesha kujua mpangilio wa tasnifu unaotakiwa kufuatwa pamoja na mambo mengine ya kitaaluma.

Utafiti wa maktabani uliniwezesha kuyapitia maandishi mbalimbali yanayohusu Mathias Mnyampala na kazi zake. Kupitia maandishi hayo niliweza kupata habari zaidi kuhusu Mnyampala na kazi zake. Aidha, mapitio ya maandishi yaliniwezesha kupata kujua watafiti wengine walipofikia kuhusiana na suala la utafiti. Mapitio haya yalinibainishia mapengo ya utafiti wa awali na ambayo yanaweza kuzibwa na matokeo ya utafiti huu. Kadhalika, nilitalii tovuti ili kupata matini mbalimbali katika tovuti na wavuti zilizohusiana na suala la utafiti.

### 1.8.3.2 Utafiti Nyanjani

Mtafiti alikwenda nyanjani Iringa, Dar es Salaam na Dodoma nchini Tanzania ili kupata data za kimsingi na fuatizi za utafiti huu. Uteuzi wa mikoa ya Iringa, Dar es Salaam na Dodoma ulitokana na ukweli kwamba Dar es Salaam kuna Chuo Kikuu cha kwanza nchini Tanzania ambacho kina wahadhiri wengi ambao wanafundisha ushairi na pia wamehakiki kazi mbalimbali za ushairi wa Kiswahili. Wataalamu hao wamekuwepo tangu miaka ya sitini hadi sasa. Pia, kuna wanafunzi wa uzamili na uzamifu wanaopatikana katika chuo hicho. Vilevile, Dar es Salaam kuna watunzi wa ushairi wa kipindi cha mtaalam huyu na jamaa wa karibu wa Mnyampala wanaoishi sehemu hii. Kadhalika, kwa kuwa Mnyampala alikuwa mmojawapo wa wanazuoni na kiongozi wa chama cha UKUTA, hivyo taarifa zake pamoja na maandishi mbalimbali ya kazi zake yaliweza kupatikana kwa urahisi katika mkoa huo.

Uteuzi wa mkoa wa Dodoma ulitokana na sababu kwamba huko ndiko nyumbani kwa Mathias Mnyampala ambako mkewe ama familia yake na ndugu wa karibu wa Mnyampala wanapatikana. Pia, nyaraka mbalimbali za Mathias Mnyampala zinapatikana kwa mke wa mtoto wa Mathias Mnyampala (Marehemu Charles Mnyampala). Aidha, kuna marafiki wa karibu wa Mathias Mnyampala waliowahi kufanya kazi pamoja naye, ambao mtafiti aliweza kuwahoji.

Uteuzi wa mkoa wa Iringa ulitokana na kwamba Prof. Madumulla kwa sasa anafanya kazi katika Chuo Kikuu cha Iringa. Profesa huyu ni mmojawapo wa watafiti ambao wamefanya utafiti mwingi juu ya Mathias Mnyampala. Isitoshe, ndiye aliyeanzisha kozi inayohusu kazi za ushairi za Mnyampala katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Zaidi ya hayo, Prof. Madumulla yupo karibu sana na familia ya Mathias Mnyampala kutokana na kufanya utafiti kuhusu mtunzi huyu na kuwapeleka wanafunzi wa Chuo

Kikuu cha Dodoma kufanya utafiti nyumbani kwa Mnyampala. Sambamba na hilo, ndiye aliyewahamasisha wadau wa Kiswahili kujengea kaburi la Mathias Mnyampala.

#### **1.8.4 Sampuli na Usampulishaji wa Utafiti**

Sampuli ya utafiti huu ni kazi sita za ushairi za Mathias Mnyampala zilizochapishwa na zisizochapishwa. Data zilipatikana kwa kuchambua kazi teule za ushairi za Mathias Mnyampala. Kwa kuwa sio rahisi kutafiti kazi zote za ushairi zilizoandikwa na Mathias Mnyampala, mtafiti alifanya usampulishaji.

Uteuzi wa sampuli hutegemea taarifa, muda na fedha zitakazotumika katika utafiti huo. Katika utafiti huu tulitumia aina tatu za usampulishaji; usampulishaji makusudi (usio nasibu), usampulishaji nasibu na usampulishaji tajwa. Usampulishaji makusudi ulitumika kuteua mtunzi Mathias Mnyampala na kazi zake za ushairi. Kwa hiyo, usampulishaji makusudi ulitumika kuteua kazi za ushairi za Mathias Mnyampala ambazo zimechapishwa na hazijachapishwa. Utafiti wetu ulibaini kazi tatu tu za ushairi ambazo hazijachapishwa, hivyo kazi hizo zote tatu zilitumika katika utafiti huu. Kazi hizo ni *Hazina ya Washairi*, *Mashairi ya Vidato* na *Mahadhi ya Kiswahili*. Kwa upande wa kazi za ushairi zilizochapishwa tulitumia usampulishaji wa makusudi kuchagua kazi hizo kwa kuziorodhesha na kisha kuchagua kazi tatu (3) kinasibu. Kazi hizo ni *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965) na *Ngonjera za UKUTA Na. 1* (1970).

Aidha, mtafiti alichagua matini au data kimakusudi ndani ya kazi teule ambazo aliona ni muhimu katika uchanganuzi wa data zake. Pia, kazi za ushairi teule zilitumika kama kiwakilishi cha kazi zote za ushairi zilizoandikwa na Mathias Mnyampala.

Zaidi ya hayo, utafiti huu ulitumia usampulishaji makusudi na tajwa kuteua maeneo ya utafiti na watafitiwa waliohusika katika utafiti huu. Vilevile, wawakilishi wanne wa familia ya Mathias Mnyampala walichaguliwa kimakusudi. Sababu ya kuchagua wasailiwa wanne wa familia ya Mathias Mnyampala ni kwamba; ndugu wa karibu wa Mnyampala walitoa ruhusa kwa hao jamaa wanne ambao waliona wanaweza kutoa taarifa muafaka kuhusiana na utafiti huu. Waliohusika katika utafiti huu ni Mary Mangwela (mkewe Mathias Mnyampala), mke wa Charles Mnyampala (Beatrice Laban Mhogolo, ndiye anayetunza nyaraka za Mathias Mnyampala), Katarina (mdogo wake Mathias Mnyampala) na Stephano (Mboje) (mtoto wa mdogo wake Mathias Mnyampala). Kupitia watafitiwa hawa tulifanikiwa kupata historia ya maisha ya Mathias Mnyampala na maandishi mbalimbali aliyoandika ikiwemo barua, picha, kazi zilizochapiswa na miswada ya kazi ambazo hazikuchapishwa.

Usampulishaji tajwa ulifanyika kwa jamaa na marafiki wa karibu walioishi na kufanya kazi na Mathias Mnyampala wakati wa uhai wake. Usampulishaji huu ni ule unaohusu urejeleaji wa watafitiwa wale ambao wanasadikika kuwa na taarifa ama data za kile kinachotafitiwa. Hivyo kuna baadhi ya watafitiwa waliotuelekeza kwa watafitiwa wengine ambao walisadiki kuwa wanaweza kutoa taarifa sahihi juu ya Mnyampala kwa kuwa walifanya kazi pamoja ama wote walijihusisha katika utunzi wa mashairi na shughuli mbalimbali za kiutamaduni, kijamii na kisiasa. Kupitia usampulishaji tajwa tulipata watafitiwa watano ambao tuliweza kuwahoji mahojiano nao na walitoa data ambazo zilitufaa katika utafiti huu. Aidha, kupitia kwa watafitiwa hao, tulifanikiwa kupata historia ya maisha ya Mnyampala, tungo zake ambazo zimechapishwa. Pia walitueleza kuwa kuna baadhi ya miswada ya kazi zake ambazo hazijachapishwa. Vilevile watafitiwa hawa walitueleza juu ya barua alizokuwa

anaandikiana na viongozi wa kisiasa na kijamii pamoja na washairi mbalimbali wa kipindi hicho.

Watafitiwa wengine ni wahitimu wawili wa ngazi ya uzamili na uzamifu pamoja na wahadhiri na wahakiki wawili wa kazi za ushairi wa Kiswahili. Watafitiwa hawa tuliwapata kwa kutumia usampulishaji makusudi. Watafitiwa hawa walitusaidia kupata historia ya Mnyampala na maeneo ambayo yameshughulikiwa. Kwa ujumla, watafitiwa kumi na watatu walihusika katika utafiti huu.

### **1.8.5 Njia za Kukusanyia Data**

Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano yaliyofanywa kati ya mtafiti na watafitiwa. Mwongozo wa maswali ya utafiti uliandaliwa ili kupata taarifa kamili zilizotarajiwa katika utafiti huu. Mbinu hii ilituuliwa kutokana na uelewa wa watafitiwa na upeo wa kijiografia katika eneo husika.

#### **1.8.5.1 Mahojiano**

Kiutafiti mahojiano yanaweza kuwa funge, nusu-funge na huru. Mtafiti aliwahoji watafitiwa kila mmoja kwa wakati wake. Katika utafiti huu mahojiano huru yalitumika baina ya mtafiti na watafitiwa ambao ni familia ya Mathias Mnyampala. Mbinu hii inaruhusu muundo wa namna ya uendeshaji wa mahojiano kubadilika kulingana na mtu anayehojiwa na mahali ambapo mahojiano hayo hufanyika (Mligo, 2012). Mbinu hii ilituwezesha kupata taarifa kuhusu historia ya mwandishi na kazi zake zilizochapishwa na zisizochapishwa. Mahojiano nusu-funge yalitumika kwa wanazuoni, wahakiki wa kazi za Mnyampala pamoja na jamaa na marafiki wa karibu wa Mnyampala. Mahojiano ya aina hii yanaruhusu maswali ibuka hasa pale ufafanuzi utakapohitajika. Mahojiano yalifanyika ana kwa ana, ofisini ama nyumbani kwa wasailiwa.

Wakati zoezi la mahojiano likiendelea, mtafiti alitumia kalamu na kitabu cha kumbukumbu kunukuu maelezo yanayohusu historia ya Mnyampala na kazi zake. Aidha, mtafiti alitumia kinasu sauti kwa idhini ya watafitiwa, kunasa mahojiano yaliyokuwa yakifanyika, kuhusu historia ya Mnyampala na kazi zake ili kuwarejelea baadaye wakati wa kuchanganua data. Aidha, mtafiti alipiga picha za kawaida zinazohusu historia ya maisha ya Mathias Mnyampala na za watafitiwa, ambazo zimeambatanishwa mwishoni mwa kazi hii na zingine ndani ya kazi, zote kwa pamoja zimekuwa sehemu ya uchambuzi wa kazi hii. Mambo yote yalifanyika kwa idhini yao na kama ithibati ya ukweli wa tukio na uhalali wa data.

Hali kadhalika, kulikuwapo na mahojiano kwa njia ya simu na barua pepe hasa katika sehemu ambayo ilikuwa vigumu kuonana na watafitiwa ana kwa ana kutokana na sababu za umbali wa kijiografia pamoja na matatizo mbalimbali ya kiafya na kiuchumi. Pia ilitokana na utofauti wa muda ambao tulitakiwa kukutana. Baadhi ya watafitiwa kwa mfano, Mathieu Roy (Mfaransa), tulifanya mahojiano kwa njia ya barua pepe na simu kwa kutumia ‘*WhatsApp messenger*’. Aidha, tulihojiana na Elias Makaka anayefanya kazi huko Kilimanjaro, kupitia barua pepe. Watafiti hao walitusaidia kutupa historia ya Mnyampala na maeneo ambayo wao waliyashughulikia katika tafiti zao.

## **1.8.6 Vifaa vya Utafiti**

### **1.8.6.1 Tarakilishi Pakatwa (Tarakilishi)**

Tarakilishi pakatwa ilitumiwa na mtafiti kutafuta matini katika tovuti na wavuti na kuhifadhi data mbalimbali ambazo zilipigwa picha, zilirekodiwa na kuchambuliwa na kutolewa mahitimisho ya utafiti. Kinyonyi kilitumika kuhifadhi kumbukumbu zote za utafiti huu. Kalamu na shajara au daftari vilimsaidia mtafiti kunukuu data

alizokusanya kwa kusoma machapisho na vitabu teule. Kadhalika vilimwezesha kuhifadhi baadhi ya data za msingi kama vile tarehe, majina ya wahojiwa, mahali ambapo mahojiano yalifanyika pamoja na data zilizokuwa zinajibu malengo na maswali ya utafiti. Wakati mwingine daftari lilitumika kama kifaa cha kuhifadhi na kuchambua data za utafiti huu.

#### **1.8.6.2 Simu na Kinasa Sauti**

Simu ya mkononi ilitumika kwa ajili ya mawasiliano baina ya mtafiti na watafitiwa ili kujua muda na wakati muafaka wa kukutana. Vilevile, simu ilitumika kufanyia usaili baina ya mtafiti na watafitiwa pamoja na kuchukua picha na kunasa sauti wakati wa utafiti. Kinasa sauti kilitumika katika kunasa sauti wakati wa ukusanyaji wa data za utafiti. Kifaa hiki kilitumika nyanjani ambako mtafiti alirekodi mahojiano baina yake na watafitiwa kwa kuzingatia maadili ya utafiti.

#### **1.9 Itikeli ya Utafiti**

Katika utafiti huu itikeli ilizingatiwa katika hatua zote za utafiti. Mtafiti aliomba idhini ya watafitiwa kurekodi na kuchukua picha kwa ajili ya utafiti husika. Kadhalika, tuliomba idhini ya kila mmoja kuyatumia maelezo yao kwenye tasnifu hii pamoja na kutaja majina yao halisi na miaka yao. Kwa ujumla watafitiwa walitoa idhini yao kwa hiari na walionyesha ushirikiano wakati wa kukusanya data. Taarifa zilizorekodiwa kwenye kinasa sauti zilitumika katika uchambuzi wa data. Pia, tuliomba kibali chuoni, wilayani na mkoani.

#### **1.10 Uchanganuzi wa Data**

Data zilizokusanywa ziliwasilishwa kwa njia ya maelezo ama kitaamuli. Cohen na Lawrence (2000) pamoja na Mligo (2012) wanadai kuwa, mchakato wa awali wa uchambuzi wa data huanza wakati mtafiti akiwa katika eneo la utafiti. Maelezo ya

wataalamu hawa yanadokeza kuwa mtafiti hujifunza mazingira, aina ya watafitiwa na kiwango cha data zinazotolewa. Mtafiti alipomaliza ukusanyaji wa data, data hizo zilipangwa na kuchambuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na kuhakikiwa kwa msingi wa Nadharia ya Mwingilianomatini. Data zote zilizokusanywa zilihakikiwa na kupangwa kimantiki ili kubaini kwa urahisi data zinazojibu maswali ya utafiti. Hivyo basi, katika utafiti huu mtafiti amechambua data kwa kuzingatia hatua zifuatazo: Kusoma kazi teule za Mathias Mnyampala ili kuchambua muktadha wa kijamii, kisiasa na kiuchumi uliomsukuma mtunzi katika kazi teule za Mnyampala, kuhakiki mbinu za kifani zilivyotumika kuibua maudhui katika kazi husika. Aidha, mtafiti, alitathmini mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Data za msingi zilizochambuliwa zilizotokana na kazi teule sita pamoja na mahojiano yanayohusu maisha ya Mathias Mnyampala kwa lengo la kupambanua muktadha wa utunzi na historia yake kikamilifu. Kadhalika, tulichambua data za msingi na fuatizi kutoka maktabani na hasa kutokana na makala, majarida na data za kielektroniki. Aidha, upekuzi wa maktabani ulituwezesha kupata maoni ya wahakiki na watafiti wengine kuhusu Mathias Mnyampala na kazi zake katika fasihi ya Kiswahili.

### **1.11 Hitimisho**

Sura hii imeangazia usuli wa suala la utafiti na kuangazia historia ya maisha ya Mathias Mnyampala kutokana na data tulizokusanya kutoka nyanjani na maktabani. Tumefanya hivyo ili kutoa mwanga juu ya historia ya maisha ya Mnyampala kwa lengo la kuelewa vyema usuli na suala la utafiti. Aidha, tumeelezea suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti yaliyotokana na malengo hayo. Pia, tumepambanua sababu na umuhimu wa kufanyika kwa utafiti huu. Vilevile, tumeeleza upeo na mipaka ya utafiti. Hatimaye, tumefafanua mbinu za utafiti ambamo kuna



mkabala wa utafiti, vyanzo vya data kutokana na upekuzi maktabani na utafiti nyanjani, sampuli na usampulishaji, vifaa vya utafiti, itikeli ya utafiti na uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Sura inayofuata imeshughulikia mapitio ya maandishi yanayohusu mada ya utafiti na misingi ya nadharia.

## SURA YA PILI

### MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

#### 2.0 Utangulizi

Sura hii inafafanua mambo mawili ambayo ni mapitio ya maandishi kuhusu mada ya utafiti na misingi ya nadharia ya utafiti. Kwanza, tumepitia maandishi mbalimbali yanayohusu ushairi wa Kiswahili pamoja na maandishi kuhusu kazi za Mathias Mnyampala. Lengo ni kubainisha yaliyokwishafanywa kuhusiana na mada ya utafiti, mapengo yaliyopo na jinsi utafiti huu utakavyochangia kuyaziba mapengo haya.

#### 2.1 Mapitio ya Maandishi

Katika sehemu hii tumeangazia mapitio ya machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti. Mosi, inahusu ushairi wa Kiswahili, pili, muktadha katika ushairi na tatu, ni mapitio ya maandishi kuhusu kazi za Mnyampala.

##### 2.1.1 Ushairi wa Kiswahili

Ushairi wa Kiswahili ni utanzu wenye historia ndefu katika fasihi ya Kiswahili. Hadi sasa historia ya maendeleo ya ushairi wa Kiswahili pamoja na misingi yake ya kiuajumi imegubikwa na utata mwingi. Kutokana na urefu wa historia hiyo si rahisi kueleza ni lini hasa ushairi wa Kiswahili ulianza (Chiraghdin na wenzake, 1975 na Mulokozi na Sengo, 2005). Mawazo haya yanathibitishwa na Wamitila (2008:226) anayesema kuwa “Wataalamu wamekubaliana kuwa utanzu huu una historia ndefu.” Harries (1962) anaeleza kuwa ushairi wa Kiswahili una mchango mkubwa katika historia ya fasihi na jamii kwa jumla. Harries anasema kuwa ushairi wa mwanzo wa Kiswahili ni *Tambuka* (tabuka) ulioandikwa mwaka 1728.

Naye Knappert (1979) anaeleza kuwa utungo wa kwanza wa ushairi ni *Hamziyya* ulioandikwa mnamo mwaka 1652. Hata hivyo Mulokozi na Sengo (2005) wanasema

kuwa huenda wote wawili (Harries na Knappert) wamekosea na kwamba ushairi andishi wa mwanzo wa Kiswahili umekuwepo tangu wakati wa Fumo Liyongo ambaye anaaminika kuishi karne ya 13 huko Pate katika pwani ya Kenya. Wakati huo huo, Mulokozi na Sengo wanakiri kuwa huenda nyaraka nyingine zitagunduliwa baadaye ambazo zitasababisha tutambue kuwa ushairi wa mwanzo wa Kiswahili ulianza kuandikwa pale tu ambapo taaluma ya maandishi ilipoingia Afrika Mashariki.

Maoni ya Kimani (1983) yanaafikiana na ya Mulokozi (2017) wanapoeleza kuwa, ushairi wa Kiswahili ni wa kwanza katika taaluma ya fasihi na lugha ya Kiswahili. Wanasisitiza kuwa ushairi ni sehemu ya historia ya Afrika Mashariki kwa msingi kwamba ulikuwepo tangu enzi za usimulizi, chimbuko lake ni nyimbo na ngoma (Mulokozi, 2017). Hata hivyo, wataalamu hao wa ushairi wanakubaliana kuwa mashairi mengi yalianza katika muundo wa tenzi. Mulokozi na Sengo (2005) wanadai kuwa utenzi wa *Swifa ya Mwana Manga/Kumsifu Yanga* (1532) ndio unaosemekana kuwa wa kwanza kuandikwa. Hata hivyo, wataalamu hawa wanahamasisha wahakiki na wataalamu wa fasihi wafanye utafiti wa kina katika ushairi.

Kezilahabi (1983) anaunga mkono hoja ya wataalamu waliotangulia kuhusu historia ya ushairi wa Kiswahili. Kezilahabi amelezea historia hiyo kwa kuigawa katika mihula minne mikuu ambayo ni: muhula wa Urasimu, muhula wa Utasa, muhula wa Urasimu Mpya na muhula wa Sasa. Akirejelea muhula wa Urasimi, Kezilahabi anadai kuwa ni vigumu kueleza ni lini hasa ushairi wa Kiswahili ulianza kuchukua umbo lake la kimapokeo na ni vigumu kueleza lini shairi fulani lilianza kuonekana katika hali ya maandishi. Mfano wa tungo zinazolingia katika muhula huu ni: *Utenzi wa Tambuka* (1728), *Utenzi wa Hamziya* (1749), *Utenzi wa Al-Inkishafi* (1810-1820),

*Utenzi wa Ayubu* (1822), *Utenzi wa Mwanakupona* (1858) na nyinginezo zilizoandikwa kabla ya 1885.

Pili, Muhula wa Utasa ni kati ya mwaka 1885-1945. Kwa mujibu wa Kezilahabi mashairi machache sana yaliandikwa katika muhula huu. Maandishi mengi yalikuwa ya Hemed Abdallah ambayo ni *Utenzi wa Vita vya Majimaji* na *Utenzi wa Vita vya Uhuru*. Kezilahabi anadai kuwa kihistoria kulikuwa na tungo chache kwa sababu mataifa ya Ulaya yalikuwa yakigawana Afrika na ulikuwa wakati wa Vita Vikuu vya Dunia. Kimaandishi, ulikuwa wakati wa ubadilishaji wa hati za maandishi (Kiarabu kwenda Kirumi). Kulingana na Kezilahabi, mambo haya yalidumaza maendeleo ya utunzi wa fasihi andishi ya Kiswahili kwa muda. Aidha, yalichangia kanuni za uandishi wa mashairi kuanza kupotea.

Tatu ni muhula wa Urasimi Mpya (1945-1960). Kezilahabi anadai kuwa wakati huu ndio ulikuwa wa kufufua kanuni za ushairi na ulikuwa wakati wa washairi kama vile: Shaaban Robert, Amri Abedi, Khamis Amani, Mathias Mnyampala na Ahmmed Nassir. Anaeleza kwamba miaka ya 1960-1967 ilikuwa miaka ya kuyumbayumba kwa ushairi wa Kiswahili. Hali hii ilisababishwa na kutokuwa na malengo maalum kwa nchi za Afrika Mashariki baada ya uhuru na wakati huo washairi wawili mashuhuri (Amri Abedi 1964 na Shaaban Robert 1962) walifariki (Kezilahabi, 1983). Vifo vya washairi hao maarufu vilikuwa pigo kubwa katika sanaa ya ushairi wa Kiswahili na vilichangia kuyumba kwa tasnia hii wakati huo. Kezilahabi ameziweka tungo za Mathias Mnyampala katika muhula wa urasimi mpya. Hoja ya Kezilahabi inashadidiwa vyema na Shitemi (2010) anayeeleza kuwa tungo za Kaluta Amri Abedi, Shaaban Robert, Mathias Mnyampala na Akilimali Snow White zinaingia katika kipindi cha urasimi mpya.

Kwa upande wake Indende (2008) anatofautiana kwa kiasi fulani na mawazo ya Kezilahabi na Shitemi. Indede anadai kuwa uandishi wa Mathias Mnyampala ulijikita katika nadharia ya urasmi mkongwe pamoja na urasmi mpya. Mawazo ya Indende hayana mashiko sana, kwa vile utafiti huu umebainisha kwamba kazi za Mnyampala zimesheheni mawazo ya kimapinduzi na yenye kuakisi uhalisia wa jamii iliyokuwepo wakati huo. Kwa hiyo baadhi ya kazi za mwandishi huyu zinaingia katika muhula wa Urasmi Mpya. Waandishi wengine waliojikita katika mkondo huo ni Shaaban Robert, Amri Abedi, Akilimali Snow White na Saadan Kandoro.

Muhula wa nne ni wa Sasa. Kezilahabi anaeleza kuwa muhula huu ulianza miaka ya 1967 hadi leo. Katika kipindi hiki mataifa mengi ya Kiafrika yalikuwa yanatafuta uhuru kamili katika lengo la kufikia ujamaa. Aidha kisanaa, huu ulikuwa ni wakati ambao mgogoro juu ya kanuni za ushairi uliongezeka. Kutokana na mawazo ya Kezilahabi tunaweza kusema kuwa hali hii ya kisiasa ilipelekea waandishi wengi kujitokeza kuandika kazi mbalimbali kuhusiana na masuala ya kisiasa akiwemo Mathias Mnyampala ambaye aliandika *Ngonjera za UKUTA Na. 1 na 2 na Mashairi ya Azimio la Arusha* ya Topan na Grant (1971).

Kwa upande wa mgogoro wa ushairi wa Kiswahili, Mulokozi (2017) anaeleza kuwa mgogoro huo ulichangia kupevuka kwa taaluma ya ushairi wa Kiswahili hususani kuhusu ufafanuzi wa dhana ya ushairi, mawanda yake, bahari zake na mbinu zake za kijadi. Anadai kuwa wanausasa walijifunza mengi kutoka kwa wanaujadi na wanaujadi walijifunza mengi kutoka kwa wanausasa. Vitabu na makala nyingi ziliandikwa na kuchapishwa, ushairi ulikomaa na kupevuka kutokana na juhudi hizo. Vilevile, fani na bahari mpya za ushairi wa Kiswahili zilipata nafasi ya kuibuka na kushamiri (kwa mfano tungo za mtiririko, bongo fleva na nyinginezo). Hivyo

waandishi wa kimapokeo na wanausasa walijitokeza kuandika mashairi mengi kuhusiana na mgogoro huo. Kwa mfano wanamapokeo walitunga zaidi katika magazetini na vipindi vya redio. Wanamapinduzi waliandika vitabu mbalimbali vya ushairi kwa kufuata mabadiliko waliyokuwa wakisisitiza, mfano wa waandishi na vitabu vilivyoandikwa ni Kezilahabi (1974) *Kichomi*, Mulokozi na Kahigi (1976), *Malenga wa Bara* na *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (1979). Hali hii ilipelekea maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kifani na kimaudhui na kukua kwa sanaa ya ushairi wa Kiswahili.

Kutokana na maelezo ya Kezilahabi na Indende, tunapata maswali mengi kuhusu mgawanyo huo na nafasi ya Mathias Mnyampala. Tunapata utata kuhusu madai ya Indende na Kezilahabi kuhusu Mathias Mnyampala na tungo zake. Ijapokuwa Kezilahabi amemweka Mathias Mnyampala katika muhula wa Urasmi Mpya, je, kazi alizoandika Mnyampala zinazohusu ujamaa, zinaingia wapi? Je, tunaweza kuziingiza katika muhula wa sasa? Je, muhula wa sasa unaishia wapi? Kezilahabi alitoa mpangilio huu wa mihula na kusaidia kutoa picha ya maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kwa mtazamo wa kifasihi. Hivyo, tunaweza kukubali au kurekebisha. Katika utafiti huu tumebaini kuwa kulingana na mihula aliyobainisha Kezilahabi kazi za ushairi za Mnyampala zinajitokeza katika muhula wa Urasmi Mpya na Usasa.

Kadhalika, Senkoro (1987) anaelezea matapo ya fasihi ya Kiswahili na kumtazama Mnyampala kuwa ni mmoja kati ya waandishi wengi waliojitokeza kuandika kuhusu ushairi wa Kiswahili katika tapo la Urasimi Mpya. Senkoro anaeleza kuwa kuanzia kwa Shaaban Robert, Amri Abedi na Mathias Mnyampala kulikuwa na dalili za Urasimi Mpya. Senkoro anaongezea kuwa kilio cha washairi kuhusu “Ushairi wa Zamani” kama vile Amri Abedi katika utangulizi wa kitabu cha *Sheria za Kutunga*

*Mashairi* (1954), Mathias Mnyampala katika *Waadhi wa Ushairi* (1965) na Utangulizi wa *Kielelezo cha Fasihi* (1973) cha Shaaban Robert, tunapata maelezo kuhusu ushairi utakiwao, ambao ni mfano mzuri wa urasimi mpya katika fasihi ya Kiswahili. Kwa ujumla, katika maandishi hayo Senkoro hajajikita katika kuhakiki kazi za waandishi hao. Kusudi lake lilikuwa kuwatazama waandishi hao katika matapo ya fasihi ya Kiswahili, mahali wanapojitokeza watunzi hao kutokana na utunzi wao wa mashairi.

Oslon (1975) anadai kuwa ushairi wa Kiswahili ni chombo cha kuhamasisha matarajio na matamanio ya Waswahili na jamii kwa ujumla katika kutetea maendeleo ya jamii. Aidha, anaeleza kuwa ushairi wa Kiswahili umechukua nafasi kubwa kama chombo cha mawasiliano baina ya jamii. Oslon anatoa mfano kuwa ikiwa mshairi haridhiki na namna jambo fulani linalofanywa, huweza kutunga shairi kuelezea jambo hilo. Kadhalika, mshairi anaweza kutunga shairi kusifia mambo mbalimbali yanayoridhisha ama yanayotokea katika jamii kwa nia ya kuleta maendeleo katika jamii. Mawazo ya Oslon yanatusaidia kutambua kwamba ushairi wa Kiswahili hufungamana na mazingira ya jamii. Ni kutokana na mwelekeo huo ambapo utafiti huu unafanyika ili kuelezea muktadha, mbinu za kifani zilivyotumika kuibua maudhui katika kazi teule pamoja na mchango wa Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

Licha ya ufafanuzi huo mzuri, Oslon ametoa ufafanuzi huu pasi na kufanya uchambuzi wa kazi za ushairi ili kuthibitisha hoja zake. Utafiti wetu umeyatekeleza haya kwa kuzingatia kazi teule za ushairi za Mathias Mnyampala. Tumehakiki kazi za ushairi wa Mathias Mnyampala kwa kupambanua mintarafu ya muktadha wa utunzi wa tungo teule, mbinu za kifani na maudhui yanayoibuliwa pamoja na kutathmini mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

### 2.1.2 Muktradha katika Ushairi

Muktradha katika fasihi umefafanuliwa na wataalamu wengi kwa kuzingatia vipengele vya mahali, wakati na mazingira au hali mbalimbali zinazojitokeza wakati waandishi wanatunga kazi zao. Kwa mfano Hirsch (1960) anaonyesha umuhimu wa muktradha wa mtunzi katika kazi yoyote ya fasihi ili kuelewa maana ya mwandishi katika kazi ya fasihi. Naye Holman na Harmon (1986) wanasema kwamba muktradha ni mahali halisi au mahali pa kufikirika au kubuniwa ambapo tendo la kimasimulizi ama kiuandishi hufanyika. Mambo yanayoweza kusimuliwa au kuandikwa ni riwaya, drama, hadithi fupi, novela na ushairi. Hivyo, ni muhimu kuelewa muktradha wa kazi ya kisanaa ili kuhakiki kazi hiyo kikamilifu. Kwa hiyo, kumpuuza mwandishi kuna maana kwamba maana asilia ya mwandishi haitakuwa na umuhimu wowote katika kazi ya fasihi. Ili kuelewa maana aliyokusudia mwandishi ni muhimu kuelewa muktradha wa kazi yake. Kwa vyovyote vile hatuwezi kutenganisha maana ya kazi ya fasihi na muktradha wa mwandishi kwa sababu tathmini ya hiyo kazi ya fasihi haitakuwa kamilifu.

Njogu na Chimerah (1999), King'ei na Kemoli (2001), Mumbo na Indede (2004), Madumulla (2009) na Mulokozi (2017) wanafafanua muktradha kuwa ni mazingira yaliyozua utungo unaohakikiwa. Wanaongezea kuwa mazingira hayo huweza kuwa ya kihistoria (lini?), kijiografia (wapi?), kijamii (nani?) ama kiutendaji (vipi?). Wanaeleza pia kuwa muktradha hurejelea mambo yaliyomzunguka mwandishi wakati wa utungaji wake na kufichua masuala muhimu ya kazi ya fasihi katika viwango vya maudhui na fani. Kupitia muktradha wa utungaji, mhakiki huelewa dhamira za mtunzi husika. Hivyo, kutokana na maelezo ya wahakiki hawa ni bayana kuwa ili kupambanua mwingilianomatini wa kazi za ushairi za Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kifani na kimaudhui ni lazima tuhakiki kwanza



muktadha wa kijamii, kisiasa, kiuchumi na kimwingilianomatini uliomsukuma kutunga tungo zake.

Wamitila (2008) anaeleza kuwa muktadha wa ushairi wa Kiswahili unaingiliana na kukamilishana kimahali, kiwakati na mahusiano binafsi yanayozua tungo husika. Uchunguzi wetu unaafikiana na Wamitila ambaye anaona kuwa muktadha unaoweza kuchunguzwa katika ushairi ni ule wa kimahali, kiwakati na mahusiano binafsi. Katika muktadha wa mahusiano binafsi, mtafiti huelezea mazungumzo ama mawasiliano ya wahusika wa utungo wa kifasihi. Mahusiano hayo huhusisha msemaji, mwandishi, msemewa, mlengwa na hadhira. Mawazo ya Wamitila yametufaa katika kuchunguza muktadha wa utunzi wa kazi teule za Mathias Mnyampala.

Sunkuli na Miruka (1990) wanasema kuwa kigezo cha wakati ni muhimu katika kuelezea muktadha wa kazi za fasihi. Sunkuli na Miruka wanaongezea kuwa matukio ya kisanaa hufanyika katika muktadha mahsusi wa kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Maelezo hayo ya wahakiki hao hayatofautiani na ya Omwega (2016) anayeeleza kuwa kufahamu muktadha wa kazi ya mtunzi ni muhimu sana katika kuhakiki kazi zake. Omwega anafafanua zaidi kuwa mazingira ambayo humzingira mtunzi anapoandika kazi zake, humsukuma kuandikia masuala mazito kwa njia ya kimafumbo ili kuwasilisha ujumbe wake. Kwa hiyo, mazingira ya mtunzi hayana budi kuoana na yale anayoyaandika. Kwa kawaida fasihi yoyote sharti ichunguzwe katika muktadha wa kumhusisha mtunzi sio tu na nguvu za kimaumbile, bali pia na nguvu zinazotokana na jamii yake. Kwa kuwa ushairi ni mojawapo ya tanzu za fasihi, katika uhakiki wa kazi za ushairi, ni muhimu kuzingatia muktadha wa mtunzi ili kutathmini yaliyoandikwa.

Kutokana na maelezo hayo, ni bayana kuwa suala la muktadha ni telezi kwani ni hali au mazingira na ni vigumu kuweka mpaka bainifu baina ya muktadha mmoja na mwingine. Miktadha mbalimbali huingiliana, hutegemeana na kukamilishana. Hata hivyo utafiti huu umeangazia miktadha minne ambayo ni muktadha wa kijamii, kisiasa, kiuchumi na kimwingilianomatini. Hii ni kwa sababu katika kuchunguza mwingilianomatini wa tungo za mwandishi, muktadha ni muhimu kuchunguzwa. Kadhalika, muktadha hujumuisha mazingira wakati na mahali ambamo tendo la kifasihi linatendeka. Katika muktadha wakati ni muhimu kwa kuwa huweza kuwa kipindi mahususi cha kihistoria au mazingira yanayomzunguka mwandishi. Vilevile, muktadha huweza kuhusisha wakati uliozoeleka kwa kuwa mwandishi wa kazi ya fasihi huweza kurudi nyuma kiwakati au kwenda mbele kiwakati na hata kutoka nje ya wakati.

### **2.1.3 Yaliyoandikwa kuhusu Tungo za Mathias Mnyampala**

Kazi za Mathias Mnyampala zimehakikiwa na watafiti mbalimbali walioandika makala ya kazi zake, na ni wachache waliohakiki kazi zake katika kiwango cha uzamili na uzamifu. Katika uhakiki wao baadhi ya wataalamu wanaeleza kuwa Mnyampala ni mmoja kati ya washairi mashuhuri waliochangia pakubwa kwenye tasnia ya ushairi wa Kiswahili (Williams, 1974; Kihore, 1978 na Mmbaga, 1981). Watafiti hao wanasisitiza kuwa Mnyampala alitoa kijejezi cha tendi, na kwamba ndiye mwanzilishi wa chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA). Aidha, ndiye alifufua sanaa ya ngonjera. Wahakiki wengine wa ushairi wa Kiswahili wamemtaja Mnyampala kama mwanzilishi wa sanaa ya ngonjera (Abdulaziz, 1969; Komba, 1969 na Mwangomango, 1971). Hata hivyo kuna wale wanaodai kuwa Mnyampala aliufufua tu utanzu wa ngonjera ambao ulikuwepo tangu kipindi cha fasihi simulizi (Williams, 1974; Gibbe, 1978; Kihore, 1978 na Madumulla, 2011).

Naye Gibbe (1994) anafafanua kuwa kutokana na ugumu wa mashairi ya Mnyampala, wahakiki wa ushairi hawajawahi kuyapekua na kuyahakiki kikamilifu kifani na kimaudhui kwa kujikita katika mwingilianomatini wa kazi za ushairi. Mawazo hayo yametupa hamasa ya kuangazia mchango wa kazi teule za Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kimwingilianomatini.

Kwa upande mwingine wapo wahakiki wanaodai kuwa Mnyampala hajachangia katika ushairi wa Kiswahili. Hawa ni pamoja na Lambert (1966), Harries (1972), Ndulute (1985) na Frolova (2008). Mfano Lambert (1966) anadai kuwa *Diwani ya Mnyampala* ina mashairi mengi yanayohusu masuala ya kawaida ya kila siku na yanasisitiza fikra za kifalsafa. Lambert anaongezea kuwa Mnyampala alishikilia mno vina na mizani hadi kazi yake ikaathiriwa vibaya na kanuni hizo. Lambert anaeleza kuwa kwa kushikilia mno vina na mizani, mashairi yake hayakufaulu kisanaa.

Naye, Harries (1972) anaeleza kuwa Mnyampala hajafaulu kuwasilisha maudhui kwa jamii husika kutokana na matumizi ya msamiati mgumu katika kazi zake. Kadhalika Frolova (2008) anaeleza kuwa Mathias Mnyampala aliandika tendi na mashairi. Pia aliandika ngonjera, ambapo aliwakilisha mazungumzo ya kishairi huku akihifadhi umbo la jadi kwa kubadilisha mada tu.

Ndulute (1985) ameangalia siasa katika kazi za Mathias Mnyampala kwa kuegemea zaidi katika ngonjera. Ndulute anadai kuwa hakuna upya wowote katika ngonjera hizo kwa sababu alikuwa anajifunza siasa na kuisisitiza fikra na falsafa zilizokuwepo wakati huo. Anaongezea kuwa maudhui pamoja na ufundi uliotumika kwenye ngonjera hizo ni marudio ya vitu vilivyokwishajadiliwa na wasanii wengine, kama vile Mwalimu Julius K. Nyerere. Ndulute anaeleza kuwa taifa haliwezi kujengwa na tabia zinazooneshwa katika utunzi wa Mnyampala. Zaidi anaelezea kuwa ngonjera

alizoandika Mnyampala hazina upya wowote katika ushairi wa Kiswahili, bali zimetokana na fasihi simulizi, hususani nyimbo.

Hivyo anaona kwamba yale yote aliyoyaeleza Mnyampala katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1, na 2* ni mambo ya kawaida kama vile maana ya ngonjera, TANU na Siyasa Yake, Viongozi Wetu, Ujamaa, Azimio la Arusha, Elimu ya Utamaduni, Siku ya Taifa, Uhusiano Mwema na Mafumbo. Anasema kwamba haya ni mambo yaliyokuwa yakizungumzwa katika kipindi hicho na kila mtu. Kimsingi Ndulute anaona kuwa aliyoandika Mnyampala ni marudio ya mawazo ya Rais Nyerere. Nyerere aliandika kuhusu serikali yake katika “Uhuru na Umoja” na “Elimu ya Kujitegemea.” Sababu nyingine anayotoa ni kwamba, wakati ngonjera za Mathias Mnyampala ziliibuka kulikuwa bado kuna mawazo au maudhui ya uhuru, umoja, elimu ya kujitegemea. Haya yote yalitokana na sera ya Ujamaa na Kujitegemea. Swali ni kuwa, je, ni makosa watunzi kuandika juu ya mambo yaliyopo katika jamii? Je, hali hii haitokei katika tungo zingine za kifasihi kama vile riwaya na tamthilia?

Mawazo ya Ndulute (1985), Harries (1972) na Frolova (2008) yalitupa hamasa ya kufanya utafiti juu ya ushairi wa Mnyampala. Uhakiki alioufanya Ndulute juu ya kazi za Mathias Mnyampala unaonyesha kana kwamba kazi hizo zinatoka katika ombwe, wakati kazi yoyote ya fasihi huingiliana na kukamilishana pia hutokana na muktadha wa kijamii, kisiasa na kiuchumi uliomzaa, uliomlea na kumkuza msanii. Hata hivyo, maoni ya watafiti hao ni muhimu kwa kuwa yanahimiza uchunguzi wa tungo mahsusi upya kimwingilianomatini na kwa misingi maalum ya kinadharia. Kwa kuegemea Nadharia ya Mwingilianomatini tunaweza kutathmini mantiki ya maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu mchango wa Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Aidha, utafiti huu umehakiki kazi mahususi za Mathias Mnyampala ili

kuchunguza mwingilianomatini wa kazi za ushairi wa Mathias Mnyampala na mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

Kwa upande mwingine, wahakiki kama vile Williams (1974), Gibbe (1978), Kihore (1978), Issa (2013) na Ali (2014) wanaeleza kuwa Mathias Mnyampala ni mshairi muhimu katika taifa la Tanzania na Afrika Mashariki. Wanadai kuwa Mnyampala alikuwa katika mstari wa mbele kukuza Kiswahili. Aidha, Mathias Mnyampala ndiye aliyekuwa mshairi wa kwanza kueneza itikadi za sera ya Azimio la Arusha katika muundo wa ngonjera. Japo wahakiki hawa wameangazia kazi za Mnyampala, hawajafanya utafiti wa kina na mpana. Kati ya watafiti hao, wengine wamehakiki kazi moja, wengine kuanzia mbili na kuendelea kwa kifupi. Kwa mfano, Williams (1974) ameandika makala iitwayo “Diwani ya Mnyampala” na kuhakiki *Diwani ya Mnyampala, Waadhi wa Ushairi na Ngonjera za Ukuta* na kuangazia fani na maudhui kwa ufupi na hakutumia kiunzi cha nadharia katika uhakiki wa kazi hiyo. Gibbe (1978) katika makala yake ameangazia diwani ya *Waadhi wa Ushairi, Diwani ya Mnyampala, Ngonjera za UKUTA Na. 1, Ngonjera za UKUTA Na. 2, Utenzi wa Zaburi na Utenzi wa Injili*. Hata hivyo, Gibbe ameangazia kazi zote hizo kwa kugusia tu baadhi ya vipengele ndani ya kazi hizo kwa ufupi.

Kihore (1978) ameandika makala iitwayo “*Waadhi wa Ushairi*” na kuchambua maudhui yaliyomo ndani ya diwani hiyo. Anaeleza kuwa maudhui yaliyomo kwenye diwani hiyo ni siasa, dini, malezi na maisha ya kawaida ya mazingira ya nchi yake ya Tanzania. Naye Issa (2013) ameshughulikia mhusika mwanamke anavyosawiriwa katika *Diwani ya Mnyampala na Waadhi wa Ushairi*. Kwa upande mwingine Ali (2014) ameshughulikia nafasi ya mwanamke katika ushairi wa Kiswahili kwa kuchunguza kazi za ushairi za Shaaban Robert na Mathias Mnyampala ili kubaini falsafa zao juu ya mwanamke katika jamii.

Simala (2000) amehakiki sitiari za uana katika ushairi wa Kiswahili. Katika kazi hiyo Simala anaeleza kuwa Mnyampala ametumia sitiari za uana katika kazi zake. Simala anatoa mfano katika shairi la “Ua hili ua gani?” (uk. 85) katika *Diwani ya Mnyampala*. Anaeleza kuwa Mnyampala ni miongoni mwa washairi waliosifia ua katika mashairi yake. Kadhalika Simala (2000:137) anaeleza kuwa Mnyampala ametilia mkazo hoja isemayo “Mwanamke ni heri ya Mungu” katika ubeti wa tisa usemao “ua hili liliumbwa na kuletwa na Karimu katika ulimwengu.” Vilevile Simala anaongezea kuwa Mnyampala amemsawiri mwanamke kama maua mazuri katika shairi la “Maua Mazuri” (uk. 56) katika *Waadhi wa Ushairi*. Simala anasema kuwa Mnyampala anazungumzia uzuri wa mwanamke mintarafu ya sifa za maua. Anaongezea kuwa Mnyampala anasema kuwa ingawa wanawake wazuri hupendeza, huwa hawadumu. Kadhalika Simala anaeleza kuwa Mnyampala amemsawiri mwanamke kama pambo la utukufu kwa mumewe katika shairi la “Taji la Nyumba” (uk. 11) katika *Waadhi wa Ushairi*. Aidha, Simala alijikita katika kuangalia sitiari za uana (ujinsia) katika kazi za waandishi mbalimbali wa ushairi wa Kiswahili akiwemo Mnyampala.

Mihale (2011) amechambua vipengele vya kiujumi vinavyopatikana katika ushairi wa Mnyampala. Mihale amechambua vipengele hivyo katika kazi ya *Diwani ya Mnyampala*, *Waadhi wa Ushairi* na *Ngonjera za UKUTA Na. 1*. Katika uhakiki wake alitumia Nadharia ya Ki-Marx. Mihale amelinganisha vipengele vya kiujumi vinavyopatikana katika vitabu teule vya Mathias Mnyampala na hali halisi ya maisha ya jamii ya Kitanzania. Vilevile, amebainisha athari za kiujumi zilizopo katika ushairi wa Mnyampala kwa maisha ya jamii ya Kitanzania. Mtafiti huyu amejikita zaidi katika kuangalia uzuri na ubaya wa ushairi wa Mathias Mnyampala kwa kutumia Nadharia ya Ki-Marx. Kutokana na uhakiki wa ujumi uliofanywa kuhusu ushairi wa

Mathias Mnyampala, ijapokuwa yeye hajaangazia mchango wake, tunaweza kubaini kwa kiasi fulani mchango wa Mathias Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili. Hata hivyo mtafiti huyu alijikita kwenye kazi tatu zilizochapishwa na hakugusia kazi zisizochapishwa wala muktadha wa utunzi wa kazi za Mnyampala kimwingilianomatini.

Murusuri (2011) amechunguza utamthiliya katika ngonjera, mifano kutoka *Ngonjera za UKUTA namba 1 na 2*. Murusuri amejikita katika kuangazia utamthiliya unavyojitokeza katika ngonjera kwa kutumia mihimili ya tamthilia. Amebainisha vipengele vya utamthilia katika ngonjera, ameeleza sababu za kuwepo kwa vipengele vya utamthilia katika ngonjera na alitathmini umuhimu wa utamthiliya katika jamii katika kipindi kilichopita na cha sasa. Murusuri ameangazia ulinganishi wa tamthiliya na ngonjera akikazia zaidi fani na kujikita katika kipengele cha muundo na mtindo wa ngonjera za Mnyampala pasi na kuangazia maudhui ya tungo zenyewe.

Samandito (2011) amemchunguza Mnyampala kama muumini wa dini ya Kikristo, na anaeleza kuwa Mnyampala ni miongoni mwa washairi wa kwanza wa Kikristo katika uga wa ushairi. Pia anasema kuwa ni mshairi ambaye alikuwa mwanadini na muumini mzuri wa dini ya Kikristo ambaye hakuwa na ubaguzi wa kidini. Alishirikiana na wenzake katika utunzi wa ushairi na shughuli nyinginezo bila ya kujali dini, kabila wala rangi. Samandito alijikita katika dhamira ya dini na uchambuzi wake aliuchambua bila kuhusisha muktadha wa utunzi na mbinu zilizotumika kuibua maudhui kimwingilianomatini.

Madumulla (2011) anaeleza historia ya maisha ya Mathias Mnyampala kwa kuanzia kuzaliwa, maisha yake ya utotoni, harakati za kujiendeleza, maisha ya ndoa yake, kazi, kuugua na kifo chake pamoja na maandishi yake. Katika kuelezea hayo

Madumulla anafafanua kuwa Mathias Mnyampala aliandika kazi nyingi za ushairi na nathari kwa Kiswahili. Aidha, aliweza kuvumisha ushairi wa majibizano na kuupatia jina ‘ngonjera’ kutoka katika lugha ya Kigogo, likiwa na maana ya twende pamoja/tushirikiane. Kwa upande wa nathari, Mathias Mnyampala aliandika hadithi, insha na vitabu vya habari mbalimbali. Madumulla anaongezea kuwa licha ya juhudi alizokuwa nazo Mathias Mnyampala katika kazi na utunzi, amesahaulika katika taaluma ya Kiswahili na jamii kwa ujumla. Anafafanua kuwa:

6. Mnyampala aliifanyia mambo mengi Tanzania, zaidi ya kuwa mfanyakazi hodari, mwaminifu na mtiifu wa serikali ya Tanzania wakati huo. Lakini kwa bahati mbaya, mchango wa Mathias Mnyampala haujatambuliwa vizuri kwa sababu haujarekodiwa ipasavyo. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (sasa inaitwa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili – TATAKI) iliandika kidogo tu kuhusu mtu huyu, na sasa hivi... inayadurusu maandishi ya gwiji huyu kwa madhumuni ya kuyachapisha. Katika mataifa yaliyoendelea, mtu wa namna ya Mathias Mnyampala angepewa nafasi maalum ya kutukuka. Tukichukua mfano wa nchi ya Uingereza, wana jumba kubwa lililotengwa karne kadhaa zilizopita ambamo watu wao mashuhuri huhifadhiwa (2011:19).

Hivyo basi, Madumulla anawahimiza watafiti kufanya utafiti wa kina kuhusu Mathias Mnyampala ili ikiwezekana kuandaa kitu kama ‘Kanzi ya Mnyampala’ (*The Mnyampala Data Bank*) na kuwa rejeleo kuhusu mtaalamu huyu maarufu. Kuhusu urudufu wa maandishi ya Mnyampala tunaweza kusema kuwa inasikitisha kuwa mpaka sasa TATAKI, bado haijadurusu maandishi hayo. Mawazo hayo ya Madumulla yalitolewa siku ya uzinduzi wa kitabu cha *Historia ya Hayati Kaluta Amri Abedi: 1924-1964*, katika ukumbi wa Karimjee Dar es Salaam mwaka 2011, na mawazo hayo ndiyo yametuhamasisha kufanya utafiti huu.

Makaka (2012) amemhakiki Mathias Mnyampala kama mtu mwenye karama mbalimbali. Aameangazia historia, maisha na vipawa vya Mathias Mnyampala



vinavyomfanya kuwa mtunzi maarufu pamoja na kutathmini upekee wake unavyochangia maendeleo ya lugha ya Kiswahili na fasihi kwa ujumla. Makaka amezingatia zaidi kuelezea historia na maisha ya Mnyampala kwa ujumla, hakujikita katika kuhakiki kazi za Mnyampala, jambo ambalo katika utafiti huu limeangaziwa. Makaka pia amejikita zaidi kuelezea mchango wa Mnyampala katika kukuza Kiswahili na fasihi kwa ujumla pasipo kufanya uchambuzi wa kazi alizoziandika. Licha ya hivyo rejeo hili limetufaa katika kujua baadhi ya taarifa kuhusu historia ya maisha ya mwandishi huyu pamoja na kazi alizoandika wakati wa uhai wake.

Mgute (2012) amechunguza mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Mtafiti huyu ameangazia kazi tano teule za Mnyampala ambazo ni *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Waadhi wa Ushairi* (1965), *Ngonjera za UKUTA 1* (1970), *Ngonjera za UKUTA 2* (1971) na *Kisa cha Mrina Asali na Wenzake Wawili* (1982). Aidha, Mgute aliangalia mchango wa Mnyampala katika fasihi kiujumla mno na kujiegemeza katika kazi zilizochapishwa tu. Mtafiti huyu ameishia kutaja tu vipengele vya fani na maudhui pasi na kufanya uchambuzi wa kina wa vipengele hivyo. Hata hivyo uhakiki wake haukujikita katika mwingilianomatini wa tungo hizo. Haya yanajidhihirisha katika mapendekezo yake anapoeleza kuwa kuna haja ya kufanya utafiti wa kina kuhusu vipengele vya fani na maudhui pamoja na tungo ambazo hazijachapishwa ili kubaini mchango wa Mnyampala kikamilifu. Hivyo ni dhahiri kuwa utafiti wake haukufanywa kikamilifu. Hivyo, katika utafiti huu, tumepata data zaidi kuhusu mchango wa Mathias Mnyampala katika kazi zake za ushairi zilizochapishwa na zisizochapishwa, jambo ambalo halikushughulikiwa kikamilifu na Mgute.

Mutembei (2012) anaangalia korasi katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* na *2*. Mutembei anafafanua kuwa dhima ya mashairi haya ni kutoa mafunzo kwa kutumia lugha teule

ambayo si ya kashfa. Hivyo, Mutembe alifanya uchambuzi huo mdogo ili kuthibitisha kuwa Nadharia ya Korasi inaweza kutumika katika uhakiki wa tungo za ushairi wa Kiswahili. Mutembe anaeleza kuwa mashairi hayo yamesheheni maudhui maalum. Katika uchambuzi huo hakuangazia mchango wa Mnyampala bali yeye alijikita zaidi katika kuchunguza endapo korasi inaweza kutumika kuhakiki ushairi wa Kiswahili. Kazi ya Mutembe ilituchochea kuangazia mchango wa kazi za Mnyampala kimwingilianomatini.

Roy (2013) alifanya utafiti kuhusu Mnyampala na ujenzi wa taifa la Tanzania kwa kutumia nadharia za kibiolojia na falsafa. Alilenga kuangalia vitu vilivyoanza na kuunda nadharia mpya za uhakiki. Roy anaeleza kuwa Mnyampala ameandika mambo mengine mengi yanayohusu historia ya Ugogo, siasa ya ujamaa, dini na maisha ya watu maarufu kama vile Mtemi Mazengo na Kaluta Amri Abedi. Roy anaeleza kuwa mchango wa Mathias Mnyampala katika fasihi ya Kiswahili na taifa lake ni tukufu na kwamba anastahili kupewa heshima kubwa. Hata hivyo, Roy amegusia mchango wa Mnyampala kwa ujumla sana. Pia katika kufanya utafiti wake hajaangazia muktadha wa tungo maalum za Mathias Mnyampala ambapo ni kitu muhimu katika uhakiki wa kazi yoyote ya fasihi. Aidha, Roy alijikita zaidi katika kuangalia sarufi ya Kiswahili kwa kuangalia misamiati na uundaji wa maneno ya Kiswahili. Kwa hiyo, japo anamrundikia Mnyampala sifa mashuhuri utafiti wake si wa kina kifasihi.

Ponera (2015) amechunguza nafasi ya Ukristo katika ushairi wa Mnyampala kwa kutumia *Diwani ya Mnyampala na Waadhi wa Ushairi*. Ponera alijikita katika dhamira moja tu ya dini kwa kuangalia sababu na faida ya Mnyampala kujielekeza katika kuandika mashairi ya dini ya Kikristo. Ponera anaeleza kuwa uchambuzi huo umemsaidia kuibua maneno mbalimbali ya Kiswahili yenye mwelekeo wa Ukristo na

hivyo kukuza taaluma ya ushairi. Ponera (2015:65) katika kipengele cha maoni yatokanayo na utafiti wake anaeleza kuwa “mchango wa Mnyampala haujatambuliwa vizuri licha ya watafiti mbalimbali kuzihakiki kazi zake na taaluma za Kiswahili.” Kauli hiyo ndiyo iliyotupa hamasa ya kufanya utafiti huu. Aidha, kutokana na utafiti wa Ponera tumeweza kupata mwanga kuhusu imani ya Mnyampala. Katika utafiti huu tumekwenda mbele zaidi kwa kuchunguza muktadha na mbinu za kifani zilizoibua maudhui mbalimbali katika kazi teule pamoja na mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Katika utafiti wetu dini imejadiliwa kama sehemu muhimu ya muktadha wa kijamii, kama maudhui na kama mojawapo ya mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

Kutokana na ufinyu wa tafiti hizo kisampuli au kinadharia, mahitimisho yanayotolewa yanazua maswali kuhusiana na mchango wa mtunzi huyu katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia muktadha wa utunzi. Aidha, watafiti wengi waliotangulia wamejikita katika kuchunguza kazi zilizochapishwa za Mnyampala na kuziacha kazi zisizochapishwa. Katika utafiti huu tumebaini kuwa kazi zote zilizoandikwa na Mnyampala pamoja na alizokusanya na kuzihariri zina mchango mkubwa katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Kwa hiyo, utafiti huu umechangia katika kutoa mchango wa Mnyampala kimwingilianomatini na kwa kutumia nadharia ya uhakiki ya Mwingilianomatini na kutumia sampuli pana ya mashairi ya Mathias Mnyampala yaliyochunguzwa.

## **2.2 Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu umekitwa kwenye Nadharia ya Mwingilianomatini katika kuchunguza mwingilianomatini wa ushairi wa Mathias Mnyampala. Allen (2000) anaeleza kuwa Nadharia ya Mwingilianomatini ilianza katika nadharia za isimu za karne ya ishirini,

hasa katika kazi za mwanaisimu wa Kiswizi Ferdinand de Saussure na kazi za mwananadharia wa Kirusi Mikhail Bakhtin. Anaendelea kueleza kuwa juhudi za Kristeva za kuunganisha nadharia za lugha na fasihi zilizoasisiwa na de Saussure na Bakhtin ziliweka msingi wa mwanzo wa nadharia ya Mwingilianomatini katika miaka ya 1960. Aidha, neno mwingilianomatini lilizuka katika kipindi cha mpito katika miaka ya 1960 huko Ufaransa. Wakati huo umuundo ulikuwa unajadiliwa sana, jambo lililosababisha kuibuka kwa umuundo mpya au umuundoleo (Allen, 2000). Neno mwingilianomatini kwa mara ya kwanza lilijitokeza katika kazi za Julia Kristeva za *Word, Dialogue and Novel* (1966) na baadaye katika *The Bounded Text* (1966-7).

Bauman (2004) anaeleza kuwa mwanzo wa Nadharia ya Mwingilianomatini umewashughulisha wananadharia wa fasihi kwa muda mrefu, kutoka enzi za kale za Wayunani au Wayahudi; bila shaka kuanzia Aristotle alipofikiria kuhusu umuhimu wa muundo wa tanzia zenye msingi wake kwenye *Iliad* (1961) na *Odyssey* (1974). Bauman naye anasema kuwa nadharia hii iliibuka kwenye nadharia za lugha jamii, hususani nadharia za fasihi na lugha zilizoasisiwa na Mrusi aliyeitwa Mikhail Bakhtin iitwayo Usemezano. Kutokana na maelezo hayo, ni bayana kuwa Kristeva alipata maelezo ya mwanzo ya Nadharia ya Mwingilianomatini kutoka kwenye nadharia za lugha na fasihi za de Saussure na Bakhtin na kuathiriwa na mawazo yao. Bakhtin (1981) anasema kuwa lugha huwa na sifa za kiusemezano na kanuni za usemezano ni muhimu sana kwa kuwa mbali na kuchochea, hutawala katika uandishi wowote ule. Bakhtin alisisitiza kuwa maana ya tamko haina budi kuangaliwa katika usemezano. Kwa Bakhtin matini ya fasihi ni kama uwanja fulani na kwenye uwanja huo kuna mwingiliano wa sauti anuwai au za aina mbalimbali za semi. Bakhtin (1981) aliamini kuwa tanzu za fasihi zina uwezo wa kuingiza vipengele vya tanzu zingine lakini ukabakia na sifa zake kama utanzu. Vilevile, Bakhtin alifafanua kuwa kuwepo kwa

vipengele vingine vya fasihi ndani ya utanzu fulani wa fasihi hakuondoi hadhi ya utanzu huo. Anaongezea kuwa msingi mkuu wa nadharia ya mtindo wa mwingilianomatini umo katika jinsi kazi za fasihi zinavyohusiana, kuumbana na kukamilishana.

Kutokana na mawazo ya Allen (2000) na Bauman (2004) tunakubaliana nao kuwa Mwingilianomatini kama nadharia yenye mwelekeo wa kutumika kama nadharia ya uhakiki wa kifasihi umeanzishwa na Kristeva. Kristeva naye aliathiriwa na mawazo kutoka kwa watangulizi wake kama ilivyobainishwa hapo awali. Kristeva (1980) anaeleza kuwa kila matini ni matokeo ya mwingiliano wa matini nyingine ambapo matini inaundwa kwa mkusanyiko wa matini nyingine mbalimbali. Anaongezea kuwa hakuna maana moja inayoweza kutolewa kuhusu mwingilianomatini bali ni mazungumzo au mjadala baina ya maandishi kadhaa. Kristeva anafafanua zaidi kuwa Mwingilianomatini ni mbinu inayoelezea maana ya matini kwa kutumia uhusiano, mfanano, tofauti pamoja na kuhusisha muunganiko wa matini moja na nyingine. Kutokana na mawazo hayo ni dhahiri kuwa nadharia hii ya uhakiki inazingatia urejelezi wa matumizi ya matini kadhaa za fasihi pamoja na matini za kiutamaduni ndani ya matini nyingine ya fasihi.

Katika fasihi, Mwingilianomatini hujitokeza pale ambapo kazi ya fasihi huhusiana, huumbana na kuchangamana na kurejelea kazi nyingine tangulizi kwa kichwa cha habari ama maudhui yaliyomo. Mathalani *Utenzi waFumo Liyongo* (Kijumwa, 1913) unarejelewa katika tamthilia ya *Fumo Liyongo* (Mbogo, 2009) na *Utenzi waSundiata* (Niane, 1965) unarejelewa katika tamthilia ya *Sundiata* (Mbogo, 2011). Wamitila (2008) anaeleza kuwa uhusiano wa tungo wa mshairi mmoja na mwingine umejitokeza katika diwani ya *Malenga wa Mvita* inapohusishwa na *Diwani ya*

*Muyaka al Ghassanity* na utungo wa Shaaban Robert wa ‘Utenzi wa Hati’ unaohusiana na *Utenzi wa Mwana Kupona*. Aidha, katika kazi hizo, muundo, mtindo, wahusika, mandhari, maudhui na muktadha wake huingiliana na kukamilishana.

Allen (2000) anaeleza kuwa katika kazi za fasihi mtu hawezi kuelewa usemi au hata kazi iliyoandikwa kama vile ilikuwa na maana inayojitosheleza au inayojitegemea. Hapa Allen anamaanisha kuwa hakuna maana isiyounganishwa na usemi au kazi zilizopita kwani hakuna kazi ya kifasihi yenye sifa za pekee. Kwa hiyo, mwandishi wa kazi ya fasihi haumbi kazi au matini yake kutoka katika akili zake za asili lakini huziunganisha kutoka katika matini zilizotangulia. Matini si kitu binafsi au cha pekee, bali ni muunganiko wa umatini wa kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi.

Bauman (2004) akimnukuu Bakhtin (1986) anaeleza kuwa maana ya ndani ya Mwingilianomatini ni kuishi ndani ya ulimwengu wa maneno ya watu wengine. Kwa maneno hayo, ni wazi kuwa hakuna matini inayoweza kujitegemea kimaana pasipo kutegemea matini nyingine tangulizi. Vilevile, Clayton na Rothstein (1991) wanadai kuwa katika nafasi ya matini fulani, semi mbalimbali zilizochaguliwa kutoka matini nyingine huingiliana, huathiriana na kukamilishana. Kwa hivyo, athari ya kazi moja huweza kujitokeza moja kwa moja katika kazi nyingine, hata kama waandishi wake ni tofauti kiuzoefu, kiwakati, kimazingira na kijamii.

Kwa kuwa kazi yoyote ya fasihi inahitaji kuhusishwa na kazi nyingine tangulizi, Nadharia ya Mwingilianomatini ni muhimu sana katika kazi za fasihi ikiwemo ushairi, pamoja na kazi zinazojadili mchango wa wataalamu katika maendeleo ya ushairi na fasihi kwa ujumla. Uchambuzi wa kazi za ushairi wa Mathias Mnyampala unaonyesha kuwa hakuna kazi ya mwandishi ambayo kwa hakika ni ya asili, mpya na inajitegemea. Uhusiano wa muktadha, mbinu za utunzi na dhamira, ujumbe pamoja na

lugha, vinaonyesha vyema utegemezi wa kimwingilianomatini katika kubainisha mchango wa ushairi wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

Kwa hiyo, kutokana na mawazo ya Kristeva (1966, 1980), Barthes (1977), Allen (2000), Kehinde (2003), Wamitila (2002), Clayton na Rothstein (1991) na Widawsky (2014), tunapata mihimili ifuatayo ya Nadharia ya Mwingilianomatini:

1. Binadamu hawezi kukamilika kwa sababu hubadilika kila wakati, hivyo matini zote zilizoandikwa na binadamu hurejelea matini nyingine zilizotangulia. Kwa upande wa matini ile inayonukuliwa huibadili na kuielezea upya matini husika kwa kuiambatanisha na muktadha mwingine wa kiisimu na kijamii uliopo. Na matini hiyo mpya huweza kutofautiana kimiundo na kimazungumzo na matini tangulizi.
2. Kazi yoyote ya fasihi husheheni sifa mbalimbali za matini tangulizi moja au zaidi.
3. Hakuna matini inayoweza kustahimili pasipo kutegemea mtandao wa uhusiano wa kimatini unaosababishwa na mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali zilizowekwa na kazi tangulizi za fasihi, misimbo na utamaduni ambamo kazi za fasihi husika huibuka.
4. Katika uhakiki wa kazi za fasihi, mhakiki huathiriwa na kazi nyingine katika kuhakiki kazi husika, kwa kuwa kila usomaji na uhakiki wa matini huwa ni kijazilizo cha matini tangulizi.
5. Matini za fasihi zinahusisha udokezaji, udondozi, unukuzi, tafsiri, uigaji kwa namna ya kubeza au kurejelea kwa namna moja au nyingine kazi zingine za sanaa au matini nyingine.

Misingi ya nadharia hii imetufaa katika kuchunguza uhusiano wa kimwingilianomatini baina ya matini za fasihi. Kwa ujumla, uhusiano huo hupatikana katika tanzu zote kuu za fasihi simulizi na andishi. Kutokana na mapitio ya maandishi mbalimbali tuliyosoma tumebaini kuwa nadharia hii imetumika zaidi katika kuhakiki utanzu wa riwaya kuliko utanzu wa ushairi na tamthilia. Hivyo basi katika utafiti huu tumetumia nadharia hii kwa kuwa inafaa katika mjadala wa kifasihi katika tanzu zote ikiwemo ushairi. Aidha, tumetumia nadharia hii ili kutimiza malengo ya utafiti huu pamoja na kujibu maswali ya utafiti. Nadharia hii imetuwezesha kuonyesha jinsi kazi teule za Mathias Mnyampala zilivyoingiliana na muktadha uliomlea na alimokulia mtunzi wa kazi husika. Isitoshe, imetusaidia kutambua matini zinavyoingiliana katika vipengele mbalimbali vya fani na maudhui na namna mbinu za kifani zilivyotumika kuibua maudhui katika kazi teule za Mnyampala zilivyoingiliana na kazi tangulizi.

Kadhalika, tumebaini kuwa maendeleo ya ushairi hayakuibuka tu bali yametokana na mwingiliano wa vipengele anuwai vya fasihi simulizi pamoja na mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yaliyosababisha kuibuka kwa mbinu mpya za utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Kama asemavyo Kehinde (2003), kuwepo kwa utamaduni wa namna moja miongoni mwa watu, huwafanya waandishi kuandika kwa kuzingatia kazi zilizotangulia. Hivyo kuwapo kwa binadamu kumezungukwa na namna ileile na matatizo yaleyale yanayojirudia kama vile magonjwa, uongozi mbaya pamoja na matatizo mengine ya kijamii na kiontolojia. Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa uchunguzi wa mwingilianomatini wa ushairi wa Mathias Mnyampala na mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili umetekelezwa kwa kutumia nadharia hii.



### 2.3 Hitimisho

Sura hii imepitia na kujadili machapisho yanayohusu mada ya utafiti na misingi ya nadharia ya utafiti. Tumerejelea maandishi yanayohusu ushairi wa Kiswahili, muktadha na maandishi yanayohusu kazi za Mathias Mnyampala. Kutokana na maandishi hayo tumebaini kuwa hakuna mtafiti ambaye ameshughulikia kikamilifu mchango wa Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Watafiti wengi wameishia kutaja tu mchango bila ya kuchambua kazi zake, na wengine wameishia kudokeza kidogo tu katika hitimisho la kazi zao. Baadhi ya wahakiki wameishia kumbeza Mnyampala kuwa hakuwa na mchango wowote kwa kuwa aliandika yale yaliyokuwepo katika jamii kipindi hicho na kwa kuwa ametumia lugha ngumu ambayo si rahisi, kueleweka hakufanikisha kuwasilisha maudhui yake. Kwa upande wa nadharia tumefafanua Nadharia ya Mwingilianomatini na kueleza mawazo ya wataalamu mbalimbali kuhusu nadharia hiyo na mihimili ya nadharia hii. Nadharia ya Mwingilianomatini ni nguzo na mwongozo katika utafiti huu na ndiyo iliyotuongoza kujibu malengo na maswali ya utafiti huu. Istoshe nadharia hii ndiyo imetuongoza katika ukusanyaji na ufafanuzi wa data za utafiti huu. Sura inayofuata inachunguza muktadha ulioibua utunzi wa kazi teule za Mathias Mnyampala.

## SURA YA TATU

### ATHARI YA MUKTADHA KATIKA MASHAIRI YA MATHIAS MNYAMPALA

#### 3.0 Utangulizi

Sura hii inachambua data zilizokusanywa kutoka nyanjani na maktabani. Data zinazowasilishwa hapa zinahusiana na lengo la kwanza pamoja na swali la kwanza la utafiti huu. Lengo hilo linahusu muktadha uliomsukuma Mnyampala kutunga kazi zake teule za ushairi. Mukadha hurejelea mambo yaliyomzunguka mwandishi wakati wa utungaji wake na kufichua masuala muhimu ya kazi ya fasihi katika viwango vya maudhui na fani. Aidha, kupitia muktadha wa utungaji, mhakiki huelewa dhamira za mtunzi husika kupitia kazi zake (Njogu na Chimerah, 1999; Mumbo na Indede, 2004).

Kutokana na mawazo ya watafiti hao, kuna aina mbalimbali ya miktadha. Hata hivyo, miktadha iliyotumika katika utafiti huu ni minne tu ambayo ni muktadha wa kijamii, kisiasa, kiuchumi na mwingilianomatini. Aidha, muktadha wa kimwingilianomatini unajitokeza pia katika miktadha ya kijamii, kisiasa na kiuchumi pale ambapo matini moja inaingiliana na matini nyingine katika nyanja hizo. Miktadha mingine imeweza kutumika pale tu ilipobidi kwa lengo la kushadidia hoja husika. Kazi za kifasihi zilizochunguzwa ni *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965), *Ngonjera za UKUTANA. 1* (1970), *Hazina ya Washairi*, *Mashairi ya Vidato* na *Mahadhi ya Kiswahili*. Kabla ya kuendelea na uchambuzi tunawasilisha muhtasari wa kazi teule za Mnyampala.

#### 3.1 Muhtasari wa kazi Teule za Mathias Mnyampala

Kabla ya uchambuzi wa muktadha wa utunzi wa kazi za Mnyampala ni vyema kutoa muhtasari wa kazi zake teule.

### 3.1.1 *Diwani ya Mnyampala (1965)*

*Diwani ya Mnyampala* ni kitabu kilichochapishwa kwa mara ya kwanza na East African Literature Bureau, Dar es Salaam, mwaka 1965. Diwani hii ina jumla ya mashairi 178 ambayo yamegawanyika katika sehemu nne kuu. Kwa kiasi kikubwa diwani hii imesheheni mashairi yanayofuata kanuni za ushairi wa kimapokeo<sup>19</sup>. Aidha, mashairi tisa (9) kuanzia shairi Na. 139 la “Natunga Msisitizo” yanayopatikana katika (uk. 121) hadi shairi Na. 147 “Amezaliwa Mwokozi” (uk. 130) yametungwa kwa mtindo wa msisitizo (mtindo ambao kila ubeti una kipande cha kusisitiza maudhui yaliyomo katika ubeti husika)<sup>20</sup>. Mtindo wa msisitizo ni tofauti na mtindo wa kimapokeo. Hivyo mtindo uliotumiwa na Mnyampala katika diwani hii tunaweza kuuita ni mtindo mpya katika ushairi wa Kiswahili kwa sababu ndiye aliyetumia mtindo huu kwa mara ya kwanza. Maudhui ya diwani hii yameangazia masuala ya kijamii, kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi. Baadhi ya mashairi hayo ni: “Ndoa Akiridhi Nani” (uk. 4), “Mali Pepo ya Dunia” (uk. 7), “Wastara Hazumbuki” (uk. 9), “Mali mfano Maua” (uk. 11), “Pambo la Ndoa Mapenzi” (uk. 45), “Kitambi Kiso Mapesa” (uk. 69), “Amezaliwa Mwokozi” (uk. 130) na “Uhuru Uwe wa Kheri” (uk. 145).

### 3.1.2 *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi (1965)*<sup>21</sup>

Kitabu hiki kina mkusanyiko wa mashairi ya washairi mbalimbali mashuhuri nchini Tanzania akiwemo Mnyampala. Kitabu hiki kwa mara ya kwanza kilitolewa na chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA). Mashairi yaliyomo ndani ya kitabu hiki yalikusanywa na Mathias Mnyampala na kuyaweka katika kitabu hiki

<sup>19</sup> Mashairi yanayofuata kanuni ya urari wa vina na mizani, ujumi wa lugha na idadi ya mistari, hususani unne (tarbia).

<sup>20</sup> Shairi la “Natunga Msisitizo” limeambatanishwa kwenye tasnifu hii ili kuonesha muundo na mtindo wake

<sup>21</sup> Katika utafiti huu tumetumia toleo la pili (1968) ambalo lina mashairi mengi zaidi ukilinganisha na toleo la kwanza (1965).

mwaka wa 1965. Toleo la pili la kitabu hiki liliandikwa mwaka wa 1968. Katika toleo la pili yaliongezeka mashairi ambayo katika toleo la kwanza hayakuwamo (Mnyampala, 1968). Diwani hii inaitwa *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*. Maana ya *Mashairi ya Hekima* ni yale yaliyotungwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere. Alitunga shairi la “Usawa wa Binadamu” na “Chombo cha Taifa.” Kwa upande mwingine *Malumbano ya Ushairi* ni mashairi ya washairi wengine na Mnyampala akiwemo. Mashairi hayo yalitokana na shairi alitunga Kaluta Amri Abedi liitwalo “Raha” na ambalo lilisababisha malumbano au mzozo mkubwa wa kishairi. Shairi hilo la “Raha” lilifikiriwa vingine na baadhi ya washairi. Fikiria yao iliwatuma kuwa Amri Abedi alitunga shairi hilo kwa ajili ya kumhukumu mtu fulani maarufu nchini Tanzania aliyepata kushitakiwa na kupelekwa mahakamani (Mnyampala, 1965). Hatimaye malumbano hayo yaliisha na watunzi hao wakapatana na kurudia hali yao ya awali (Mnyampala, 1965:21).

Mashairi mengine yaliyomo katika kitabu hiki ni ya Kaluta Amri Abedi, aliyetunga shairi la “Mwasifiwa Tangu Kale,” “Raha” na “Dhana.” Yapo mashairi ya Khamis Amani Khamis (Nyamaume) ambayo ni “Mtego,” “Jiti” na “Saa.” Pia, kuna mashairi ya Mahmoud Hamdouniy (Jitukali) wa Dodoma yaitwayo “Dunia Duara,” “Dunia Nyama ya Tembo” na “Mizani.” Vilevile, kuna shairi la Mathias Mnyampala liitwalo “Ni Waadhi Ushairi.” Naye Sheikh Mohamedi Ali wa Dar es Salaam alitunga “Mtego Umefyatuka,” na Akilimali Snow White wa Kigoma aliandika shairi la “Dhana,” “Ushairi ni Waadhi” na “Duwa la Kuku Uongo.” Kadhalika, kuna shairi la Mohamed Selemani (Mtu-chake) wa Dar es Salaam aliyetunga shairi la “Ndovu Wanapigana.” Isitoshe, kuna shairi la R.A. Gwiji (Watendewao) wa Dar es Salaam aliyeandika shairi la “Jiti.” Baadaye yalifuata mashairi mengine ambayo yalikuwa yanatoa mawaidha mbalimbali, kuna shairi la Sheikh Mohamed Ali liitwalo “Dodoma,” shairi la Sheikh

Shaaban Robert “Uzee,” na Mwinyihatibu Mohamedi aliyetunga shairi la “Cheo.” Baada ya mashairi hayo kuna mashairi yanayosifu lugha ya Kiswahili na sanaa ya ushairi; Mohamed Ali aliyeandika shairi la “Mashairi ni Sanaa” na Mathias Mnyampala aliandika “Johari ya Tanzania.” Mashairi hayo yalihusu haki za binadamu, utu, upendo, na kuikuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Katika uchambuzi wa tasnifu hii tumetumia mashairi yaliyotungwa na Mnyampala; mashairi mengine yametumika pale tu yalipohitajika kwa lengo la ufafanuzi wa hoja husika.

### 3.1.3 *Mashairi ya Vidato (1966)*

*Mashairi ya Vidato* ni mswada wa mashairi uliotungwa na Mathias Mnyampala bado hayajachapishwa hadi sasa. Mashairi haya yaliandikwa mwaka 1966 na mwaka 1967<sup>22</sup>. Kwa mujibu wa Mnyampala (1966) maana ya vidato ni tungo mpya za kubadilishana vina, yaani kina cha mwisho huja katikati kwenye ubeti wa pili na kuzua kina kipya kwa ubeti unaofuata. Aidha, katika mahojiano<sup>23</sup> yaliyofanywa baina ya mtafiti na Madumulla ilibainika kuwa mashairi ya vidato yalikuwapo tangu enzi za Muyaka bin Haji. Mashairi yaliyokuwamo katika mswada huo yana majina kama ifuatavyo: “Uaminifu” (uk. 1), “Mungwana” (uk. 2), “Saba-saba” (uk. 3), “Kiasi” (uk. 4), “Kuuawa kwa Kennedy” (uk. 5), “Nasaba Yangu Mpenzi” (uk. 6), “Kitung’ati<sup>24</sup>” (uk. 7), “Mtaka nyingi Nasaba” (uk. 8) na “Tanzania ya Amani” (uk. 9). Mashairi mengine ni “Jarida la Kiswahili” (uk. 10), “Wanafunzi na Fadhili” (uk. 11), “Tusiseme Hatuwezi” (uk. 12), “Awezalo Binadamu” (uk. 13), “Dunia” (uk. 14), “Upendacho” (uk. 15), “Majuto” (uk. 16), “Hatukinai na Pato” (uk. 17) na “Dunia

<sup>22</sup> Mnyampala katika mswada huu wa Mashairi ya Vidato kila shairi ameandika tarehe, mwezi na mwaka ambao shairi hilo lilitungwa. Kupitia mswada wake tumeweza kubaini kipindi muafaka ambapo mashairi hayo yalitungwa. Aidha, mfano wa shairi moja la mtindo wa vidato tumeambatanisha kwenye tasnifu hii.

<sup>23</sup> Mahojiano hayo yalifanyika katika Chuo Kikuu cha Iringa (zamani kilijulikana kama Chuo cha Tumaini), tarehe 14/10/2016.

<sup>24</sup> Mnyampala katika mswada wake huu, anatoa maana ya neno Kitung’ati kuwa ni mtu shujaa sana mwenye elimu ya kuongoza majeshi yake, mwenye shabaha na hatimaye kufaulu katika vita. Mtu huyo akipangiwa jambo wafuasi wake wanaamini kuwa bila shaka watafaulu tu, na kwa kweli wanafaulu.

Hatukinai” (uk. 18). Kimaudhui mashairi ya mswada huu yanagusa nyanja mbalimbali za kisiasa, kijamii na kiuchumi. Mnyampala alikuwa anajaribu kutunga mashairi ambayo yataleta upya kifani na kimaudhui katika sanaa ya ushairi, kama aelezavyo mwenyewe katika mswada huu kuwa:

7. Mtindo huu wa vidato ni aina fulani ya mashairi makuu kama yale mengine yaliyowahi kusifiwa ulimwenguni humu katika lugha mbalimbali za ulimwenguni. Kama vile mashairi ya akina Shakespeare wa Stratford-on-Avon, Uingereza Upanishad, Mahabharata na Hamayana za Bara Hindi ya Kale, Iliad na Odyssey za Kiyunani cha Kale na Virjili ya Kirumi cha kale, n.k. (Mnyampala, 1966:69)

Kutokana na maelezo ya Mnyampala, tunabaini kuwa mashairi ya vidato yalitungwa kwa ufundi wa hali ya juu ili yaweze kuwiana na mashairi maarufu ulimwenguni. Licha ya kuandika mashairi hayo mazito (kwa mujibu wa Mnyampala mwenyewe na tulivyoyaona sisi katika utafiti huu) mashairi hayo hadi sasa hayajachapishwa wala kufanyiwa utafiti wa kutosha. Hivyo katika utafiti huu tumeyachambua mashairi hayo na kuchunguza muktadha wa utunzi pamoja na kutathmini mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

#### **3.1.4 Hazina ya Washairi (1966)**

*Hazina ya Washairi* ni mswada wa mashairi ya waandishi mbalimbali. Mashairi hayo yalikusanywa na Mathias Mnyampala mwaka 1966. Ni mashairi yanayohusu washairi maarufu wa karne ya ishirini na katika miaka tofautitofauti. Mashairi yaliyokusanywa ni mashairi ya kuanzia mwaka 1935 hadi 1965. Mashairi yaliyomo kwenye mswada wa *Hazina ya Washairi* yanahusu mijadala, mawaidha na ngonjera mbalimbali kama ilivyo desturi ya washairi na malumbano yao (Mnyampala, 1966). Mashairi hayo yamekusanywa na Mnyampala katika vyanzo vikuu vitatu, mosi ni kutoka katika magazeti kwa idhini ya wenye magazeti. Pili, ni kutoka katika Chuo cha Uchunguzi

wa Lugha ya Kiswahili<sup>25</sup>. Tatu, kupitia kwa watunzi wenyewe ambao walimpatia mashairi yao kwa ridhaa yao. Magazeti yaliyotumika katika ukusanyaji wa mashairi hayo ni *Mapenzi ya Mungu*, *Ngurumo* na *Mambo Leo*. Mnyampala anaeleza kuwa lengo la kunakili mashairi hayo lilikuwa kutaka mashairi hayo yahifadhiwe kwa ajili ya manufaa ya taifa zima pamoja na kujenga lugha ya Kiswahili kwa faida ya vizazi vijavyo. Mashairi yaliyomo kwenye mswada huo yanahusu masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Vilevile, mashairi yaliyomo katika mswada huo hufunza na kuelimisha jamii kuachana na mila potofu. Katika uchambuzi wetu tumetumia mashairi mengine yaliyoandikwa na Mnyampala, pale ambapo yalihitajika kwa ufafanuzi wa hoja husika.

### **3.1.5 Mahadhi ya Kiswahili (1967)**

*Mahadhi ya Kiswahili* ni mswada wa kitabu cha nyimbo kilichoandikwa na Mathias Mnyampala mwaka 1967. Ni mswada wenye mkusanyiko wa nyimbo mbalimbali zilizokusanywa na Mathias Mnyampala kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania na baadhi ya pwani ya Kenya (Mnyampala, 1967)<sup>26</sup>. *Mahadhi ya Kiswahili* unahusu nyimbo za rika mbalimbali, nyimbo za watoto, nyimbo za wazazi (hasa wanawake) wanazowaimbia watoto wao kwa kufuata jinsia. Pia, kuna nyimbo za kutafuta mchumba, nyimbo za mapenzi na mahaba kwa wanandoa na wanaokaribia kuingia kwenye ndoa na nyimbo za jando. Mnyampala katika dibaji yake anafafanua kuwa alizikusanya nyimbo hizo, kwa lengo la kuzihifadhi zisije zikapotea kwa vizazi vijavyo, kwa kuwa aliona vijana wengi wa kipindi hicho walijali zaidi utamaduni wa kigeni kuliko wa jamii zao.

<sup>25</sup> Chuo cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili kwa sasa kinajulikana kama Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI).

<sup>26</sup> Mnyampala anaeleza kuwa nyimbo nyingi alizipokea kutoka Unguja kwa rafiki yake Sheikh Haji Chum na nyingine ni za Mnyampala mwenyewe ambazo alitunga wakati akiwa Mutribu, akipiga ala za vinanda vya Kiswahili kama vile Tashikoto na Harmonia.

Maudhui yaliyomo katika mswada huu yanahusu utamaduni wa jamii. Mnyampala (1967) anaeleza kuwa mahadhi ya nyimbo ni mojawapo ya utamaduni maarufu kwa taifa. Utamaduni wa taifa unahusisha mila na desturi za jamii katika masuala ya malezi, uzazi, kuposa mchumba na ndoa, jando, wivu wa mapenzi na masuala ya dini. Kwa upande wa fani, nyimbo zilizomo kwenye mswada huu zimetumia tamathali za semi, mafumbo, methali, nahau, kuchanganya lugha za kikale, kikabila (Kibantu), Kiarabu na Kiingereza (hii inatokana na mwingiliano wa tamaduni). Pia, kuna mbinu ya majibizano ndani ya nyimbo hizo hasa nyimbo za mapenzi. Wahusika ni watoto, vijana, wanawake, wanaume na Mungu. Mhusika Mungu amepewa majina mbalimbali kama vile Mola, Maliki, Kariha na mengineyo. Kwa ujumla, mkusanyiko wa *Mahadhi ya Kiswahili* unahusu maudhui ya mapenzi na ndoa au mahusiano ya kimapenzi kati ya mke na mume. Nyimbo zilizoshughulikiwa ni zile alizotunga Mnyampala na zingine zimetumika pale tu zilipohitajika kwa ufafanuzi wa hoja husika.

### **3.1.6 Ngonjera za UKUTA Na.1 (1970)**

*Ngonjera za UKUTA Na. 1*, ni kitabu cha ushairi kilichochapishwa na Oxford University Press, Dar es Salaam mwaka 1970. Kitabu hiki kina jumla ya mashairi 48, yaliyogawanywa katika makundi tisa (9). Makundi hayo ni kama yafuatayo: Ngonjera ni Kitu gani, TANU na Siyasa yake, Viongozi wetu, Ujamaa, Azimio la Arusha, Elimu na Utamaduni, Sikukuu ya Taifa, Uhusiano Mwema na Mafumbo. Pia, mashairi ya kitabu hiki yameandikwa kwa mtindo wa drama<sup>27</sup>, ambapo huwasilishwa kwa njia ya majibizano ya kimaigizo. Mara nyingi ushairi huu una pande mbili zinazolumbana. Huu ndio msingi wa kutumia neno ngonjera. Neno hili ni la Kigogo lenye maana ya kwenda pamoja au mshikamano.

<sup>27</sup> Drama ni aina mojawapo ya sanaa za maonyesho ambayo usanii wa utendaji wake hutegemea zaidi vitendo na uongeaji.



Kwa upande wa UKUTA ni neno lilitokana na ufupisho wa chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania. Hivyo basi ngonjera za UKUTA maana yake ni mshikamano au usambamba katika washairi wanaounda chama hiki cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA). Kipindi ambacho kitabu hiki kilitungwa kilikuwa cha harakati za usanifishaji wa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuipa lugha ya Kiswahili mawanda mapana ya kimatumizi. Kawawa (1970) katika utangulizi wa *Ngongera za UKUTA Na. 1* anaeleza kuwa kila taifa lina utamaduni wake, lugha yake, siasa yake na shabaha yake ya kuendeleza taifa husika. Kwa ujumla, *Ngongera za UKUTA Na. 1* zilihusu masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika taifa la Tanzania na masuala ya ujenzi wa taifa hilo mara baada ya uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 na muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964. Baada ya kupata muhtasari wa vitabu teule, sehemu inayofuata inachambua lengo la kwanza la utafiti huu.

### **3.2 Muktaba wa Uandishi wa Kazi Teule za Mathias Mnyampala**

Sehemu hii inahusu uchambuzi wa muktaba wa uandishi wa kazi teule za ushairi za Mathias Mnyampala. Kazi hizo zimetumika kama kielelezo cha kazi zote zilizotungwa na mwandishi huyu. Kadhalika kazi zingine zimetumika kuelezea muktaba pale ilipobidi kujazilizia hoja. Kwa mujibu wa Friedrich (1986) muktaba ni suala linalohusu mazingira yanayomzunguka binadamu ama mwandishi wakati wa uandishi wa kazi husika. Muktaba pia huhusisha mielekeo na maoni ya mtu binafsi. Naye Walibora (2007) anaeleza kuwa watunzi wa vizazi vyote waliochagua kutumia Kiswahili kama nyenzo ya kusambazia mawazo na hisia zao walikuwa wakiandika mambo yaliyokuwa yanaendana na nyakati na mazingira yao. Mawazo ya watafiti hao tumeweza kuyachanganua kwa muktaba uliokuwapo wakati wa uandishi wa kazi teule za Mnyampala. Kazi hizo ni *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Mashairi ya*

*Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965), *Ngonjera za UKUTA I* (1970), *Hazina ya Washairi*, *Mashairi ya Vidato na Mahadhi ya Kiswahili*. Mwingilianomatini katika kazi ya fasihi hauwezi kutengwa na muktadha wa kijamii, kisiasa au kiuchumi ambao huweza kuchochea mahusiano fulani ya kazi zinazohusika (Wamitila, 2008).

### **3.2.1 Muktadha wa Kijamii**

Muktadha wa kijamii ni mambo au mazingira ya kijamii yaliyomlea, kumkuza au kumzunguka mtunzi wa kazi ya sanaa wakati wa uandishi wa kazi yake. Mazingira hayo kwa kiasi kikubwa huathiri fani na maudhui ya kazi husika. King'ei na Kemoli (2001) wanasema kuwa msanii anapoandika kazi yake anachochewa na mazingira pamoja na maudhui yake katika jamii anamoishi. Kwa mujibu wa data zilizopatikana maktabani na nyanjani, uandishi wa Mnyampala ulichochewa na masuala mbalimbali ya kijamii, zikiwemo kazi alizowahi kufanya wakati wa uhai wake. Mwandishi huyu alifahamu vizuri jamii yake ya Wagogo na nchi yake ya Tanzania na hata aliweza kuizungumzia nchi yake kupitia kazi zake za kifasihi. Muktadha wa kijamii katika kazi zake teule umejitokeza kupitia vipengele mbalimbali (ambayo tunaiita miktadha midogomidogo inayojenga muktadha wa kijamii), navyo ni: mwingiliano wa mila na desturi za Kiafrika na za kigeni, uzazi na malezi, kuathiriwa na waandishi wengine, masuala ya dini, mapenzi na ndoa, na kushamiri kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Usawiri wa miktadha hiyo katika kazi zake unachambuliwa hapa chini kama ifuatavyo:

#### **3.2.1.1 Maingiliano ya Mila na Desturi za Kiafrika na Kigeni**

Eliot (1988) anaeleza kuwa mila ni suala muhimu sana katika jamii na hujumuisha historia inayohusisha mitazamo ya jamii iliyopita na uliyopo. Anaongezea kuwa mtazamo wa kihistoria humwezesha mshairi kuandika nje ya jamii yake kwa kuzingatia vionjo vya kifasihi. Naye Madumulla (1988) anafafanua kuwa mila ni

taratibu za maisha ya kila siku ya watu, ambayo inahusu sana asili ya watu na hivyo hupokezwa kizazi hadi kizazi. Hivyo, mila hujumuisha mambo kama vile malezi kutoka utoto hadi uzeeni, miiko, mapokeo, historia, matibabu, matambiko, heshima, adabu na sheria zihusuzo taratibu za jamii kama vile ndoa, uzazi, urithi na vifo. Kwa vile mila hizi ni tunu kwa jamii husika, jamii hiyo huwa tayari kuzitetea kwa hali yoyote ile. Eliot anasema mila mahususi husaidia kueleza uhusiano uliopo kati ya mshairi na jamii yake. Mila kwa namna fulani ni katiba ya jamii ambayo hutokana na uzoefu wa watu wenyewe (Madumulla, 1988). Kutokana na mawazo ya wataalamu hao, tunaweza kusema kuwa mila huimarishwa na kurekebishwa na desturi za jamii ambazo kwa kifupi ni mazoea ya jamii katika muhula maalum wa historia. Aidha, mila ni tofauti na desturi, wakati mila ni uzoefu uliohibitishwa na hudumu, desturi ni mazoea ya matendo ambayo yanaweza kubadilishwa na baadaye kupokelewa kama mila ya jamii.

Desturi za jamii hujumuisha vitu kama vile namna zao za mavazi, ujenzi, salamu, vyakula na namna ya kula. Mambo haya yote hubadilika haraka sana jinsi watu wanavyobadilisha mbinu zao za uzalishaji mali. Desturi pia hubadilika wakati watu wanapopanua upeo wa mawasiliano na jamii zingine wanavyokutana na wageni ndivyo wanavyopokea desturi mpya na kuziambatanisha na desturi zao. Hivyo desturi ndiyo kichocheo cha jamii cha kupokea mawazo mapya na kuyasanifu kwa mahitaji yao ya kijamii.

Hivyo basi mila na desturi hurejelea tabia zote za makundi ya watu katika jamii fulani. Mfano wa tabia hizo ni kusalimiana kwa kushikana mikono, uvaaji wa mavazi, ulaji wa vyakula vinavyofanana, lugha na mengineyo. Kwa kawaida mila na desturi zimo katika muundo wa mahusiano ya jamii. Mila na desturi hutofautiana kati ya

jamii moja na nyingine. Aidha, mila na desturi huweza kurejelea mambo tuliyoapokea au tuliyorithi kutoka vizazi vilivyopita. Mambo hayo yanaweza kuwa mafundisho ya zamani ama mazoea ya watu katika jamii zilizotangulia na zilizopo wakati uliopo. Mila na desturi hujumuisha lugha, itikadi, sanaa, mshikamano, sheria au taratibu fulani zinazofuatwa na jamii. Hata hivyo, mila na desturi za jamii huweza kubadilika kutokana na mwingiliano wa jamii moja na nyingine.

Mtunzi wa kazi za fasihi huandika kazi zake kwa kuegemea katika mila na desturi zilizomlea na kumkuza. Maingiliano ya jamii mbalimbali humfanya mtunzi kuchanganya mila na desturi zake na mpya ili kukidhi matakwa ya jamii iliyopo. Kutokana na data zilizopatikana kutoka nyanjani na maktabani, tumebaini kuwa muktadha huu wa kijamii kupitia mila na desturi za kijadi na kigeni zimemuathiri kwa kiasi kikubwa mtunzi wa kazi teule. Mwandishi ameandika kazi zake kwa kuegemea mazingira mbalimbali yaliyopita, yaliyopo na yanayotarajiwa. Muktadha wa mwingiliano wa mila na desturi una mchango mkubwa katika utunzi wa kazi teule za Mathias Mnyampala. Kwa kuwa kazi zake zimeibuliwa katika muktadha wa mwingilianomatini wa mila na desturi za kijadi na kigeni. Kwa mfano, katika mswada wa *Mashairi ya Vidato* katika shairi la “Uaminifu” masuala ya uaminifu katika jamii yametokana na usawiri wa muktadha wa mila na desturi za Kiafrika ambazo zimesisitiza masuala ya uaminifu katika mazingira mbalimbali. Aidha, muktadha uliokuwapo katika kipindi hicho ulikuwa unasisitiza masuala ya uaminifu katika jamii, kwa kufuata misingi ya mila na desturi za jamii ya Kiafrika na dini za kigeni.

Ontolojia ya Kibantu<sup>28</sup> inatoa msisitizo juu ya masuala ya uaminifu, hivyo ontolojia hiyo ipo ndani ya mila na desturi (Mbiti, 1969 na Nicholas, 2011). Mnyampala

---

<sup>28</sup> Ontolojia ya Kibantu inahusu taaluma, nadharia na falsafa inayomhusu Mwafrika na imani yake kwa kujumuisha maisha, mazingira na fikra zake. Vilevile, inahusu kuwapo yaani yaliyokuwapo na ambayo hayakuwapo.

katika uandishi wake anasukumwa na masuala ya utu unaopatikana katika misingi ya utamaduni wa Mwafrika pamoja na masuala ya imani ya dini za kigeni. Hii ndiyo iliyofanya mashairi mengi ya Mnyampala kujadili mawaidha yanayohusu upendo kwa watu wote na kuwa na ushirikiano na umoja katika jamii. Mfano katika *Diwani ya Mnyampala* shairi la “Tenda Tendo la Kulinda” (uk. 75), Mnyampala anaeleza kuwa:

8. Tenda ridhisho la tendo, tenda watu wanaopenda,  
Tenda tendo la muundo, lile jema kulinda.  
Tenda tendo la mgando, mapendo yenye kuganda,  
Tenda tendo la kulinda, tendo ovu usitende.  
(ubeti wa kwanza, uk.75)

Katika dondoo hili mtunzi anasisitiza kutenda matendo mema na kuacha maovu. Kwa ujumla, masuala ya kutenda wema yanapatikana katika muktadha wa mila na desturi za kijadi na za kigeni. Vilevile, muktadha huu unapatikana pia katika kitabu cha Khatibu (2014) kuna mashairi ya Shaaban Robert na Muyaka bin Haji yanayohusu maudhui ya maadili na kuwa na utu katika jamii.

Kwa upande wa *Ngonjera za UKUTANA*. 1, katika muktadha wa kijamii kipengele cha mwingiliano wa mila na desturi kimejitokeza vyema kupitia ngonjera zilizokuwemo katika kitabu hicho. Ushairi huu ulilenga kuelimisha taifa kuhusu umuhimu wa kuendeleza utamaduni wa jamii na kuondoa mawazo potofu yaliyoletwa na wakoloni kuwa mila, desturi na utamaduni wa Waafrika ni wa kishenzi. Muktadha uliokuwapo kipindi hicho ulikuwa ni ule wa kupuuza mila na desturi za Kiafrika na kutukuza mila na desturi za kigeni. Katika kitabu hiki masuala haya ya mila na desturi yanajitokeza katika ngonjera ya “Elimu na Utamaduni” na “Utamaduni kitu gani” (uk. 58-59). Katika kipengele cha jawabu ubeti wa pili, wa tatu, wa tano na wa sita zinaeleza juu ya mila na desturi. Kwa mfano ubeti wa tano na sita unaeleza kuwa:

### 9. Jawabu

Na ufinyanzi wa vyungu, nazo ngoma zetu nchini  
 Na nyimbo zetu za tangu, sauti zetu ngomani  
 Mbali mila za Kizungu, ziwe kwao Uzunguni  
 Jina la utamaduni, ni ustarabu wetu (ubeti wa tano, uk. 59)

Kazi zetu za asili, zilizofanywa zamani  
 Za mikono na fasili, sidharau tukuzeni  
 Tumieni Kiswahili, na nyimbo zetu ngomani  
 Jina la utamaduni, ni ustaarabu wetu (ubeti wa sita, uk. 59)

Nukuu hiyo inadhihirisha kuwa mwandishi aliandika kitabu chake katika kipindi ambapo viongozi walikuwa wanapambana kutoa elimu kwa taifa ili kuenzi utamaduni wao ambao ulikuwa ni mzuri na wenye kuleta maendeleo kwa jamii. Hivyo muktadha uliokuwapo wakati huo ulikuwa wa kufufua mila na desturi za jamii ambazo zilikuwa nzuri lakini walipokuja wakoloni walizipuuza. Kutokana na data za utafiti huu, tumbaini kuwa muktadha unaosawiriwa hapa ni mwingiliano wa mila na desturi za Kiafrika na za Kizungu ambapo zile za Kiafrika zinaathiriwa kifikra. Waandishi wengi nyakati hizo waliandika kuelimisha jamii ili watambue mwingiliano uliokuwapo ili wafanye upembuzi wa kina kuhusu mila na desturi za kigeni na za jadi. Aidha, matumizi ya mbinu ya majibizano iliibuka ili kutimiza haja iliyokuwapo wakati huo.

Kwa mfano, Kawawa (1970) katika utangulizi wa *Ngonjera za UKUTA Na. 1 na 2*, anasema kuwa ngonjera za UKUTA ziliwafunza vijana chipukizi kujali utamaduni wa taifa lao ili kuachilia mbali desturi na utamaduni wa kigeni. Anafafanua zaidi kuwa wengi waliosoma vizuri Kiingereza wanafahamu sifa za mashairi na michezo mingi ya mashairi maarufu kama vile Shakespeare wa Uingereza. Kwa bahati taifa letu pia limevumbua njia au mbinu za ushairi wa michezo inayofanana na hiyo ya

Shakespeare, lakini yenye mazingira ya Kitanzania na lugha ya Kiswahili, utamaduni wa Mtanzania kwa shahada maalum ya Kitanzania.

Maelezo ya Kawawa yanasawiri vyema mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini ambayo inasema kuwa hakuna matini inayoweza kustahimili pasipo kutegemea mtandao wa uhusiano wa kimatini unaosababishwa na mfumo, misimbo na utamaduni ambamo kazi za fasihi huibuka (Kristeva, 1980). Fasihi haitoki katika ombwe kwani watunzi wanasoma kazi mbalimbali za kifasihi na kuathiriwa na kazi hizo na hatimaye kuibuka na mitindo mipya inayohusiana na kazi mbalimbali zilizosomwa kama ilivyojitokeza katika ngonjera za Mnyampala.

Katika kipengele cha mwingiliano wa mila na desturi za kijadi na kigeni katika uandishi wa tungo za Mnyampala kimesawiriwa vyema. Tumetambua kuwa Mnyampala aliweza kutumia mbinu mbalimbali za uandishi kulingana na maudhui aliyotaka kuandika pamoja na muktadha uliokuwapo wakati wa utunzi wa kazi husika. Mnyampala ni mtamaduni ambaye alipenda mila na desturi za jamii yake. Mnyampala alisisitiza suala la wanajamii kupenda utamaduni wao na kutupilia mbali mila potofu. Aidha, Mnyampala katika kazi zake amejenga muktadha wake kwa kuegemea pande zote mbili kulingana na mabadiliko yaliyokuwapo wakati huo; amezungumzia mila na desturi za kijadi na za kigeni. Suala la mila na desturi za kigeni ndizo zilizoonekana zimetawala katika fikra za mwandishi na kazi zake. Mojawapo ya mila na desturi za kigeni zilizomuathiri mwandishi wa kazi teule ni dini za kigeni, yaani Ukristo na Uislamu. Kadhalika katika uandishi wake, Mnyampala hakuacha kuwahimiza wasomaji kuheshimu tamaduni za Kiafrika zinazofaa kuendelezwa. Kwa ujumla, mwingiliano wa utamaduni wa kigeni na kijadi uliathiri

sana kazi za fasihi za kipindi hicho. Kwa hiyo, ukale na usasa unapojitokeza kwa pamoja mara nyingi usasa unakuwa na nguvu zaidi.

Kwa upande wa mswada wa *Mahadhi ya Kiswahili*, kwa ujumla nyimbo zilizokuwemo katika mswada huo zinasawiri vyema muktadha wa kiutamaduni wa jamii wenye mchanganyiko wa utamaduni wa kigeni na kijadi. Nyimbo alizoandika Mnyampala zimesheheni muktadha wenye mchanganyiko wa mila na desturi za kijadi na kigeni. Katika mswada huu kuna suala la mwanamume kutafuta mpenzi mwenyewe kwa kuandika barua na kumpelekea mwanamke, na mwanamke anamjibu kwa njia hiyo hiyo. Mtindo huu wa mahusiano na uandishi unatokana na utamaduni wa kigeni uliosababishwa na elimu ya kikoloni. Katika (uk. 13) kuna wimbo usemao:

10. Barua yangu ikifika, soma ukitulizana,  
Majibu yangu nataka, nijibu yenye maana,  
Roho yangu ikitoka, tahamala sina tena, (mwandika barua)

Ulipoleta barua, mimi nilikuwa sipo,  
Laiti ningalikuwa, ningajibu papa hapo,...(mpenziwe alijibu)  
Hapa inaonekana kuna muktadha wa elimu ya kikoloni ulioingiza mila na desturi za kigeni zinazompa nafasi mwanamke kuwasiliana moja kwa moja na mwanamume kuhusu masuala ya mapenzi. Kwa ujumla, katika utaratibu wa Kiafrika masuala ya mapenzi na ndoa yalikuwa yanaratibiwa na wazazi. Elimu ya kigeni ndiyo iliyoingiza mabadiliko hayo.

### 3.2.1.2 Uzazi na Malezi

Kipengele kingine cha muktadha wa kijamii ni uzazi na malezi. Suala la uzazi linajitokeza katika kazi teule za Mnyampala. Mfano katika *Diwani ya Mnyampala*, muktadha wa kijamii umetumika katika kumsawiri mwanamke kama mzazi na mlezi. Wamitila (2008) anaeleza kuwa muktadha wa kimwingilianomatini unahusisha shairi fulani kuashiria au kuelekezwa katika shairi lingine ambalo ni muhimu katika fasiri na



uelewaji wa shairi husika. Hivyo, Mnyampala (1965) anaeleza kuwa Akilimali Snow White alipinga shairi lake la “Tusitukane Wakunga” kwa kuandika shairi la “Kuzaa si Kazi.” Ndipo Mnyampala alipomjibu tena kupitia shairi la “Tutalea Mwana Gani?” Hivyo katika *Diwani ya Mnyampala* kuna mwingilianomatini, yaani mawazo ya Akilimali Snow White yanajibiwa ndani ya diwani hiyo.

Mwandishi kupitia shairi la “Tutalea Mwana Gani?” (uk. 18-19) anaeleza masuala ya uzazi na malezi, kuwa mwanamke mwenye tatizo la ugumba anataabika huku na kule ili kusaka tiba itakayomsaidia kupata mtoto ili kuepukana na adha mbalimbali (tazama beti za 8, 9 na 10) kama zinavyoonekana hapa:

**11.** Watu hufunga ndarama, wakaenda ugangani,  
Huifunga nayo ndama, ya kupeleka dawani,  
Watokane na kilema, kukosa mwana nyumbani,... Ubeti wa nane

Mwanamke hawi mama, hadi kuzaa Dani,  
Kwani mwana ndilo Boma, na stara maishani,  
Hutoka na lawama na watu kumlaani,... Ubeti wa tisa  
Asozaa ni nakama, sikitiko duniani,  
Ana huzuni daima, humuomba Rahmani,  
Tuache anojinyima, kwa sheria za kidini,  
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga? Ubeti wa kumi

Katika shairi hilo Mnyampala anazungumzia wanawake wanaopata ujauzito lakini hunyonga watoto wao wakati wa kujifungua. Masuala ya uzazi na malezi yanayoelezwa katika diwani hii yanachochewa na muktadha wa ontolojia ya Kibantu (utamaduni wa Mwafrika). Mbiti (1969) na Nicholas (2011) wanaeleza kuwa masuala ya uzazi ni mojawapo ya vipengele vya falsafa za Kiafrika. Kwa ujumla, jamii mbalimbali za Waafrika zinathamini sana masuala ya uzazi. Hivyo basi, Mnyampala anaziangazia jamii za Kiafrika, hususani Watanzania ambao wana utamaduni unaosisitiza suala la uzazi. Uzazi huhakikisha maendeleo ya jamii yao ulimwenguni.

Malezi ya watoto na familia ni mojawapo ya masuala yanayojitokeza katika muktadha wa suala la uzazi na malezi. Mnyampala katika *Diwani ya Mnyampala* ameathiriwa na muktadha huu kwa kumwonesha mwanamume na mwanamke kuwa walezi wa watoto na familia. Ijapokuwa jamii nyingi za Kiafrika zinaonesha kuwa suala la malezi ndilo limempa mwanamke upekee na umuhimu katika jamii. Kwa upande mwingine Mnyampala katika diwani hii, hususani katika shairi la “Je Nafsi na Upenzi,” anazungumza kuwa suala la malezi ni jukumu linalomhusu pia mwanamume. Katika ubeti wa sita mwandishi anasisitiza haya:

12. Wapenzi nawaheshimu, baba na mama wazazi,  
 Ndio wangu muhashimu, walezi wenye mbawazi,  
 Napenda kuwahudumu, awajalie Mwenyezi,  
 Je nafsi na upenzi, ni kipi kilicho muhimu?

Mnyampala hapa anasisitiza kwamba ushirikiano wa wanaume na wanawake ni muhimu katika kuwalea watoto kimaadili. Ni jambo linalohitajika katika familia na jamii kwa ujumla. Malezi ni jukumu la wazazi wote wawili. Hali hii inaakisi suala la mwingiliano wa kijamii. Katika muktadha wa jamii za Kiafrika, suala la malezi aliachiwa mama. Hata hivyo Mnyampala anaelekea kuathiriwa na utamaduni wa kigeni uliokuja na wakoloni na Ukristo. Yeye kama Mkristo amechota mawazo yake kutokana na utamaduni huo na hivyo tunaona mwingiliano wa kiutamaduni ukimsukuma kuandika anavyoandika katika ubeti huo.

Kadhalika katika ubeti huo Mnyampala anasisitiza masuala ya kuwaheshimu baba na mama. Suala hili linasisitizwa katika jamii za kijadi na kigeni. Katika damaduni za kigeni suala la kuwaheshimu baba na mama ni mojawapo ya amri za Mwenyezi Mungu. Hiyo ni Amri ya nne kati ya amri kumi za Mungu. *Biblia Takatifu* inasema: “Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi

upewayo na BWANA, Mungu wako” (Kutoka 20:12). Mukstadha huu unaakisi suala la mwingiliano wa jamii, masuala haya katika jamii za Kiafrika kulingana na mukstadha wa kijamii, suala la malezi aliachiwa mama. Hivyo, kutokana na mwingiliano wa tamaduni za kijadi na kigeni Mnyampala ametumia mukstadha wa kijadi na kigeni uliokuwapo wakati huo, kusisitiza umuhimu wa kuwaheshimu wazazi. Pia amezungumzia malezi ya watoto kuwa ni jukumu la wazazi wote wawili. Malezi ya mtoto kuwa jukumu la wazazi wote wawili limezungumzwa zaidi katika dini za kigeni na tamaduni za kigeni zinasisitiza haki sawa kwa jinsia zote.

Mnyampala anaelekea kuathiriwa na utamaduni wa kigeni uliokuja na wakoloni na kupelekea mwingiliano wa kitamaduni. Hivyo mwingiliano wa tamaduni za kigeni na za kijadi ndizo zilizomfanya Mnyampala kuandika kazi zake kwa kuchota mawazo huku na kule ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii husika. Kristeva (1966) anasema kuwa matini yoyote imeundwa kwa mkusanyiko wa nukuu na ni ufyonzaji wa matini nyingine.

### **3.2.1.3 Kuathiriwa na Waandishi Wengine**

Katika mukstadha wa kijamii kuna mwingiliano wa mbinu za utunzi wa kazi za Mnyampala na za watunzi wengine ndani ya nchi na nchi za kigeni. Katika utunzi wake ameathiriwa kimawazo na mbinu za utunzi wa mashairi alizozipata kwa kusoma kazi mbalimbali za watunzi wengine ulimwenguni. Haya anayasema mwenyewe katika mswada wa *Mashairi ya Vidato* kuwa:

13. Vidato ni aina fulani ya mashairi makuu kama yale mengine yaliyosifiwa ulimwenguni kama katika lugha mbalimbali za ulimwenguni – kama vile mashairi ya akina Shakespeare wa Stratford-On-Avon, Uingereza Upanishad, Mahabharata na Hamayana za bara Hindi ya kale, Iliad na Odyssey za Kiyunani cha kale na Virjili ya Kirusi cha kale, n.k. (uk. 12)

Kupitia dondoo hili tunaelewa kuwa Mnyampala alikuwa hodari wa kusoma mashairi mbalimbali ili kujifunza mbinu mbalimbali za utunzi na kuvumbua mitindo mipya ya uandishi ambayo itawavutia wasomaji wa ushairi wa Kiswahili na kufikisha mawaidha kwa jamii husika. Kwa mfano mtindo wa mashairi ya vidato ulitumiwa pia na Muyaka bin Haji katika uandishi wa mashairi (rejea *Diwani ya Muyaka*, shairi la “Twangaliana kwa Mato” uk. 85). Huu ni mwingilianomatini ambao unaonyesha namna gani kazi za mwandishi huyu zinarejelea kazi nyingine za fasihi. Mwandishi alikuwa na mawanda mapana ya muktadha na wala hakujikita katika muktadha uliomlea na kumkuza tu aliweza kurudi nyuma na hata kuvuka mawanda wakati uliokuwepo. Anayoyafanya Mnyampala yanaafikiana na maoni ya Allen (2000) kuwa nadharia ya Mwingilianomatini inahusisha matini zilizopo kuunda matini mpya. Kwa kweli mwingilianomatini hujitokeza pale ambapo kazi ya kifasihi huingiliana na kurejelea kazi nyingine tangulizi ama zilizopo kwa kichwa cha habari, muundo, mtindo, wahusika, mandhari na katika muktadha wa usimulizi na muktadha wa kijamii. Hali hii ilijitokeza wazi katika tungo za Mathias Mnyampala. Ni bayana kuwa kazi za Mnyampala zinaonyesha mwingiliano wa muktadha wa utunzi wa kazi zake na waandishi wengine. Kama asemavyo Kawawa (1970) katika utangulizi wa *Ngonjera za Ukuta Na. 1* kuwa:

**14.** Kwa bahati njema, taifa letu nalo limevumbua njia za ushairi wa michezo inayofanana na hiyo ya Shakespeare, lakini yenye mazingira ya Watanzania wenyewe, lugha ya Kiswahili, utamaduni wa Kitanzania na shabaha maalum ya Kitanzania. (Uk. 1)

Nukuu hiyo inatudhihirishia kuwa Mnyampala aliathiriwa na muktadha wa kazi nyingine za watunzi maarufu kama vile Shakespeare pamoja na mazingira ya jamii yake ya Kitanzania. Aidha, kitabu hicho kiliandikwa kipindi cha Azimio la Arusha kilichotawaliwa na muktadha wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Aidha, waandishi

wengi wa ushairi walitunga kazi mbalimbali za ushairi wakisifu na kupongeza jitihada zilizofanywa na viongozi hadi kuanzishwa kwa Azimio la Arusha. Miaka hiyo Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alitafsiri tamthiliyaza Shakespeare ambazo ni *Mabepari wa Venisi* (1966) na *Julius Kaizari* (1966). Hivyo, waandishi mbalimbali walivisoma vitabu hivyo na kuongeza maarifa juu ya utunzi na mitindo mbalimbali ya uandishi wa kazi za fasihi. Mnyampala alipenda kusoma kazi mbalimbali za waandishi wengine zikiwemo za Shakespeare na kujifunza mbinu za utunzi huo pamoja na mbinu za usimulizi zilizokuwepo katika jamii. Mukstadha huo wa kazi za Shakespeare ulimwezesha Mnyampala kuibuka na mtindo wa ngonjera za Kiswahili zenye maudhui ya Kitanzania yenye kusawiri hali halisi ya jamii za Watanzania. Mnyampala aliathiriwa na mtindo wa tamthilia za Shakespeare kwa sababu tamthilia hiyo ina mtindo wa ushairi wa kidrama ambao ni uwasilishaji wa maudhui ya mchezo katika muundo wa ushairi wa maigizo. Hivyo Mnyampala kutumia mbinu hiyo katika ushairi wake wa ngonjera na kuzifanya ngonjera kuwa za kimaigizo.

#### **3.2.1.4 Dini**

Mukstadha wa dini ni mojawapo ya mambo yaliyomuathiri Mnyampala katika uandishi wa kazi zake za ushairi. Data zilizokusanywa nyanjani na maktabani zinaonyesha kuwa makuzi ya Mnyampala yaliathiriwa sana na dini ya Kikristo. Suala la dini ya Kikristo lina mchango mkubwa katika kuumba maudhui ya kazi zake. Hata hivyo, Mnyampala hakuathiriwa na mukstadha wa dini ya Kikristo tu, bali pia aliathiriwa na mukstadha wa dini ya Kiislamu aliyojifunza baadaye. Aidha, kuingia kwa dini za kigeni hususani dini ya Kiislamu kuliathiri mtindo na muundo wa ushairi wa Kiswahili. Kutokana na dini hizo kulitokea mwingilianomatini katika kazi za sanaa, ambapo waandishi walichukua vipengele mbalimbali vya dini ya Kiislamu na Kikristo na kuviweka katika sanaa zao. Mfano wa vipengele hivyo ni kuanza na dua

na kumaliza na dua, maneno yanayotaja Mungu wa dini za kigeni kwa mfano Jalia, Maanani, Karimu, Kristo, Masiya na mengineyo. Kwa upande wa dini ya Kikristo, muktadha huo umejitokeza katika utunzi wa mashairi yake na umethibitisha kuwa Mathias Mnyampala alikuwa Mkristo si kwa jina tu bali hata kwa matendo na aliipa dini ya Kikristo uzito hata katika ushairi wake.

Mfano katika *Waadhi wa Ushairi* (1965) shairi la “Dini” anasema kuwa; “Aso dini ni kipofu, hajui mbele ni nini” (uk. 34) katika ubeti wa kwanza. Kutokana na nukuu hiyo ni dhahiri kuwa katika kipindi hicho ilimpasa kila mmoja kuwa na dini, ama ya Kiislamu au Kikristo. Dini ya kijadi kipindi hicho ilihesabika kama upagani na ushetani. Usawiri wa muktadha wa dini ya Kikristo unajitokeza zaidi katika kazi zake za ushairi za *Utenzi wa Injili* na *Utenzi wa Zaburi* kuanzia majina yenyewe ya vitabu na maudhui yaliyomo katika vitabu hivyo. Kwa mfano katika *Utenzi wa Injili*, Mnyampala ameunda utenzi huo kwa kufuata kitabu cha maandiko matakatifu yaani *Biblia*. Kupitia *Utenzi wa Injili* Mnyampala amewasilisha mawazo ambayo yanapatikana katika Agano Jipya na sehemu ya injili nne ambayo ni Injili ya Mathayo, Marko, Luka na Yohana. Tenzi hizo zinatudhihirishia kuwa Mnyampala aliathiriwa na muktadha wa dini ya kigeni (Kikristo) ndio maana katika kazi hizo alitunga tenzi za dini hiyo.

Katika *Diwani ya Mnyampala* suala la dini ya Kikristo linajitokeza katika mashairi mbalimbali. Baadhi ya mashairi hayo ni “Rabbi Yesu Kazaliwa” (uk. 39), shairi hili linatokana na *Biblia Takatifu*, Luka 2:1-14. Mfano katika ubeti wa tisa na kumi, mwandishi anawaelezea Mariamu na Yosefu walivyokwenda kuhesabiwa na kukosa nyumba ya kulala wageni na kusababisha Yesu kuzaliwa pangoni mahali pa kulishia wanyama. Katika ubeti wa tisa anasema:

**15.** Mariamu na Yosefu, walikwenda kuhesabiwa,  
Kwa mtemi maarufu, kwao waliotawaliwa,  
Nafasi kuwa kosefu, pangoni wakapangiwa,  
Siku ya kushangiliwa, ndio hii takatifu.

Haya yanajitokeza katika Luka 2:7, inayosema “*akamzaa mwanaye, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori la kulia ng’ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.*” Nukuu hii ya Injili ya Luka inaonekana ina mwingiliano na mawazo ya shairi la “Rabbi Yesu Kazaliwa” (uk. 39). Kwa kuwa Mnyampala alikuwa muumini wa kanisa Katoliki, bila shaka alichukua mawazo kwenye *Bibilia*, yanayohusu masimulizi ya kuzaliwa kwa Yesu katika *Bibilia* na kuyaweka kibunifu katika ushairi wake.

Vilevile, shairi la “Amezaliwa Mwokozi” (uk. 130) ni usimulizi unaohusu siku ya Chrismass au Noeli. Wakristo wanaamini kuwa siku hii ni kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo. Sherehe hizo hufanyika tarehe 25 Desemba kila mwaka. Kadhalika, Mnyampala katika shairi la “Kiongozi Mtukufu” (uk. 26) anazungumzia sikukuu ya Pasaka<sup>29</sup> ambayo mara nyingi huwa mwezi wa Aprili na mara chache hutokea mwezi Machi. Kwa mujibu wa kanisa Katoliki sikukuu ya Pasaka inatanguliwa na Kwaresma ambapo waumini wanatakiwa kufunga siku arobaini. Kipindi hiki ni cha toba ambacho waumini hutubu dhambi zote na kumrudia Mungu kwa moyo wote. Mfano ubeti wa sita unaeleza kuwa:

**16.** Nyoyo zisitulegee, kwa juhudi jikalifu,  
Na Pasaka isogee, kwa siku zake “Tawafu,”  
Ni Karibu tutegee, na Tuyaache machafu,  
Kwa sifa na utukufu, kiongozi wendelee. (uk. 26)

Hapa mwandishi anahimiza watu kuacha dhambi na kumrudia Mungu, kwa kufunga na kuomboleza pamoja na kudhamiria kuacha dhambi na kuwa na moyo safi kama

<sup>29</sup> Pasaka ni kumbukumbu ya ufufuko wa Yesu Kristo, ambayo huadhimishwa na Wakristo kila mwaka.

theluji. Maelezo yanayopatikana katika shairi hilo yanaendana na maandiko yaliyomo katika vitabu vitakatifu. Mfano *Biblia Takatifu* kitabu cha Yoeli 2: 12-13; kinasema:

17. Lakini hata sasa, asema Bwana,  
Nirudieni mimi kwa mioyo yenu yote,  
Na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuomboleza,  
Rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu,  
Mkamrudie Bwana, Mungu wenu...

Katika shairi la “Kiongozi Mtukufu,” mwandishi ameathiriwa na muktadha wa dini za kigeni katika utunzi wa kazi zake za ushairi. Inasemekana kuwa katika maisha yake, baada ya kuoja alijihusisha sana na masuala ya dini na kuifahamu *Biblia Takatifu* ili aweze kufundisha vizuri somo la dini alilokuwa akifundisha huko Mzogole (taz. sehemu ya 1.1.1.5 na kiambatisho cha mafunzo ya *Biblia* ndani ya tasnifu hii).

Muktadha huu wa dini unasawiri vyema Nadharia ya Mwingilianomatini kama asemavyo Wolfreys (2004) kuwa Mwingilianomatini ni njia ambayo matini zote zilizoandikwa na kusimuliwa hurejelea matini nyingine. Hapa anamaanisha kuwa uundaji wa maana ya matini hutegemea matini nyingine. Kwa mfano, katika *Diwani ya Mnyampala* kama tulivyoona hapo juu, Mnyampala ametumia *Biblia Takatifu* kutunga mashairi ya kuelimisha jamii kwa kufuata mwongozo wa dini ya Kikristo katika kazi zake za ushairi.

Kadhalika, masuala ya dini ya Kikristo yanajitokeza katika *Diwani ya Mnyampala* akiwaombea na kuwapa wosia wanawe Aloyce, Charles na Edward. Mnyampala aliwatungia shairi liitwalo “Maombezi kwa Kizazi” (uk. 154). Ubeti wa tatu hadi wa tano, anasema:

18. Aloisi nakutuma, mwanangu mtangulizi,  
Hapo nitakapohama, kwenda mbele ya Mwenyezi,  
Badala yangu simama, kitini uwe mwamuzi,  
Maombezi kwa kizazi, hasa ni kitu muhimu (Ubeti wa tatu)



Charles shika huruma, moyo wenye mbawazi,  
Mwendo wangu umesoma, sikupenda majikwezi,  
Utaipata ghanima, jaza utahozzi,... (Ubeti wa nne)

Edward kua salama, pasipo na kizuizi,  
Mungu akujalie mema, sizuke upatilizi,  
Na uipate neema, hata kupata ngazi,... (Ubeti wa tano)

Dondoo hilo ni dhahiri kuwa dini za kigeni zilimwathiri Mnyampala katika utunzi wa kazi zake na hata katika malezi ya wanawe. Katika shairi hilo aliwataja wanawe watatu ambao ni Aloyce, Charles na Edward akiwaombea maisha marefu, washike dini, na waepuke maovu. Kwa ujumla, Mnyampala alitoa mawaidha ya namna ya kuishi pindi atakapoaga dunia. Kutokana na makuzi ya dini ya Kikristo Mnyampala ameathiriwa katika utunzi wa kazi zake na dini hiyo kama alivyoathiriwa Shaaban Robert na dini ya Kiislamu katika utunzi wa kazi zake. Kwa upande mwingine Mnyampala aliathiriwa na dini ya Kiislamu ambayo alijifunza alipokuwa anapanua maarifa.

Aidha, dini ya Kiislamu imetoa msukumo katika utunzi wa mashairi teule ya Mathias Mnyampala. Hata katika maandishi yake kama vile *Diwani ya Mnyampala*, ametumia maneno mengi ya Kiarabu yanayohusiana na Mungu kama vile Karima, Maliki, Jariha, Rahmani na mengineyo aliyoweza kuyatumia katika utunzi wake. Kutokana na data tulizopata kutoka nyanjani na maktabani, imebainika kuwa Mnyampala alijifunza na kuifahamu kwa kiasi fulani lugha hiyo. Ujifunzaji wa Mnyampala wa lugha ya Kiarabu na dini ya Kiislamu unadhihirika waziwazi katika mswada wa kitabu chake cha *Fasili: Johari ya Mashairi* (uk. 18) asemapo:

**19.** Ama kwa hakika Kurani Tukufu ndicho kiwango  
cha asili ya maghani bora sana yatokanayo na uimbaji  
wa mashairi, kadhalika na kasida ya maulidi kutokana  
na Barazanje.

Hapo Mnyampala anasifia *Kurani Tukufu* kuwa ndiyo chanzo cha asili ya maghani bora ya ushairi. Ukweli ni kwamba ushairi wa kimapokeo umebeba athari nyingi kutoka kwa Waarabu ambao walihusiana kwa muda wa karne nyingi na wenyeji wa mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki. Uhusiano huo uliingia kupitia utamaduni wao hasa katika kipengele cha dini ya Kiislamu. Waswahili walipokea utamaduni huo kupitia mashairi ya Waarabu kama vile Qaswida za dini zilizotungwa kwa kufuata mlingano wa sauti za kumalizia kila ubeti (Ngugi, 1998). Hili pia tunaliona katika kazi za ushairi wake ambapo anatoa mawaidha ya dini zote mbili maarufu nchini, yaani Kikristo na Kiislamu. Kadhalika katika vitabu vyake kwa mfano *Diwani ya Mnyampala, Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* na mswada wa *Hazina ya Washairi*, Mnyampala amehusisha mashairi ya watunzi wa dini ya Kikristo na Kiislamu pasi na ubaguzi wowote. Kwake yeye alichozingatia ni ubora wa kazi za shairi pamoja na thamani yake katika kukuza lugha ya Kiswahili na utamaduni wa Mtanzania.

Katika kazi zake teule Mnyampala ametumia maneno mengi ya Kiarabu ambayo yanathibitisha kuwa aliyajua kutokana na kusoma Kurani na kujifunza Kiarabu. Vilevile Mnyampala aliwahi kuwa Kadhi<sup>30</sup> wa Mahakama ya Waislamu. Kwa kawaida, huwezi kupewa kazi ya kusimamia na kuhukumu kesi za Waislamu kama hufahamu vizuri misingi ya dini hiyo. Mukstadha huo wa dini ya Kiislamu unajitokeza zaidi katika *Diwani ya Mnyampala*. Mashairi mengi katika *Diwani ya Mnyampala* yanaanza na dua na yana maneno mengi ya Kiarabu yanayosawiri vyema dini ya Kiislamu kama tulivyosema hapo awali. Hivyo ni dhahiri kuwa Mnyampala ameathiriwa na mukstadha wa kidini katika uandishi wa kazi zake ikiwemo *Diwani ya*

---

<sup>30</sup> Mahakama ya Kadhi hushughulikia mirathi, ndoa na talaka kwa kufuata sheria ya Uislamu. Hii ilikuwa ni mara ya kwanza na haijawahi kutokea tena mahakama hiyo kuongozwa na Mkristo nchini Tanzania.

*Mnyampala*, kama asemavyo Gibbe (1978) katika *Diwani ya Mnyampala*, msimamo wa Mnyampala kuhusu dini ulikuwa mkali sana na hakuacha kuielezea dini na kuwaasa waumini wazingatie dini zao. Gibbe anaongezea kuwa Mnyampala hakuchoka na kudadisi baadhi ya vipengele vinavyohubiriwa na dini.

Mifano kadhaa kuhusu usawiri wa dini ya Kiislamu inapatikana katika *Diwani ya Mnyampala*. Mathalani, katika shairi la “Hata Sheikh Ameradhi” (uk.16), mhusika Sheikh ni kiwakilishi cha imani ya Kiislamu ambaye ni kiongozi wa dini anayetoa mawaidha msikitini. Vilevile, shairi la “Siraji Ng’aza Sirati” (uk. 135), Siraji na Sirati ni maneno yenye asili ya Kiarabu yanayotumika katika dini ya Kiislamu kumaanisha taa au nuru (siraji) na njia (sirati). Mnyampala ametumia maneno mengi ya Kiarabu katika kazi zake. Shairi lingine lililosawiri dini ya Kiislamu katika diwani hii ni “Hima Hima Islamu” (uk. 6), shairi hili linawahimiza Waislamu kufunga kipindi cha mwezi wa Ramadhani ambacho ni kipindi cha toba kwa Waislamu wote duniani.

Vilevile, Mnyampala alikuwa anavifahamu baadhi ya vifungu vya *Kurani Tukufu*.

Mnyampala (1962:6) analithibitisha hili katika *Utenzi wa Injili* anaposema kuwa:

20. Enjili hizo nne hazikuaminiwa na Wakristo peke yao tu la, lakini pia hata waumini wa madhehebu mengineyo nao wanakiamini kitabu cha Enjili. Kwa mfano imani ya dini ya Kiislamu inahimiza kwamba kila Islamu lazima kuviamini vitabu vinne-Torati ya Nabii Musa, Zaburi, Injili ya Nabii Issa (Yesu Kristu) na mwisho ni Furkani ya Mtume Muhammadi (S.A.W). ...Lakini Islamu wanaamini kwamba Yesu hakuuawa na kuzikwa na kufufuka bali wanaamini ya kwamba “alirufaishwa.” Yaani alichukuliwa na mwenyezi Mungu kwenda mbinguni na mwili wake. Na mahali pake aliuawa mtu mwingine aliyetengenezwa sura kuwa sawa kama yeye lakini si yeye.

Dondoo hilo linathibitisha kuwa Mnyampala alikuwa na uelewa fulani wa dini zote mbili, yaani ya Kikristo na Kiislamu. Kwa upande mwingine tunaweza kusema kuwa

aliandika hivyo ili kujenga jamii moja yenye upendo na mshikamano. Hivyo aliweza kusawiri vyema muktadha wa dini za kigeni katika kazi zake kutokana na ufahamu wake kuhusiana na maandiko matakatifu ya dini hizo. Kadhalika, Mnyampala aliweza kuunga na kuhamasisha wananchi kuunganisha dini hizo mbili na kushauri jamii iwepo siku ya kuadhimisha sikukuu hiyo. Shairi linalothibitisha hilo ni “Ya Watakatifu Wote” (uk. 132), shairi hilo linahusu dini ya Kiislamu na Kikristo. Kama asemavyo katika ubeti wa kwanza wa shairi hilo kuwa:

21. Kila dini na Imani, walivyofunzwa wafate,  
Huwa msingi wa Dini, ni lazima tuambate,  
Na leo tumo Kanisani, wa Vigulu na Viwete,  
Ya watakatifu wote, tarehe mosi Novemba.

Katika shairi hili mwandishi anahimiza kila mmoja kufuata mafundisho kulingana na imani ya dini yake. Hakuna sehemu hata moja ambayo aliweza kutoa mafunzo ya kushawishi mtu kuacha imani yake. Wala hakuweza kukosoa dini za wenzake kuwa ni mbaya na kuiona yake ni nzuri bali yeye alisisitiza kila mtu ashike mafundisho ya dini yake na kumfuata Mungu pasi na kuwepo na ubaguzi wowote. Mawazo hayo yalitokana na muktadha wa kijamii uliokuwepo wakati huo ambao uliwataka watu washirikiane na kuheshimiana bila kujali tofauti zilizopo za kiimani na hata kikabila. Hii ndiyo maana katika utunzi wake hakuacha kutoa mawaidha kuhusu dini na kuwasisitiza watu kushika sana imani za dini zao kama Shaaban Robert alivyosisitiza. Mnyampala kama Shaaban Robert aliyeishi na kutunga tungo zao kwa kuhimiza umoja wa wanajamii pasi na ubaguzi.

Kwa ujumla utamaduni uliokuwepo kipindi hicho ni wa kutukuza tamaduni na dini za kigeni, hali iliyosababisha kushamiri kwa dini za kigeni na kufifia kwa dini za kijadi. Kushamiri kwa dini za kigeni kulisababisha waandishi wengi kuandika kwa kuegemea katika dini hizo. Kehinge (2003) anaeleza kuwa kuwapo kwa utamaduni

mmoja miongoni mwa watu, huwafanya waandishi kuandika kwa kuzingatia kazi zilizotungwa awali kwa kuwa kuwapo kwa binadamu kumezungukwa na muktadha wa namna ileile ya matatizo yaliyopo katika jamii. Aidha, utamaduni wa jamii huweza kubadilika kutokana na maingiliano ya jamii moja na nyingine. Mnyampala katika diwani zake anathibitisha kuwa muktadha uliokuwepo wakati wa utunzi wake ulikuwa na mwingiliano wa dini za kigeni na kijadi. Vilevile wakati huo, dini za kigeni zilikuwa na mashiko zaidi kuliko dini za jadi.

Kwa upande wa *Mashairi ya Vidato*, Mnyampala anasisitiza masuala ya kumtanguliza Mungu katika kila jambo. Pia, anasisitiza wanajamii kumwomba Mungu awasaidie katika mambo mbalimbali wanayofanya katika maisha yao ya kila siku. Haya yamejidhihirisha katika shairi la “Saba-Saba” ubeti wa kumi, usemao:

22. Sabasaba yetu nia, nia idumu amani,  
Na amani ya dunia, itande ulimwenguni  
Lazima kuililia, tuzidi mwomba Manani,  
Saba ya Saba iwini, iwini kwa Sabasaba. (uk. 3)

Katika shairi hili mwandishi anasisitiza masuala ya amani na anawasihi wananchi kuomba amani wakati wa sabasaba ili Mungu adumishe amani na dunia iwe na amani. Sabasaba ilikuwa siku ambayo chama cha TANU kilizaliwa ambayo ilikuwa tarehe 7/7/1954. Vilevile, masuala ya dini yanasawiriwa katika shairi la “Kuuawa kwa Kennedy.” Katika shairi hilo Mnyampala anawasihi watu wamuombe Mungu (Maliki) amrehemu Kennedy<sup>31</sup> ambaye aliuawa kwa kuwa alikuwa kiongozi bora mpenda haki na asiyependa ubaguzi wa aina yoyote. Kiitikio cha shairi hilo katika beti zote ni “Tunakuomba Maliki<sup>32</sup>, Umrehemu Kennedy.” Kiitikio hicho kinasawiri vyema dini ya Kiislamu na Kikristo (dhehebu la Katoliki). Dini hizo zinasisitiza kuombea marehemu.

<sup>31</sup>Rais wa Marekani ambaye aliuawa tarehe 22/11/1963

<sup>32</sup> Maliki ni neno lenye asili ya Kiarabu linalomaanisha Mungu.

Kwa upande wa *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, masuala mengi yaliyozungumziwa katika ngonjera hizi ni yale yanayohusiana na muktadha wa dini za kigeni. Mfano ngonjera za “TANU na Siyasa Zake” ( uk. 7-24), “Ujamaa” (uk. 36-44) “Azimio la Arusha” (uk. 45-55) na “Uhusiano Mwema” (uk. 71- 89) kwa kiasi kikubwa zinahubiri usawa wa binadamu, ambapo katika maandiko matakatifu, masuala ya usawa wa binadamu yanasisitizwa sana. Pia kuna masuala ya umoja na ushirikiano baina ya wanajamii, ambayo pia hujitokeza katika muktadha wa vitabu vya dini.

Katika kuthibitisha hili Mnyampala katika mswada wa *Azimio la Arusha na Maandiko Matakatifu* (1968) anajadili siasa za Azimio la Arusha na ahadi za mwana TANU kwa kuhusisha maandiko matakatifu. Mnyampala anasema kuwa ahadi ya kwanza ya mwana TANU ni: binadamu wote ni ndugu zangu. Azimio la Arusha lilijengwa katika muktadha wa kijamaa ambao lengo lake lilikuwa ni kuthamini na kuwaheshimu binadamu wote. Mnyampala anabainisha haya kupitia maandiko matakatifu, *Biblia* kwa mfano kitabu cha Mwanzo kinasimulia namna Mungu alivyomuumba binadamu kwa mfano na sura yake. Mwanzo 1:26-27 inasema:

23. Mungu akasema, “Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.” Mungu akamuumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimuumba mwanamume na mwanamke aliwaumba.

Hapo inadhihirisha kuwa binadamu wote ni sawa kwa kuwa wote wameumbwa kwa mfano wa sura ya Mungu. Suala la kutambua kuwa binadamu wote ni sawa linasisitizwa na mfumo wa ujima na ujamaa pamoja na dini ya Kiislamu na Kikristo katika muktadha wa kijamii.

Kwa hiyo katika *Ngonjera za UKUTA*, muktadha uliotawala ni wa kuanzishwa kwa siasa ya ujamaa ambayo ilikuwa inahamasisha usawa kwa wote. Katika kuzungumzia masuala ya Ujamaa, kuna muktadha wa kidini unaojitokeza katika baadhi ya ngonjera. Kwa mfano, katika ngonjera ya “Viongozi Wetu” kipengele cha Zawadi Gani Tumpe? (uk. 25-27), Mnyampala anauliza zawadi ya kumpatia Mwalimu Nyerere kwa kazi nzuri aliyoifanyia nchi yake pamoja na watu wake kwa kupigania uhuru na kuondoa ubaguzi miongoni mwa wanajamii. Katika ngonjera hizo anaona zawadi ya kumpatia Nyerere ni maombi; kumuomba kwa Manani ili ampe afya njema, amani, busara, hekima, furaha, maisha marefu na ashinde majaribu ya shetani. Ngonjera nyingine ambayo Mnyampala amesawiri muktadha wa dini za kigeni inapatikana katika (uk. 92) ubeti wa mwisho unaosema:

#### 24. Hojaji

Nashukuru na kuimba, kupata hili zinduko  
Majibu umeyapamba, kila fani kwa vituo  
Nakuomba Muumba, akupe mema makuo  
Ulimwengu una nguo, kweli nami nakubali

Katika ngonjera hiyo mwandishi anamaliza kwa kumshukuru Mungu. Mwandishi kwa upande wa hojaji anamuomba mhusika mwenzake kwa kumpatia jibu la kuwa ulimwengu una nguo. Kwa ujumla, utunzi wa ngonjera umetawaliwa na dini za kigeni pamoja na msisitizo wa elimu ya kigeni katika ujenzi wa jamii mpya. Mambo mengi yaliyozungumziwa katika Siasa ya Ujamaa na TANU yamejengwa katika misingi ya dini za kigeni.

Kadhalika, katika mjadala huo tumetambua kuwa kazi nyingi za Mnyampala zilitungwa wakati dini za kigeni zimeingia na kushamiri katika jamii za Kiafrika na Mnyampala ametumia matini za kidini katika tungo zake. Kupitia muktadha huu tumebaini kuwa kuna mwingilianomatini kati ya maudhui yaliyomo katika vitabu vya

dini na ushairi wa Mnyampala. Kwa hivyo Mnyampala aliweza kusawiri vyema kipengele cha muktadha wa dini bila kubagua dini licha ya yeye kuwa Mkristo.

### 3.2.1.5 Mapenzi na Ndoa

Haya ni masuala yanayopatikana katika muktadha wa kijamii. Kwa ujumla masuala ya mapenzi na ndoa yamegubikwa na muktadha wa mgongano kati ya ukale na usasa. Kwa mfano masuala ya kuolea na kuoa, katika mila za kijadi mwanamke alikuwa anachaguliwa mume wa kumuoa. Baada ya wakoloni kuja Afrika walianza kukomesha mila hiyo kwa kuingiza mila zao za kutambua haki ya mwanamke na mwanamume, kuchagua mwenzi wa kuishi naye.

Muktadha wa mapenzi na ndoa umejitokeza katika mashairi yanayohusu masuala ya ndoa katika *Diwani ya Mnyampala, Hazina ya Washairi* na *Mahadhi ya Kiswahili*. Kwa mfano, katika *Diwani ya Mnyampala*, Mnyampala ameusawiri muktadha huu katika diwani hiyo kwa kumsifia mkewe Mary Mangwela ambaye alikuwa mshairi na jina lake la usanii alijulikana kwa lakabu ya Wastara<sup>33</sup>, na anatajwa hata katika baadhi ya kazi za Mathias Mnyampala. Hili linajitokeza pia katika Mnyampala (1965) kwenye Dibaji ya *Diwani ya Mnyampala*, pale anapoeleza kwamba “Mashairi yaliyomo kitabuni humu baadhi yake yalipewa jina la Bi. Mary Mangwela (Wastara) ambaye ni mke wangu.” Pia katika diwani hiyo kuna shairi liitwalo “Wastara Hazumbuki” (uk. 9), shairi hilo linahusu wasifu wa mkewe Mary. Shairi lingine linalohusu muktadha wa mapenzi na ndoa ni la “Mzazi Kuridhi Ndoa” (uk. 12). Katika shairi hili Mnyampala anaeleza kuwa mzazi kuridhi ndoa yalikuwa mawazo ya zamani na sasa haiwezekani, ya kale yamepita. Kwa sasa, mwanamke au binti mwenyewe ndiye anayeridhi ndoa iendeleo na akikataa ndoa haiwezi kuendelea. Hata hivyo, masuala ya kuchagua mtu wa kuolewa naye lipo chini ya binti mwenyewe,

<sup>33</sup> Mahojiano yaliofanywa baina ya mtafiti na Bi Mary Mangwela, Jijini Dodoma tarehe 27/10/2016.



hata akipingwa na wazazi wake, binti anaweza akaamua anachotaka pasipo kuwasikiliza wazazi.

Masuala ya mwanamke kuridhi ndoa yamezungumzwa pia katika *Hazina ya Washairi* katika shairi la “Mzazi Kuridhi Ndoa” la Mathias Mnyampala (uk. 35) katika majibizano na washairi wengine kuhusiana na mada hiyo. Mfano shairi la “Wawili Wapendanao” (uk. 29) lililoandikwa na Mahmoud Hamdouniy, “Nikahi Aridhi Binti” (uk. 31) la Bi Nuru, “Ndoa ya Shuruti Mbaya” (uk. 34) la Ramadhani Mwaruka, na “Ndoa Aridhi Binti” (uk. 35) la Amri Abedi, mashairi haya yana mwingilianomatini wa fani na maudhui yake. Kama asemavyo Allen (2000) kuwa hakuna matini ambayo ni asilia na ya kipekee inayojitosheleza yenyewe, bali kila matini imeundwa kwa kurejelea matini nyingine kwa kufanya udondozi, unukuzi na urejeaji wa matini zilizotangulia. Aidha, katika *Diwani ya Mnyampala* kuna uhusiano wa maudhui katika mashairi yanayohusu mapenzi na ndoa. Baadhi ya mashairi hayo ni “Hata Sheikh Ameradhi” (uk. 16), “Unyumba si Fani Moja” (uk. 40), “Pambo la Ndoa Mapenzi” (uk. 45), “Je Nafsi na Upenzi” (uk. 48) na “Ua hili Ua Gani?” (uk. 85).

Kwa hiyo katika mashairi haya, Mnyampala anazungumzia masuala ya mapenzi na ndoa, huku akitoa mawaidha juu ya ndoa, kudumisha upendo, utii, heshima na wajibu wa kila mwanandoa. Katika utunzi wa mashairi haya Mnyampala anaonekana amesawiri vyema muktadha wa kijamii unaothamini ndoa na mapenzi ya dhati kwa wanandoa. Hivyo katika mashairi hayo kuna mwingilianomatini wa mawazo ya kidini na mila na desturi za kijadi. Vilevile, mambo mengi aliyosisitiza katika ndoa yamejengwa katika muktadha wa dini ya Kikristo na Kiislamu.

Katika mswada wa *Mahadhi ya Kiswahili*, nyimbo zilizotungwa na Mnyampala zimeegemea katika muktadha wa mapenzi na ndoa. Masuala hayo yalitokana na

nyimbo nyingi zilizokuwapo katika kipindi hicho ambazo ziligusia masuala ya mapenzi na ndoa. Vilevile, baadhi ya nyimbo alizokusanya Mnyampala pamoja na zile alizotunga zinahusu muktadha wa kijamii hasa masuala ya mapenzi na ndoa kama yalivyodhihirika katika jamii yake. Genette (1997) anaeleza kuwa matini za fasihi huchota, hunukuu, hugeza, huiga kwa namna ya kubeza au hurejelea kwa njia moja au nyingine matini za fasihi. Hivyo nyimbo nyingi zilizokuwapo kipindi hicho zilitokana na muktadha wa kijamii uliohusu masuala ya mapenzi na ndoa.

Mnyampala amegusia pia masuala ya mapenzi na ndoa katika mswada wa *Mashairi ya Vidato na Ngonjera za UKUTANA*. 1. Katika *Mashairi ya Vidato* muktadha wa mapenzi na ndoa umejitokeza katika Shairi la “Uaminifu” ubeti wa tatu, unaoeleza kuwa:

25. Mke mwema usikose, mtii mwenye heshima,  
Na amri afuase, akulee kama mama,  
Kama macho aepese, huko afanye dhuluma,  
Japo unatunzwa vema, haja kubwa uaminifu.

Katika shairi hilo mwandishi anaeleza sifa za mke mwema kuwa ni yule mwenye utii na heshima, mwenye kufuata amri za mwanamume na mwenye kuchukua nafasi ya mama kwa mwanamume kwa kumlea vizuri. Masuala hayo yanasisitizwa pia katika maandiko matakatifu, mfano Waefeso 5: 22-24 inasisitiza wanawake kuwatii waume zao nao waume wawapende wake zao.

Kwa upande wa *Ngonjera za UKUTANA*. 1, katika ngonjera ya “Utamaduni ni Kitu Gani?” (uk. 59), ubeti wa tisa, Mnyampala anaelezea ndoa za kijadi au kimila kuwa ni zile zilizosherehekewa nyumbani na zilizotunzwa kikabila. Ndoa za jadi zilijali uzazi na kuwepo kwa heshima iliyotumika zamani kwa kufuata mila na desturi za jamii husika. Mawazo haya ya Mnyampala yamejengwa katika muktadha wa mawazo ya

utamaduni wa kijadi ambao ulithaminiwa katika kipindi cha kabla ya uhuru na miaka hiyo ya 1960. Wakati huo mwanamke alionekana kiumbe duni ambaye anatakiwa kufuata na kutii sheria na mawazo ya mwanaume na hakuwa na uwezo wa kufanya jambo lolote bila ya kumhusisha mwanamume. Hii ni tofauti na nyakati hizi, ambapo wanawake wanaweza kufanya mambo yao hata bila ya kuwashirikisha waume zao. Senkoro (1988) akieleza kwamba mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika mifumo mbalimbali ya uzalishaji mali katika jamii anabainisha kwamba baada ya jamii kuanza kuwa na mifumo ya kitabaka na kuanza kumiliki mali kibinafsi (kibepari), ndipo suala la kukandamizwa na kuonewa kwa mwanamke lilijitokeza. Suala hilo liliambatana na mambo ya mahari pamoja na kumuona mwanamke kuwa ni mojawapo ya milki hizo za kibinafsi. Senkoro anaeleza kuwa hali za namna hiyo hazikuwepo katika kipindi cha ujima.

Mnyampala aliwataka wanajamii kujua tamaduni njema na mbaya ili waweze kuchukua tamaduni njema na kuziendeleza na kuachana na mila ambazo hazifai. Hivyo tunaweza kueleza kuwa utunzi wa Mnyampala ulijengwa katika misingi ya dini, mwingiliano wa mila na desturi za kigeni na kijadi, na mwingiliano wa ukale na usasa. Mnyampala aliandika kwa kuzingatia zaidi usasa uliotokana na wageni. Hivyo isingekuwa rahisi kutenganisha utunzi wake na usasa uliokuwa ukijitokeza wakati huo.

### **3.2.1.6 Kushamiri kwa Matumizi ya Lugha ya Kiswahili**

Lugha ni kipengele kimojawapo cha muktadha wa kijamii. Kazi za Mathias Mnyampala kwa kiwango kikubwa ziliathiriwa na muktadha wa lugha ya taifa ya Tanzania, yaani Kiswahili. Mnyampala aliupenda utamaduni wake ikiwemo lugha yake na ya taifa lake. Kama asemavyo Abdulaziz (1969) kuwa, Mnyampala alikuwa

anakereka sana na matumizi ya lugha ya kigeni mahala ambapo hapana sababu ya kuitumia. Hivyo alipendekeza Halimashauri Kuu ya UKUTA itayarishe ‘Operation Kiswahili’. Abdulaziz anaeleza kuwa “kwa bahati mbaya ‘Operation Kiswahili’ haikufanyika katika uhai wa Mnyampala” (uk. 2). Mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na jamaa wa karibu wa Mnyampala<sup>34</sup> yanadhihirisha kuwa Mnyampala akiwa diwani aliishawishi serikali na kusababisha majina ya barabara na mitaa yaliyokuwa yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza mjini Dodoma yaondolewe na kuandikwa kwa Kiswahili. Wito huo uliitikiwa na Halmashauri ya Mji wa Dodoma ilichukua hatua ya kufuta majina mengi ya barabara na mitaa yaliyokuwa yameandikwa kwa Kiingereza na yakaandikwa kwa Kiswahili<sup>35</sup>.

Mifano ya majina ya mitaa na barabara iliyoandikwa kwa Kiswahili kutokana na ushauri wa Mnyampala ni kama: Mtaa wa Hatibu, Mtaa wa Madeneni, Mtaa wa Jamatini, Mtaa wa Nyerere, Barabara ya Sabasaba, Barabara ya Kikuyu, Barabara ya Hospitali na Barabara ya Keeka (Makaka, 2012)<sup>36</sup>. Aidha, Makaka anaeleza kuwa Mnyampala alikuwa mwendeshaji wa vipindi mbalimbali vya redio nchini Tanzania, vilivyojishughulisha na ukuzaji wa Kiswahili. Baadhi ya vipindi vilivyotangazwa katika redio hiyo vilihusu “Ngano na Ushairi, Je Hii ni Busara na Mbinu za Kiswahili.”

Kadhalika, Mnyampala alikuwa mzalendo wa kutumia lugha hiyo katika kazi zake. Kama aelezavyo Abdulaziz (1969) kuwa Mnyampala kwa upande wa lugha alikuwa anaamini kwa dhati kuwa lugha ya taifa, yaani Kiswahili, huhimili mazingira yote ya taifa. Mnyampala ameandika kazi zake kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

<sup>34</sup> Mahojiano hayo yalifanywa baina ya mtafiti na Balozi Jobu Lusinde, nyumbani kwake Kilimani, Dodoma. Tarehe 12/05/2017.

<sup>35</sup> Taarifa hizi tulizipata katika mahojiano yaliyofanyika baina ya mtafiti na jamaa wa karibu waliofanya kazi na Mathias Mnyampala kipindi cha uhai wake huko Dodoma. Tarehe 12/05/2017.

<sup>36</sup> Maelezo haya yaliyotolewa na Makaka tuliweza kuyathibitisha katika mahojiano yaliyofanyika baina ya mtafiti na watafitiwa mkoani Dodoma.

Hivyo basi, kipindi ambacho kazi za Mnyampala zinaandikwa kulikuwa na kampeni ya kueneza na kukuza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Lugha ya Kiswahili ndiyo ilikuwa ikiwaunganisha wananchi wakati wa kudai uhuru wa nchi hiyo. Kadhalika, kilikuwa kipindi cha kushamiri kwa fasihi andishi na kudumaa kwa fasihi simulizi. Rais Julius K. Nyerere pamoja na makamu wake wa pili Rashidi Mfaume Kawawa mwaka 1967 walitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa ya Tanzania. Kutokana na tamko hilo, kazi mbalimbali za kigeni zilitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na waandishi wa fasihi walihamasishwa kuandika kazi zao kwa lugha ya Kiswahili. Mathalani, Mnyampala katika *Diwani ya Mnyampala*, anahamasisha wanajamii kuenzi Kiswahili kwa kutunga shairi liitwalo, “Lugha Yetu Kiswahili” (uk. 123). Shairi hilo linaeleza umuhimu wa kuenzi na kutumia lugha za kienyeji na Kiswahili. Pia katika kitabu chake cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*, kuna shairi lake linalohusu Kiswahili linaloitwa “Johari ya Tanganyika.” Katika shairi hilo, Mnyampala anasifu washairi na lugha ya Kiswahili. Pia ni wakati huu ambapo taasisi mbalimbali zilizohusu lugha ya Kiswahili zilianzishwa, kwa mfano taasisi ya Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili mwaka 1962 na baadaye TUKI mwaka 1970, UKUTA mwaka 1967 na BAKITA mwaka 1967. Isitoshe, Mnyampala amezungumzia Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili na umuhimu wake katika kukuza lugha ya Kiswahili katika *Mashairi ya Vidato*, shairi la “Jarida la Kiswahili” (uk. 9).

Majarida na magazeti mbalimbali yalianzishwa ili waandishi waweze kuandika kazi zao na kuziweka humo ili ziweze kusomwa na wananchi. Mfano katika *Diwani ya Mnyampala* (uk. 66-69), Mnyampala ameandika mashairi yanayohusu gazeti la *Mwananchi*. Mnyampala alitunga mashairi yake kuombea gazeti hilo na kulitakia kila la kheri. Mfano wa mashairi hayo ni “*Mwananchi* Usonge Mbele” (uk. 66), “*Mwananchi* Utabalaji” (uk. 67), “*Mwananchi* Kua Salama” (uk. 68) na “*Johari*

Ninakupamba” (uk. 68). Kwa ujumla, kupitia lugha ya Kiswahili, pamoja na lugha nyingine, ushairi hutungwa, misamiati na methali huibuliwa kulingana na muktadha wa kijamii. Aidha, lugha huweza kutumiwa kutolea hotuba, maghani katika shughuli mbalimbali za kijamii na kuleta maendeleo ya nchi husika.

Japo Mnyampala alitunga mashairi kwa Kiswahili, hali ya wingi-lugha iliyoshamiri katika jamii yake ilimfanya kuingiza maneno ya kigeni katika tungo zake. Kwa hiyo, kwa kiasi fulani katika kazi zake kuna mchanganyiko wa lugha nyingine kama vile lugha za Kibantu pamoja na lugha nyingine za kigeni kama vile Kiarabu na Kiingereza. Walibora (2007) anafafanua kuwa ili kufaidi uhondo na utamu wa mashairi sharti tujitolee kuijua lugha, na si lugha ya Kiswahili tu, bali pia lugha nyingine yoyote ambayo tunataka kufurahia mashairi yake. Kutokana na kauli hiyo ni dhahiri kuwa ujuzi wa lugha mbalimbali unachangia sanaa ya utunzi kufana. Aidha, kazi za watunzi wa ushairi wa kimapokeo, akiwamo Mnyampala, walitumia lugha ya Kiswahili na hata maneno ya lugha nyingine kama vile Kiarabu kutokana na mwingiliano uliokuwepo kati ya Waswahili na Waarabu, hususani katika pwani ya Afrika Mashariki.

Ngugi (1998) anaeleza kuwa ushairi wa kimapokeo ulibeba athari nyingi sana kutoka kwa Waarabu ambao walihusiana na Waafrika kwa muda wa karne nyingi. Anaongezea kuwa athari hizo ziliingia kupitia utamaduni wao hasa katika kipengele cha dini ya Kiislamu. Waswahili walipokea utamaduni huo kupitia mashairi ya Waarabu kama vile Kaswida za dini, zilizotungwa kwa kuhusianisha mlingano wa sauti za kumalizia kwa kila msitari. Hapa inaonyesha kuwa ushairi na fasihi ya Kiarabu ilichochea Waswahili kuchukua baadhi ya mitindo ya Kiarabu na kuiboresha kwa kubuni mitindo mipya na desturi mpya katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili.

Kama wasemavyo Ngesa na wenzake (2015) kila matini huwa ni kijalizo cha matini tangulizi na hivyo basi matini mpya huigeuza kwa kiwango na kuelezea upya kauli ya asili kwa kuiambatanisha na muktadha mwingine wa kiisimu na kijamii.

Kupitia Kiswahili wananchi walijifunza siasa za nchi, maadili na utamaduni wa nchi pamoja na masuala ya uchumi wa nchi yao. Katika *Diwani ya Mnyampala*, mwandishi anajadili masuala ya lugha ya taifa na anahimiza watu waenzi na kuithamini lugha hiyo. Katika diwani hiyo mwandishi amesawiri vyema muktadha wa kijamii na kumwezesha kuandika mashairi yake kwa kuchanganya lugha. Katika mashairi yake kumekuwa na mwingiliano wa lugha. Mwingiliano huo umetokana na muktadha uliomlea na kumkuza Mnyampala. Katika baadhi ya mashairi, ametumia Kiswahili sanifu lakini katika mashairi mengine amechanganya lugha ya kawaida na Kiswahili cha zamani (lahaja ya Kiswahili) au lugha za Kibantu. Kwa mfano katika shairi la “Lugha Yetu Kiswahili” (uk. 123) mwandishi anazungumza umuhimu wa lugha ya Kiswahili na ametumia lugha sanifu. Hata hivyo, shairi la “Haiba Imepungua” (uk. 104) hali ni tofauti kama inavyodhihirika katika ubeti wa pili uonekanavyo hapa:

26. Wa Kiswahili fasihi, ofisinikatuleka,  
Fasaha iso kirihi, kinena twafarijika,  
Twampenda wetu ahi, nenda na njema baraka,  
Haiba imepungua, kwa kuondoka Dodoma.

Katika nukuu hiyo, baadhi ya maneno mwandishi hajatumia Kiswahili sanifu, mfano ‘katuleka’ katika mstari wa kwanza ni neno la kilugha ama kitarafa au Kibantu lenye maana ya ‘katuacha’. Aidha, Kiswahili cha kale kinaonekana pia katika shairi la “Yapi Yawele 1959?” (uk. 90) ambapo neno ‘watoshile’ katika ubeti wa pili lina maana wanatosha. ‘Watoshile’ ni Kiswahili cha kikale.

Vilevile, Mnyampala katika diwani hiyo amechanganya Kiswahili na Kiingereza katika baadhi ya mashairi yake. Hii inatokana na athari ya muktadha wa elimu ya kikoloni aliyoipata wakati wa kujiendeleza na mahali mbalimbali alikofanya kazi. Katika shairi la “Yapi Yawele 1959?” (uk. 91) ubeti wa saba, mwandishi ametumia neno la Kiingereza “Nominated.” Pia katika shairi la “Msaka Thani Rubiya” (uk. 133) maneno ya Kiingereza yanajitokeza kama yanavyoonekana hapa:

27. A nice melody is wine, when touches an ear,  
As entered in mine, eyes effected to ear,  
I tasted the vine, thank you my dear,  
Msaka than rubiya, kama hadha muuzeni.

Sauti nzuri ni divai, inayogusa sikio,  
Iliyoingia mwangu, macho yanaathiriwa,  
Nilijaribu divai, nakushukuru mpendwa, (tafsiri yetu)

Ubeti huu uliodondolewa hapa unatumia maneno ya Kiingereza kwa wingi zaidi. Matumizi ya maneno ya Kiingereza, Kiarabu na hata Kiebrania (mfano, pasaka) yalitokana na muktadha wa kijamii uliokuwepo wakati huo. Hii ilitokana na athari ya mfumo wa kikoloni kwa Waafrika kulazimisha matumizi ya lugha ya kigeni. Muktadha huo ulisababishwa hasa na elimu ya kikoloni pamoja na dini za kigeni.

Kadhalika, muktadha wa kushamiri kwa lugha ya Kiswahili umejitokeza katika mswada wa *Mashairi ya Vidato* katika shairi la “Jarida la Kiswahili,” katika ubeti wa nane, mtunzi anasema:

28. Kama wataka jalisi, maneno yenye murua,  
Ya lugha na ufanisi, na mbinu zake kujua,  
Hakuna lilo halisi, na mafumbo kufumbua!  
Kiongozi atatua, Jarida la Kiswahili. (uk. 9)

Ubeti huu na beti nyingine katika shairi hili zinaelezea masuala ambayo jarida la *Kiswahili* linashughulika nayo kwa lengo la kukuza lugha ya taifa. Mwandishi



anafafanua jitihada mbalimbali zinazofanywa na jarida hilo ili kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania. Katika shairi hilo, Mnyampala anasisitiza wanataaluma kukuza Kiswahili kwa kuandika makala. Vilevile, anaeleza kuwa kupitia jarida hili tunaweza kupata lugha sanifu, wahariri, mashairi, hotuba, methali na mengineyo mengi. Jarida la *Kiswahili* ndilo kongwe lililokuwepo tangu miaka ya 1930. Jarida hili lilianzishwa kwa lengo la kukuza Kiswahili. Kwa kuwa Mnyampala alifanya kazi katika Chuo cha Dar es Salaam miaka ya 1960, aliweza kulifahamu jarida hilo ndio maana aliweza kulitungia shairi hilo.

Katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, kuna muktadha wa lugha katika ngonjera za “Elimu na Utamaduni” hasa ngonjera zinazoeleza kuhusu “Kiingereza Lugha Nzuri?” (uk. 60-61). Katika shairi hili Mnyampala anaeleza kuwa utamaduni wetu uko kwenye lugha zetu za asili, hivyo ni muhimu kuthamini lugha za jamii zetu kuliko lugha ya Kiingereza. Pia anasisitiza katika beti zote kuwa lugha nzuri ni ya Kiswahili. Beti zinazomhusu Mzalendo katika (uk. 60-61), kibwagizo chake kinasema kuwa “Lugha nzuri ya kupenda, ni hii ya Kiswahili.” Hapo mwandishi anaonyesha kuwa muktadha uliokuwepo katika kipindi hicho ulikuwa wa kuhimiza matumizi ya Kiswahili na kuthamini utamaduni wa jadi na kutupilia mbali desturi za kikoloni. Wananchi kipindi hicho walikuwa wanaenzi sana utamaduni wa kikoloni na kupuuza utamaduni wa jadi. Bado ni tatizo hadi nyakati za sasa. Ni muhimu kwa jamii kutambua na kuthamini lugha za kwetu kwa kuwa utamaduni wa jamii tunaupata kupitia lugha hizo. Aidha, Kiswahili ni lugha inayokua kwa kasi na ni lugha muhimu kwa Waafrika kwa sababu ina uwezo wa kuwaunganisha Waafrika wote.

### 3.2.2 Muktradha wa Kisiasa

Kazi nyingi za ushairi alizoandika Mnyampala zimeathiriwa pia na muktadha wa kisiasa. Lasswell (1951) anaeleza kuwa siasa ni mchakato unaohusu ushawishi wa madaraka wenye kujikita katika mgawanyo wa rasilimali za nchi, na lazima mgawaji awe na madaraka yaani (nguvu za dola). Maana hii ya Lasswell imeegemea sana katika rasilimali na kuacha masuala ya siasa ya nchi na muundo wa serikali kwa ujumla, ambavyo ndio msingi wa serikali endapo kuna mamlaka ya mtu kwa watu na mengineyo. Omary (2011) anafafanua siasa kuwa ni sanaa au sayansi ya kutawala na kuongoza nchi kwa kutumia taasisi mbalimbali za serikali. Anadai kuwa katika kuongoza na kutawala, serikali hudhibiti masuala yake ya ndani na yale ya nje ili kuleta uwiano sahihi utakaofanikisha utawala na uongozi bora kwa maendeleo ya nchi husika. Mawazo ya Omary ni mazuri ila tunapingana naye anavyosema kuwa siasa ni sanaa au sayansi. Kwa ujumla siasa ni mchakato na sio sanaa wala sayansi.

Kernell na wenzake (2014) wanaeleza kuwa siasa ni mchakato ambao unawafanya watu ama kundi la watu kufikia makubaliano yaliyowekwa na kupingana na vitendo viovu visivyotarajiwa. Kutokana na mawazo ya wataalamu hao, siasa ni uchukuaji wa madaraka na utekelezaji wa mamlaka kati ya watawala na watawaliwa kwa kufuata misingi ya katiba inayowaongoza watu kwa manufaa ya watu wote. Hivyo, siasa iliyopo katika nchi husika huwa kichocheo kwa waandishi kuweza kuandika kazi zao kwa kusifia ama kukosoa siasa iliyopo. Kwa ujumla, kipindi cha miaka ya 1950 hadi 1960 kilikuwa ni kipindi cha kupigania uhuru na kujipatia uhuru. Waandishi wengi akiwemo Mnyampala wakati huo waliandika kwa kusifia siasa iliyokuwepo. Katika kujadili muktadha wa kisiasa, tumejikita katika kuangalia mambo mbalimbali yaliyojitokeza katika kazi za Mnyampala. Mambo yaliyochunguzwa ni siasa za harakati za kupigania uhuru na kipindi cha uhuru,

Ujamaa na Kujitegemea, muungano wa Tanganyika na Zanzibar na uhusiano wa mtunzi na viongozi.

### **3.2.2.1 Harakati za Kupigania Uhuru na Kipindi cha Uhuru**

Muktadha wa uhuru wa Tanganyika na nchi nyingine za Kiafrika umesawiriwa vyema katika kazi za Mathias Mnyampala. Kutokana na data tulizokusanya nyanjani, ni bayana kuwa Mnyampala alikuwa karibu na viongozi wa kisiasa na kijamii. Ukuruba wake na viongozi wa kisiasa ulimwezesha Mnyampala kujifunza itikadi za viongozi na chama tawala cha TANU. Katika mahojiano tuliyofanya baina ya mtafiti na ndugu na jamaa wa karibu inabainika kuwa, Mnyampala aliwahi kuwa diwani wa chama cha TANU mnamo mwaka wa 1967. Kutokana na uhusiano mzuri pamoja na ukuruba na viongozi, Mnyampala katika kazi zake aliweza kuwasawiri vyema viongozi wake katika mazingira ya kisiasa yaliyokuwepo wakati wa ukoloni, kupigania uhuru na uhuru. Muktadha wa kisiasa umeathiri utunzi wa mashairi ya Mnyampala kimaudhui na kifani. Wamitila (2003) anasisitiza kuwa muktadha fulani wa kisiasa huweza kuathiri kazi fulani ya fasihi sio tu katika usimulizi wa kazi hiyo bali hata katika mtindo wake kwa ujumla. Mnyampala katika kuwasawiri viongozi ametumia muktadha wa uhuru wa nchi na malengo ya uhuru katika kuelezea baadhi ya viongozi wa kisiasa na kijamii katika kazi zake. Vilevile, ameonesha namna ambavyo viongozi wanatakiwa kuwatumikia wananchi katika kuleta maendeleo kwa nchi zao, bila kuwepo na ubaguzi wowote.

Katika *Diwani ya Mnyampala*, mwandishi anaonyesha tabia ya viongozi maarufu kama vile Mwalimu Julius Nyerere na namna alivyokuwa mwadilifu katika uongozi wake. Kwa hiyo, Mnyampala anaona kuwa tabia ya mtu binafsi huweza kuwa

kielelezo kwa tabia ya mtu mwingine katika jamii husika. Haya yanajitokeza katika shairi la “Yapi Yawele 1959?” (uk. 90), ubeti wa nane usemao:

29. Madaraka mng’an’ano, pato letu lifikile,  
Za madaraka yano, si fumba la kolekole,  
Tuyahazi mfatano, bure wasione gele,  
Yaliyopita si ndwele, tugange yanayokuja.

Shairi hilo limetokana na muktadha wa kupigania uhuru chini ya chama cha TANU. Kadhalika katika shairi la “Mungu Muongoze Rubani” (uk. 137), “Ni Madaraka Kamili” (uk. 139), “Mola Dumisha Amani” (uk.141) na “Uhuru Uwe na Heri” (uk. 144) yametungwa kutokana na muktadha wa uhuru ambapo Mnyampala anamsifu Mwalimu Nyerere kwa kupigania uhuru kwa amani na anaiombea nchi ya Tanzania uhuru uwe wa amani.

Baadhi ya mashairi yaliyomo katika kazi za Mnyampala yametungwa kwa kufuata muktadha uliokuwepo wakati huo ambao ulikuwa ni muktadha wa nchi nyingi za Kiafrika kupigania na kupata uhuru kutoka kwa wakoloni. Mashairi mengine ya Mnyampala yanasawiri wakati wa ukoloni, harakati za kupigania uhuru, kipindi cha uhuru na hata baada ya uhuru. Hii ni ithibati tosha kuwa fasihi kwa kawaida inatungwa kwa kufuata muktadha uliopita au uliokuwepo na hata utarajiwao na jamii ya mtunzi.

Kadhalika, katika mswada wa *Mashairi ya Vidato* kuna mashairi yanayoelezea masuala ya uhuru, muungano, masuala ya siasa za TANU na viongozi wa kisiasa wasiopenda ubaguzi. Katika shairi la “Kuuawa Kennedy” (uk. 5) kwa mfano ubeti wa tatu unasema:

30. Rais mwenye hekima, ubaguzi hautaki,  
Waziwazi alisema, kwamba yeye hashiriki,  
Aliwapenda yatima, aliwapa zao haki,

Tunakuomba Maliki, umrehemu Kennedy.

Katika shairi hili Mnyampala anaelezea kuhusu kuuawa kwa Rais Kennedy wa nchini Marekani. Rais huyo alikuwa hapendi ubaguzi. Aliuawa tarehe 22/11/1963 huko Marekani<sup>37</sup>. Vilevile, katika shairi hilo Mnyampala anamlinganisha Rais Kennedy na Rais Nyerere kwamba ni marais waliojali usawa wa watu wote katika jamii zao. Mathalani, Rais Nyerere punde baada ya uhuru wa Tanganyika, alitaka wananchi kuishi maisha yenye usawa kupitia chama cha TANU na Ujamaa na Kujitegemea.

Inadhihirika pia kwamba, Mnyampala ameelezea muktadha wa uhuru kupitia shairi la “Kitung’ati” (uk. 7), ambapo katika shairi hilo anamwelezea mtu shujaa wa majeshi ambaye akiwa vitani hakuna wa kumshinda. Hapa anazungumzia wakati Rais Julius Kambarage Nyerere alipoongoza taifa la Tanzania hadi likapata uhuru pasi na kumwaga damu. Aidha, Nyerere anaelezwa kuwa kiongozi asiyependa ubaguzi na aliyesisitiza usawa wa binadamu ndani ya nchi ya Tanzania. Nyerere ni kiongozi aliyewajenga watu katika umoja na kufanya kazi kwa bidii ili kuleta maendeleo ya nchi yao. Masuala haya yalihimizwa sana miaka ya 1960 mara baada ya kupata uhuru na muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Kwa upande wa *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, muktadha wa kisiasa hasa masuala ya uhuru wa nchi unajitokeza vyema kupitia viongozi wake. Mnyampala anamsifu Mwalimu Julius K. Nyerere katika ngonjera za “Viongozi Wetu” (uk. 25-35). Anadai kuwa ndiye aliyeleta uhuru, muungano, usawa wa watu wote, siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na kuwafanya watu wapende utamaduni wao. Kwa ujumla, Mnyampala aliandika kazi zake kwa kusawiri hali mbalimbali zilizopita, zilizokuwepo na zilizokuwa zinategemewa kuwapo nyakati hizo hasa kuhusiana na wasifu wa Baba wa

<sup>37</sup>Taarifa hizi tumezitoa katika <https://www.google.com/search?source=hp&ei=WMoGW8HDKsbkvgSO2aagDA&q=the+death+of+president+kennedy&oq> tarehe 22/5/2018.

Taifa, viongozi wengine wa serikali na nchi yake. Mnyampala alizitungia mashairi kauli mbalimbali zilizotolewa na viongozi wa kisiasa na kutangaza siasa hizo ili kutoa elimu kwa jamii kupitia tungo zake.

Katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, mwandishi ameathiriwa na muktadha wa kisiasa hasa siasa za TANU na Azimio la Arusha. Nyerere (1967) anaeleza kuwa Azimio la Arusha limekusudia kuleta maisha bora kwa Watanzania, kwa kuwa binadamu wote ni sawa na hakuna mwenye haki na mamlaka ya kumnyonya mwingine. Usawa wa binadamu ndio ulikuwa mhimili wa siasa za Azimio la Arusha. Mnyampala katika muktadha huu, amezungumzia sana masuala ya haki sawa, usawa wa binadamu na masuala ya umoja na mshikamano katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya kijamii.

Kwa ujumla, Mnyampala alijiegemeza katika muktadha unaohusu sera za TANU, kipindi cha kupigania uhuru na wakati wa uhuru. Washairi wengine wa kipindi hicho walioandika kazi zao kwa kuzingatia muktadha wa kisiasa ni Shaaban Robert na Saadan Kandoro. Wao waliandika mashairi ya kuhamasisha watu kupigania uhuru (Kezilahabi, 1973; Biersteker, 1996 na Kitogo, 2001). Kitogo (2001) anathibitisha hilo anaposema kuwa washairi mbalimbali kama vile Saadan Kandoro wana mchango mkubwa katika kukuza na kueneza siasa nchini Tanzania. Baada ya kuanzisha Azimio la Arusha waandishi wengi walilieleza Azimio la Arusha kama chombo kilichosaidia kupunguza tofauti za kisiasa, kijamii na kiuchumi pamoja na kupunguza matabaka katika jamii. Baadhi ya wataalam na watunzi waliounga mkono sera ya Ujamaa na Kujitegemea iliyokuwa ndani ya siasa ya Azimio la Arusha ni Kandoro (taz. 1972, 1978). Kwa hiyo Mnyampala kama mwanafasihi alichota malighafi ya kazi zake kutokana na muktadha wa kisiasa kama unavyodhihirika katika tungo zake.

### 3.2.2.2 Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea

Ujamaa na Kujitegemea ni muktadha wa kisiasa uliotumika katika kazi za Mnyampala. Muktadha huu umejitokeza vyema katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* na umesawiriwa kwa kiasi kidogo katika mswada wa *Mashairi ya Vidato*. *Mashairi ya Vidato* ni mswada ulioandikwa kipindi cha vuguvugu la siasa ya Ujamaa ambayo ilikuwa ikienezwa chini ya mwamvuli wa Azimio la Arusha. Azimio hili lilianzishwa mwaka 1967 chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Azimio la Arusha lilikusudia kuleta haki sawa kwa wote pamoja na kuinua uchumi wa nchi na wanajamii kwa ujumla.

Katika mswada wa *Mashairi ya Vidato*, Mnyampala anasisitiza kuheshimu na kulinda siasa za ujamaa. Kwa hiyo mashairi yaliyomo katika mswada wa *Mashairi ya Vidato* yanahusu muktadha wa Ujamaa na Kujitegemea. Mfano wa mashairi yaliyogusia masuala ya Ujamaa ni shairi la “Saba-Saba” (uk. 3), “Tanzania ya Amani” (uk. 9), na “Uaminifu” (uk. 1). Mfano shairi la “Uaminifu” linaeleza kuhusu siasa ya Ujamaa na Kujitegemea kama vile kuepuka misaada inayovunja siasa za nchi zinazoendelea ama zilizotoka kupata uhuru. Aidha, katika shairi la “Kitung’ati<sup>38</sup>” (uk. 7) Mnyampala anaeleza jinsi baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alivyokuwa anatangaza siasa za ujamaa. Masuala haya yanajitokeza waziwazi kupitia ubeti wa sita. Mwandishi anasema:

31. Nguvu-moja ndiyo haja, siasa ya Ujamaa,  
Sawa sawa wote waja, tabaka moja kukaa,  
Kazi-yetu ni kuchuja, na kupunguza tamaa,  
Kama alivyoandaa, Mwalimu wa KITUNG’ATI. ( uk. 7)

<sup>38</sup> Kitung’ati ni mtu shujaa sana mwenye elimu ya kuongoza majeshi yake, mwenye shabaha na hatimaye kufaulu katika vita. Mtu huyo akipangiwa jambo wafuasi wake wanaamini kuwa bila shaka watafaulu tu, na kwa kweli wanafaulu (Mnyampala, 1967).

Hapo mwandishi anazungumzia sera za siasa ya ujamaa inayosisitiza usawa wa binadamu, kuondoa matabaka katika jamii, kuchukua mambo mazuri yanayoleta maendeleo katika nchi na kupunguza tamaa ya vitu mbalimbali vinavyodidimiza uchumi wa nchi. Kadhalika, Mnyampala katika ubeti wa saba anazungumzia masuala ya kujitegemea na anasisitiza watu kufanya kazi kwa nguvu na kuleta maendeleo ya nchi na jamii kwa ujumla. Katika sera ya Ujamaa, Mwalimu Nyerere alikuwa mstari wa mbele katika kupigana na adui watatu ambao ni ujinga, maradhi na umaskini. Hili linabainishwa katika ubeti wa kumi usemao:

32. Nguvu-moja kusimama, adui zetu kushinda,  
 Adui watatu kama, wanenepe waliokonda,  
 Kazi-yetu kuwachoma, tupige na kuwaponda,  
 Kama anavyopenda, Mtukufu KITUNG'ATI. (uk. 7)

Katika ubeti huu Mnyampala anaeleza kwamba Rais Nyerere alikuwa anawataka wananchi kushirikiana katika kupambana na maadui watatu. Mnyampala hapa anasisitiza zaidi muktadha wa sera zilizokuwepo ili jamii yote ipambane na kwa umoja kuondoa umaskini, maradhi na ubaguzi.

Muktadha wa Ujamaa na Kujitegemea unajitokeza pia katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* katika ngonjera za “Utukufu wa Taifa” (uk. 12-18). Ngonjera hizo zinafafanua maadui watatu ambao ni ujinga, umaskini na maradhi. Kwa ujumla, *Ngonjera za UKUTA Na. 1* na 2, zilitungwa kipindi cha Azimio la Arusha na kuchapwa mwaka 1970 na 1971. Mwandishi ametunga mashairi yake kwa kuegemea katika muktadha wa kisiasa, hususani Siasa za TANU (chama kilichoanzishwa mwaka 1954) na Azimio la Arusha lililoanzishwa mwaka 1967. Hivyo mbinu za utunzi zilizomo katika vitabu hivyo zimekitwa katika muktadha wa siasa za Ujamaa na Kujitegemea. Muktadha huo ndio uliofufua mtindo huu wa mashairi ya ngonjera kwa lengo la kuwezesha wanafunzi na jamii kwa ujumla kufahamu siasa iliyokuwepo katika muktadha huo kwa namna ya uigizaji wa vitendo halisi. Nyerere ndiye alitoa rai kwa



waandishi kutunga kazi za fasihi zinazotangaza sera ya Azimio la Arusha ili jamii iweze kuelewa sera hiyo vizuri. Kama aelezavyo Mnyampala (1971:3) katika dibaji yake kuwa fani ya ngonjera ilipatiwa msukumo kwa mara ya kwanza na Mwalimu Nyerere, kama aelezavyo hapa:

33. Ngonjera hizi nimezitunga kwa ajili ya Azimio la Arusha ili lipate kutangazwa zaidi kwa njia hii na, hasa kwa ajili ya kutekeleza maagizo ya Mtukufu Mwalimu Julius K. Nyerere aliyotuagiza wakati alipotwita washairi wote wa Kiswahili, tukaonana naye Ikulu tarehe 6 Juni, 1968. Siku hiyo Mwalimu alisema, “Tangazeni Azimio la Arusha, na kutukuza Utamaduni wa Taifa letu.”

Kutokana na maneno hayo washairi wengi, akiwemo Mnyampala, waliandika kazi zao kwa kuegemea katika muktadha wa Ujamaa na Kujitegemea na kutukuza utamaduni wa taifa la Tanzania kwa dhati. Kutokana na maelezo ya Mnyampala tunaweza kusema kuwa lisingelikuwepo Azimio la Arusha, labda hata fani ya ngonjera ingelikuwa bado imefifia. Aidha, ngonjera zilipata umbo jipya kutokana na mabadiliko ya kijamii na kisiasa yaliyokuwepo wakati huo. Alfaro (1996) anaeleza kuwa matini hupata umbo jipya kutokana na marudio pamoja na mabadiliko ya matini nyingine zilizotumika ndani ya matini hiyo na kuipa matini ya awali upya zaidi kulingana na muktadha uliopo katika jamii wakati huo. Hili tunalionga katika kazi za Mnyampala ambapo muktadha wa kijamii na kisiasa ulimsaidia mwandishi huyu kufufua mitindo iliyosahaulika kama vile ngonjera na mashairi ya vidato ili kuelimisha jamii kuhusu masuala ya siasa za nchi ya Tanzania.

### **3.2.2.3 Muunganowa Tanganyika na Zanzibar**

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulifanyika tarehe 26/04/1964. Tukio hili lilifanyika baada ya kupata uhuru kutoka kwa wakoloni ambao walitawala miaka mingi katika nchi ya Tanganyika na Zanzibar. Kipindi cha muungano ni mojawapo ya

muktadha ulioathiri utunzi wa Mnyampala. Hivyo, kutokana na hali hiyo waandishi wengi wa kipindi hicho waliandika kazi zao wakigusia masuala ya muungano kwa kuwa ndilo jambo lililokuwa linavuma wakati huo. Mnyampala kama mmoja wa waandishi mashuhuri naye aliathiriwa na muktadha huo. Hivyo katika mashairi yake kuna mashairi yanayozungumzia masuala ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Katika *Diwani ya Mnyampala* shairi la “Muungano Utupambe” (uk. 147), Mnyampala anaomba Mungu muungano uwe wa amani na kushirikiana kwa pamoja bila kuwepo na mikwaruzo wala vita baina ya nchi hizo.

Aidha, mswada wa *Mashairi ya Vidato* shairi la “Tanzania ya Amani” (uk. 9), linazungumzia masuala ya muungano. Shairi hili liliandikwa tarehe 10/07/1966 baada ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ulikuwa tarehe 26/04/1964. Ubeti wa sita wa shairi hilo unasema:

34. Tuliungana pamoja, wa visiwani na bara,  
Tanganyika na Unguja, Mwingano wetu imara,  
Lakini wao wangoja, hadi waende ahera,  
Hebu itie fikira, na yetu vinafanana? (uk. 9)

Mwandishi katika ubeti huo anasawiri muktadha wa muungano wa bara na visiwani na anaeleza kuwa muungano uliopo ni imara na unapaswa kuheshimiwa. Mnyampala anaeleza kuwa wengine wanatamani kuungana lakini wanashindwa kwa sababu ya kukosa mwelekeo. Pia, muktadha wa muungano umezungumziwa katika shairi la “Kitung’ati” (uk. 7) ubeti wa tano, mtunzi anaeleza kuwa:

35. Nguvu-moja ya kukata, ya Tanzania mirija,  
Tukate bila kusita, tangu bara na Unguja,  
Kazi-yetu ni kupata, pato letu la pamoja!  
Kawa alivyoitaja, mtukufu wa KITUNG’ATI.

Katika ubeti huu mwandishi anaonyesha muktadha wa muungano kwa kuelezea malengo ya muungano. Malengo yake yangehakikisha kuwepo kwa pato la pamoja, kuondoa ubaguzi na kuwa na nguvu moja katika kuimarisha uchumi wa muungano wa Jamhuri ya Tanzania. Kutokana na mashairi hayo ni dhahiri kuwa waandishi hutunga kazi zao kwa kuzingatia muktadha husika. Watunzi wa fasihi huchota maudhui yaliyomo katika jamii na kuyaweka katika sanaa kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusiana na mambo yanayoendelea katika jamii. Mambo hayo huwasilishwa kisanaa kiasi kwamba hadhira inaelimishwa na wakati huohuo inapata burudani.

Aidha, muktadha huu wa muungano pia umesawiriwa katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, mfano ngonjera ya “Sikukuu ya Muungano” (uk. 66-67). Ngonjera hii inaonesha mwananchi na mwanasiasa. Mwananchi anauliza swali kuhusu sikukuu ya muungano kuwa ni kitu gani? na iliundwa Tanzania kwa nini? Mwanasiasa anatoa jibu kuwa muungano ni siku mashuhuri na ya kujivunia nchini Tanzania ambayo iliunganisha Unguja na Bara na kuunda Tanzania. Hapa mwandishi alikuwa anatoa ufafanuzi kwa jamii hasa kwa wale ambao hawajui muungano ni kitu gani, pia inadhihirisha kuwa kilikuwa ni kipindi cha kutoa elimu kwa wananchi juu ya muungano na faida zake.

#### **3.2.2.4 Mtunzi kuwa na Uhusiano wa Karibu na Wanasiasa**

Mnyampala alikuwa na uhusiano wa karibu na viongozi wakuu wa nchi yake. Data tulizopata katika mahojiano na hata kutoka maktabani ni dhahiri kuwa Mnyampala alikuwa karibu sana na viongozi wa kisiasa. Mnyampala katika upande wa siasa alihusiana na viongozi mbalimbali wa dini na madhehebu tofauti. Kwa mfano, alikuwa na mahusiano ya karibu na Kaluta Amri Abedi ambaye alikuwa rafiki yake kipenzi, huyu alikuwa Mwislamu. Hayati Mwalimu Julius Nyerere (Mkatoliki),

Marehemu Rashid Mfalame Kawawa (Mwislamu) na Balozi Jobu Lusinde (Mwanglikana). Mnyampala alishirikiana na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Kaluta Amri Abedi katika kitabu chake cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* na Kaluta Amri Abedi alishirikiana naye katika mswada wa *Hazina ya Washairi*.


Kutokana na ukaribu huo, aliandika kazi zake akisifia siasa za nchi yake pamoja na viongozi wake. Hii inaweza kuwa sababu ya yeye kutunga kazi zake nyingi akielezea viongozi na sifa za viongozi bora. Aidha, katika tungo zake nyingi kipengele cha ‘Utangulizi’ wa kazi zake mara nyingi kiliandikwa na viongozi. Kama tuonavyo katika jedwali namba 1.

**Jedwali Namba 1: Viongozi walioandika utangulizi/dibaji ya kazi za Mnyampala**

<b>Kazi ya Fasihi</b>	<b>Mwandishi wa Dibaji/Utangulizi</b>	<b>Cheo/Wadhifa</b>
<i>Waadhi wa Ushairi</i>	Kaluta Amri Abedi	Waziri wa Maendeleo na Utamaduni
<i>Ngonjera za UKUTA Na. 1 na 2</i>	Rashidi M. Kawawa	Makamu wa Pili wa Rais Tanzania
<i>Ufasaha wa Kiswahili Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi</i>	Elifoo Mgonja Mwl. Julius K. Nyerere	Waziri wa Elimu Rais wa Tanzania
<i>Mswada wa Azimio la Arusha na Maandiko Matakatifu</i>	Mwl. Julius K. Nyerere	Rais wa Tanzania

Kwa mfano, katika *Waadhi wa Ushairi* (1965), utangulizi wake uliandikwa na Kaluta Amri Abedi ambaye alikuwa Waziri wa Maendeleo na Utamaduni na alikuwa rafiki

yake wa karibu sana (Mnyampala, 2011)<sup>39</sup>. Pia, katika nyaraka zake tuliweza kupata barua nyingi ambazo aliweza kuwaandikia viongozi kuhusiana na kazi zake alizokuwa ameandika, akiomba wamsomee na/au wamuandikie utangulizi wa miswada yake. Haya tunayaona kwenye barua iliyoandikwa na Rais wa Taifa la Tanzania hapa chini.



Picha namba 4: Barua iliyoandikwa na Mwalimu Julius Nyerere kumjibu Mnyampala (tarehe 3/11/2016).

<sup>39</sup>Vilevile katika mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na mtoto wa Amri Abedi pamoja na Hamsini Mubiru walieleza kuwa Mnyampala alikuwa rafiki wa karibu sana na Kaluta Amri Abedi.

Kutokana na barua hii ni dhahiri kuwa Mnyampala alikuwa karibu na viongozi wa wakati huo. Hii ndio maana katika kazi zake alizoziandika alipenda viongozi hao wamuandikie utangulizi wa kazi zake ili ziweze kukubalika katika jamii. Kutokana na ukaribu aliokuwa nao na viongozi hao, Mnyampala alipata nafasi ya kuwafahamu viongozi mbalimbali pamoja na mienendo yao. Hali hiyo iliathiri maudhui ya kazi zake ambapo kila mara aliweza kuzungumzia masuala ya viongozi na sifa za viongozi wake pasipo kukosoa.

Kwa mfano, katika *Diwani ya Mnyampala* mwandishi amewazungumzia viongozi na sifa zao. Katika mashairi ya “Mungu Mwongoze Rubani” (uk. 137), “Ni Madaraka Kamili” (uk.139), “Tuongoze kwa Mteremo” (uk. 143) na mengineyo yanayohusu viongozi, Mnyampala anamzungumzia Baba wa Taifa la Tanzania, Mwalimu Julius K. Nyerere ambaye aliweza kuhamasisha watu kudai uhuru kwa amani. Aidha, mashairi hayo yanahusu muktadha wa viongozi kudai uhuru na wakati wa uhuru. Mnyampala alitunga mashairi haya kwa lengo la kumuomba Nyerere na viongozi wengine pamoja na kumshukuru Nyerere na kumsifu kwa kuongoza vizuri wananchi katika kipindi hicho cha harakati za uhuru hadi ukapatikana.

Sambamba na hilo, mswada wa *Mashairi ya Vidato* umeathiriwa na muktadha huo. Kuna baadhi ya mashairi yanayoeleza namna kiongozi anavyotakiwa awe, mfano huo tunaupata katika shairi la “Kuuawa Kennedy” (uk. 5). Katika shairi hilo kuna mwingilianomatini wa maudhui, ambapo katika shairi hilo mtunzi amechukua mfano wa Rais wa Marekani aliyeuawa na Wamarekani kwa sababu alikuwa mtu asiyependa ubaguzi wa aina yoyote katika nchi yake. Mwandishi ametumia mfano huo kuelezea masuala ya uzalendo wa viongozi katika nchi zinazoendelea ambao huwapenda watu wote bila kuwepo kwa ubaguzi wa rangi, kabila, siasa na hata maeneo ya kijiografia. Mwandishi anaeleza kuwa kuna viongozi wachache sana katika dunia hii wenye sifa

na tabia kama hizo. Mwandishi ameyaonyesha haya, hasa katika ubeti wa kwanza na wa sita, anaposema:

36. Chama hakina salama, na kidumu vema hiki,  
 Hupata nyingi zahama, kwa shabuka na mikiki,  
 Waovu hukisukuma, kwa teke hawakitaki,  
 Tunakuomba maliki, umrehemu Kennedy. (ubeti wa kwanza, uk. 5)  
 Yuko wapi mahatma, wa India Mashariki?  
 Ijapokuwa alisimama, hadi kujitia dhiki,  
 Hakuambua la wema, kauawa kwa hamaki,  
 Tunakuomba Maliki, Umrehemu Kennedy. (ubeti wa sita, uk. 5)

Hapo mwandishi anaeleza kuwa viongozi wenye maadili, yaani wenye kupenda kusaidia yatima na kujali watu wengine, mara nyingi hupingwa na mataifa yaliyoendelea. Kwa mfano katika Afrika viongozi wanaokumbukwa kwa juhudi zao za kuweka maslahi mbele ya umma ni kama vile: Hayati Nelson Mandela wa Afrika Kusini, Patrice Emery Lumumba wa DRC au Jamhuri ya Kongo na Mwalimu Julius K. Nyerere wa Tanzania.

Kadhalika, katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, kuna muktadha unaosawiri ukaribu wa mwandishi na viongozi wake, katika ngonjera ya “Viongozi Wetu” (uk.25-35), mwandishi anawaongelea viongozi wa taifa la Tanzania, hususani Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Makamu wa Kwanza wa Rais Sheikh Abedi Karume (uk. 28-29). Mnyampala anamuelezea Karume kuwa alikuwa kiongozi wa Afro-Shirazi Party, aliyewaongoza wananchi wa Zanzibar kumfukuza Sulutani mwaka 1964 na kukubali kuunda muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar. Vilevile, amemzungumzia Makamu wa Pili wa Rais ambaye ni Rashidi Kawawa katika (uk. 29-30), na kumwita Simba wa Vita. Kawawa kupewa lakabu ya Simba wa Vita ni ishara ya mwingilianomatini baina ya fasihi na dini ya Kikristo ambapo katika *Biblia Takatifu*, Yesu anaitwa Simba wa Yuda. Yesu aliitwa hivyo kwa sababu alikuwa na

uwezo wa kufanya mambo ambayo ni ya kishujaa kama vile kutuliza dhoruba baharini (Luka 8: 22-25). Kawawa aliitwa hivyo kwa kuwa alipambana kwa bidii na ushujaa katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mnyampala katika ngonjera hii anawaongelea Nyerere, Karume na Kawawa, mawaziri na wabunge. Lengo la kuwaelezea ni kutaka wananchi wawafahamu vizuri viongozi wao pamoja na wajibu wao katika taifa la Tanzania. Aidha, Mnyampala na washairi wengine wa kipindi hicho walifanyia kazi kila kilichoelezwa na viongozi wa nchi pasi kufanya uchambuzi yakinifu. Ukweli ni kwamba kipindi hicho waandishi wengi hawakuwa na elimu ya kutosha ya kuchambua na kuhakiki masuala mbalimbali yanayotokea katika jamii.

Kwa ujumla muktadha wa kisiasa umejitokeza vyema katika kazi za Mnyampala. Mnyampala kwa kiasi fulani alikuwa mtunzi mwanasiasa aliyeweza kutunga kazi zake kisanii ili kueleza viongozi na siasa za nchi yake. Kutokana na mjadala wetu tunaweza kusema kuwa Mnyampala aliandika kazi zake kuhusiana na siasa na dini. Katika muktadha huu tumejadili vipengele mbalimbali vya kisiasa kama vile harakati za kupigania uhuru na kipindi cha uhuru, siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, muungano wa Tanganyika na Zanzibar na uhusiano wa mtunzi na viongozi mbalimbali. Ni dhahiri kwamba Mnyampala aliathiriwa sana na muktadha wa kisiasa katika utunzi wa kazi zake za ushairi.

### **3.2.3 Muktadha wa Kiuchumi**

Kwa mujibu wa data za utafiti huu, muktadha wa kiuchumi umesawiriwa vyema katika kazi teule za Mathias Mnyampala. Nchi ya Tanzania ni mfano mzuri wa nchi za ulimwengu wa dunia ya tatu, ambapo watu wake ni maskini. Kwa mujibu wa takwimu za kiuchumi Mtanzania wa kawaida huishi chini ya kiwango cha wastani wa dola moja kwa siku. Mazingira haya yameweza kuchochea waandishi mbalimbali



kuandika kazi zao kwa kuzungumzia masuala ya uchumi wa nchi ili kutafuta njia za kuinua uchumi huo.

Kutokana na hali mbaya ya uchumi iliyokuwepo kipindi cha miaka ya 1960, ambayo ilisababishwa na athari ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia na kujitawala kwa Waafrika, Mnyampala anatoa mawaidha ili kuinua uchumi wa nchi na wanajamii. Kwa hiyo muktadha wa uchumi uliokuwepo kipindi hicho umekuwa na mchango mkubwa katika uandishi wa kazi za Mnyampala kwa kiasi kikubwa. Muktadha wa uchumi unahusisha masuala ya uchumi wa Kisoshalisti, utafishaji wa mali na ujenzi wa jamii mpya.

### **3.2.3.1 Uchumi wa Kisoshalisti**

Uchumi wa Kisoshalisti unahusu ujamaa na namna ya mgawanyo wa mali. Baada ya uhuru Tanzania ilikuwa inafuata mfumo huu wa kiuchumi. Mwandishi anayetumia muktadha huu mara nyingi kusudi lake ni kuwataka wananchi kufanya kazi kwa ushirikiano na kufaidi matunda ya kazi au uchumi wa nchi pamoja. Kazi ni mojawapo ya mambo yaliyozungumziwa na ushairi wa Mnyampala. Kazi zinazozungumziwa katika vitabu hivi teule ni za kilimo na huduma za maofisini. Mnyampala katika maandiko yake ametumia muktadha wa uchumi wa kisoshalisti katika kuelimisha jamii kujituma na kuwajibika katika shughuli mbalimbali kwa lengo la kujipatia kipato na kuinua uchumi wa Taifa la Tanzania. Kwa ujumla, Mnyampala alitambua kuwa kazi ndiyo ingefanya maisha yavutie kwani kila mafanikio ya mwanadamu hutokana na kufanya kazi kwa bidii na maarifa. Hii ilitokana na muktadha wa kipindi hicho ambacho msisitizo mkubwa ulikuwa katika kazi za kilimo na kwa wasomi kufanya kazi za maofisini au viwandani.

Waandishi wengi waliokuwepo kipindi hicho waliandika kazi zao wakisisitiza masuala ya kilimo kama nguzo ya kuleta maendeleo ya nchi. Hali hiyo iliwafanya waandishi wengi wa kipindi hicho, akiwemo Mnyampala, kuzungumzia zaidi masuala ya kilimo kuliko kazi zingine. Mfano katika *Diwani ya Mnyampala* mashairi kama vile: “Jembe Huleta Halasa” (uk. 57), “Fadhila ya Mkulima” (uk. 58), na “Tenda Tendo la Kulima” (uk. 75), yalidhihirisha waziwazi mazingira ya kilimo. Vilevile, kuna mashairi mengine yaliyotokana na muktadha wa dini, siasa na uchumi kwa kugusia muktadha wa kilimo ndani yake.

Aidha, Mnyampala anazungumzia pia masuala ya kazi za maofisini katika diwani hiyo katika shairi la “Watumishi Tushikamane” (uk. 43), ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Katika ubeti huo anahamasisha wafanyakazi kudai na kuongezewa mishahara. Hapa tunapata muktadha wa ukinzani katika malipo baina ya watumishi na mwajiri. Katika shairi hili Mnyampala anataka kupandishwa mishahara badala ya kupambana na mfumo wa kitabaka uliokuwepo. Anaona kwamba mishahara mdogo ni sawa na mabaki ya wakoloni. Muktadha huu umejitokeza pia katika kitabu chake cha *Maisha Kugharimia* (uk. 68) ambapo ameeleza kuwa alipotaka kurudishwa kazini katika hazina ya wenyeji aliuliza kuhusu mishahara, alivyoambiwa ataanza na mishahara wa chini aliamua kutorudi kazini.

Masuala hayo ya kazi pia yamezungumziwa katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*. Katika *Ngongera za UKUTA Na. 1*, Mnyampala amezungumzia pia muktadha wa uchumi wa taifa, kwa kuwataka watu wafanye kazi kwa bidii. Kwa ujumla *Ngonjera za UKUTANA.1* zilitokana na muktadha wa uchumi wa nchi kupitia Azimio la Arusha, mfano ngonjera ya “Tanu<sup>40</sup> na siasa yake” (uk. 7-24). Muktadha huu unajitokeza pia katika masuala ya kujitegemea na kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kuleta

---

<sup>40</sup> TANU ni chama cha wakulima na wafanyakazi kilichopigania uhuru wa Tanzania miaka ya 1950.

maendeleo ya nchi. Ujamaa na Azimio la Arusha (uk. 36-55) ni mambo yanayoendana na muktadha wa kazi. Mnyampala alisisitiza wanajamii kufanya kazi kwa bidii ili kutokomeza umaskini uliopo ndani ya nchi.

Kwa ujumla, masuala ya uchumi yalielekezwa zaidi katika siasa za Azimio la Arusha ambazo Mnyampala alizieleza katika *Ngonjera za UKUTA Na 1*. Kimsingi kusudi la azimio hilo lilikuwa kuwahamasisha watu kufanya kazi za mashambani na maofisini kwa bidii ili taifa liweze kujitegemea. Mnyampala pia amezungumzia masuala ya maliasili za jamii kama vile mbuga za wanyama na kuhimiza jamii kutunza na kuwalinda wanyama waliopo katika jamii.

Vilevile, katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, Mnyampala anaeleza kuwa mikopo kwa nchi zinazoendelea ni kikwazo katika maendeleo ya nchi hizo. Masuala ya mkopo ameyazungumza katika ngonjera ya “Mkopo wa Fedha” (uk. 22-24). Aidha, katika sehemu ya utangulizi wake anaeleza kuwa: “Azimio la Arusha linasema ‘Kujitawala kwa kweli hakuwezekani ikiwa taifa moja linategemea misaada na mikopo ya taifa jingine kwa maendeleo yake’ hivyohivyo haifai binadamu kutegemea mikopo kutoka kwa binadamu mwingine kwa maendeleo au haja zake” (uk. 22).

Katika dondoo hilo muktadha wa kishoshalisti umejitokeza katika mawazo ya mwandishi aliyetaka kila mtu afanye kazi kwa bidii na kupata kipato chake bila kutegemea mikopo kutoka kwa wengine ili kuinua uchumi wa nchi na jamii kwa ujumla. Ngonjera zilizopo katika sehemu hiyo ya “Mkopo na Fedha,” zinaeleza masharti mbalimbali yanayotolewa wakati mkopaji anataka kukopa fedha kwa mwenye pesa ama tajiri. Ngonjera hizo zilitungwa katika muktadha ambao kulikuwa na uhamasishaji katika nchi kufanya kazi kwa bidii ili kujitegemea bila kutegemea misaada kutoka nje. Kipindi hicho kilikuwa cha Ujamaa na Kujitegemea chini ya

Azimio la Arusha. Kwa ujumla ngonjera zilizomo katika kitabu hiki ziliandikwa katika kipindi cha Azimio la Arusha ambalo lilikuwa linahimiza kuinua uchumi wa nchi ya Tanzania kupitia siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, Vijiji vya Ujamaa na Elimu ya Kujitegemea na mengineyo yaliyokuwepo kipindi hicho.

Aidha, katika *Mashairi ya Vidato* shairi la “Kitung’ati” (uk. 7), linarejelea kauli za Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere zinazohusu umuhimu wa kilimo. Mnyampala anaeleza kauli hizo katika ubeti wa tano (5) usemao:

37. Nguvu-moja tuitupe, kwenye ardhi kulima,  
Tusiwe watepetepe, si wagonjwa tu wazima,  
Kazi-yetu iwe yape, pasi kuwa na dhuluma!  
Kama alivyoitaja, Mtukufu KITUNG’ATI. (uk. 7)

Hapa Mnyampala anazungumzia muktadha uliokuwepo wakati baba wa Taifa alipokuwa anahimiza umoja na kufanya kazi kwa nguvu zote bila uzembe wa aina yoyote ili nchi iweze kujitegemea yenyewe. Muungano huo ulikuwa na nia ya kujenga uchumi mmoja wa Tanzania ili kuleta maendeleo ya nchi kwa nguvu za wananchi wenyewe. Uchumi huo ni kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya taifa pasi na kutegemea misaada kutoka nje. Katika ubeti huo mwandishi anahimiza kilimo. Anawataka wananchi walime kwa bidii bila kuwepo kwa ulegevu wowote. Hayo yote yalitokana na sera ya Baba wa Taifa ya wakati huo. Mwandishi alizichunguza na kuziwasilisha katika muundo wa sanaa ya ushairi. Hapo kuna mwingilianomatini kati ya sera za siasa za Mwalimu Julius Nyerere na maudhui ya mtunzi. Hii inadhihirisha kuwa hakuna maana isiyunganishwa na usemi au kazi zilizopita kwani hakuna kazi ya fasihi yenye sifa za uasilia na upekee (Allen, 2000). Mnyampala kama mwanafasihi aliathiriwa na kauli za wanasiasa wa kipindi chake na hasa falsafa ya Rais Julius Nyerere.

### 3.2.3.2 Utaifishaji wa Mali

Muktadha wa utaifishaji wa mali za wakoloni umesawiriwa katika kazi za Mnyampala. Kipindi hicho kilikuwa cha kutaifisha mali na kuzifanya za serikali kwa manufaa ya wote. Katika *Diwani ya Mnyampala*, suala hili limejitokeza katika shairi la “Uhuru uwe wa Heri” (uk.145). Mnyampala anazungumzia masuala ya kutaifisha mali ya watu wote waliopata mali kwa njia ambazo si za halali. Haya yalitokea baada ya uhuru, kama asemavyo katika ubeti wa saba kuwa:

38. Pasizuke mushikeli, wa mizozo na kikiri,  
Wageni kupokwa mali, maisha kuwa hatari,  
Huo ni ubaradhuli, ni kujipalia nari,  
Uhuru uwe wa Kheri, na udumu kwa amani.

Katika ubeti huu Mnyampala aliona wanyonyaji na wakoloni waliokuwa wameshikilia uchumi wa nchi wakati huo waendeleo kulinyonya taifa, kwa kuwa kuzitaifisha mali hizo kungesababisha ghasia na pengine vita katika nchi. Mawazo hayo yanaonyesha kuwa Mnyampala alikuwa bado hajakomaa katika masuala ya siasa na hakuelewa maana ya uhuru uliokuwa unaongelewa. Mnyampala pia amezungumzia vizuri suala hili la utaifishaji wa mali za wakoloni katika *Ngonjera za UKUTA Na 1*. Katika ngonjera za Azimio la Arusha hasa katika ngonjera za “Azimio Lakomesha Mirija” (uk. 47-51), Mnyampala anaeleza kuwa mali za mabepari, makabaila na mabwanyeye zinatakiwa kutaifishwa kuwa chini ya serikali ili kuondoa unyonyaji katika nchi. Hapa Mnyampala amebadili mawazo aliyokuwa nayo katika *Diwani ya Mnyampala*, kutokana na muktadha wa sera ya uchumi iliyokuwepo wakati huo.

### 3.2.3.3 Ujenzi wa Jamii Mpya

Ujenzi wa jamii mpya ni mojawapo ya mambo yaliyozungumziwa katika mashairi ya Mnyampala. Harakati za ujenzi wa jamii mpya ni muktadha uliokuwepo katika kipindi cha uhuru na baada ya uhuru. Viongozi walisisitiza ujenzi wa jamii mpya kwa kusisitiza elimu ili watu waweze kujitambua na kuleta mabadiliko katika jamii. Suala la ujenzi wa jamii mpya huweza kuingizwa katika muktadha wa kisiasa, kijamii na kiuchumi. Hivyo kutokana na mwingiliano wa kipengele hiki, tumeamua kukiweka katika muktadha wa kiuchumi. Ujenzi wa jamii mpya unategemea zaidi uchumi wa nchi. Nyerere (1967) anaeleza kuwa hatua ya kwanza ya kujenga jamii zetu ni kutoa elimu na watu kujifunza ili waweze kujitambua wao ni akina nani na wana jukumu gani katika kuleta maendeleo katika jamii zao pamoja na kuinua uchumi wa nchi yao. Hivyo kipindi hicho elimu ilisisitizwa sana ili kuweza kujenga jamii mpya inayojitegemea katika nyanja zote, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Mnyampala katika uandishi wake aliathiriwa na muktadha wa ujenzi wa jamii mpya. Huu ndio ulikuwa msingi wa kuandika mashairi yake kwa kusisitiza masuala ya ujenzi wa jamii mpya. Omary (2011) anasema kuwa muktadha wa ujenzi wa jamii mpya umemsaidia mwandishi kuyajenga mashairi yake yaliyopo katika *Diwani ya Mnyampala, Ngonjera za Ukuta Na. 1* na *Ngonjera za Ukuta Na. 2*.

Aidha, uandishi wa kazi za Mnyampala ulifungamana na muktadha wa kiuchumi uliopita, uliopo wakati huo na uliotarajiwa. Hivyo aliweza kujihusisha katika ujenzi wa jamii mpya kwa kuheshimu haki na usawa wa binadamu miongoni mwa wanajamii kipindi cha uhuru na chini ya Azimio la Arusha. Kwa mfano katika *Diwani ya Mnyampala*, alihamasisha ujenzi wa jamii mpya wakati huo. Katika shairi la “Mtoto Kuomba Pesa” (uk. 4) anasisitiza maadili mema kwa watoto ili kujenga jamii

mpya yenye maendeleo bila kutegemea misaada kutoka kwa watu wengine. Vilevile katika shairi la “Yaliyopita Yamepita” (uk. 120) ubeti wa pili unasema:

**39.** Ya uhuru yatungeni, ya ugomvi yamepita,  
Tanganyika nchi amani, nchi haina wasalata,  
Washairi unganeni, na utunzi kutakata,  
Ya ugomvi yamepita, na tugange ya uhuru. (uk. 120)

Katika ubeti huo Mnyampala anawataka watunzi waungane katika kuleta amani na kujenga taifa lao kwa kutunga mashairi yanayohusu uhuru wa nchi na umuhimu wake kwa jamii.

Kwa upande wa *Ngonjera za UKUTA Na 1*, Katika ngonjera hizo Mnyampala alitangaza Azimio la Arusha kwa kuwataka wananchi wafanye kazi kwa bidii na kudumisha utamaduni unaofaa na kutupilia mbali utamaduni usiofaa. Hivyo Mnyampala aliwataka wananchi wote wawajibike ipasavyo mfano katika ngonjera ya “Natuondoe Makupe” (uk. 54) na “Elimu ya Kujitegemea” (uk. 56). Ngonjera hizo zinasisitiza ujenzi wa jamii mpya katika nyanja zote za kijamii. Kadhalika katika mswada wa *Mashairi ya Vidato*, kuna mashairi yanayoeleza ujenzi wa jamii mpya. Kwa mfano shairi la “Usiseme Hatuwezi Awezalo Binadamu” (uk. 13). Ubeti wa nane anasema:

**40.** Ikiwa bingwa Wazungu, mambo mengi wataalamu,  
Wajua mingi mizungu, ya mengine na elimu,  
Vipi sione uchungu, tujifunze kwa muhimu?  
Tusiseme ‘jambo gumu’, awezalo binadamu.

Katika dondoo hilo na shairi hilo Mnyampala anasisitiza masuala ya ujenzi wa jamii mpya kupitia elimu na sayansi na teknolojia. Mnyampala anawataka wanajamii kupambana kama Wazungu wanavyopambana ili kuleta maendeleo katika taifa lao.

Kwa ujumla, utunzi wa kazi teule za Mnyampala aliathiriwa na muktadha wa ujenzi wa jamii mpya na hii ndiyo maana kazi zake zimejikita katika kuzungumzia muktadha huo. Kama tulivyogusia awali, muktadha wa kijamii, kisiasa na kiuchumi yote inaingiliana na kujihusisha na masuala ya ujenzi wa jamii mpya. Hivyo basi muktadha ulioathiri kazi za Mnyampala ni wa kimwingilianomatini zaidi na masuala mbalimbali yaliyokuwepo katika jamii wakati huo.

### 3.2.4 Muktadha wa Kimwingilianomatini

Muktadha wa Mwingilianomatini ulijitokeza pia katika miktadha ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Licha ya kujitokeza katika miktadha hiyo ni vyema kuujadili kama mojawapo ya miktadha kwa kuwa kazi za Mathias Mnyampala zimeathiriwa pakubwa na muktadha huu. Aidha, mwingilianaomatini umetumika katika kazi zake zote teule. Umejitokeza zaidi katika diwani ya *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi na Hazina ya Washairi*. Ikifuatiwa na *Ngonjera za Ukuta Na. 1, Mahadhi ya Kiswahili na Diwani ya Mnyampala*. Wamitila (2008) anaeleza kuwa muktadha wa mwingilianomatini unavuka mpaka wa shairi moja maalum na kuunganisha na muktadha wa shairi lingine. Anaeleza kuwa shairi moja huweza kuashiria au kuelekeza katika shairi jingine ambalo ni muhimu katika fasiri na uelewekaji wa shairi lenyewe. Matalani, sehemu ya pili ya kitabu cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* inahusu malumbano ya ushairi yaliyotokana na shairi la “Raha” (uk. 8) lililotungwa na Kaluta Amri Abedi. Muktadha wa mwingilianomatini unajitokeza pale ambapo washairi mbalimbali wanajibizana kuhusiana na shairi hilo. Mnyampala (1968) katika dibaji ya toleo la pili anaeleza kuwa:

41. Kisa cha kuingia mashairi haya ni kutokana na shairi la “RAHA” lililotungwa na Sheikh Amri, ambalo lilifikiriwa vingine na baadhi ya washairi wengine. Fikra yao iliwatuma kuwa eti Sheikh Amri alitunga shairi hilo kwa ajili ya kumjugumu mtu fulani maarufu nchini Tanzania



aliyepata kushtakiwa na kupelekwa Mahakamani. Washairi hao waliandika mashairi yao wakimjibu marehemu Sheikh Amri ili kumtetea mtu huyo. Yalizuka malumbano makubwa ya kishairi, lakini mwisho malumbano hayo yalikwisha.... (uk. v)

Kwa hiyo, mashairi yaliyofuata kuanzia shairi la “Raha” (uk. 8) hadi shairi la Saa (uk. 20) yameundwa katika muktadha wa mwingilianomatini, na yote yanalenga kuelezea shairi la “Raha.” Hivyo baada ya Amri Abedi kuandika shairi lake la “Raha,” alijibiwa na Khamis Amani Khamis (Nyamaume) kwa shairi lake la “Mtego” (uk. 9), baadaye akafuatiwa na Mahmoud Hamdouniy na shairi lake la “Dunia Duara” (uk. 10), “Dunia Nyama ya Tembo” (uk. 11) na “Mizani” (uk. 12). Pia alifuatia Sheikh Mahmud aliyetunga shairi la “Hujuvywa Asiyejua” (uk. 12), Mashairi haya yalikuwa yanamtuhumu Amri Abedi. Baadaye yalitokea mashairi ya kujibu hawa waliomtuhumu Amri Abedi. Mashairi hayo ni “Ni Waadhi Shairi” la Mathias Mnyampala, akafuatiwa na Mohamedi Ali aliyeandika “Mtego Umefyatuka” (uk. 14) na Amri Abedi mwenyewe na shairi la “Dhana” (uk. 15). Baadaye mjadala huu uliendelezwa na Akilimali Snow White aliyetunga shairi la “Dhana” (uk. 15), “Ushairi ni Waadhi” (uk. 16) na “Duwa la Kuku Uongo” (uk. 17).

Kadhalika, alifuatia Mohamed Selemani (Mtu-Chake) na shairi la “Ndovu Wanapopigana” (uk. 18), Khamis Amani Khamis (Nyamaume) alitunga shairi la “Jiti” (uk. 19) akieleza kwa fumbo kitu wanachogombea. Shairi hili la “Jiti” (uk. 19) lilijibiwa na Bwana Gwiji, aliyeandika shairi liitwalo “Jiti” (uk. 20). Kisha Khamis Amani Khamis alitunga shairi jingine aliloliita “Saa,” ubeti wa kwanza (uk. 20) unasema:

42. Saa za huku na huko, zimekosana majira,  
Sababuye mzunguko, kuzunguka mduara,  
Sasa rai iliyoko, ni kurekebisha Dira,  
Saa zatupa majira, mabingwa rekebisheni.

Hapa mwandishi anamaanisha kuwa mawazo ya washairi wa upande wa Amri Abedi na ambao wako upande mwingine yamekosana kifikira. Naye Mnyampala (1968) anaeleza kuwa Nyamaume alimaanisha kuwa saa za mikono, ukutani na mezani inafaa zirekebishwe kwa kufuata saa kubwa ya mnara, endapo saa hiyo ya ukutani itakuwa imepoteza majira hata hizo nyingine zitapoteza majira yake. Katika shairi hili Nyamaume alikuwa anawataka washairi wamalize tofauti zao, hasa kwa kuanza na washairi mabingwa. Mnyampala (1968) anafafanua kuwa shairi hilo la “Saa” lilisababisha washairi wenyewe kuandikiana barua ili kurekebisha hitilafu zao na kuelewana kama ilivyokuwa hapo zamani, na udhia huo ukaisha.

Vilevile, kuna muktadha wa mwingilianomatini katika *Diwani ya Mnyampala* (uk. 18). Katika diwani hiyo Mnyampala anaeleza kuwa Snow White alipinga shairi lake la “Tusitukane Wakunga” (uk. 17-18) kupitia shairi lake la “Kuzaa si Kazi Kubwa, Kazi Kulea Mwana.” Mnyampala alimjibu tena katika shairi la “Tutalea Mwana Gani?” ambalo linapatikana katika diwani hiyo (uk. 18). Hapa kuna muktadha wa mwingilianomatini unaoibuliwa na majibizano baina ya Mnyampala na Akilimali Snow White.

Muktadha huo wa mwingilianomatini umejitokeza pia katika shairi la “Nakuageni Wakuu” (uk. 102) ambalo liliandikwa na Mnyampala. Mnyampala katika (uk. 103) anaeleza kuwa shairi hilo lilijibiwa na bwana M. J. D. Mwanoga na Bwana Y. I. Salimu wa Dodoma kwa shairi la “Kwa Heri Nenda Salama” (uk. 103) na “Haiba Imepungua” (uk. 104) kwa mfuatano huo. Baada ya mashairi hayo Mnyampala alitunga shairi la “Tumefika Salama” (uk. 105) naye D. K. Adamu Saleh alimkaribisha Mnyampala kwa shairi<sup>41</sup> ambapo Mnyampala alimjibu kwa shairi la “Karibu Yako Fususi” (uk. 106).

<sup>41</sup> Shairi la Bwana D.K. Adamu Saleh halijaandikwa ndani ya diwani hii, ila Mnyampala (uk.106) ameeleza kuwa mshairi huyo alimtungia shairi la kumkaribisha.

Isitoshe, Mnyampala katika diwani hiyo aliweza kutunga mashairi mengine kutokana na marafiki zake walivyomuomba kwa mfano shairi la “Ukishindwa Kuubeba” (uk. 64-65) na “Sakubimbi Hana Njama” (uk. 71-72), Mnyampala mwenyewe anasema kuwa alitunga mashairi hayo kwa maombi ya bwana Bakari wa Dodoma. Sambamba na hilo, Mnyampala anaeleza kuwa alitunga shairi la “Sanduku Limenishinda” (uk. 65-66) kwa ajili ya rafiki yake Hamdu Haji Khatibu wa Unguja kwa kufuata desturi za kwao. Vilevile, shairi la “Ahsante Bwana Fondo” (uk. 73), alitunga kwa maombi ya rafiki yake M. J. D. Mwanoga wa Dodoma. Pia kuna mashairi ndani ya diwani hiyo yaliyotungwa kwa ajili ya gazeti jipya la *Mwananchi* lililoanzishwa wakati huo (Mnyampala, 1965). Mashairi yaliyotungwa kwa ajili ya gazeti hilo ni “Mwananchi Kua Salama” (uk. 68) na “Johari Ninakupamba” (uk. 68-69). Mnyampala anaeleza kuwa mhariri wa gazeti hilo alimuomba Mnyampala alipambe gazeti hilo jipya. Tukitazama mashairi hayo niliyoyataja ni wazi kuwa yanasawiri vyema muktadha wa mwingilianomatini katika diwani hiyo.

Muktadha huu unajitokeza pia katika mswada wa *Hazina ya Washairi*. Katika mswada huu kuna mkusanyiko wa mashairi ya watunzi mbalimbali ambao walitunga kazi zao kwa kuegemea katika muktadha wa mwingilianomatini. Muktadha wa mashairi haya unahusiana kwa kiasi kikubwa na muktadha wa mashairi yaliyomo katika kitabu cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*. Hata hivyo Mnyampala (1966) katika dibaji yake ya *Hazina ya Washairi* anasema kuwa, mawazo ya kukusanya mashairi yaliyomo katika mswada huo aliyapata baada ya kukumbushwa na Rais wake Mwalimu Julius K. Nyerere wakati alipoandika toleo la pili la kitabu cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*. Nyerere (1968:i) katika utangulizi huo anasema:

43. Ninawashukuru pia jamaa wa chama cha washairi kwa kutoa kijitabu hiki. Ninalowaomba zaidi ni kwamba wajitayarisha kututolea kitabu kikubwa zaidi kuliko hiki.

Hapo Nyerere aliwataka washairi wakusanye mashairi mengi zaidi kama yalivyokusanywa katika kitabu cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* ambacho kilikuwa na mashairi ya washairi mbalimbali na ya kwake yakiwemo. Kwa hiyo mashairi yaliyokuwemo kwenye mswada wa *Hazina ya Washairi*, yameundwa katika muktadha wa mwingilianomatini. Katika mswada huo mtunzi mmoja anatunga shairi na wengine wanaibuka kutunga mashairi yao kwa kuhusisha na muktadha wa shairi la awali, kwa kujibu, kuuliza ama kuchangia hoja. Lengo hasa ni kuonyesha jinsi mashairi yanayofuata yanavyohusiana na shairi lililotangulia. Aidha, Wamitila (2008) anafafanua kuwa muktadha wa mwingilianomatini unapanua muktadha finyu wa ushairi mmoja na kuliweka katika mawanda mapana zaidi ya ushairi na kuweza kuonyesha jinsi shairi hilo linavyoweza kukamilishana na shairi lililotangulia.

Hivyo basi, mashairi yote yanayopatikana ndani ya mswada wa *Hazina ya Washairi* yanatokana na muktadha wa mwingilianomatini. Mwingiliano wa shairi la Mnyampala na wenzake umejitokeza kuanzia (uk. 34-35). Katika majibizano ya washairi kuhusu masuala ya ndoa, Mwaruka alitunga shairi la “Ndoa ya Shuruti Mbaya” (uk. 34) na Mnyampala aliandika shairi la “Mzazi kuridhi Ndoa” (uk. 35). Shairi hilo linaingiliana na mawazo ya shairi la Mwaruka pamoja na shairi alilotunga Kaluta Amri Abedi la “Ndoa Aridhi Binti” (uk. 35). Aidha, shairi hili la Mnyampala la “Mzazi Kuridhi Ndoa” (uk. 12) linapatikana katika *Diwani ya Mnyampala*. Vilevile, mashairi hayo yanaingiliana na shairi la Mnyampala la “Ndoa Akiridhi Nani” (uk. 4) linalopatikana pia katika *Diwani ya Mnyampala*. Kwa ujumla, mashairi yote yaliyomo

ndani ya mswada wa *Hazina ya Washairi* yametungwa katika muktadha wa mwingilianomatini.

Muktadha wa mwingilianomatini umetumika pia katika kitabu cha *Ngonjera za UKUTA Na. 1* na *2*. Mnyampala ametumia muktadha wa mwingilianomatini kwa kuwa mada alizozitungumzia katika kitabu cha *Ngonjera za UKUTA Na. 1* zimejadiliwa pia katika kitabu cha *Ngonjera za UKUTA Na. 2* kwa upana zaidi. Kwa mfano, katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* ametumia mada zifuatazo: Ngonjera ni kitu gani, Tanu na Siyasa Yake, Viongozi wetu, Ujamaa, Azimio la Arusha, Elimu na Utamaduni, Sikukuu za Taifa, Uhusiano Mwema na Mafumbo. Katika *Ngonjera za UKUTA Na. 2* ametumia baadhi ya mada hizo na kuzifafanua zaidi. Kwa mfano katika kitabu cha kwanza, kuna ngonjera za TANU na Siyasa yake na katika kitabu cha pili pia kuna mada inayohusu Chama cha TANU lakini amefafanua zaidi yale yaliyoelezwa katika kitabu cha kwanza kwa kuelezea imani na madhumuni ya TANU.

Kadhalika, katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* kuna mada ya Ujamaa na katika *Ngonjera za UKUTA Na. 2* anaelezea “Siasa ya Ujamaa” ambapo ndani yake amefafanua vipengele vinne: “Hakuna Unyonyaji,” “Njia kuu za Uchumi ni Chini ya Wakulima na Wafanyakazi,” “Kuna Demokrasi,” na “Ujamaa ni Imani.” Katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* Mnyampala alilenga kuwaelimisha zaidi wananchi kuhusu Ujamaa kwa kutumia mtindo wa maswali na majibu lakini katika *Ngonjera za UKUTA Na. 2* Mnyampala anaelezea maana ya siasa ya Ujamaa, misingi yake na madhumuni ya siasa ya kujitegemea na Azimio la Arusha nchini Tanzania. Hivyo katika utunzi wa vitabu hivi, Mnyampala ameegemea katika muktadha wa mwingilianomatini kwa kuhusisha na muktadha wa kisiasa uliokuwepo wakati huo, hivyo *Ngonjera za UKUTA Na. 2* ni mwendelezo wa *Ngonjera za UKUTA Na. 1*.

Utunzi wa nyimbo za *Mahadhi ya Kiswahili* pia umetokana na muktadha wa mwingilianomatini. Mathalani, nyimbo alizokusanya Mnyampala kutoka kwa Bwana Haji Chum wa Unguja (uk.7-9) zinaelekeana na nyimbo zilizoandikwa na kukusanywa na Mnyampala mwaka 1943-1953 wakati alipokuwa fundi na mutribu wa vinanda – *tashkota* na *harmonia*. Mnyampala (uk. 10) anasema nyimbo hizo aliandika mwenyewe na nyingine zilitungwa na Bwana Mbabe Athmani na wengineo. Nyimbo hizo zimeandikwa kwa pamoja bila kuonesha mtunzi husika (taz. *Mahadhi ya Kiswahili* uk. 10-14). Hivyo ni vigumu kujua wimbo na mtunzi mahususi. Kwa ujumla, nyimbo zote zilitungwa katika muktadha wa kimwingilianomatini ndio maana ziliwekwa pamoja kwa kuwa zinahusiana.

### **3.3 Hitimisho**

Sura hii imechambua data zinazohusiana na lengo la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu ambalo ni kupambanua muktadha uliomsukuma mwandishi kuzitunga kazi zake za ushairi. Tumeshughulikia mambo yafuatayo: Mosi, muhtasari wa kazi teule za Mathias Mnyampala. Pili, muktadha wa kijamii, hapa tumeelezea mwingiliano wa mila na desturi za Kiafrika na za kigeni, suala la uzazi na malezi, kuathiriwa na waandishi wengine, dini, mapenzi na ndoa, na kushamiri kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Tatu, muktadha wa kisiasa, ambapo tumeelezea siasa za harakati za kupigania uhuru na kipindi cha uhuru, Ujamaa na Kujitegemea, muungano wa Tanganyika na Zanzibar na uhusiano wa mtunzi na viongozi wa kitaifa. Nne, muktadha wa kiuchumi ambao unahusu uchumi wa kishoshalisti, utaifishaji wa mali na ujenzi wa jamii mpya. Tano, tumejadili muktadha wa mwingilianomatini ambao hasa unahusu kuhusiana kwa tungo mbalimbali.

Kwa ujumla, kazi teule za Mnyampala zimeandikwa kutokana na muktadha wa kijamii, kisiasa, kiuchumi na kimwingilianomatini. Katika uandishi wake alizingatia muktadha wa kijamii, kisiasa, kiuchumi na wa kimwingilianomatini ili kuielimisha umma kuhusiana na tamaduni zao. Kwa msingi wa Nadharia ya Mwingilianomatini tumebaini kuwa hakuna kazi inayotoka katika ombwe ambayo haifungamani na muktadha uliomlea na kumkuza mtunzi wa kazi husika. Sura inayofuata inajadili mbinu za kifani zilizotumika kuibua maudhui mbalimbali katika kazi teule za Mathias Mnyampala.

## SURA YA NNE

### MBINU ZA KIFANI ZINAZOIBUA MAUDHUI KATIKA KAZI TEULE ZA MATHIAS MNYAMPALA

#### **4.0 Utangulizi**

Sura iliyopita ilishughulikia muktadha wa kazi za ushairi wa Kiswahili za Mathias Mnyampala. Sura hii ya nne imejikita katika kujadili lengo la pili na swali la pili la utafiti ambalo ni kuhakiki mbinu za kifani zinazotumika kuibua maudhui katika kazi teule za ushairi za Mathias Mnyampala. Katika kufanya uchambuzi huu tumeongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini. Senkoro (2011) anaeleza kuwa fani na maudhui ni pande mbili za sarafu moja. Hivyo, hatuwezi kuvitenganisha vipengele hivi kwa sababu hukamilishana na hutegemeana katika kazi yoyote ya fasihi. Katika kujadili mbinu za kifani tumejadili pia maudhui yaliyoibuliwa na mbinu hizo.

#### **4.1 Mbinu za Kifani Zinazoibua Maudhui katika Kazi Teule za Ushairi wa Mathias Mnyampala**

Kwa kawaida katika kazi ya fasihi maudhui ndiyo yanazua mbinu za kifani. Kama asemavyo Abedi (1954: viii) kuwa “Mawazo ya mtungaji yazue vina, sio vina kuzua mawazo.” Dhana za maudhui na fani zimefafanuliwa na wahakiki mbalimbali. Senkoro (2011) anaeleza kuwa maudhui hujumuisha mawazo na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma mtunzi ama msanii huyo hadi kutunga kazi ya fasihi. Maudhui yanajumuisha dhamira, ujumbe, migogoro, falsafa na msimamo au mtazamo. Kwa mujibu wa Senkoro, fani ni ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kazi zake. Fani hujumuisha wahusika, mandhari, lugha, mtindo na muundo. Hata hivyo katika utafiti huu tunajihusisha na mbinu za kifani zinavyoibua maudhui kwa sababu fani na



maudhui hukamilishana na kutegemeana. Mbinu za kifani tunazoshughulikia katika lengo hili ni mtindo na matumizi ya lugha. Katika vipengele hivyo vya kifani tumejadili mbinu tano. Mbinu hizo ni taswira, methali, misemo, ushairi-drama (au ushairi wa maigizo) na nyimbo. Kwa upande wa maudhui tumejikita katika vipengele vya ujumbe na dhamira. Ufuatao ni uchambuzi wa mbinu za kifani tulizoainisha hapo juu.

#### **4.1.1 Taswira**

Taswira ni mbinu ya kifasihi au kisanaa inayotumiwa na waandishi wa fasihi kupitisha maudhui kwa hadhira lengwa. Mulokozi na Kahigi (1979) wanafasili kuwa taswira ni mbinu ya picha katika utungo na katika mawazo ya msomaji au msikilizaji wa utungo huo. Pia wanaona kwamba picha ni matumizi mazuri ya lugha yanayopambanuliwa na uteuzi mzuri wa maneno, uangalifu na udhahiri wa maelezo wenye kuhusisha na kujumuisha dhana moja ili kuleta taswira au athari maalum katika mawazo ya msomaji. Naye, King'ei (1987) anaeleza kuwa taswira lazima ijengwe kutokana na msingi wa ulinganifu baina ya dhana, jambo au chombo kinachorejelewa na taswira ile iliyochorwa. Wamitila (2002) anasema kuwa taswira ni picha ambazo humjia msomaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Anaongezea kuwa picha hizo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au tamathali za usemi anazotumia. Wamitila anasema kuna taswira zinazotokana na maelezo na ambazo hazina maana nyingine ya ziada; hujulikana kama taswira za kimaelezo. Aidha, anasema kuwa zipo taswira ambazo huwa na namna nyingine ya ziada (yaani siyo ile ya picha tu, ipo ya ziada) hizi nazo huitwa taswira za kiishara. Madumulla (2009) anasema kuwa taswira si lazima imaanishe picha ya akilini kwani kuna picha halisi, picha ya kutambulika na picha ya kidhana.

Kutokana na mawazo haya ni bayana kwamba taswira ni picha ijengwayo akilini ambayo si lazima iwakilishe kitu kingine. Aidha, taswira husaidia kuona, kuhisi, kunusa, kugusa, kusikia, kuonja, kufikiri na kuleta joto wakati wa kusoma kazi husika. Taswira ni muhimu sana katika kazi ya fasihi kwa lengo la kuwasilisha ujumbe wa mshairi kwa wasikilizaji na wasomaji wa kazi husika. Kezilahabi (1974) anafafanua kuwa katika uhakiki wa mashairi inafaa kuweka mkazo katika matumizi ya taswira au picha. Anaongezea kuwa uzito wa maudhui ya shairi umu katika matumizi ya picha zinazotumiwa ili kuleta hisia fulani kwa msomaji. Naye Ngure (2004) anaeleza kuwa matumizi ya taswira ni muhimu katika utungaji wowote ule kwani husaidia kuvuta picha na hisia ya kitu kiongelewacho. Taswira huiwezesha hadhira kunasa akilini kitu kinachosimuliwa kwa namna ambayo hakiwezi kusahaulika. Kulingana na mawazo ya Kezilahabi (1974) na Ngure (2004), taswira zinasaidia kuonyesha hisia za mshairi. Kwa hiyo katika kazi hii tunawajibika kuhakiki na kuchambua taswira zinazojitokeza katika kazi teule zinavyotumika kuibua maudhui mbalimbali katika ushairi wa Mnyampala.

Senkoro (2011) anasema taswira ni mkusanyiko wa picha mbalimbali zinazotumiwa pamoja na maelezo ya wasanii katika kazi za fasihi. Senkoro anaona kuwa taswira zinafumbatwa na sitiari na tashbiha. Pia katika taswira kuna ishara mbalimbali zinazowakilisha mawazo, dhana, vitu au watu na maumbile mbalimbali. Mnyampala ametumia taswira mbalimbali kuibua maudhui anuwai katika kazi zake teule. Senkoro (2011) anaeleza kuwa Mnyampala ametumia taswira za aina tatu (zionekanazo, za mawazo na za hisi). Yeye ameziangalia katika kitabu kimoja tu ambacho ni *Diwani ya Mnyampala* pasipo na kuangazia maudhui yaliyomo ndani ya taswira husika. Kwa upande mwingine Masungwa (2012) anaeleza kuwa kuna aina tano za taswira katika kazi za Mnyampala, ambazo ni taswira za tafakuri au kufikirika, zionekanazo, hisi,

usambamba au ulinganishi na taswira za mviringo. Aidha, katika utafiti huu tumebaini kuwa, aina ya usambamba na mviringo ni taswira zinazoweza kupatikana katika taswira za kuonekana, hisi na mawazoni. Kwa ujumla, taswira zinazopatikana katika kazi za Mnyampala zinaingiliana na kukamilishana hivyo ni vigumu kuzihakiki kwa kuzitenganisha. Kutokana na mwingiliano uliopo ndani ya taswira hizo, tumejadili taswira bila ya kuziweka katika makundi ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza kutokana na uainishaji huo. Aidha katika mbinu hii tunapata picha ya kuona, kugusa, kuonja, kuhisi na kufikirika. Kadhalika katika tasnifu hii taswira na picha vinajadiliwa kama visawe.

Taswira (picha) imetumika na Mnyampala katika kazi zake teule za ushairi ili kuibua maudhui mbalimbali katika kazi hizo. Tukianza na *Diwani ya Mnyampala*, mwandishi ametumia taswira mbalimbali. Mnyampala ametumia taswira ya *Panya* katika shairi la “Panya Simwonyeshe Pamba” (uk. 52), hapa tunapata picha ya kuona panya akiharibu pamba. Taswira ya panya imetumika kuelezea watu waovu na wasio na maadili. Mtunzi anasihi hadhira kuchukua tahadhari dhidi yao. Katika taswira hii, tunapata maudhui ya namna ya kuishi na watu wenye utovu wa nidhamu au wasio na utu katika jamii yetu. Kama tunaona hilo katika beti zifuatazo:

44. Hatosheki na mafuta, ataruka kama komba,  
Falau akitaka, mfano amebeba mimba,  
Ambayo ataikata, aende kukaa chemba,.... (Ubeti 3, uk. 52)

Tamati hutampata, tundu amesha lichimba  
Ndani anafurukuta, pamba amekwisha kumba,  
Wabaki kucheza kwata, masikini umewamba,  
Panya usimwonjesha pamba, pindi utakuja juta. (Ubeti 5, uk. 52)

Katika shairi hili Mnyampala ametumia taswira ya panya kuelezea matukio mbalimbali yanayotokana na watu wadhalimu katika jamii na taifa kwa ujumla.

Mnyampala anaitaka jamii iwe na tahadhari na watu wanaoishi nao kwa kujua tabia zao kabla ya kuwashirikisha mambo yao. Taswira hiyo inaelezea dhamira za shairi hilo kama vile tamaa, umaskini, ubinafsi, fitina, unyonyaji, ufujaji wa mali na kuondokana na marafiki wasiofaa katika maisha. Kadhalika shairi hili linatupa ujumbe kwamba hatuna budi kujihadhari na marafiki zetu, maana adui wa mtu ni mtu aliye karibu naye. Hivyo mtu yeyote anapotaka kumshirikisha kitu kizuri mtu anatakiwa awe amejiridhisha kwanza na tabia yake.

Taswira nyingine imejengwa na matumizi ya neno asali katika shairi la “Je Asali ni Halali?” (uk. 51). Taswira hii inatupa picha ya kuona jinsi asali ilivyo. Vilevile, kuna picha ya kuhisi, kunusa na kuonja ili kupata ladha ya asali inayozungumziwa. Katika taswira hii, mtu anaweza kuona na kupata hisia mbalimbali kutokana na namna ambavyo asali inatengenezwa. Aidha, msomaji au msikilizaji anaweza kuhisi kinyaa, wasiwasi na woga wa kutumia asali. Kwa kawaida asali ni tamu na kila aonjaye anatamani kuendelea kulamba. Kadhalika asali ina harufu nzuri yenye kuvutia na kutamani kuonja. Kutokana na utamu wake mtu akionja hatamani kuacha. Ndio maana kuna methali isemayo “mchovya asali hachovi mara moja” au “mchovya asali huchonga mzinga.” Hii inamanaisha kuwa anayeonja kitu kitamu lazima arudie tena na tena. Katika taswira hii mwandishi anatumia utamu wa asali kuelezea mambo mazuri yanayomzunguka mwanadamu kuwa na tahadhari nayo. Kwamba si kila unachokiona kizuri kinafaa kuliwa, kuna vitu vingine vizuri lakini havifai kuliwa. Kama asemavyo katika ubeti wa pili na 5:

45. Naulizani walimu, mashehe na Maliwali  
Misheni na Islamu, Wanyonge na majahili  
...Je, asali ni halali? Mnambie wajuaji. (ubeti 2, uk. 51)

Nyuki huchuma madimu, na mizoga ya tumbili  
 Twawakuta kemu-kemu, penye zoga la fahali,  
 Na kohozi lenye pumu, hutengeneza asali,... (ubeti 2, uk. 51)

Kupitia dondoo hili tunamuona mwandishi akiuliza maswali iwapo asali ni halali kwa kuwa inatokana na mchanganyiko wa midimu, mizoga, makohozi ya pumu na vitu vingine vichafu. Mnyampala anaeleza kuwa kila mtu alambaye asali hulamba mizoga, mavi, makohozi ya pumu na vitu vingine vichafu ambavyo vimetengeneza asali. Hapa Mnyampala anawaelimisha wanajamii kuwa si kila kitu kitamu ni kizuri, ni muhimu kuchunguza kwanza namna ya utengenezaji wa vitu vitamu. Katika taswira hii tunapata ujumbe kwamba ni vyema kuwa waangalifu na watu au vitu vinavyoonekana ni vizuri katika maisha kwani vingine havifai. Katika maisha haitakiwi kuvamia vitu au mtu kwa pupa lazima kuwa waangalifu. Kupitia shairi hili tunapata dhamira za maadili, uadilifu, uchunguzi na uangalifu katika maisha.

Katika *Diwani ya Mnyampala* kuna taswira nyingi alizotumia Mnyampala ili kufikisha maudhui kwa jamii. Kwa mfano shairi la “Mtoto Kuomba Pesa” (uk. 4), ametumia taswira ya *mtoto*. Kwa ujumla picha tunayoipata kutoka katika shairi hilo ni ya kuona mtoto anayeomba pesa kwa watu. Kitendo cha mtoto mdogo kuombaomba pesa kwa watu mbalimbali wanaokuja nyumbani wenyeji kwa wageni ni tabia mbaya. Mnyampala anakemea tabia hiyo na anatoa ujumbe kwa jamii kuwa inafaa kuwafundisha watoto malezi mema yanayofaa katika jamii. Kupitia taswira hiyo kuna dhamira ya malezi mema kwa watoto kwa kuwaongoza na kuwafundisha tabia njema. Katika shairi hili anatumia taswira ya mtoto na mzazi, kuelimisha jamii ili kuwafunza watoto ambao ni taifa la kesho wasipende kuwa ombaomba ama watu wanaopenda pesa bila ya kufanya kazi. Katika ubeti wa tatu mshairi anaeleza zaidi kwa kusema:

46. Heshimayo wapoteza, wazazi kwetu ni kosa,  
 Si hivyo kudekeza, bora mwana kumuasa,  
 Wengi mama huwafunza, “Huyo muombe mapesa,”  
 Mtoto kuomba pesa hii ni tabia gani? (ubeti 3, uk. 4)

Katika dondoo hili Mnyampala anakemea tabia ya kuwaendekeza watoto kuomba pesa kwa watu au wageni. Vilevile, anawataka wazazi wawafundishe watoto wao kutokupenda pesa za bure na kuwafundisha watoto maadili yafaayo kwa kuwaasa wasiombe pesa pindi wanapotembelewa na wageni nyumbani kwao. Katika ubeti wa nane, anawaasa wazazi na jamii kwa ujumla kuwafundisha watoto maadili mema na kujifunza kujitegemea katika maisha. Kwa upande wa taswira ya kiishara, taswira ya mtoto inaweza kuwakilisha mataifa machanga kimaendeleo ambayo yanaomba misaada kutoka kwa Wazungu. Mnyampala anayataka mataifa machanga kuacha kuomba misaada kutoka kwa Wazungu ili kuleta uhuru wa kweli ndani ya nchi zao. Dhamira na ujumbe tunaopata hapa ni kukwepa misaada, malezi mema na maadili kwa watoto ili baadaye waweze kujenga jamii mpya yenye maendeleo bila ya kutegemea misaada kutoka kwa wengine.

Taswira nyingine inayojitokeza ni shetani katika *Diwani ya Mnyampala*. Taswira tunayoipata hapa ni ya kimawazo au kufikiria kuwa shetani ni kiumbe kisichofaa katika jamii. Aidha, shetani ni kiumbe anayedhaniwa kuwa anasababisha wanadamu kutenda maovu. Binadamu anayetenda maovu mara nyingi anafananishwa na shetani kwa kuwa watu wanaamini shetani ndiye husababisha watu watende maovu. Taswira hii inajitokeza katika shairi la “Ukungu Kuziba Mbele” katika ubeti wa nne (uk. 23) unao sema:

47. Nyuma ananinyatia, shetani kaziba mbele,  
 Mashaka amenitia, sasa nakuna upele,  
 Dhiki imenipitia, mwili umepata ndwele,  
 Ukungu kuziba mbele, na nyuma aninyatia. (uk. 23)

Katika nukuu hii taswira ya shetani imetumika kuelezea maovu, mabaya na shida mbalimbali anazopitia mwandishi. Katika maisha yake amesongwa na mabaya ama shida mbalimbali na haoni pa kukimbilia. Hapa taswira ya shetani imetumika kuashiria shida nyingi zimpatazo mtu maishani ambazo zinaweza kuwa zimesababishwa na yeye mwenyewe au binadamu anaishi nao. Hivyo, anakuwa amesongwa na adha nyingi kiasi cha kushindwa kupata jibu la kuondokana na adha au shida anazopitia. Katika muktadha wa dini shetani ni kiumbe wa kidhahania ambaye ni chanzo cha maovu yote. Waumini wa dini ya Kikristo na Kiislamu wanaamini kuwa shetani anasababisha madhara mengi katika jamii. Ndiye chanzo cha vita, ugomvi, mauaji, mafuriko na kila jambo ambalo linasadikika kuwa ni baya katika jamii. Watu wanaamini kuwa shetani ana umbo la kutisha, ijapokuwa hakuna mtu aliyewahi kumuona kwa macho na wala hakuna ithibati ya kisayansi kuhusu kuwepo kwake. Kwa ujumla dhamira tunazozipata kutokana na taswira hiyo ni maovu, machafuko, dini na tabia mbaya iliyokithiri katika jamii.

Vilevile, taswira hii ya shetani imejitokeza katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* katika ngonjera ya “Zawadi Gani Tumpe” ubeti wa nne unaosema:

48. Tumtakie busara, na hekima ya kichwani  
 Ayashinde mazingira, na hila za ushetani  
 Yasimfike madhara, awe na afya mwilini  
 Atuongoze nchini, Rais wetu Nyerere

Katika nukuu hiyo mwandishi anamuomba Rais awe na hekima na busara njema asiwe na hila za shetani. Katika shairi hili taswira ya shetani imelinganishwa na

ukosefu wa hekima na busara. Hivyo, ushetani umetumika kama hila mbaya ama maovu mbalimbali afanyayo mtu. Katika ngonjera hiyo taswira ya shetani imetumika kuibua dhamira ya matendo maovu na uongozi mbaya. Hata hivyo kujitokeza kwa taswira ya shetani katika kazi mbili tofauti za Mnyampala ni suala la mwingilianomatini katika kazi zake. Kama asemavyo Kehinde (2003) kuwepo kwa utamaduni wa namna moja miongoni mwa watu huwafanya waandishi kuandika kwa kuzingatia kazi zilizotangulia; ama za kwake mwenyewe au za wengine. Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa kazi za Mnyampala zina mwingilianomatini. Vilevile, kuna mwingilianomatini wa kazi zake na za watunzi waliotangulia au waliofuata. Dhana ya shetani imetokana na matini za Kibiblia ambazo alizisoma katika dini za Kikristo.

Taswira nyingine ni ya upepo katika shairi la “Daima Pima Upepo” (uk. 27-28), katika *Diwani ya Mnyampala*. Mfano katika ubeti wa kwanza Mnyampala anasema:

49. Kinga moto uwakapo, na uzime uzimapo,  
Zima hapo uanzapo, ni hatari uwachapo,  
Moto hauna mkwepo, pande zote uzingapo,  
Chunga sana upepo, ni wapi welekeapo.

Piga ngoma za makopo, waite wasokuwapo,  
Na nyumba ziunguapo, nao panya wahamapo,  
Vyombo viteketeapo, ndipo shida yangukapo,... (ubeti wa pili)

Katika dondoo hili kuna taswira nyingine kama vile moto na ngoma za makopo kwa kuzitaja chache. Taswira zote zilizomo katika shairi hilo zinaingia kwenye taswira ya upepo. Hapa mwandishi anawaasa wanajamii kuwa na tahadhari katika maisha. Jambo baya linapotokea kama linaweza kuzuiliwa ni vema kufanya hivyo mapema ili lisilete madhara. Taswira hii ya upepo imetumika kumuasa mtu kuwa mwangalifu katika kila jambo alifanyalo kwa kuangalia nyakati na majira yaliyopo. Dhamira



iliyobebwa na taswira hii ni kuhusu maisha ya mwanadamu, yaani namna ya kuishi vizuri na walimwengu. Kadhalika katika shairi hili, kuna taswira nyingi ambazo Mnyampala amezitumia kwa mfano, moto, ngoma za makopo, panya, popo na ua. Taswira hizo zote zinaashiria mabadiliko yanayojitokeza katika maisha ya mwanadamu. Mwandishi anawasihi wasomaji wawe waangalifu na wenye kuchunguza mazingira yaliyopo pamoja na watu wanaoishi nao ili waweze kuwafahamu vizuri na kuishi nao kwa tahadhari. Vilevile, mwandishi anawataka watu wawe makini na wachunguze kwanza mambo wanayotaka kuyafanya ili wasije wakapata matatizo. Kwa ujumla katika shairi hili tunapata ujumbe kwamba tuwe waangalifu katika jamii siku zote. Kutokana na taswira zilizomo katika shairi hilo msanii anatoa ujumbe na dhamira mbalimbali kama vile kuchukua tahadhari dhidi ya marafiki, majirani na watu wote wanaokuzunguka, kufanya mambo kwa uhakika na uangalifu, hofu, mashaka, unafiki na usaliti katika maisha.

Mnyampala pia ametumia taswira ya chawa katika shairi lake la “Chawa hatoki Nguoni” (uk. 44-45) katika *Diwani ya Mnyampala*. Chawa ni mdudu anayependa kuishi maeneo machafu na kumuathiri binadamu. Katika taswira hii tunapata taswira ya kuona chawa alivyo na mazingira anayopatikana. Kwa ujumla, watu wanaoathiriwa na chawa ni wale wanaoishi katika mazingira duni yaani tabaka la chini, wachafu na wanaoishi mazingira yasiyoridhisha. Hapa mwandishi anatumia taswira ya chawa na wadudu wengine kama vile viroboto na kunguni katika ubeti wa tatu na saba. Wadudu hawa hunyonya damu za binadamu. Mwandishi ametumia taswira ya chawa, viroboto na kunguni akimaanisha matatizo mbalimbali yaliyomo katika jamii hayawezi kuondoka bila ya kufanya jitihada zinazotakiwa. Kupitia shairi hili mwandishi anaelimisha jamii kutumia juhudi na maarifa kutafuta suluhu ya matatizo yaliyopo katika jamii. Mnyampala katika ubeti wa sita anaeleza kuwa:

50. Tumia maji moto, kayachemshe motoni,  
 Chovya nguo msokoto, ukaanike juani,  
 Piga pasi miburuto, ukinyoosha mezani.  
 Chawa hatoki nguoni, shuruti kwa chomo la moto. (uk. 45)

Mnyampala anatoa suluhisho la kuangamiza chawa hao ambalo ni kwa kutumia kwato, maji ya moto na pasi. Mnyampala anasisitiza kupambana na matatizo yaliyopo katika jamii ili kuyatokomeza. Katika taswira hii, dhamira zinazoibuliwa ni kupinga umaskini, unyonyaji na kufanya kazi kwa bidii na maarifa. Ujumbe anaotoa hapa ni kwamba, wananchi wanatakiwa kuwajibika ipasavyo ili kuondokana na hali ngumu ya maisha na kuletea maendeleo ya jamii.

Hali kadhalika, Mnyampala ametumia taswira ya wadudu kama kupe na kunguni pamoja na taswira ya mrija katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*. Mirija imejitokeza katika ngonjera ya “Azimio Lakomesha Mirija” (uk. 47), “Kukata Mirija” (uk. 52), ubeti wa nne unasema:

51. Mwanasiasa  
 Hudhoofisha uchumi, ya mbalimbali mirija  
 Kama vile mbu haumi, kama hana wa kudoja  
 Damu iliyojaa nomi, hufyonza ikavuja  
 Neno *kukata mirija*, kuondoa unyonyaji

Kwa kawaida mrija ni bomba dogo lenye uwazi litumikalo kupitisha vimiminika kama vile juisi, maji, maziwa, damu na vinginevyo. Katika dondoo hili mtunzi ametumia taswira ya mirija kumaanisha unyonyaji na anatuelezea katika shairi hili kuwa maana ya kukata mirija ni kuondoa unyonyaji na kuacha kufuja mali zilizopo ili kuleta maendeleo katika familia, jamii na nchi. Hivyo dhamira tunazopata hapa ni kuondoa unyonyaji ili kuleta maendeleo ya nchi.

Aidha, taswira ya mirija inaendana na taswira ya kupeiliyotumika katika ngonjera ya “Natuondoe Makupe” (uk. 54), ubeti wa nane na wa tisa unasema:

52. Mume

Kaka yako ndiye kupe, anatumyonya nyumbani  
Na kila kitu tumpe, wala hana shukrani  
Madeni mengi tulipe, waleta hawa wahuni  
Heri watoke nyumbani, wote waende shambani

Mke

Na wako pia ni kupe, Azimio labaini  
Linasema tuwakwepe, wasio kazi mjini  
Wanyonyaji tuwatupe, wajitegemee nchini  
Heri watoke nyumbani, wote waende shambani

Katika nukuu hiyo taswira ya kupe imetumika kuwaelezea watu wanaoishi bila ya kufanya kazi na huku wakitegemea watu wengine kwa kila kitu. Watu aliokuwa anawazungumzia katika shairi hilo ni ndugu wenye umri wa kujitegemea waliokuwa wanaenda kuishi kwa ndugu zao mjini, bila ya kuwa na kazi maalumu ya kufanya na kuwategemea ndugu kwa kila kitu. Aidha, Mnyampala katika dibaji (uk. 4) *Ngonjera za UKUTA Na 2*, amejadili taswira ya mirija na makupe kama tuonavyo katika ubeti wa tano usemao:

53. Tatu tuikateni mirija, tuwaondoe hao makupe

Kumbe sisi jasho latuvuja, na wengine kazi wazikwepe  
Mirija yao waje tudoja, tubaki pepe pepe peupe  
Tangu leo hivi tuwakwepe, kunyonyana tusije kufanya

Katika nukuu hiyo, Mnyampala ametumia taswira ya mirija na makupe kusesitiza kuwaondoa wanyonyaji katika jamii zetu. Watu na ndugu ambao hawataki kufanya kazi lakini wanataka kufaidi na kujineemesha kwa jasho la wengine. Hivyo mwandishi huyu anawataka wananchi kushirikiana kuwaondoa wanyonyaji waliopo katika jamii. Hapa mwandishi ametumia wahusika wadudu na vitu visivyo na uhai kama mirija ili kupeleka ujumbe kwa jamii kuwa wanatakiwa kupinga unyonyaji

katika jamii. Matumizi ya wadudu na viumbe visivyo na uhai ni suala ambalo mara nyingi hutumiwa katika fasihi simulizi. Athari za kimwingilianomatini imemfanya Mnyampala kutumia wahusika hao katika kazi yake. Hii inatudhihirishia kuwa fasihi haitoki katika ombwe na mwandishi hutoa mawazo yake kwa kutegemea matini nyingine tangulizi.

Aidha, taswira ya mirija na kupe zimeweza kutumiwa ndani ya vitabu tofauti. Hili pia ni suala la mwingilianomatini baina ya mawazo ya mtunzi. Kwa ujumla mwandishi ametumia taswira za mirija na makupe kuwasilisha dhamira ya unyonyaji, kazi, ukombozi wa jamii na ujamaa na kujitegemea miongoni mwa wanajamii. Ujumbe tunaopata hapa ni kwambatupinge unyonyaji katika nyanja mbaimbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi ili tuweze kuleta maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla. Aidha, kupitia taswira hizo Mnyampala anasisitiza kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi afanye kazi kwa juhudi na maarifa ili aweze kujitegemea na kujikwamua kiuchumi.

Taswira nyingine ni nchi katika shairi la “Nchi Gani Iliyotoweka?” (uk. 55), katika *Diwani ya Mnyampala*. Hii ni taswira ya kufikirika au ya mawazoni kama asemavyo Senkoro (2011) kuwa shairi la “Nchi Gani Iliyotoweka” ni mfano mzuri wa taswira ya mawazoni. Taswira hii inamfanya msomaji awaze juu ya nchi iliyotoweka baada ya dunia kuwapo. Mfano ubeti wa tatu unasema:

54. Ilitoweka machoni, tena haijaonekana,  
Kabisa hionekani, ilikwisha kuponyoka,  
Unitoe mashakani, Mshairi mwaminika,  
Nchi gani ilotoweka, baada dunia kuwa?

Katika dondoo hili tunapata taswira ya kufikirika au kuwazika. Tunajiuliza maswali mengi kichwani ambayo yatatupelekea kujua ni nchi gani ilipata kutoweka tangu misingi ya dunia. Taswira hii inawakilisha imani ya kila mmoja na mazingira yake.

Hivyo taswira hii inatufanya kuhusisha imani na mazingira yanayomzunguka msomaji. Taswira hii kwa Wakristo inaturudisha katika masuala ya dini, kwa mfano katika *Biblia Takatifu*, tunaweza kusema kuwa nchi iliyowahi kutoweka ni ile ya bustani ya Edeni, ambayo ilitoweka baada ya Adamu na Hawa kukiuka masharti waliyopewa na Mungu ya kutokula tunda walilokatazwa. Baada ya kukiuka masharti hayo walifukuzwa katika bustani ya Edeni, hii tunaipata katika Mwanzo 3: 23-24 inasema:

55. Kwa hiyo Bwana Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa. Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kulinda njia ya mti wa uzima.

Kama tuonavyo hapo, binadamu wa kwanza yaani Adamu na Hawa, walifukuzwa katika bustani hiyo, ambayo ilikuwa na amani na raha tele na hadi sasa nchi hiyo haijawahi kuonekana. Kwa upande mwingine Mnyampala ametumia taswira hiyo akimaanisha kutoweka kwa amani katika jamii ni jambo ambalo linaweza kusababisha madhara mengi katika jamii. Kwa hiyo Mnyampala kupitia taswira hiyo kuna dhamira ya dini za kigeni na amani katika jamii. Suala la kuchota maudhui ya imani ya dini za kigeni na kuyasawiri kisanii ni suala la kimwingilianomatini. Kama asemavyo Kristeva (1986) kuwa matini yoyote ni mkusanyiko wa matini mbalimbali za fasihi. Hivyo Mnyampala ametumia taswira hiyo ya kwenye *Biblia Takatifu* kuwasilisha maudhui ya dini yanayohamasisha kutenda matendo mema, kuishi kwa upendo na amani na kulinda amani katika nchi kwa kuwa amani ndio msingi wa mambo yote.

Pia kuna taswira ya kitambi katika shairi la “Kitambi Kiso Pesa” (uk. 69) katika *Diwani ya Mnyampala*. Kupitia taswira hii ya kitambi tunapata picha ya kuona. Mara

nyingi katika jamii inaaminika kuwa mtu mwenye kitambi ana kipato kizuri. Aidha, katika hali halisi mtu anaweza kuwa na kitambi lakini kipato chake kikawa duni. Kadhalika mtu anaweza kuwa na kitambi alichopata kutokana na pesa za wizi, ulaghai ama kuhujumu uchumi. Hivyo kupitia shairi hilo Mnyampala anataka watu wachunguze mtu mwenye kitambi ni mtu wa namna gani. Mnyampala anaeleza kuwa mtu maskini ambaye hana kipato akipata kitambi ni lazima kujiuliza imekuwaje. Mfano katika ubeti wa saba anasema:

56. Kitambi cha masikini, chanishangaza kabisa,  
Hana pato hana tini, hali yake kama kasa,  
Malazi yake ni chini, wala godoro kugusa,  
Kitambi kiso mapesa, hiyo ni ishara gani? (uk. 69)

Hapa Mnyampala anaona kuwa si rahisi kwa mtu ambaye hana pesa kumudu maisha, kwa hiyo akiwa na kitambi itakuwa ajabu kwa jamii. Mwandishi anamaanisha kuwa mtu mwenye kitambi lazima awe na pesa na mara nyingi ni yule anayejishughulisha katika jamii. Lakini kwa mtu ambaye hali yake ni duni hata kupata milo mitatu kwa siku kwake ni vigumu na akiota kitambi ujue anaumwa. Kupitia taswira hii tunapata dhamira ya umaskini, maradhi, unyonyaji na matabaka katika jamii. Vilevile mwandishi anatoa ujumbe kwa wanajamii kujibidiisha ili kuondokana na umaskini katika jamii.

Katika shairi la “Ua hili ua gani” (uk. 85) kuna taswira ya ua. Tunaposoma shairi hili tunapata taswira ya kuona, kugusa na kunusa ua. Ubeti wa tatu na sita zimesaidia kujenga taswira hizo kama tuonavyo hapa:

57. Sio ua la Mdimu, ninalijua zamani,  
 Si la maji zamuzamu, lililopandwa bondeni,  
 Ama lanitia hamu, kuchuma ni mashakani,  
 Ua hili ua gani, ihwani niambieni. (ubeti wa tatu)

Huondoa saumu, ikiwa harufuye puani,  
 Huondoa balaghumu, iliyoshika kooni,  
 Hupooza wataalamu, wafikapo fukutoni, ... (ubeti wa sita)

Kutokana na nukuu hiyo tunapata taswira inayomgusa msomaji anaposoma shairi hilo na kutaka kugusa, kunusa na kuona ua. Ujumbe tunaopata hapa ni kwamba mwanamke ni muhimu katika maisha na anafaa kuthaminiwa. Kupitia shairi hili tunapata dhamira ya nafasi ya mwanamke katika jamii pamoja na mapenzi na ndoa.

Kadhalika, kuna taswira ya taa ambayo mwandishi ameitumia katika *Diwani ya Mnyampala* kwa namna tofautitofauti. Mnyampala ametumia taswira ya taa kutuonesha taa inayowaka na inayozima. Katika shairi la “Taa Mitaa Hung’ara” (uk. 81) taa iliyowaka inamaanisha TANU. Vilevile, taswira hii imetumika kuashiria uhuru wa Tanganyika na jamii katika shairi la “Siraji Ng’aza Siraji” (uk. 135). Kadhalika taswira ya taa imetumika kama taa iliyozima ikiashiria kufa kwa mshairi maarufu mwaka 1962 katika shairi la “Kifo cha Bwana Robert” (uk. 151). Hapa kuna mwingilianomatini wa mawazo ya mwandishi mwenyewe katika kazi zake. Taswira hii ya taa imeweza kuwasilisha dhamira ya uhuru, amani, furaha na kifo.

Kwa mfano, *taa* katika shairi la “Taa Mitaa Hung’aa” (uk. 81) mwandishi anamaanisha nuru iangazayo katika maisha ya mwanadamu hasa baada ya uhuru; taa hiyo anamaanisha TANU. TANU imesaidia kuleta uhuru ambao ni mwanga wa kuleta maendeleo ya nchi. Kwa ujumla, Mnyampala anazungumzia masuala ya chama cha TANU na siasa zake na namna chama hicho kilivyoleta uhuru wa nchi ya Tanganyika. Mnyampala anamaanisha kuwa wakati wa ukoloni nchi ya Tanzania ilikuwa kwenye

giza totoro hivyo TANU ilisaidia kuleta uhuru wa nchi hiyo chini ya kiongozi Mwalimu Julius Nyerere. Katika ubeti wa nne anasema:

58. Taa mulika wachanga, wana wanolia ng'aa,  
Taa lea vifaranga, vile vya kugaa-gaa,  
Taa zifunue kunga, toa na kutapakaa,  
Taa mitaa hung'aa, ndipo kiza kutoweka. (uk. 81)

Hapa Mnyampala anaelezea umuhimu wa taa katika maisha ya mwanadamu. Taa hutumika kuleta mwanga na kuondoa giza ili watu waweze kuonana vizuri. Taa inaleta amani palipo na hofu. Mahali palipo na mwanga hufanya mambo yaende vizuri. Taa huleta uhuru mahali ambapo hakuna uhuru kwa kuwa huondoa vikwazo katika jamii. Kwa upande mwingine taa imetumika kuelezea umuhimu wa uhuru chini ya chama cha TANU. Kwamba chama hicho kitumike kuleta mwanga, amani, uhuru na maendeleo kwa taifa changa kama Tanzania. Hivyo Mnyampala katika shairi hilo anatoa ujumbe kwa chama cha TANU kuwa imara ili kuwezesha taifa changa kama Tanzania pamoja na wananchi kupitia chama hicho kujenga taifa lao. Hivyo mwandishi anaona chama cha TANU kimesaidia sana kuleta mwanga ama uhuru nchini Tanzania. Ndio maana mwandishi ametumia taswira ya taa kumulika mitaani ili mitaa ipate mwanga. Mwandishi alimaanisha kuwa TANU iendelee kuleta mwanga pale ambapo pana giza na kuondoa udhalimu na unyonyaji katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Vilevile, kuna taswira ya 'taa' katika shairi la "Siraji Ng'aza Siraji" (uk. 135). Katika shairi hili, taswira hiyo inaelezea masuala ya uhuru wa nchi kipindi hicho. Siraji na sirati ni maneno ya Kiarabu yanayomaanisha mwanga na njia. Hivyo, katika shairi hilo Mnyampala ametumia taswira hizo akimaanisha nuru ama taa iangaze njia,



maovu au mabaya yasiwakumbe. Mtunzi anataka mwanga uwepo katika jamii ili kusiwepo maovu ndani ya jamii yake. Katika ubeti wa tatu anasema:

59. Mwanzo uwe Dibaji, tena njema na dhati,  
Kwa nyumbani na mahaji, waume na zaujati,  
Kwa Mungu tuwe wachaji, dumu tuwe madhubuti,  
Siraji ng'aza sirati, ghururi isitukumbe. (uk.135)

Katika nukuu hiyo anataka taa itoe nuru au mwanga kwa watu wote waume kwa wanawake na kila mahali ili maovu, ghasia na mabaya yasiwakumbe. Katika ubeti wa nane na tisa Mnyampala anaongelea masuala ya uhuru. Hapa, anamaanisha uhuru na kujitegemea kwa nchi uwe mwanzo endelevu na wenye manufaa kwa wananchi wote. Katika ubeti wa tisa mwandishi anaisifia Tanganyika na kuiombea isije ikawa kama Kongo ambao walikuwa wanapigana wakati huo. Katika shairi hilo Mnyampala anatoa maudhui ya dini, uhuru na amani katika jamii na nchi kwa ujumla.

Kwa upande mwingine taswira ya taa iliyozimika imeashiria matatizo au kifo. Taswira hiyo imetumika katika shairi la “Kifo cha Bwana Robert” (uk. 151) ubeti wa pili usemao:

60. Ni hasara nchi nzima, ninayosema kwa dhati,  
Ni kama taa kuzima, usiku wa katikati,  
Kiswahili tainama, kwa kukosa kalafati,  
Kifo cha bwana Robert, hasara kwa Kiswahili.

Taswira ya taa kuzimika usiku wa katikati inaelezea kifo cha Shaaban Robert aliyefariki mwaka 1962. Taswira hiyo inaonyesha nafasi aliyokuwa nayo Shaaban Robert katika jamii ya kukuza na kuendeleza Kiswahili kupitia fasihi ya Kiswahili. Mnyampala anaona kwamba kifo cha Shaaban Robert kimesababisha Kiswahili na fasihi kwa ujumla kurudi nyuma. Aidha, Mnyampala ametumia taswira hiyo kuelezea namna alivyosikitishwa na kifo hicho cha Shaaban Robert, ambaye alikuwa mtunzi

wa kazi za fasihi hususani ushairi na riwaya. Kupitia taswira ya taa tunapata mwingilianomatini wa taswira moja kutumika katika mashairi mbalimbali ndani ya kazi ya mwandishi mmoja. Tunaungana na wafuasi wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanaoamini kuwa hakuna kazi ya fasihi inayoweza kujitegemea bila ya kuingiliana na matini nyingine. Taswira ya taa imekuwa ikitumika pia katika kazi za fasihi za waandishi wengine kama vile Shaaban Robert, Amri Abedi na Saadani Kandoro.

Taswira nyingine ni bahari kuwaka moto katika shairi la “Bahari kuwaka Moto” (uk. 110), ambapo mwandishi ametumia taswira za vitu vinavyoonekana kuwafanya wasomaji kutafakari zaidi. Kupitia taswira hii tunapata picha ya mawazoni kwa sababu kwa hali ya kawaida si rahisi bahari kuwaka moto. Kwa hiyo, mwandishi kupitia taswira hii anawataka wasomaji kutafakari kwa kina ili kujua kitu anachomaanisha mwandishi anaposema hivyo. Kutokana na taswira hiyo mwandishi anazungumzia maovu, vita, mauaji na machafuko mbalimbali yanayotokea katika maisha. Kwa ujumla, mwandishi katika taswira hiyo anamaanisha machafuko mbalimbali yaliyotokea kipindi hicho. Mfano wa baadhi ya machafuko hayo ni Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia vilivyotokea mwaka 1914-1918 na Vita Vikuu vya Pili vya Dunia vilivyotokea mwaka 1939-1945. Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia vilianza kabla Mnyampala hajazaliwa lakini viliisha akiwa na mwaka mmoja. Vita Vikuu vya Pili vya Dunia vilitokea Mnyampala akiwa kijana. Vita hivyo ni tukio la kihistoria lakini mwandishi analijadili kifasihi. Mwandishi ametumia sanaa ya ushairi kutukumbusha historia ya ulimwengu. Hili ni suala la kimwingilianomatini, kama Allen (2000) anavyoeleza kuwa waandishi hawaundi matini zao kutokana na akili zao za asili, bali wanazitunga kutoka matini zilizopo kwa kiasi kikubwa, matini ni

mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi katika kuunda matini mpya. Katika ubeti wa kumi Mnyampala anasema:

61. Si motoni si peponi, Bahari ina mapito,  
Si Bahari ya Ziwani, Bahari ile ya mvuto,  
Ile kuwa duniani, yenye Ramani ya kwato,  
Bahari kuwaka moto, ajabu ya Buruhani. (uk. 110)

Mwandishi hapa anazungumzia matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii. Anamaanisha kuwa kuna majaribu na misukosuko katika maisha tunayoishi na hali ngumu ya maisha ipo kila mahali. Aidha katika shairi hilo pia kuna taswira zingine nzito alizotumia akielezea kuwa si bahari ya ziwa, bahari ya mvuto, ile kuwa duniani, yenye ramani ya kwato. Katika taswira hizi tunapata picha ya kuona ramani ya kwato ilivyo na kufananisha na bahari aizungumziayo, tunapata maudhui yanayohusu sehemu za maumbile ya siri ya mwanamke. Aidha, katika shairi hili anazungumzia pia dhamira ya mapenzi na ndoa na thamani ya mwanamke katika ndoa, pia kuna vita na ghasia katika maisha. Hivyo kupitia shairi hili tunapata ujumbe kuhusu maisha, Mnyampala anawataka wanajamii kuwajibika vyema katika maisha ili kuondokana na matatizo mbalimbali yanayoweza kupelekea vita na ghasia katika jamii na nchi kwa ujumla. Kadhalika Mnyampala anatoa ujumbe kwa jamii kuwaheshimu wanawake ili kudumisha mapenzi na ndoa zao.

Kwa upande wa *Ngonjera za Ukuta Na. 1*, kwa taswira ya mkopaji na mkopwaji katika ngonjera ya “Mkopo wa Fedha” (uk. 22-24). Mnyampala anazungumzia mikopo katika taswira ya mkopaji na mkopwaji. Kama tunavyoona kupitia ngonjera ya “Mkopo wa Fedha” (uk. 24), katika ubeti wa kumi na nne na kumi na tano, mwandishi anasema:

## 62. Mkopwaji

Saini nimeiona, bali vibaya yakaa  
 Hapa hakupiga kona, kidogo amejikwaa  
 Nitakwenda kumuona, kusahihisha yafaa  
 Hebu njoo Ijumaa, bado nashauri moyo (uk. 24)

Mkopaji  
 Mbona waniherereza, kutwa kutwa majiani?  
 Sasa umenitatiza, sijui nifanye nini  
 Nakuona hutoweza, maneno mengi kinywani  
 Siji tena hunioni, heri kujitegemea (uk. 24)

Katika dondoo hilo na ngonjera nzima tunaona picha ya mkopaji na mkopwaji wakijibizana na namna mkopwaji anavyotoa masharti mengi ili kumkatisha tamaa yule mkopaji. Katika ngonjera hiyo Mnyampala ametumia taswira ya Mkopaji na Mkopwaji ili kuwataka wananchi kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kuweza kujipatia kipato cha kutosha na kukwepa mikopo kwa kuwa ni chanzo cha kudidimiza uchumi wa mtu, jamii na nchi kwa ujumla. Hivyo kupitia shairi hilo tunapata dhamira ya matabaka, ujamaa, kujitegemea, mikopo na kazi. Mwandishi anatoa ujumbe kwa jamii kuwa mtu hawezi kupata maendeleo kwa kutegemea misaada na mikopo kutoka kwa ndugu na jamaa wa karibu. Kila mmoja anatakiwa kuwajibika ili kujipatia kipato chake na kuleta maendeleo katika jamii na taifa kwa ujumla.

Pia kuna taswira ya ulimwengu una nguo katika shairi la “Ulimwengu una Nguo” (uk. 91) katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*. Kwa kawaida nguo hutumika kusitiri mwili wa binadamu. Hivyo tunaposikia ulimwengu una nguo tunapata picha ya mawazoni kwamba ulimwengu umevaa nguo. Hapa mwandishi ametumia taswira kwamba ulimwengu una nguo akizungumzia mabadiliko ya majira ya mwaka katika nyakati na mazingira ya ulimwengu. Mabadiliko hayo yanapotokea husababisha kuwepo kwa majira mbalimbali na hata mabadiliko ya nyakati katika dunia. Mwandishi anaona kwamba mabadiliko hayo yanaufanya ulimwengu kuwa na mchana na usiku, mchana

kunaweza kuwa na jua na usiku mbalamwezi. Mabadiliko ya majira kama vile masika, kiangazi, kipupwe na vuli. Mnyampala ameyawasilisha kwa kutumia taswira ya nguo. Hivyo kupitia taswira hiyo kuna dhamira ya majira ya mwaka, kazi na dini. Hapa mwandishi anaelimisha jamii kuhusu majira ya mwaka na kufanya kazi kulingana na mabadiliko ya majira yanayotokea katika dunia pamoja na kumtanguliza Mungu katika maisha.

Taswira nyingine ni ya *simba* katika shairi la “Ni Nani Simba wa Vita” (uk. 29). Hapa tunapata taswira ya kuona mnyama simba. Simba ni mnyama mwenye nguvu na anayeogopwa na wanyama wengine pamoja na binadamu. Taswira hii imetumika katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, mfano ubeti wa kwanza na wa pili zisemao:

63. Hojaji

Mwenzangu nakuuliza, tafurahi kuambiwa  
 Huyu nani nieleze, jina la Mheshimiwa  
 Na sifaze kutukuza, kama inavyotakiwa  
 Ningependa kuambiwa, ni nani simba wa vita?

Jawabu

Kama ulivyouliza, na kutaka kuambiwa  
 Nani takueleza, na upate furahiwa  
 Ndiye Bunge huongoza, maswali yakajibiwa  
 Ndiye Rashidi Kawawa, Makamu wa Pili huyu (uk. 29)

Katika beti hizi, simba wa vita inawakilisha Rashidi Kawawa ambaye alikuwa Makamu wa Pili wa Rais kwa kipindi hicho. Hivyo tunaona namna ambavyo Kawawa alikuwa na uwezo mkubwa wa kuongoza bunge, wafanyakazi na kusimamia sera zilizowekwa na TANU ili ziweze kutekelezwa. Taswira hii imetumiwa na Mnyampala kurejelea viongozi shupavu wenye uwezo wa kuliongoza taifa pasipo na kutetereka kama Kawawa. Kadhalika, taswira hii ya simba tunaikuta katika vitabu vya dini hususan *Biblia Takatifu* katika Ufunuo: 5:5 inasema: “Na mmojawapo wa wale wazee akaniambia, “Usilie; tazama, Simba aliye kabila ya Yuda, Shina la Daudi, yeye

ameshinda apate kukifungua kile kitabu, na ile muhuri zake saba.” Katika kitabu hicho taswira ya Simba imetumika kumaanisha Yesu ndiye mwenye mamlaka ya kufungua kitabu ambacho wote walishindwa kukifungua. Kwa hiyo, taswira ya simba kujitokeza katika vitabu vya dini na ngonjera za Mnyampala ni suala la mwingilianomatini katika kazi za fasihi. Kwa mujibu wa Clayton na Rothstein (1991) semi mbalimbali katika matini huweza kuingiliana, kukamilishana na kuathiriana. Kwa hiyo nadharia hii inaonyesha jinsi matini zinavyotegemeana, kuathiriana na kukamilishana kwa matini zilizokuwepo awali na zilizopo wakati huo.

Mnyampala katika shairi la “Ni Nani Simba wa Vita” anamfananisha Makamu wa pili wa Rais Rashidi Kawawa na simba. Hapa anamaanisha kuwa Kawawa alikuwa simba wa vita wakati wa uongozi wake kwani alikuwa msitari wa mbele kuendeleza mapambano na matatizo mbalimbali yaliyokuwa yanajitokeza katika serikali ya awamu ya kwanza. Kadhalika, alikuwa simba wa vita katika kuleta maendeleo ya nchi ya Tanzania baada ya uhuru. Vilevile, alikuwa msitari wa mbele kukuza na kuendeleza Kiswahili nchini Tanzania. Hivyo mwandishi anaona kiongozi huyu alikuwa anawajibika na kupambana na matatizo ya nchi bila hofu kwa lengo la kuleta maendeleo ya jamii na nchi ya Tanzania. Hapa tunapata dhamira ya uongozi bora, uadilifu na uajibikaji na uzalendo wa viongozi ndani ya nchi husika. Kwa ujumla kupitia taswira hii tunapata ujumbe kuwa uongozi bora ni nguzo ya maendeleo ya nchi na jamii kwa ujumla. Mnyampala anataka viongozi wawe shupavu kwa kuiga matendo ya viongozi waliokuwa shupavu katika nchi ili kujenga uchumi wa taifa.

Aidha, katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* kuna taswira ya ukungu katika ngonjera ya “Kuhofia Mtihani” (uk.63). Katika ngonjera hiyo Mnyampala ametumia ukungu kama inavyoonekana hapa:

## 64. Mwenye Hofu

Unaonaje mwenzangu, utapita mtihani?  
 Na utatue ukungu, ulioziba nyusoni?  
 Na upate lako fungu, na upate namba wani?  
 Nauofia mtihani, sijui kama tutapita. (Uk. 63)

Jasiri  
 Kitazama ruya zangu, sipati kuzibaini  
 Kama tashinda ukungu, uliotanda machoni  
 Ni heri tumwombe Mungu, tatujalia Manani  
 Tutashinda mtihani, na salama tutapita (Uk. 63)

Katika ngonjera hii tunapata picha ya kuona ukungu uliotanda. Mara nyingi ukungu unapotokea huwezi kuona kilicho mbele. Mara nyingi ukungu hutokea kipindi cha mvua na ukungu huweza kusababisha ajali kwa wale wanaoendesha magari na kuleta madhara mbalimbali. Katika ngonjera hiyo taswira ya ukungu imetumika kumaanisha ukosefu wa elimu (ujinga), wanafunzi wanapata elimu ili kuondoa ujinga (ukungu) waliokuwa nao. Katika ngonjera hiyo taswira ya ukungu imetumika kuibua dhamira ya elimu. Ujumbe tunaoupata ni kuwa elimu ni msingi wa maisha ya binadamu. Aidha, taswira hii ya ukungu pia imejitokeza katika *Diwani ya Mnyampala* katika shairi la “Ukungu Kuziba Mbele” (uk. 22). Katika diwani hii taswira hii imetumika kuelezea matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii. Kwa hiyo mwandishi anawataka wananchi watafute namna ya kuondokana na matatizo yaliyopo katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni. Kwa kufanya hivyo wataweza kuleta maendeleo ya nchi yao kwa manufaa ya wote. Taswira moja kutumika katika matini zaidi ya moja ni suala la kimwingilianomatini. Barmford (2011) anafafanua kuwa hakuna matini inayoweza kustahimili bila kutegemea mtandao wa kimauhusiano wa matini nyingine za fasihi.

Taswira nyingine iliyotumika ni *mwenye nyumba* katika ngonjera ya “Visa vya Mwenye Nyumba” (uk. 86) katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, mfano ubeti wa pili usemao:

65. Mwenye Nyumba

Nikipata mwingine, azidishaye mapesa  
Anipe hesabu nene, moyo wangu kutakasa  
Yule budi tugombane, kwa ghasia na ufyosa  
Kila njia tamtesa, na ndani kumfukuza

Katika nukuu hiyo tunapata picha ya namna mwenye nyumba anavyowanyanyasa wapangaji wenye kipato kidogo. Taswira ya mwenye nyumba inatuonyesha kuwa mwenye nyumba ana tamaa ya pesa na hana utu. Kutokana na ngonjera hiyo tunaona namna mwenye nyumba anavyowabagua wapangaji wake kutokana na kipato chao na tamaa ya pesa. Katika ngonjera ya “Mwenye Nyumba na Mpangaji” (uk. 87-88) mwenye nyumba anamfukuza mpangaji wake ili kumweka mwingine mwenye pesa zaidi. Kupitia taswira hii tunapata dhamira ya utu, haki za binadamu, upendo na ubinafsi miongoni mwa wenye nyumba. Pia inatoa ujumbe kuwa tamaa haifai katika maisha. Aidha, utu wa binadamu ni bora zaidi kuliko pesa na binadamu wote ni sawa, hivyo inatakiwa kuwaheshimu watu wote bila ya kuangalia kipato cha mtu.

Vilevile kuna taswira ya *mpangaji* katika ngonjera ya “Vitimbi vya Mpangaji” (uk. 88-89) katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*. Mfano ubeti wa tatu na nne unasema:

66. Mwenye Nyumba

Maneno mengi sitaki, toa pesa humu ndani  
Mbona ngomani huchoki, daima uko dansini?  
Kulewa hakukatiki, kila mara ulevini  
Ugomvi sitaki ndani, tafadhali lipa kodi

Mpangaji

Bughudha yako sitaki, mimi si wako mtani  
Na kodi hailipiki, natufike mashtakani  
Na humu ndani sitoki, nione tafanya nini?  
Sina fedha mfukoni, za kulipa kodi



Katika taswira hii tunapata picha ya kuona mpangaji jeuri, mtata ambaye hataki kulipa kodi na hatimaye kuibua ugomvi na mwenye nyumba. Katika jamii yetu wapo wapangaji wa namna hii ijapokuwa ni wachache. Mara chache huweza kutokea mpangaji aliye mkorofi. Katika taswira hii dhamira ya utu, kufuata taratibu za upangaji na kuwajibika katika maisha. Kadhalika, tunapata ujumbe kuwa wenye nyumba wawe waangalifu kwa wapangaji wanaowapangisha. Pia mwenye nyumba na mpangaji, kuwepo na sheria na taratibu zinazowaongoza ili kila mmoja atimize wajibu wake ipasavyo.

Katika mswada wa *Mashairi ya Vidato* pia kuna taswira ya kipimo katika shairi la “Kiasi” (uk. 3). Katika shairi hilo mwandishi anasisitiza kuwa kila kitu kifanyike kwa kiasi. Katika shairi hilo Mnyampala amezungumzia dhamira ya mapenzi, uvumilivu, wema na huruma kwa jamii. Ujumbe tunaopata kutokana na shairi hili ni kwamba kila kitu kikizidi hugeuka kuwa kichungu, hivyo kila kitu katika maisha kifanywe kwa kiasi. Kuwe na kipimo cha wastani katika utekelezaji wa majukumu katika jamii. Mnyampala anasema hayo katika ubeti wa kumi na mbili, kiitikio chake kinasema: “Kipimo kingi sizidi, kisijepita Kiasi” (uk. 3) katika beti zote amepigia msitari neno kipimo na kiasi, kuashiria kuwa kila unachokifanya kwa mfano ukarimu, kazi, upendo, mapenzi na vinginevyo vyote vitendeke kwa wastani. Taswira hii inakwenda sambamba na taswira ya mizani iliyotumika katika *Ngonjera za UKUTA Na. 2*, ngonjera ya “Ni Yapi Mapishi Bora?” Mnyampala ametumia taswira ya mizani katika ubeti wa pili, nne, sita na wa saba. Katika ubeti wa saba (uk. 20) mshauri anasema:

#### 67. Mshauri

Mayai kweli matamu, ni kitu chenye thamani  
 Kwa afya kitu muhimu, huleta siha mwilini  
 Bali hutaka elimu, na kipimo cha mizani  
 Mapishi yawe mizani, ya leo hutia afya (uk. 20)

Hapo mwandishi anawaasa watu kula vyakula bora vyenye mchanganyiko wa madini mbalimbali na kuwa na kipimo sahihi katika ulaji wa vyakula hivyo, kwa kuwa kila kitu kikizidi ni hatari kwa maisha ya binadamu. Kupitia taswira ya *kipimo* na *mizani* katika ubeti na shairi hili tunapata dhamira ya mapishi, ukarimu, upendo, uaminifu, kazi na utu katika maisha. Matumizi ya taswira ya mizani na kipimo katika diwani tofautitofauti za Mnyampala yanasawiri vyema Nadharia ya Mwingilianomatini ndani ya kazi zake mwenyewe. Kazi ya fasihi hutokana na fasihi yenyewe (Wamitila, 2008). Kwa kawaida mwandishi yeyote wa fasihi ni msomaji wa matini zingine za fasihi. Hivyo, kazi zake hubeba athari za kila aina kutoka katika muktadha wa mtunzi na matini zingine andishi na simulizi ama zungumzwa.

Vilevile, katika *Mashairi ya Vidato* kuna taswira ya kitung’ati katika shairi la “Kitung’ati” (uk. 7). Mnyampala (1966) anaeleza kuwa kitung’ati ni mtu shujaa sana na mwenye elimu ya kuongoza majeshi yakafaulu katika vita vyao. Hii ni taswira inayoonekana akilini mwa msomaji wa kazi ya fasihi. Hivyo kupitia neno kitung’ati tunapata picha ya mtu shupavu, jasiri, hodari na mzalendo katika nchi yake. Mwandishi ameitumia taswira hiyo kuwakilisha viongozi wazalendo katika nchi za Kiafrika. Viongozi ambao huweza kupamabana na kila hali inayowakabili katika mataifa yao kwa manufaa ya taifa zima. Mfano ubeti wa kumi unasema:

68. Nguvu moja kusimama, adui zetu kushinda,  
 Adui watatu kona, wanenepe walikonda,  
 Kazi yetu kusakama, tuwapige na kuwaponda,  
 Ndivyo anavyopenda, mtukufu Kitung’ati. (uk. 7)

Kupitia nukuu hii tunapata picha ya kiongozi anayejituma katika kuongoza taifa lake, mfano Rais wa Tanzania Mwalimu Julius K. Nyerere wakati wa kupigania uhuru wa nchi na mawazo yake ya kuikwamua nchi kutoka katika umaskini, ujinga na maradhi.

Mwandishi anaonyesha kwamba kiongozi huyo alikuwa mfano wa kuigwa katika jamii kwa kuwa alikuwa jemedari hodari na uongozi wake ulitukuka katika mataifa mengi. Katika shairi hili taswira hii imetumika kuibua dhamira za uzalendo, uongozi bora, maadili, umoja, mshikamano na uhuru wa nchi. Kadhalika mwandishi anatoa ujumbe kwa jamii na viongozi wa umma kuwa wazalendo katika nchi zao ili kujenga taifa lenye maendeleo na kujitegemea katika nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Katika mswada wa *Mashairi ya Vidato* kuna taswira ya kifo cha Kennedy katika shairi la “Kuuawa kwa Kennedy” (uk. 5) ubeti wa sita usemao:

69. Yuko wapi Mahatma, wa India Mashariki,  
Ijapo alisimama, hadi kujitia dhiki,  
Hakuambua la wema, kauawa hamaki,  
Tunakuomba Maliki, umrehemu Kennedy. (uk. 5)

Katika nukuu hii picha iliyojengwa akilini mwa msomaji ni ya Kennedy ambaye amekufa. Katika shairi hili Mnyampala anamzungumzia Kennedy ambaye alikuwa Rais wa nchi ya Marekani. Kiongozi huyu alikuwa na hekima na mwenye kufuata misingi ya utu wa binadamu na asiyependa ubaguzi wa rangi. Katika taswira ya kifo cha Kennedy, mwandishi anasisitiza dhamira ya viongozi kupenda uzalendo, utu, uwajibikaji, kupinga ubaguzi na kupenda amani ndani ya nchi zao. Kwa ujumla, Mwandishi anatoa ujumbe kwa viongozi kuwa kiongozi hapaswi kutumia utawala wa mabavu bali anatakiwa kuwa mfano bora kwa jamii, mwenye kujali utu wa binadamu na kufuata misingi ya haki za binadamu.

Taswira nyingine ni miba katika shairi la “Mtaka Nyingi Nasaba” (uk. 7). Miba ni kitu chenye ncha kali ambacho mara nyingi huota porini na huweza kumchoma mtu asipokuwa makini. Hapa picha inayojengeka akilini ni ya kuona miba inayochoma na

kuleta maumivu makali katika mwili wa mnyama akiwemo binadamu. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

70. Ukarimu unaponza, hutia ndani ya *miba*,  
 Pengine huleta manza, ulie ‘Ya Rabi Toba’,  
 Ya dunia huwafunza, wana kuleta misiba,  
 “Mtaka nyingi nasaba, Hupata mingi misiba” (uk. 7)

Kupitia nukuu hii taswira ya miba imetumika kumtahadharisha mwanadamu kuwa mwangalifu na watu anaoishi nao. Mwandishi anasisitiza kuwa ukarimu ukizidi huponza na huweza kumtia mtu katika matatizo na kuleta majuto katika maisha. Hapa mwandishi anaelimisha wanajamii kuwa waangalifu katika mahusiano kwani mahusiano mabaya katika jamii huweza kusababisha simanzi, majuto na maumivu kwa baadhi ya watu. Kwa kawaida miba imchomapo mtu hupata maumivu makali na wakati mwingine huweza kusababisha kifo. Dhamira tunayopata hapa ni maadili, usaliti, utu, kuacha ubinafsi na tamaa katika maisha. Hivyo mwandishi anawataka watu wawe makini kwa yale mema wayatendayo na kila jambo linafaa kutendwa kwa kiasi.

Kutokana na mjadala uliofanywa hapo juu, tumebaini kwamba mbinu ya taswira imejitokeza zaidi katika *Diwani ya Mnyampala* na kufuatiwa na vitabu vyake vingine. Taswira zilizojitokeza ni za kuona, kuonja, kuhisi na kufikirika. Aidha, taswira hizo zimejengwa katika mtindo wa mwingilianomatini, kwani zinaingiliana na kukamilishana. Mbinu hii imejitokeza kimwingilianomatini, kwa kuwa baadhi ya taswira zimejitokeza katika mashairi tofauti na hata katika vitabu tofauti zikiashiria maana moja ama tofauti. Ujitokezaji huo ni wa kimwingilianomatini, kwa kuwa hakuna mwandishi wa kazi ya fasihi anayeweza kuumba kazi yake bila kutegemea mazingira yanayomzunguka na kazi tangulizi. Kwa ujumla kazi zote zilizojadiliwa ni

zile zilizoandikwa na Mnyampala kadhalika kuna mwingilianomatini wa maudhui ndani ya taswira zilizotumika. Pia, kuna mwingilianomatini wa kazi za mwandishi na vitabu vitakatifu vya dini, mfano Biblia. Mnyampala ametumia vyema kipengele cha taswira kuibua ujumbe na dhamira mbalimbali.

#### **4.1.2 Methali**

Methali ni mbinu nyingine inayotumiwa na waandishi wa fasihi kuibua maudhui ya kazi husika kwa kuvuta hisia kwa wasomaji wa kazi ya fasihi. Balisdya (1987) anasema kuwa methali ni misemo itumiwayo kuelezea kitu kwa njia ya picha na kwa ufupi ili itoe maadili na onyo fulani kwa jamii. Naye Amuka (1992) anaeleza kuwa methali ni ufupisho wa masimulizi yanayoweza kuelezewa kwa namna tofautitofauti. Anafafanua zaidi kuwa methali ni namna ya ndani zaidi ya ile inayoonekana, na huweza kutumika kuibua hadithi au ngano. Maelezo ya Amuka yanamaanisha kuwa methali moja huweza kuibua maudhui au maana tofauti kulingana na muktadha ama mazingira inamotumika. Kadhalika methali huweza kuwa ufupisho wa kisa kilichotendeka huko nyuma.

Maelezo hayo ya Amuka yanatudhihirishia kuwa methali zinatokana na muktadha wa matukio maalum yanayotokea katika jamii. Mulokozi (2017:66) anafafanua kuwa methali ni “usemi mfupi wa kimapokeo unaodokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yatokanayo na tajiriba (uzoefu wa maisha) ya jamii inayohusika.” Kutokana na mawazo ya Mulokozi, methali zinapatikana katika jamii na huzungumzia uzoefu wa maisha ya jamii husika. Kadhalika, Maitaria (2011) anaeleza kuwa ni kauli zinazoakisi maoni, mwelekeo na utamaduni wa jamii. Wanafafanua zaidi kuwa methali mara nyingi hutumika kutoa mafunzo na kuelimisha jamii kwa kuonya, kumwongoza mtu na kumbadilisha mtu katika mwenendo mbaya aliokuwa akienda

hapo awali. Kutokana na mawazo ya wahakiki hao, methali ni aina moja ya usemi mzito na ambao unakusudiwa kusema jambo maalum lakini kwa namna ya fumbo.

Methali kama kipengele cha lugha ya kimapokeo ya jamii, aghalabu hutumiwa mno katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili (Ligami na Barasa 2001 na Maitaria, 2017). Sababu ya kutumia methali kwa baadhi ya watunzi ni kuwa methali katika jamii huchukuliwa kama misemo ya hekima na busara inayobuniwa na kutumiwa kimapokezi katika mawasiliano ya jamii husika. Kwa hiyo Mnyampala ametumia methali kuwasilisha mawazo yake kuhusu busara au hekima kwa wanajamii. Aidha, methali kwa kiasi fulani ni dhihirisho la mwingiliano wa matini unaojitokeza katika utamaduni wa jamii maalum.

Kutokana na mawazo ya wataalamu hao methali ni kipengele ama kipera cha utanzu wa semi ambao ni mojawapo katika tanzu za fasihi simulizi. Hakuna kazi ya fasihi inayoweza kujitosheleza pasipo kutegemea kazi nyingine ili kuibuka kwa kazi husika, hivyo fasihi hutokana na fasihi yenyewe (Wamitila, 2008). Hivyo basi watunzi mbalimbali wa fasihi andishi, akiwemo Mnyampala, wanachota methali zilizopo katika jamii zenye kubeba maudhui anuwai kwa jamii. Katika kazi teule za Mnyampala methali zimetumika sana kuibua maudhui mbalimbali ndani ya kazi hizo. Lengo la matumizi ya methali hizo ni kumfanya msomaji wa mashairi hayo kupata maudhui na kuelewa ujumbe unaotolewa na mtunzi.

Williams (1974) anaeleza kuwa katika kazi za Mnyampala, falsafa za mwandishi ni nyingi kama yalivyo maadili pia. Anaongezea kuwa mawazo ya Mnyampala huonekana kutokana na mazingira na aina ya mashairi yenyewe, ikiwa ametumia methali kuandika shairi basi na falsafa yake itapatikana ndani ya hiyo methali. Naye, Mlacha (1981 na 1985) anasema kuwa, kwa kawaida methali zipo kwa nia ya kufunza

na kuwarekebisha watu ambao wametoka nje ya taratibu na misimamo ya imani ya jamii husika. Kutokana na mawazo ya watalamu hao, tunaweza kusema kuwa methali zilizomo katika kazi teule za Mathias Mnyampala zina dhamira za kuelimisha, kuadabisha, kutunza historia ya jamii na kusawiri falsafa ya mtunzi. Aidha, utafiti huu tumeshughulikia dhamira na ujumbe unaoibuliwa na methali zilizotumiwa na Mnyampala katika kazi teule. Vilevile, katika uchambuzi huu kuna mwingiliano matini wa utanzu wa fasihi simulizi (methali) na kazi teule za ushairi wa Mnyampala zilizotumia methali kuibua maudhui yake.

Katika *Diwani ya Mnyampala* (uk. 34), shairi la “Mtumikie kafiri” ubeti wa pili katika kiitikio kuna methali isemayo ‘mtumikie kafiri ili upate mradi’. Neno ‘kafiri’ asili yake ni lugha ya Kiarabu. Lina maana kuu mbili: maana ya jumla na mahsusuni. Maana ya jumla linamaanisha mtu mkanushaji au mpingaji wa jambo lolote. Maana mahusuni linatumika katika muktadha wa kidini kumaanisha mtu asiyeamini mahubiri na mafunzo ya dini, hususani dini ya Kiislamu<sup>42</sup>. Kupitia methali hii mwandishi anatoa mafunzo kuwa wakati wa shida hutakiwi kuchagua ni nani awezaye kukusaidia, inatakiwa kumuendea mtu yeyote ambaye yupo tayari kukusaidia bila kujali dini ama kabila lake. Vilevile hata katika kazi hutakiwi kuangalia ni nani unayemtumikia bali unatakiwa kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili upate faida kutokana na kazi hiyo. Kwa mfano ubeti wa tatu wa shairi hilo unasema:

71. Nawe upate mradi, mtumikie kafiri  
 Yapasa ujitahidi, uiname kwa tajiri,  
 Tumika uwe sitadi, kwake alokuajiri,  
Mtumikie kafiri, ili upate mradi. (uk. 34)

Kupitia methali hii mwandishi anahamasisha watu wawajibike ipasavyo katika sehemu mbalimbali walizoajiriwa. Katika shairi na methali hii kuna dhamira ya kazi,

<sup>42</sup>Maana ya kafiri tumeitoa katika mahojiano baina ya Mtafiti na Mzee Mahmoud Hamsini Mubiru tarehe 15/7/2016, Dar es Salaam.

wajibu na matabaka. Hapa Mnyampala anatoa ujumbe kwa wanajamii kuwaheshimu waajiri wao na kufanya kazi kwa bidii ili waweze kufanikiwa. Anawataka wanajamii kushirikiana na waajiri wao ili waweze kupata faida. Naye Gibbe (1978) anaeleza kuwa msimamo wa Mnyampala katika methali hii haukuwa sawa na imara kwa kuwa aliwahubiria wasomaji wake kushirikiana na waajiri (Wakoloni) ili wapate mradi wao. Anaongezea kuwa kitu ambacho kingefaa kusesitizwa hapo ni kupinga ukoloni na kuziasi kazi za hao waajiri, ili kukitumikia vyema chama chao cha ukombozi (TANU). Gibbe anasema kwamba Mnyampala alitakiwa kuwahamasisha watu kupinga ukoloni kwa nguvu zote kama alivyofanya Mwalimu Julius K. Nyerere alipoamua kuacha kazi ya ualimu ili aweze kujishughulisha vyema na chama cha siasa cha TANU. Tunaungana na maelezo ya Gibbe kuwa ili kufanikisha ukombozi wa nchi ni lazima mtu au viongozi wajitoe na kuwa tayari kulinda na kutetea nchi yao. Katika methali hii dhamira zinazoibuliwa ni matabaka, dini, ushirikiano baina ya waajiri na waajiriwa na kufanya kazi kwa bidii ili kuondokana na ukoloni mamboleo.

Methali nyingine ni ‘mkaidi hafaidi, hadi Idi kufika’ katika shairi la “Bingwa anapokwambia” (uk. 42). Ubeti wa kwanza unasema:

72. Mkaidi hafai, hadi idi kufika,  
 Hupiga yake fuadi, wengine awabeua,  
 Kwa hiyo hujitahidi, na mwepesi kuumia,  
 Bingwa anapokuambia, usizidi kukaidi.

Hapa Mnyampala anasisitiza kuwa watu waheshimu wakubwa na kuwatii pale wanapotoa mawaidha ya maisha. Kaidi ni neno lenye asili ya Kiarabu, maana yake ni upinzani au kwenda kinyume na taratibu zilizopo katika jamii. Mnyampala anawausia watu wote katika rika zote kuwa ukaidi haufai katika nyanja zote za maisha ya mwanadamu. Kupitia methali hii tunapata dhamira za dini, utii, maadili, nidhamu na tabia njema katika jamii. Methali hii inahimiza watu wote hasa watoto kuwa na tabia



nzuri na kuwaheshimu wakubwa ndipo watapata neema na mema duniani. Ujumbe utolewao ni kwamba, ukaidi katika jamii si kitu chema na ni tabia isiyofaa katika jamii kwa kuwa ukaidi huweza kusababisha matatizo na kukosa mambo mengi mazuri katika jamii.

Methali nyingine ni ‘kibaya kina wenyewe ingawa chanuka shombo’ inayopatikana katika shairi la “Kibaya Kina Mwenyewe” (uk. 1). Methali hiyo imetumika kama kibwagizo kwa kila ubeti ndani ya shairi hilo ili kuisitiza dhamira ya uvumilivu, ubinafsi na upendo kwa watu wote katika maisha. Aidha, mwandishi anatoa ujumbe kwa jamii namna ya kuishi na watu vizuri kwa kuvumiliana katika mambo mbalimbali yanayotokea katika jamii. Mfano katika ubeti wa nne unasema:

73. Kwa ubaya wa majambo, nami hupata kiwewe!  
Haambiwa kina nembo, kimetobolewa ndewe,  
Nami husema marembo, ya mila yangu mwenyewe  
Kibaya kina mwenyewe, ingawa chanuka shombo. (uk. 1)

Methali ya ‘kibaya kina wenyewe ingawa chanuka shombo’ inamaanisha kuwa hakuna kitu au mtu mbaya akakosa kuhitajika katika maisha, ama hakuna kibaya kisichokuwa na mwenyewe. Methali hii imetumika kuibua ujumbe kwamba hatupaswi kudharau kitu au mtu kwa sababu ya kasoro alizonazo. Mwandishi anatolea mfano wa tamaduni zetu zilizodharauliwa na wakoloni, anasisitiza kuwa hata kama wakoloni wanaona tamaduni zetu ni mbovu lakini sisi tunaona zinatufaa.

Pia Mnyampala anazungumzia ukatili wa wanawake kupitia methali ya ‘kibaya kina wenyewe ingawa chanuka shombo’ (ubeti wa kumi). Mnyampala anamzungumzia mama wa kambo anavyomlea mtoto ambaye si wake kwa mateso makali. Mwandishi anatoa ujumbe kuwa, ukiwa na mtoto wa mwenzako mpatie malezi mazuri maana kwa kumlea vizuri anaweza kukufaa katika shida na raha maishani mwako. Hivyo

katika ubeti huo kuna dhamira ya malezi na upendo. Hapa mwandishi anasisitiza upendo kwa watu wote maana huwezi kujua baadaye ni nani atakayekufaa maishani mwako. Ujumbe tunaopata hapa ni kwamba kila kitu ulichonacho ni vyema kukithamini. Mwandishi anaiasa jamii kuthamini utamaduni wa jamii, hata kama unapuuzwa na Wazungu, tusikubali kupotoshwa na wakoloni. Vilevile, methali hii inatufunza umuhimu wa kuridhika na vitu tulivyonavyo kwa kuwa vinaweza kutufaa wakati wowote ule, tofauti na vitu ambavyo si vyetu.

Katika shairi la “Mali Mfano Maua” (uk. 11) kuna methali isemayo ‘mali mfano maua’ ikimaanisha kuwa mali ni sawa na maua. Maua mara nyingi huchanua na kunyauka. Hivyo mali pia hulinganishwa na maua kwamba leo unaweza kuwa na mali na kesho ukapoteza mali zote kwa wakati mmoja. Hivyo, kupata na kukosa mali ni kitu cha kawaida duniani. Katika shairi hili mwandishi ametumia methali mbili zinazokamilishana, yaani ‘mpanda ngazi hushuka’ na ‘mali mfano maua’ ili kufikisha dhamira zinazohusu utajiri na matabaka yaliyopo katika jamii. Hili limejitokeza katika ubeti wa nne usemao:

74. Tuache kudanganyika, sikia ndugu sikia,  
Fukara hutajirika, na tajiri kufifia,  
Mpanda ngazi hushuka, wahenga waliusia,  
Mali mfano maua, hichumwa na kunyauka.

Kwa kupitia methali hizi mwandishi anaitaka jamii kuwa makini na mali wanazozipata. Mtu akipata anatakiwa asijivune na kuwadharau wengine bali awaheshimu na kuwasaidia wengine pale inapobidi. Mnyampala anagusia masuala ya utawala, kuwa mtu anaweza leo akawa kiongozi na kesho asiwe kiongozi. Mwandishi anatoa wosia kwa viongozi kutoyumba wala kujisikia vibaya wanapotoka madarakani na kusikia kashifa kutoka kwa raia waliokuwa wakiwaongoza. Mnyampala

anayasema haya katika ubeti wa kumi wa shairi hili. Aidha, katika methali ya “Mali Mfano Maua” Mnyampala anasisitiza kuwa kila kitu kinatoka kwa Mungu. Kupitia methali hii tunapata dhamira ya utajiri, uongozi bora, dini na utu kwa watu wote. Mtunzi anatoa ujumbe kuwa mali haidumu, ijapokuwa si wote ambao hufilisika kama mwandishi anavyosema katika ubeti wa mwisho. Aidha, viongozi na watu wenye mali wanatakiwa kuishi vizuri na jamii inayowazunguka ili kuifanya kesho yao kuwa njema.

Katika shairi la “Simbuko Halisimbuki” (uk. 13) kuna methali iitwayo ‘simbuko halisimbuki hadi kwa mkukuriko’. Hili linadhihirika katika ubeti wa pili unasema:

75. Haisimbuki simbiko, hadi vita kwa tiriki,  
Panga vatie matiko, wachimbue visiki,  
Waondowe hangaiko, kufunga kile na hiki,  
Simbiko halisimbuki, hadi kwa mkukuriko.

Katika shairi hili, methali hii imetumika kuelezea matatizo mbalimbali yaliyopo katika jamii kama vile ukosefu wa haki, kutosikilizana, mila potofu na dini. King’ei na Ndal (2008) wanaeleza kuwa simbiko ni uzi wa ndoana ambao unakuwa na fundo lililofundikwa karibu na ndoano na fundo hilo haliwezi kufunguka kamwe bila kurushwarushwa au kufunguliwa kwa makusudi. Hivyo, kupitia methali hii Mnyampala anasisitiza wanajamii kushirikiana kuondoa matatizo yaliyopo katika jamii. Vilevile Mnyampala anahamasisha umoja na mshikamano baina ya watunzi wa kazi za ushairi wa Kiswahili. Mnyampala anasisitiza kuwa hata kama wanajamii au watunzi wanatofautiana kwa dini au hoja zao, haitakiwi kutengana bali wapatane na kuvumiliana. Kupitia methali hii tunapata dhamira ya haki za binadamu, ndoa, ujane, ushirikiano, umoja na mshikamano baina ya watunzi, dini na kuwa na urafiki wa kweli baina ya wanajamii. Ujumbe ni kwamba umoja ni msingi wa maendeleo katika jamii.

Methali nyingine inayopatikana katika shairi la “Mcheza Hawi Kiwete” (uk. 15) kuna methali isemayo ‘mcheza hawi kiwete, ngoma yataka matao’. Ubeti wa tatu unaosema:

76. Mchezo wataka tao, na mabega wachanyate,  
Wazunguke bila kao, na moyoni wasisite,  
Twache wajikokotao, hawapendezi kwa wote  
Mcheza hawi kiwete, ngoma yataka matao. (uk. 15)

Katika shairi hilo methali ya ‘mcheza hawi kiwete, ngoma yataka matao’, neno matao limefafanuliwa na Wamitila (2001) kuwa ni mbwembwe na machachari ya mchezaji wa ngoma. Wamitila anaeleza kuwa methali hii inamaanisha kuwa mtu yeyote anayecheza ngoma hapaswi kuwa kiwete kwa kuwa ngoma inahitaji kutumia nguvu na maarifa mengi. Mnyampala katika shairi hili ametumia methali hiyo kuibua dhamira ya kazi kuwa kila kazi inahitaji kufanywa kwa juhudi na maarifa na mtu yeyote lazima ajitolee katika kazi ili aweze kufanikiwa maishani. Ujumbe tuupatao hapo ni kwamba kila jambo tunalotaka kulifanya katika maisha la kuleta maendeleo lazima kulifanya kwa kujitolea na juhudi zote bila ya ulegevu.

Katika shairi la “Kila Chombo na Wimbile” (uk. 16), kichwa cha shairi hilo ni methali. Hivyo kuna methali isemayo ‘kila chombo na wimbile’. Kama tuonavyo katika ubeti wa tatu unasema:

77. Kila kitu na pambole, si nyumba wala si banda,  
Hujazana watu tele, na askari kulinda,  
Hubomoka paziale, na kukatika mikanda,  
Kama chaja kitakwenda, kila chombo na wimbile.

Mnyampala katika shairi hili lenye kuwasilishwa na methali hii imaanisha kuwa kila kitu huwa na aina yake ya misukosuko ambayo huweza kukifanya kitu hicho kwenda vizuri au kwenda vibaya. Mwandishi anamaanisha kuwa misukosuko katika jamii ni

jambo la kawaida. Na kama jambo limekuja kwa ugumu ama misukosuko litakwenda kwa misukosuko hadi kufikia mafanikio. Hivyo, hakuna maendeleo yasiyo na misukosuko ijapokuwa misukosuko inatofautiana. Kwa hiyo, anatoa mawaidha kwa viongozi kuwa kila mtu ama kitu kina sifa yake, hivyo haifai kuiga ama kumlazimisha mtu kufanya jambo ambalo haliwezi. Misukosuko katika jamii ni jambo la kawaida, hivyo yafaa kupambana nayo kwa kutafuta njia ya kuondokana nayo. Mwandishi anawaasa wanajamii kufanya kazi zile ambazo wana uwezo wa kuzifanya. Katika shairi hili pia kuna methali inayokamilishana na methali hiyo isemayo “nyani haoni takole.” Methali hii inapatikana katika ubeti wa tisa wa shairi hili unasema:

78. Nyani haoni takole, kwa mpevu na makinda,  
Kwa chabuo lau chale, hucheka kafata tunda,  
Basi kwa methali zile, zinamsuta mponda,  
Kama chaja kitakwenda, kila chombo na wimbile. (uk. 17)

Hapa mwandishi anamaanisha kuwa nyani haoni utupu wake. Katika methali hii tunapata ujumbe kuwa tujitathmini na kuona makosa yetu kabla ya kuwakosoa na kuwalaumu wengine. Kupitia methali hizi tunapata dhamira ya upendo, utu, maadili, uvumilivu, kuondokana na ubinafsi na kujitathmini.

Methali nyingine ni ‘tusitukane wakunga na uzazi ungalipo’ katika shairi la “Tusitukane Wakunga” (uk. 17). Ubeti wa wa pili wa shairi hilo unasema:

79. Uzazi hajasimama, twatukanaje wahenga?  
Mwiba ukitusakama, na machungu kutuzinga,  
Tutakuja pata homa, tudharaupo nyanya,  
Tusitukane wakunga, na uzazi ungalipo.

Katika shairi hili maana ya methali hii ni kwamba kama uzazi bado upo hupaswi kutukana wakunga kwa kuwa utaendelea kuwahitaji kukusaidia wakati wa kuzaa. Methali hii inatupa dhamira ya uzazi, malezi na heshima kwa watu wote. Kwa upande wa ujumbe ni kuwa haitakiwi kukorofishana na mtu ambaye unajua utamhitaji kwa

msaada hapo baadaye. Hivyo basi, tunaweza kusema kuwa katika maisha ya mwanadamu ni lazima kuwa na marafiki na watu wote kwani huwezi kujua wakati wa dhiki ni nani atakayekusaidia.

Methali nyingine ni ‘situpe ubaharia sababu ya unahodha’ inayopatikana katika shairi la “Situpe Ubaharia” (uk. 19). Ubeti wa kwanza wa shairi hilo unasema:

80. Ndugu sikia waidha, wasia ninaokwambia,  
Ulimwengu una adha, pima utashuhudia,  
Ridhika na yako ridha, sije kile kurukia,  
Situpe ubaharia, sababu ya unahodha. (uk. 19)

Mnyampala ametumia methali hii kutoa mawaidha ya maisha, akimaanisha kuwa mtu asije akapuuza kile alichonacho kwa sababu ya kitu kingine akionacho mbele yake. Kupitia methali hiyo kuna dhamira ya tamaa na dharau, mwandishi anawataka watu kuacha tamaa ya vitu vikubwa wakati uwezo wa kuvipata hawana. Kwa hiyo anatoa ujumbe kuwa tusidharau ama kutupa vitu tulivyonyavyo kwa sababu ya vile tulivyonyavyo ambavyo bado hatujavipata.

Methali nyingine ni ‘muenda omo na tezi, marejeo ni ngamani’. Methali hii inapatikana katika shairi la “Muenda Omo na Tezi” (uk. 20). King’ei na Ndal (2008) wanaeleza maana ya tezi kuwa ni sehemu ya mbele ya jahazi naomo ni sehemu ya nyuma na ngama ni sehemu ya katikati wanapoketi abiria. Wanaendelea kueleza kuwa katika jahazi abiria anayetangatanga kwa kwenda mbele au nyuma ya jahazi mwisho hurudi na kuketi katikati walipoketi abiria wenzake. Methali hii inamaanisha kuwa katika maisha watu wanaohangaika na kujidai ni wajuaji zaidi mwisho wao ni aibu na hujikuta wakirudi palepale walipokuwa wanastahili kuwa. Hivyo katika maisha inatakiwa kuwaheshimu watu wote, maana ujuaji mwingi mwisho wake ni majuto.

Pia ndani ya shairi hilo la “Muenda Omo na Tezi” kuna methali nyingine katika ubeti wa tano isemayo ‘achumiaye juani hwenda lia kivulini’. Ubeti huo unasema:

81. Achumiaye juani, kwa methali ya walezi,  
Hwenda lia kivulini, falau wali kwa nazi,  
 Na ndipo pumzikoni, kuyaacha matembezi,  
Muenda omo na tezi, marejeo ni ngamani. (uk. 20)

Katika dondoo hilo Mnyampala ametumia methali mbili zinazoashiria maana moja. Hapa mwandishi anamaanisha kuwa kila afanyaye kazi kwa bidii na maarifa baadaye anaishia kufurahia matunda ya kazi yake akiwa sehemu yenye utulivu. Katika methali hizi kuna dhamira ya tamaa, kufanya kazi kwa bidii na uvumilivu ili kufanikiwa katika maisha. Mnyampala anawataka wananchi na viongozi serikalini wafanye kazi kwa bidii na kuvumilia shida na adha za kazi hizo ili hatimaye wafaidi matunda ya kazi husika. Aidha, Mlacha (1985) anaeleza kuwa methali ya ‘mwenda tezi na omo marejeo ngamani’ hutumika kufariji, kuliwaza na hata kuleta faraja. Hivyo basi methali hizo zinalingana na methali ya ‘baada ya dhiki faraja’. Kwa ujumla kufanana kwa methali hizo kunatokana na mwingilianomatini wa fasihi simulizi za jamii na nyingine. Kristeva (1980) anasema kuwa maana ya matini hupatikana kwa kutumia uhusiano, ufanano, utofauti na muunganiko wa matini husika na matini nyingine. Hii ina maana kuwa mwandishi haundi matini yake kutokana na akili yake mwenyewe ya asili bali huunda kutokana na matini zilizopo. Hivyo, mwandishi amechota kipengele cha fasihi simulizi na kutumia katika kazi zake za ushairi wa Kiswahili.

Methali nyingine inapatikana katika shairi la “Mgema Ukimsifu” (uk. 26) isemayo ‘Mgema ukimsifu, tembo hutia maji’. Kwa mfano ubeti wa tatu unasema:

82. Hukosa msifiwaji, chema hutia uchafu,  
 Sifaye ya uuzaji, waharibu kimsifu,  
 Utaacha mahitaji, mambo yanapokukifu,  
Mgema ukimsifia, tembo hulia maji. (uk. 26)

Katika methali hiyo, maana ya neno ‘tembo’ ni pombe inayotokana na mti wa mnazi, mtu anayegema tembo akipewa sifa kuwa tembo lake ni tamu mwisho huweza kuliharibu kwa kulitia maji. Mara nyingi mtu akisifiwa na kupambwa kwa sifa nyingi mwisho hupata kiburi na kuharibu tabia yake. Hapa kuna dhamira ya maadili, kiburi, ukosefu wa uaminifu na maringo kwa mtu anayesifiwa. Mwandishi anawataka wanajamii kuwa waangalifu wanapomsifia mtu au kiongozi yeyote, kwani huanza maringo, hujiona anafaa kuliko wengine, huzidisha mbwembwe na hata kufanya mambo yasiyofaa. Hivyo ujumbe utolewao hapa ni kwamba wanajamii wawe makini na sifa wanazotoa kwa wanajamii na hata kwa viongozi wao. Kwa kuwa sifa huweza kuleta matatizo mengi katika jamii.

Kadhalika, kuna methali isemayo ‘tamaa huzaa baa’ katika shairi la “Tamaa Huzaa Baa” (uk. 76). Kwa mfano ubeti wa nne unasema:

83. Tamaa una muluki, kasha unazaa baa,  
Tamaa haufutiki, siku zote unajaa,  
Tama hakutaziki, na ulishwe mnanaa,  
Tamaa huzaa baa, rafiki huyu mwepuke. (uk. 76)

Katika shairi hilo kichwa cha shairi ni methali. Maana ya methali hii ni kwamba kila mtu mwenye tamaa kwa kila jambo mwisho wake hupata balaa au hasara. Methali hii inafanana na methali isemayo: “tamaa mbele mauti nyuma.” Kufanana huku kunatokana na ufanano wa mila na desturi za kijamii na fasihi simulizi za jamii ambazo zipo kimwingilianomatini. Mwingilianomatini huchukulia kwamba kila kazi ya kifasihi inahusiana na kazi iliyoandikwa kabla kwa namna moja au nyingine, nazo kazi za Mnyampala zinahusiana na zina uhusiano na matini nyingine tangulizi. Hivyo, methali hizi zinalingana na kukamilishana kimaudhui. Mwandishi ametumia methali ya ‘tamaa huzaa baa’ kuwasilisha dhamira ya usaliti, ubinafsi na tamaa ambayo huleta



maovu katika jamii. Vilevile, kuna dhamira ya majuto, kazi, kutowajibika, kifo na ukoloni mamboleo. Aidha, mwandishi katika shairi hilo anatoa mafunzo kwa wanajamii kuepuka tamaa ya mambo mbalimbali kama vile tamaa ya mali, uongozi na mambo mengineyo mengi. Mwandishi anaiasa jamii kuondokana na misaada maana misaada husababisha nchi kuwa tegemezi na kutetereka katika maamuzi mbalimbali. Mnyampala anatoa ujumbe kwa wananchi wafanye kazi kwa bidii na kuepuka tamaa kwa kuwa tamaa huweza kusababisha majuto na hata kifo.

Kadhalika, katika shairi la “Wakati Titi la Nyati” (uk. 79) kuna methali isemayo ‘wakati titi la nyati hukamuliwa kwa shaka’, wengine wanatamka methali hii kama ‘titi la nyati halikamuliwi kwa shaka’. Ubeti wa tisa wa shairi hilo unasema:

84. Wakati kama mnyama, vyepesi kukusaliti,  
Wakati hauna mwema, huja nyuma kama koti,  
Wakati tena hukoma, uanguke kama mti,  
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka. (uk.79)

Katika methali hii kwa kawaida nyati ni mnyama mkali sana, hivyo kwa yeyote anayetaka kukamua titi la nyati ni lazima awe na hofu ya kupata matatizo au kuangamia. Mnyampala ametumia methali hii kuibua dhamira ya usaliti, mabadiliko, hofu na mashaka katika maisha. Mshairi anaonyesha kuwa maisha ya mtu ni ya hofu na mashaka na hubadilika kulingana na wakati. Mnyampala anawataka wananchi kuwa wavumilivu wanapokumbana na mabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kimazingira na kiwakati. Methali hii inatoa ujumbe kwamba wananchi hawana budi kuwa na tahadhari katika maisha na kuwa tayari kukabiliana na mabadiliko yanayojitokeza katika jamii. Anasisitiza kuwa kila kitu kina wakati wake, mambo magumu na yenye hatari yafaa kuepukwa kwani huweza kuleta matatizo katika jamii. Kupitia methali hii Mnyampala anatoa maadili kwa jamii na viongozi kuwa mambo magumu na yenye hatari yasitekelezwe bila ya kuwa na maandalizi. Naye Senkoro

(2011:33) anaeleza kuwa “shairi la “wakati titi la nyati” linafananisha hali ya wasiwasi na ile ya hofu ya mtu anayejaribu kukamua titi la nyati.” Aidha, taswira hii inasaidia kuongeza uzito wa maudhui ya shairi hususani kuhusu maisha. Kwa ujumla methali hii inatufundisha kuwa wavumilivu na wenye kuchukua tahadhari katika maisha.

Methali nyingine ni ‘ya ugomvi yamepita, na tutunge ya uhuru’ inayotokana na ‘yaliyopita si ndwele tugange yajayo’ inayopatikana katika shairi la “Yaliyopita Yamepita” (uk. 120). Ubeti wa pili wa shairi hilo unasema:

85. Ya uhuru yatungeni, ya ugomvi yamepita,  
Tanganyika nchi amani, nchi haina wasalata,  
Washairi unganeni, na utunzi kutakata,  
Ya ugomvi yamepita, na tugange ya uhuru. (uk. 120)

Katika shairi hili mtunzi amebadilisha maneno ingawa maana imebaki ileile ya ‘yaliyopita si ndwele tugange yajayo’. Mnyampala alifanya mabadiliko hayo ili kuwasilisha maudhui aliyokusudia kwa jamii husika. Katika methali hii kuna dhamira ya uhuru, ushirikiano, umoja na mshikamano katika jamii. Mshairi anasema “ya ugomvi yamepita na tutunge ya uhuru.” Mnyampala anamaanisha kuwa kama kulikuwa na mikwaruzano na matatizo kabla ya uhuru, jamii iyasahau bali iendeleze taifa kwa umoja na ushirikiano. Aidha, katika ubeti wa kwanza na pili, Mnyampala anawataka watunzi waungane, wasahau mambo ya nyuma na watunge mashairi kuhusu uhuru na amani ili kuendeleza nchi yao. Waandishi wengine waliohamasisha muungano wa washairi katika kazi zao ni Julius Nyerere (1967) na Saadani Kandoro (1972).

Kwa upande wa *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, mwandishi ametumia methali isemayo “mcheza kwao hutunzwa” katika utangulizi wa ngonjera ya “Zawadi Gani Tumpe?”

(uk. 26). Methali hii inamaanisha kuwa kwa kila afanyaye mambo mazuri na kufuata maadili ya jamii yake, mwishowe hupewa zawadi na jamii husika. Zawadi hiyo inaweza kuwa hata kuombewa baraka kwa Mwenyezi Mungu katika maisha yake. Hivyo, katika methali hii tunapata dhamira ya kazi, amani, uongozi bora na uwajibikaji. Methali hii inaendana na methali ya “Amlipaye mwimbaji ndiye huchagua wimbo” katika *Ngonjera za UKUTA Na. 2* (uk. 29). Methali hizo zina mawazo yanayoshikamana na kuhusiana ijapokuwa zinajitokeza katika vitabu viwili tofauti. Methali hizo zinalenga kuwafundisha wanajamii kujitua na kuwajibika katika jamii kwa kufuata taratibu za jamii husika.

Kadhalika, katika *Mashairi ya Vidato* kuna methali kama ‘mtaka nyingi nasaba, hupata mingi misiba’ katika shairi la “Mtaka Nyingi Nasaba” (uk. 6). Kwa mfano ubeti wa kwanza wa shairi hilo unasema:

86. Ukarimu unaponza, hutia ndani ya miba,  
Pengine huleta manza, ulie ‘Ya Rabi Toba’,  
Ya dunia huwafunza, wema huleta misiba,  
Mtaka nyingi nasaba, hupata mingi misiba.

Katika shairi hili methali hii imetumika kuibua dhamira ya kuacha tamaa, dini, ukarimu, hekima, utu na kuwa na kiasi katika kila jambo. Mwandishi anawataka watu kutenda wema, ukarimu na kufanya kila kitu kwa kiasi. Mtu yeyote anayetenda mambo kwa lengo la kusifiwa huweza kubezwa na kupata matatizo mengi. Kwa mujibu wa King’ei na Ndal (2008) methali hiyo inatukanya tusiwe na tabia ya kujitakia mengi tusiyoyajua wala kuwa na marafiki wengi tusiowafahamu kwani wanaweza kutuingiza katika taabu. Hivyo methali hii inaingiliana na mafundisho ya dini za kigeni, kwa mfano dini ya Kikristo. Kitabu cha Timotheo wa Pili 4: 5 kinasema “Bali wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiza huduma yako.”

Katika Mswada huu kuna methali nyingine isemayo “Tusiseme hatuwezi, awezalo Binadamu” katika shairi la “Tusiseme Hatuwezi, Awezalo Binadamu” (uk. 13). Ubeti wa kwanza wa shairi hilo unasema:

87. Ikiwa nia hatuna, ya kufanya mazoezi,  
 Ya kufua yatatufaa, na kufanya sawa kazi,  
 Vipi mambo yatafana, nasi tuwa wagunduzi?  
Tusiseme hatuwezi, awezalo binadamu.

Katika methali hiyo mshairi anasisitiza kuwa kila jambo katika maisha lifanywe kwa juhudi na maarifa. Haipaswi kutanguliza kusema hatuwezi jambo fulani, wakati binadamu wengine wanaweza kulifanya. Mwandishi anasisitiza kufanya utafiti na uchunguzi wa mambo mbalimbali yenye kuleta maendeleo kabla ya kukata tamaa. Mnyampala anawataka wanajamii wakazane kusoma ili waweze kufanya utafiti wa mambo mbalimbali kwa mfano kuchunguza magonjwa na kutafuta suluhu ya magonjwa, uvumbuzi wa sayansi na teknolojia na mengineyo yenye kuleta maendeleo katika nchi. Katika methali hii tunapata dhamira kuhusu elimu, sayansi na tekinolojia na ujenzi wa jamii mpya. Mwandishi anawataka wasomi Waafrika wajiamini. Vilevile, anawaasa kutojidharau na kuwaona Wazungu ndio wenye akili kuliko wao. Ujumbe ni kwamba, binadamu wote ni sawa tusibaguane kwa rangi bali tutumie elimu kuleta maendeleo ya nchi.

Katika mswada wa *Mahadhi ya Kiswahili* kuna methali isemayo “ulimwengu hauna pazia” ubeti wa ishirini na tisa katika nyimbo zinazohusu wivu wa mapenzi (uk. 6) unasema:

88. Mtu salata na mtu mumbea,  
 Mimi siwapendi washuhudia,  
Ulimwengu hauna pazia.

Methali hiyo inaelimisha jamii kuwa duniani hakuna siri. Katika methali hii, kuna dhamira ya umbea katika ndoa au unyumba. Hivyo mwandishi anawaasa wanajamii kuwa wasitoe siri za unyumba au ndoa kama hatutaki zijulikane na walimwengu. Hivyo mwandishi anakemea tabia ya umbea katika jamii kwa kuwa huweza kuleta ghasia katika jamii. Vilevile, katika nyimbo za mapenzi na mafumbo (uk. 7-9), kuna methali ya “mchimba kisima huingia mwenyewe” (uk. 9). Ubeti wa themanini na mbili unasema:

89. Uwache hasama, usijizujuwe,  
Utengeze wema, wa mimi na wewe,  
Mchimba kisima, huingia mwenyewe.

Methali hii inatupa dhamira ya upendo na utu katika maisha. Methali hii inamaanisha kuwa mtu yeyote amtakiaye mwenzake mabaya mwisho wake, mabaya hayo humfika mwenyewe. Hivyo kupitia methali hii tunapata ujumbe kuwa tusiwaombee wala kuwafanyia wenzetu mabaya kwa kuwa mabaya hayo huenda yakaturudia wenyewe. Hapa mwandishi anawataka wanandoa kuwa na mapenzi ya dhati yenye kujali utu wa binadamu.

Vilevile, kuna methali nyingine katika nyimbo zilizokusanywa na Mnyampala mwaka 1953. Baadhi ya nyimbo hizo alitunga mwenyewe na zingine zilitungwa na Mbabe Athumani na wengineo. Nyimbo hizo zimechanganywa na ni vigumu kujua mwandishi yupi aliandika wimbo upi. Ndani ya nyimbo hizo kuna methali isemayo “baada ya dhiki faraji” (uk. 10). Ubeti wa tano unasema:

90. Sikipandi kilima kisicho maji,  
Kwako wewe sikujia utaraji,  
Na tukae baada ya dhiki faraja.

Kupitia methali hiyo tunapata dhamira inayohusu uvumilivu katika maisha. Ujumbe tunaopata hapa ni kuwa mtu apatapo matatizo ama misukosuko katika maisha anatakiwa kuvumilia. Pia tunapata mafunzo kuwa mara nyingi raha ama faraja huja baada ya mtu kutaabika au kupitia katika misukosuko. Methali hii imetumika kumliwaza na kumtia moyo mwanamume pale anapotafuta mke wa kuo kuwa anatakiwa kuvumilia na kupambana na magumu. Baada ya misukosuko hiyo, mwisho wake atapata raha na furaha. Methali hii inafanana na methali isemayo “hakuna marefu yasiyo na ncha.” Methali zote hizi zinatokana na fasihi simulizi zinazopatikana katika jamii za Kiafrika. Hapa pia tunapata mwingilianomatini katika tanzu za fasihi simulizi na ushairi wa Kiswahili.

Methali nyingine inapatikana katika (uk. 11) isemayo “shida ya mtungi muulize kata” katika *Mahadhi ya Kiswahili*. Ubeti wa ishirini na mbili wa nyimbo hizo unasema:

91. Kacheza na kisu kimesha mkata,  
Atokwa na damu matata matata,  
Shida ya mtungi muulize kata.

Katika methali hiyo neno kata lina maana nyingi, huweza kuwa kifaa cha kubebea kichwani au chombo cha kuchotea maji. Hapa tunachukulia kata kama kifaa cha kuchotea maji mtungini. Methali hiyo ina maana kuwa kata ndio inayoweza kutambua shida ya mtungi kwa kuwa ndiyo inayotumiwa kuchotea maji mtungini. Kupitia methali hii tunapata dhamira ya mapenzi na ndoa. Ujumbe tuupatao hapa ni kwamba yule anayeweza kuelewa na kusimulia ubaya wa ndoa au mahusiano ni yule ambaye yuko ndani ya ndoa ama katika mahusiano. Kwa hiyo, kama mtu hayupo katika mahusiano ya kimapenzi au ndoa hawezi kujua vyema mazuri na mabaya yake.

Kwa kuzingatia uchambuzi huu imedhihirika kuwa Mnyampala ametumia methali kwa lengo la kuelimisha jamii na kujenga jamii bora. Hata hivyo, katika kitabu cha

*Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* na mswada wa *Hazina ya Washairi*, hakuna methali katika mashairi yaliyoandikwa na Mnyampala. Kwa ujumla, methali alizotumia Mnyampala katika mashairi yake zimeibua dhamira anuwai kama vile mapenzi na ndoa, dini, malezi, uzazi, uzalendo, uongozi bora, uvumilivu, ushirikiano, umoja na mshikamano, haki na usawa wa binadamu. Methali hizi zimetumika kutunza amali za jamii na kukuza Kiswahili, kuhimiza uzalendo, na kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii.

#### **4.1.3 Misemo**

Misemo ni mbinu nyingine iliyotumiwa na Mnyampala kuwasilisha maudhui katika kazi teule. Wamitila (2003) anaeleza kuwa misemo ni tungo au kauli ambazo hutumika kulinganisha maisha, matukio au vitu. Anafafanua zaidi kuwa misemo hutumiwa kuelezea tungo ambazo hutumia picha, ishara na tamathali za semi kuelezea kitu au wazo kwa ufupi ili yatolewe maadili na maonyo fulani. Naye Senkoro (2011) anafafanua kuwa misemo ni maneno yanayotumika mara kwa mara kama yalivyo katika mazingira maalum kuleta maana husika. Kwa ujumla, misemo huibuka na kutoweka kufuatana na mabadiliko yanayojitokeza katika jamii. Mulokozi (2017:75) anasema kuwa misemo ni utanzu mmojawapo wa semi. Anafafanua zaidi kuwa “misemo ni semi zinazoibuka kwa muda fulani kwa madhumuni maalum na kuenea katika jamii na kisha kutoweka au kubadilika au kubaki katika kumbukumbu za watu kwa muda mrefu.” Anaongezea kuwa baadhi ya misemo baadaye huweza kuwa methali. Kutokana na maana hizo, katika kazi hii tumetumia misemo kama mojawapo ya kipengele cha lugha ambacho hutumia tungo au kauli fupifupi kuelezea mawazo ya mwandishi ili kufikisha maudhui yaliyokusudiwa kwa jamii.

Katika utafiti huu tumebaini kuwa misemo imetumika sana katika kazi teule za ushairi za Mnyampala. Katika uchambuzi huu tumejadili baadhi ya misemo iliyotumiwa na Mnyampala katika kazi zake teule. Tukianza na *Diwani ya Mnyampala*, mbinu hii imejitokeza katika shairi la “Mali Pepo ya Dunia” (uk. 7). Kichwa cha shairi hili kimekaa katika muundo wa msemu. Hivyo, katika shairi hilo kuna msemu usemao ‘mali pepo ya dunia’. Kwa mfano ubeti wa pili wa shairi hilo unasema:

92. Mali japo Sultani, atawale kwa sheria,  
Mwenye mali milioni, asisahau murua,  
Imani ndicho kiini, cha Jalali kumjua,  
Mali pepo dunia, yambatane na imani.

Hivyo katika nukuu na shairi hilo ‘mali pepo ya dunia’ ni msemu uliotumiwa na Mnyampala kutoa dhamira ya dini kwa watu wenye mali kuwa wanatakiwa kumtanguliza Mungu kwa kila jambo. Mnyampala anawataka wenye mali kutambua kuwa mali hizo ni za hapa hapa duniani na mtu akifa anaziacha mali zote wala hakuna mtu anayezikwa nazo. Ujumbe anaotoa ni kwamba mali ama uchumi ili uweze kustawi vizuri ni lazima uambatane na dini. Ukifanya biashara ama kazi yoyote ni lazima umtangulize Mungu ndipo utafanikiwa. Aidha, hata kama mtu ana mali nyingi sharti afuate sheria zilizowekwa na serikali husika. Hivyo, Mnyampala anasisitiza kufuata maongozi ya dini na sheria za jamii.

Shairi la “Uambiwacho ni Mwiko” (uk. 25) lina msemu usemao ‘uambiwacho ni mwiko usitamani kukigusa’. Mwiko ni katazo la kitu fulani. Hapa mwandishi anawasihi wanajamii kuwa kitu unachokatazwa kufanya basi usitamani kukifanya. Kupitia msemu huu tunapata dhamira ya utii na maadili kwa jamii kwamba watu wafuate maneno ya busara ya wakubwa wanayoambiwa na kuyatii. Kadhalika kuna dhamira ya anasa, tamaa na matumizi mabaya ya rasilimali zilizopo. Mtu asijidai kuwa mjuaji sana katika kuendekeza tamaa na anasa za dunia kwa sababu ya pesa



kwani mwisho wake huwa matatizo na maambukizi ya magonjwa mbalimbali. Kama tuonavyo katika ubeti wa nane unasema:

93. Na macho utapepesa, usijue utokako,  
Mwili ugeuke kasa, magamba ya kisonono,  
Hata mbwa akikunusa, atakosa na mnuko,  
Uambiwacho ni mwiko usitamani kukigusa. (uk. 25)

Mwandishi hapa anaiasa jamii kuwa mtu akikiuka miiko ya jamii aambiwayo na wakubwa mwisho wake huishia katika matatizo na mahangaiko ya dunia. Mnyampala anatoa ujumbe kwa jamii kuwa wafuate maadili ya jamii ili kuepukana na adha mbalimbali zinazoweza kuwakumba kutokana na kuvunja miiko iliyopo katika jamii.

Vilevile kuna msemu mwingine usemao ‘kipofu kaona mwezi mwenye macho hathamini’ katika shairi la “Kipofu Kaona Mwezi” (uk. 36). Ubeti wa tatu unasema:

94. Mwonaji sasa haoni, kipofu kaona mwezi,  
Kasema “Haki ni nini, mfano kama kurunzi?”  
Wenye macho tawahini, nionapo waziwazi,  
Kipofu kiona mwezi, wenye macho hawathamini.

Msemu huu unamaanisha kwamba si rahisi kwa kipofu kuona lakini endapo akikiona kitu lazima akishangae ila kwa yule aliyezoea kukiona, huona ni kawaida. Hapa mwandishi kupitia msemu huu anazungumzia uhuru wa Tanganyika. Wananchi hawakutegemea kupata uhuru huo. Katika msemu huo kuna dhamira ya uhuru na ukombozi wa nchi. Mnyampala anashangilia uhuru na kuwapongeza viongozi hasa Rais Mwalimu Julius Nyerere kwa jitihada zake za kupigania uhuru nchini Tanzania. Anaeleza kuwa wananchi wazidi kupambana na kujikwamua katika nyanja zote za maisha ili hatimaye wapate kuthamini na kupata matunda ya uhuru huo.

Msemu mwingine ni ‘bure ina sumu kali yafaa kujihadhari’ unaopatikana katika shairi la “Bure ina Sumu Kali” (uk. 37). Kwa mfano ubeti wa kwanza unasema:

95. Mpenda cha bure boza, tenaje ni baradhuli,  
Tamaaye humpumbaza, huzidi kuwa jahili,  
Vya bure humwongoza, kwa wengine ajidhili,  
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari.

Hapa Mnyampala kupitia msemu huu ameibua maudhui mbalimbali ya kisiasa na ya kiuchumi. Mwandishi anawataka wananchi na viongozi kuchunguza kwanza misaada wanayopata kutoka kwa wakoloni. Hivyo, anaiasa jamii isipende wala kuzoea vitu vya bure kwa kuwa vitu vya bure hulemaza akili na kuiweka nchi katika matatizo mengi. Mnyampala anaeleza kuwa vya bure vina matatizo mengi. Kwa hivyo, wananchi lazima wakatae misaada inayotolewa na nchi zilizoendelea. Mnyampala anasisitiza kuwa ili kuwe na uhuru wa kweli ni lazima nchi ijitegemee na wanajamii wale jasho lao, kwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kutosheleza mahitaji ya jamii husika. Ujumbe tuupatao kutokana na msemu huu ni kwamba jamii na viongozi waache kutegemea misaada kutoka katika nchi zinazoendelea ili kuleta uhuru wa kweli ndani ya nchi zilizopata uhuru. Dhana ya kujitegemea ilielezwa pia kwa kutumia methali isemayo ‘tamaa huzaa baa’ katika shairi la “Tamaa Huzaa Baa” (uk. 76). Hapa mwingilianomatini unajitokeza baina ya tanzu/vipera vya fasihi simulizi ndani ya kazi za Mnyampala. Wanjala (2015) anaeleza kuwa mwingiliano tanzu hushikilia kuwa kazi ya fasihi huumbwa kwa kuvunja mipaka ya kitanzu kwa lengo la kuibuka na kazi bora. Hivyo basi lengo la mwingiliano wa vipera hivyo ni kuifanya kazi ya sanaa kuwa bora na ubunifu zaidi. Maudhui aliyonayo anawasilisha kwa kutumia mbinu tofautitofauti na kurejelea maana ileile lengwa.

Msemu mwingine umetumika katika shairi la “Unyumba si Fani Moja” (uk. 40), ambao ni “unyumba una tabia wala si fani moja.” Msemu huu umetumika kuibua maudhui yahasuyo maisha ya ndoa. Mnyampala katika shairi hili amechora tabia za wanandoa. Ameanza kwa kumchora mwanamke kuwa ni muovu, mgomvi, hamjali

mumewe na ni mgandamizaji kwa mwanamume. Haya tunayaona katika ubeti wa saba, usemao:

96. Kweli si namna moja, sana zahitilafia,  
Wengine hawana hoja, kama picha wamekaa,  
Mke ndani huyafuja, mume anavyowania,  
Unyumba una tabia, wala si fani moja.

Katika nukuu hiyo, mwanamke anaonekana kuwa mgomvi na hamtii mwanaume. Kulingana na mila na desturi za jamii na mafundisho ya dini za kigeni, mwanamke sharti amtii mwanaume. Mfano katika vitabu vitakatifu kama *Bibilia* Waefeso 5:22-24 na 1Petro 3: 1 inasisitiza kuwa wanawake wawatii waume zao. Mfano 1Petro 3:1 tunasoma, “ninyi wake watiini waume zenu; kusudi, ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno.” Mistari hiyo inahimiza mwanamke kumheshimu na kumtii mwanamume.

Naye Issa (2013) anaeleza kuwa maneno ya Mtume (S.A.W) yanaeleza kwamba lau ingefaa kwa mwanadamu kumsujudia mwanadamu basi ingeamrisha mwanamke amsujudie mumewe kwa ukubwa na haki yake pia. Suala hili limesawiriwa vyema kimwingilianomatini kwa kuwa linajitokeza katika tamaduni zote mbili ya kijadi na kigeni. Kutokana na hoja hiyo, Barthes (1979) anaeleza kuwa mtu hawezi kueleza usemi au hata kazi iliyoandikwa kama kazi ambayo ina maana inayojitosheleza au inayojitegemea, bila kuhusianisha matini za fasihi kwa njia moja ama nyingine. Hata hivyo msemu huu umegusa pia upande wa mwanaume na mwandishi ameyaeleza hayo katika ushairi huo.

Mwandishi anafanua namna mwanamume anavyomnyanyasa mwanamke katika ubeti wa kumi na wa kumi na moja (uk. 41) zisemazo:

97. Waume wengine simba, nyumbani wana udhia,  
Kila mara wanagomba, hapana wa kuamua,

Kwa magongo humtima, mkewe huchakaa,  
Unyumba una tabia, wala si fani moja. (ubeti wa kumi)

Mke huwa na taabu, daima hulialia,  
 Mke hugeuka bubu, kitukanwa hunyamaa,  
 Wala hataki ajibu, anapomkaripia,... (ubeti wa kumi na moja)

Katika beti hizo Mnyampala anaeleza kuwa mwanamume huwa mkali kama simba muda wote ni humgombeza mwanamke kiasi cha mwanamke kuwa mnyonge na kuchakaa. Mnyampala anawataka wanaume waheshimu haki za wanawake kwa kufuata misingi ya haki za binadamu. Waefeso 5:25 inasema “enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake.” Hivyo vitabu vitakatifu navyo vinasisitiza wanaume kuwa na upendo kwa wake zao, kama alivyosisitiza Mnyampala katika maandishi yake.

Naye Senkoro (1988) anaeleza kuwa haifai mwanamke kunyanyaswa na kugandamizwa haki zake bali apate haki na nafasi sawa na mwanamume katika nyanja zote za maisha. Aidha, masuala haya yanasawiriwa vyema kupitia Nadharia ya Mwingilianomatini inayosisitiza kuwa matini si kitu binafsi, cha pekee ama kilichojitenga bali ni muunganiko wa matini mbalimbali za kifasihi na za kiutamaduni. Hivyo kupitia msemu huu mshairi anaeleza mabaya ya mwanamke na mwanamume katika ndoa. Katika msemu huu tunapata dhamira ya usawa wa kijinsia, haki za binadamu, kupinga ukatili na usaliti katika maisha ya ndoa. Vilevile, wanajamii wanapaswa kutambua kuwa ndoa si kufanya tendo la ndoa (ngono) tu bali kuonyesha heshima na upendo kwa mwanandoa mwenzako, utii, kutunziana siri, kutokuwa wanafiki na kupinga ukatili na usaliti. Hapa mwandishi anawataka wanandoa kujua haki na wajibu wa kila mmoja katika ndoa ili maisha ya ndoa yawe na furaha na amani.

Kadhalika, kuna msemu katika shairi la “Akheri Sumu ya Nyoka” (uk. 41) usemao ‘akheri sumu ya nyoka binadamu kazidia’. Msemu huu unajitokeza kama kiitikio cha kila ubeti ili kusisitiza dhamira ya dhuluma, usaliti, uonevu na unafiki. Kupitia msemu huu mwandishi anatoa ujumbe kwa jamii kuwa dhuluma, uonevu, usaliti na unafiki havitakiwi katika maisha. Mnyampala kupitia msemu huu anaiasa jamii kuwa makini na binadamu kuliko hata nyoka. Ubeti wa pili wa shairi hilo unasema:

98. Binadamu madhulumu, usidhanie dhihaka,  
Nyoka kweli ana sumu, umwonapo muepuke,  
Binadamu ni vigumu, hawezi kuepukika,  
Akheri sumu ya nyoka, binadamu kazidia. (uk. 41)

Katika ubeti huu mwandishi anasisitiza kuwa nyoka ana sumu lakini ni rahisi kumwepuka. Lakini binadamu haepukiki kwa kuwa si rahisi kujua dhamira yake. Msemu umeibua dhamira ya unafiki wa binadamu na usaliti wake. Binadamu akikusudia kutenda jambo baya kwako hata iweje huwezi kumkwepa. Awe Mwislamu, Mkristo ama kafiri wote wanatakiwa kuwa makini nao. Hivyo, tunatahadharishwa kuwa waangalifu kwa binadamu kuliko kitu chochote kwa kuwa binadamu anaweza kukufanyia jambo baya na kumkwepa ni vigumu. Katika ubeti wa mwisho mwandishi anasisitiza dhamira ya dini kuwa kila mtu ashike imani thabiti ili kuepuka kuwatendea binadamu na viumbe vingine vitu vibaya.

Katika shairi la “Pambo la Ndoa Mapenzi” (uk. 45) kuna msemu usemao ‘pambo la ndoa mapenzi’. Kwa mfano ubeti wa pili unasema:

99. Pambo la moyo mahaba, moyo kutia urembo,  
Sikilizano kwa huba, hufana kuliko Pombo,  
Mpendane kama inzi, alonaswa na ulimbo,  
Iwapo nguo ni pambo, pambo la ndoa mapenzi.

Hapa Mnyampala kupitia msemu huu anatoa dhamira ya mapenzi na maisha ya ndoa. Anaeleza kuwa mapenzi ni pambo la ndoa, bila mapenzi hakuna ndoa. Hivyo

anasisitiza kuwa kila mmoja aridhie ndoa mwenyewe bila kulazimishwa hapo ndoa itakuwa na furaha. Pia anatoa fundisho kuwa ndoa mbaya haifai maana inasababisha matatizo mengi na wengine kukonda na hata kufa. Ujumbe unaotolewa kupitia msemu huu ni kwamba raha ya mapenzi katika ndoa ni wawili kuridhia na kupendana kwa dhati pasipo kushurutishwa.

Katika shairi la “Kila Khasimu Polisi” (uk. 52), kuna msemu usemao ‘kila Khasimu polisi mhalifu wa sheria’. Ubeti wa tano wa shairi hilo unasema:

100. Si vema kumfichia, tumpe kweli upesi,  
Pasi ya kulimatia, kaziye iwe rahisi,  
Upenu alopitia, ili amfate kazi,  
Kila Khasimu Polisi, mhalifu wa sheria.

Mwandishi katika msemu huu anatoa mafunzo kwa jamii kuwa mtu muovu huogopa kila mtu kwa kuwa anaogopa kutiwa gerezani. Katika msemu huu kuna dhamira ya ulinzi na usalama, haki, ushirikiano, kuwajibika kuwafichua wahalifu, amani na kufuata sheria zilizowekwa na nchi. Hivyo, kupitia shairi hili Mnyampala anaelimisha jamii kuwa kila mmoja anatakiwa kufuata sheria na kuzishika ili asije akatiwa mikononi mwa sheria. Mnyampala anaeleza kuwa polisi hawamshiki tu kila mtu, bali wapo kwa ajili ya kulinda mali za umma, kuleta usalama na kuondoa dhuluma miongoni mwa watu. Katika shairi hili mwandishi anawaasa wanajamii kuwapa polisi ushirikiano pale inapotokea tatizo ili kutokomeza uovu miongoni mwa wanajamii. Watu waovu, wanyang’anyi, wanaodhulumu na kuiba wote wapelekwe polisi ili wachukuliwe hatua, tusifiche uovu. Ujumbe unaotokana na msemu huu ni kwamba mtu anayetii sheria hufurahia dunia na kuishi kwa amani lakini mtu anayekiuka sheria huishi kwa hofu na mashaka maishani mwake mwote.

Kadhalika, katika shairi la “Mchungu Chungu Kiunga” (uk. 74) kuna msembo usemao ‘chungu mchungaji chungu kwa mtima wa mbawazi’. Kwa mfano ubeti wa pili usemao:

101. Chungu sikia Mwenyezi, amrize alofinga,  
 Chungu uwe msikizi, mahubiri ni uganga,  
 Chungu uwe mtimizi, usidharau nyakanga,  
Chungu mchungaji chungu, kwa mtima na mbawazi.

Katika ubeti na shairi hili, msembo huu umetumika kama kibwagizo kuisisitiza dhamira mbalimbali kama vile dini hususani katika ubeti wa pili ambapo msanii anasisitiza watu kushika amri za Mungu. Vilevile katika ubeti wa nne Mnyampala anawataka wanajamii kuonyesha heshima kwa wazazi na anasisitiza watoto kuwatunza wazazi wao pale wanapohitaji msaada wao. Nao ubeti wa tano anasisitiza kuenzi tamaduni za kijadi zinazofaa na kuachana na zile zisizofaa. Katika ubeti wa sita anasisitiza malezi mema kwa watoto ili wawe na maadili mema katika jamii. Kadhalika ubeti wa saba hadi wa tisa anasisitiza kufanya mambo mema, kuwa na tabia njema, kuheshimu sheria za nchi ili tuweze kuishi kwa amani. Aidha, Mnyampala katika msembo huo anaibua dhamira zinazokemea udokozi na wizi, umalaya na tabia nyinginezo mbaya na anasisitiza umuhimu wa ndoa, siri katika ndoa, ujasiri na kulinda uhai wetu na wa watu wengine. Ujumbe wa msembo huu ni kwamba mtu akitaka maendeleo ni lazima awe tayari kuchunguza kwanza njia zinazofaa na halali zinazoleta maendeleo kulingana na sheria za nchi husika.

Katika shairi la “Mbwa Alokunja Mkia” (uk. 96), kuna msembo usemao “mbwa alokunja mkia ni vigumu kumnyosha.” Mfano ubeti wa saba unasema:

102. Chanzo chake tamaa, kumharibu tabia,  
 Kudanganya na jamaa, wasasi wa kubabia,  
 Wakavue vidagaa, vya ziwa magharibia,  
Mbwa alokunja mkia, ni vigumu kumnyosha. (uk. 96)

Mnyampala anamaanisha kuwa mtu mwenye tabia mbaya iliyoshindikana ni vigumu sana kuinyosha tabia hiyo. Mnyampala anaeleza kuwa chanzo cha tabia mbaya ni tamaa inayosababisha mtu kuwa na tabia isiyofaa katika jamii. Ili mtu mwenye tabia mbaya kubadili tabia ni muhimu afuate sheria zilizopo. Katika msemu huu dhamira zinazoibuliwa ni kutii sheria za jamii, kuwa mwadilifu, kuacha tamaa, uongo, ulaghai na unafiki ambao hautakiwi katika jamii. Ujumbe tuupatao hapa ni kwamba ni vigumu kubadilisha tabia ya mtu aliyozoea kama mbwa aliyekunja mkia. Ili kumbadilisha mtu tabia yake inahitaji nguvu ya ziada na ni wachache sana hubadilisha tabia. Hivyo msemu huu unatoa ujumbe kwa wanajamii kuepuka makundi maovu pamoja na tamaa kwani zinamfanya mtu kujiingiza katika uovu.

Msemu mwingine ni ‘akosaye hujifunza’ unaopatikana katika shairi la “Akosaye Hujifunza” (uk. 116). Mwandishi anaelimisha jamii kuwa mtu mwenye maadili na tabia njema akikosea jambo, hujifunza na hawezi kurudia kosa alilotenda. Mtu ambaye hujifunza kutokana na kosa alilotenda ni yule ambaye ni msikivu na mtiifu ambaye hapendi kutenda uovu kama asemavyo mwandishi katika ubeti wa tano na wa sita:

103. Mwepesi wa kusikia, ovu mbali hujibanza,  
Hapendi jiharibia, kwa mabaya kuyatazama,  
Maovu huyachukia, mbele yasije mtanza,  
Akosaye hujifunza, tena asijerudia. (ubeti wa tano, uk. 116)

Kosa la kujitakia, sisemi hilo napinza,  
Kila jambo hurukia, asiyependa kujifunza,  
Bali anayesikia, hujua ukewenza,  
Akosaye hujifunza, tena asijerudia. (ubeti wa sita, uk.116)

Katika ubeti wa tano mwandishi anaeleza mtu anayeweza kujifunza kutokana na kosa na ubeti wa sita mwandishi anamwelezea mtu ambaye anafanya kosa kwa makusudi na wala hataki kujifunza, huyu ni yule ambaye kila jambo hurukia bila kufanya



uchunguzi. Katika msemo huu mwandishi anaibua dhamira ya maadili, uadilifu na utu katika jamii. Kwamba mtu anapokosea anatakiwa kujutia kosa alilofanya na kujifunza kutokana na kosa hilo ili asije akakosea tena. Ujumbe anaotoa ni kwamba, kila mtu anatakiwa kujifunza kutokana na makosa na kukusudia kuacha mambo yasiyofaa katika maisha.

Katika shairi la “Wengi Wakitaka Wape” (uk. 119) kuna msemo usemao ‘wengi wakitaka wape.’ Msemo huu unatumiwa sana na wanasiasa wakati wanagombea nafasi mbalimbali za uongozi ama wakati wa kampeni zao. Mwandishi kupitia msemo huu anatoa maudhui ya masuala ya siasa kuwa watu wanapopigania kitu wale waliokuwa wengi ni lazima hushinda hata ufanyeje. Katika shairi hili anawasema wakoloni waliokuwa wakitawala nchini Tanzania na Afrika kwa ujumla, kwamba ni lazima watoe uhuru kwa nchi za Kiafrika kwa kuwa wananchi ambao ni wengi wanataka uhuru. Msemo huu unatupa ujumbe kuwa katika mashindano yoyote yale waliokuwa wengi hushinda daima. Kama asemavyo katika ubeti wa nane kuwa:

104. Pima mizani ya sudi, kulikozidi kukope,  
Si vyema kuwa hadidi, hung’ang’ana kama kupe,  
Likibidi limebidi, lazima wengi tuwape,  
Wengi wakitaka wape, ama watajitwalia. (uk. 119)

Katika ubeti huo mwandishi anasisitiza ujumbe kwamba wengi wanatakiwa kupewa madaraka, wasipopewa watajitwalia madaraka hayo wenyewe. Kupitia msemo huu tunapata dhamira zinazohusu siasa, haki na uhuru kwa wote.

Katika shairi la “Hakuna Mkamilifu” (uk. 127), kuna msemo, ‘hakuna mkamilifu’, ambapo Mnyampala anasema kuwa hakuna binadamu aliyekamilika, mkamilifu ni Mungu tu. Kupitia msemo huu tunapata dhamira ya upendo kwa watu wote. Pia kuna dhamira ya dini inayosisitiza kumtegemea na kumtanguliza Mungu katika kila jambo.

Kwa upande wa ujumbe tunasisitizwa tusiwategemee binadamu kwamba ndio wanaoweza kutusaidia kwani watu wote wana mapungufu. Mwandishi pia katika ubeti wa mwisho anasema:

105. Hapa ndio penye shina, kaditama tamatifu,  
 Ombi kushirikiana, kwa mioyo mikunjufu,  
 Mashairi tusanifu;  
 Tusanifu wenye vina, pambo kama vishaufu,  
 Ni mizani kupatana, maneno maadilifu,  
Hakuna mkamilifu, kila mtu hupungua. (uk. 127)

Katika ubeti huu mwandishi anaeleza sheria za kutunga mizani, na kukiri wazi kuwa kitu cha kufuata katika utunzi ni sheria za arudhi ya ushairi na matumizi ya maneno ya hekima. Mnyampala pia anawasihi waandishi washirikiane kuendeleza ushairi na kutambua kuwa kila mtu hukosea na hakuna mkamilifu duniani. Hapa kuna dhamira ya sheria za utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Vilevile, katika kitabu cha Abedi (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri Abedi* ameongelea masuala ya arudhi ya ushairi wa Kiswahili. Kujitokeza kwa wazo moja ndani ya kazi tofauti za fasihi ni suala la mwingilianomatini. Matini za fasihi huhusiana kwa kurejelea kazi zingine za sanaa zilizotangulia (Allen, 2000), hii ndio sababu waandishi walioandika kazi zao kipindi kinachofanana mara nyingi wanahusiana kimtazamo na hata kimawazo.

Msemo mwingine unaopatikana katika shairi la “Apendaye Kudhulumu” (uk. 129) ni, ‘apendaye kudhulumu hujidhulumu mwenyewe.’ Mnyampala anaeleza kuwa mara nyingi mtu ambaye anapenda kudhulumu wenzake hufikia wakati anawadhulumu hata ndugu zake wa karibu kwa mfano wazazi wake, watoto na hata mkewe. Kupitia msemo huu, Mnyampala anaeleza kuwa vitabu vitakatifu (Biblia na Kurani) vinakataza tabia ya kudhulumu, adhabu yake ni kutupwa kuzimu na jehanamu. Haya yanaongelewa katika ubeti wa sita usemao:

106. Hudhulumiwa mwenyewe, apendaye kudhulumu,  
Mungu hampiga mawe, na kumtupa kuzimu,  
Na kumfanya haramu;  
Haramu alaaniwe, na kutupwa Jehanamu,  
Ndani moto atiwe, Milele awe na dhamu,  
Apendaye kudhulumu, hujidhulumu mwenyewe. (uk. 129)

Msemo huu unaibua dhamira ya dini. Vilevile, dhamira hiyo imeundwa katika mtindo wa mwingilianomatini ambapo masuala ya dini na maisha ya kawaida yanaingiliana. Hili linatuhakikishia kuwa matini yoyote ya fasihi haitoki katika ombwe bali inatoka katika jamii iliyomkuza na kumlea msanii wa kazi husika. Pia, ujumbe tunaopata kupitia msemo huu ni kwamba dhuluma si kitu kizuri hata Mungu hapendi.

Katika mswada wa *Mahadhi ya Kiswahili* katika nyimbo zinazohusu wivu katika mapenzi kuna msemo usemao ‘mzigo mzito mpe Mnyamwezi’. Kama tuonavyo hapa:

107. Mzigo mzito mpe Mnyamwezi,  
Kongo inang’ara kama mbalamwezi,  
Likivaa kanga linajizuzua,  
Ni heri kaniki mawingu ya mvua. (uk. 6)

Msemo huu unamaanisha kuwa mambo yakutatizayo na ambayo hayawezekeani wahusishe wale wenye uwezo wa kukutatulia matatizo hayo. Mshirikishe Mungu na wale unaoamini wanaweza kukusaidia kutatua matatizo yako. Kuna dhamira ya dini na mahusiano mema kati ya mume na mke na jamii kwa ujumla.

Kadhalika, nyimbo zilizokusanywa na zingine zilizoandikwa na Mnyampala (uk. 10), ubeti wa tano kuna misemo miwili. Misemo hiyo ni ‘sikipandi kilima kisicho na maji’ na ‘kapewa mahaba akayachezea’. Misemo hii inaingiliana na kukamilishana katika kuibua maudhui yaliyokusudiwa. Kama tuonavyo katika ubeti huo usemao:

108. Sikipandi kilima kisicho maji,  
Kapewa mahaba akayachezea!  
Kila asherati hana mazoea! (ubeti wa tano)

Katika ubeti huo, misemo hiyo imetumika kuelezea suala la mapenzi na ndoa, mahusiano mema na utii. Hapa mwandishi anaonesha kuwa mahusiano mazuri katika ndoa ni muhimu na kila mmoja anatakiwa kuwa na mahusiano mema. Kukosekana kwa mahusiano mema katika ndoa kunaweza kusababisha mafarakano kwa wanandoa.

Misemo mingine inapatikana katika ubeti wa ishirini na sita, isemayo; ‘msitu mkubwa haukai bata’ na ‘mahaba majani popote huota’. Katika ubeti huo Mnyampala anasema:

109. Msitu mkubwa haukai bata,  
Hupiga vinanda na vitashikota,  
Mahaba majani popote huota.

Katika msemu huo, mwimbaji analinganisha mazingira anayoishi bata na mapenzi. Kuwa bata hawezi kukaa kwenye msitu mkubwa lakini mahaba ni kama majani popote huota. Hapa mwandishi anamaanisha kuwa mahaba hayachagui sehemu, kinachotakiwa ni utayari wa kila mmoja. Katika ubeti huo, kukamilishana, kuumbana na kuhusiana kwa misemo hiyo ni suala la mwingilianomatini. Misemo hiyo yote inahusu dhamira za mapenzi kwa wapendanao ama kwa wanandoa. Vilevile, kuna msemu wa mapenzi katika (uk. 11) ubeti wa ishirini na nane usemao “ukitoka wewe mwingine tayari.” Mwandishi anamaanisha kuwa wanandoa wanapotengana, wanaweza kuanzisha mahusiano na wengine.

Msemu mwingine unapatikana katika (uk.13) ubeti wa hamsini na saba, usemao “mahaba ni sindano huyachoma maini.” Kama tuonavyo hapa:

110. Ukitaka jenga nyumba kajenge njiani,  
 Na madirisha yake yatazame kusini,  
Mahaba ni sindano huyachoma maini.

Msembo huo unamaanisha kuwa mahaba ni kitu cha muhimu katika ndoa. Mahaba yakikosekana katika ndoa husababisha maumivu makali kwa mwenzi anayesalitiwa. Hivyo, katika nyimbo hizo kuna dhamira ya mahusiano mema baina ya mke na mume, maadili, upendo, uvumilivu, ushirikiano, amani na furaha maishani. Ujumbe unaotolewa hapa ni kwamba mapenzi ya dhati kwa wanandoa ni msingi wa ndoa kufana na kudumu. Kwa ujumla misemo iliyopo katika nyimbo hizi inahusu masuala ya mapenzi na ndoa.

Misemo iliyojadiliwa katika kazi teule za Mnyampala imeibua dhamira mbalimbali kwenye kazi hizo. Baadhi ya dhamira zilizoibuliwa ni uzalendo, ushirikiano, mapenzi na ndoa, usaliti, haki ya kijinsia, dhuluma na mengineyo. Kadhalika kuna maaso, jumbe na mafunzo mbalimbali yaliyotolewa na Mnyampala kuielimisha jamii namna ya kuenenda katika maisha tunayoishi. Katika mjadala huu tumebaini kuwa kuna mwingilianomatini kati ya fasihi simulizi na tamaduni za jamii. Aidha, misemo mingi iliyotumika katika kazi za Mnyampala inatokana na fasihi simulizi na pia huhusiana, huingiliana na kukamilishana katika kuibua maudhui yaliyokusudiwa na mwandishi. Mwandishi ametumia misemo mingi sana katika kazi zake. Misemo imetumika vizuri na kuufanya ushairi wa Mnyampala kuwa na mvuto wa kisanaa.

#### **4.1.4 Ushairi-Drama**

Drama ni mbinu nyingine aliyotumia Mathias Mnyampala kuibua maudhui mbalimbali katika kazi teule. Muhando (1983) anaeleza kuwa drama ni aina mojawapo ya sanaa za maonyesho ambayo usanii wa utendaji hutegemea zaidi vitendo na uongeaji. Naye Mulokozi (2017) anafafanua kuwa drama ni igizo la kifasihi lililokusudiwa kutendeka jukwani kwa ajili ya hadhira fulani. Hivyo, tamthilia huitwa mchezo wa kuigiza na tamthiliya huwa na masimulizi ambayo huigizwa na wahusika wa pande mbili au zaidi zinazogongana. Mgongano hujenga mgogoro

ambao unaposuluhishwa au kutatuliwa mchezo huwa unakamilika. Kwa ujumla mawazo ya Mulokozi yanatuwezesha kutambua kuwa katika kazi za Mnyampala kuna mbinu ya ushairi- kidrama ijapokuwa tungo zake zimetungwa kwa kanuni za ushairi wa kimapokeo. Mbinu ya ushairi drama inajitokeza vizuri katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1 na 2*.

Wamitila (2003) anasema kuwa drama ya kishairi hutumiwa kuelezea aina ya drama au tamthiliya ambapo mazungumzo yanayopatikana yana muundo wa kishairi au hutungwa kishairi na kuakisi sifa mbalimbali za kishairi. Kadhalika Wamitila (2008) anaeleza kuwa ngonjera huwasilisha mazungumzo kwa mtindo wa kidrama ambapo wahusika husemezana kuhusu suala fulani. Kama vile matumizi ya vina, mizani au wizani. Mulokozi (2017) anaeleza kuwa ngonjera ni aina mojawapo ya ushairi wa maigizo unaotendwa jukwani na ujumbe ukawafikia walengwa. Hivyo basi kutokana na mawazo ya Wamitila na Mulokozi tunakubaliana nao kuwa mbinu ya ushairi wa maigizo hutumika katika ushairi wa Kiswahili. Hivyo katika utafiti huu tumebaini kuwa mbinu ya ushairi-drama imetumiwa katika kazi za Mnyampala na ndani ya mbinu hii kuna wahusika, jukwaa, majibizano, hadhira na vipengele vingine ambavyo ni muhimu katika drama. Uchambuzi wake ni kama ifuatavyo:

#### **4.1.4.1 Wahusika**

Katika kazi teule za Mnyampala majina ya wahusika yaliyotumika ni jumuishi lakini yanayohusiana na kitu husika na yenye kujipambanua kuhusiana na muktadha wa jambo husika. Mnyampala katika *Ngonjera za UKUTA Na 1* ametumia wahusika mbalimbali wakijibizana na kuiga vitendo na tabia za hao wanaowawakilisha katika ngonjera husika. Mnyampala amewateua wahusika hao ili kuwakilisha tabia, mienendo, hali, hisia, mawazo na matendo ya mambo yanayozungumzwa ndani ya ngonjera husika. Mfano katika ngonjera ya kwanza inayohusu “Ngonjera ni Kitu

Gani?” (uk. 5-6) Mnyampala ametumia mhusika Mdadisi na Jawabu katika kueleza maana ya ngonjera. Wahusika hao pia wametumika katika ngonjera ya “Maana Yake Nini Nyama ya Ulimi?” (uk. 84-85). Katika ngonjera hiyo wahusika hao wametumika kutoa ujumbe wa kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya ulimi. Ulimi ukitumiwa vizuri huleta amani, furaha na mapenzi kwa wanandoa na hata wanajamii, lakini ulimi ukitumika vibaya huleta machafuko katika jamii. Kwa hiyo, majina hayo yametumika kuibua dhamira ya upendo, amani, furaha, maadili, utu, mapenzi na ndoa. Pia yametumika kuelimisha hadhira kuhusu maana ya ngonjera pamoja na kutoa mawaidha kuhusu maisha.

Kadhalika, katika ngonjera ya “Tanu na Siyasa Yake” (uk. 7) wahusika ambao ni mwananchi na mwanasiasa wametumika. Wahusika hao wametumika kwa lengo la kusadifu hali halisi ya siasa iliyokuwepo wakati huo. Vilevile, wahusika hao wametumika kuzungumzia masuala ya siasa ya TANU, maana ya TANU, malengo ama madhumuni ya TANU na chama cha Afro-Shirazi. Vilevile, ngonjera ya “Siasa ya Nchi Yetu” (uk. 8) na “Muundo wa Serikali” (uk.10), wahusika hao wametumika kuibua masuala ya kisiasa na viongozi wa nchi. Aidha, mwandishi katika “Utukufu wa Taifa” (uk. 12) ametumia wahusika hao kuibua dhamira ya siasa, umoja na mshikamano, kuondokana na ukabila, kukwepa ubaguzi wa dini na kusesitiza ujenzi wa jamii mpya. Pia, mashairi hayo yanaeleza masuala ya chama cha TANU na serikali ya Tanzania.

Wahusika wengine wa kidrama wamejitokeza katika ngonjera ya “Adui Yetu Ujinga” (uk. 14-15) ambapo kuna mhusika “Mjinga na Mshauri.” Wahusika hawa wametumika kutoa elimu juu ya kuondokana na ujinga kwa njia ya kutoa elimu kwa watu wote ikiwemo elimu ya watu wazima ili watu wote waweze kujua kusoma na

kuandika pamoja na kuhamasisha watu kupenda elimu ili kuondokana na ujinga. Katika ngonjera hiyo kuna dhamira ya elimu na kuondokana na adui ujinga.

Katika ngonjera ya “Adui Yetu Umaskini” (uk. 15-16), mwandishi amewatumia wahusika “Masikini na Mshauri” kutoa mafunzo kwa jamii jinsi ya kuondokana na umaskini, hasa kwa kujibidiisha katika kazi za kilimo na za maofisini bila ya kutegemea cha ndugu wala misaada ya watu wengine, hususani wakoloni na watu wenye mali. Kuna dhamira ya kufanya kazi kwa bidii ili kuondokana na umaskini. Kwa hiyo, kupitia majibizano ya wahusika, mwandishi anawataka watu wafanye kazi kwa bidii na maarifa ili kuweza kuondokana na adui masikini ndani ya taifa la Tanzania.

Aidha, katika ngonjera ya “Adui Yetu Maradhi” (uk. 17-20) kuna wahusika “Mkongo na Mshauri,” wanaozungumzia namna ya kuondokana na magonjwa mbalimbali yanayohatarisha maisha ya wananchi. Katika ngonjera hii, mwandishi amesisitiza dhamira ya usafi, elimu na kutumia madawa ya kuondoa magonjwa na kujifunza njia za kujikinga na magonjwa hayo. Kwa ujumla, mwandishi alikuwa anazungumzia maadui watatu ambao serikali ilikusudia kuwateketeza ambao ni ujinga, umaskini na maradhi.

Wahusika wengine waliotumika ni Bozi na Mwanasiasa, katika ngonjera ya “Maendeleo ya Nchi” (uk. 20-22). Wahusika hawa wametumika kuelezea utamaduni wa Kiafrika na namna ya kuenzi utamaduni wa nchi ili kuleta maendeleo katika nchi. Ngonjera hii inaendana na ngonjera ya “Kiingereza Lugha Nzuri” (uk. 60-61), ambayo pia inatumia wahusika Bozi na Mzalendo. Kwa ujumla wahusika wa ngonjera hizi wametumika kuibua maudhui yahasuyo utamaduni wa taifa na jamii na umuhimu wa matumizi ya lugha ya taifa kwa manufaa ya kuleta maendeleo ya nchi. Mwandishi



anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ni nzuri na inafaa kwa kuwa inabeba utamaduni wa jamii; ili kuleta maendeleo ya nchi ni lazima kutumia lugha ya taifa. Ujumbe anaotoa kwa jamii ni wathamini lugha yao na kuitumia kuleta maendeleo ya taifa lao.

Katika ngonjera za “Ujamaa” sehemu ya kwanza inaelezea “Siasa ya Ujamaa ni Nini” (uk. 36-37) mwandishi ametumia wahusika Mke na Mume. Na katika ngonjera ya “Ujamaa Vijijini” (uk. 38-39) mwandishi ametumia wahusika Raia na Mwanasiasa. Mme na Mke pia wametumika katika ngonjera ya “Mke Kuomba Ruhusa kwa Mume” (uk. 40-44). Kadhalika katika kujadili masuala ya Azimio la Arusha mwandishi ametumia wahusika Mwana na Baba katika ngonjera ya “Sielewi Azimio” (uk. 45-47). Katika ngonjera hii Mwana anamuuliza baba yake maana ya Azimio. Wahusika wote hao wametumika kuibua maudhui ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Mwandishi amewatumia wahusika hawa kuwasilisha dhamira ya umoja, ushirikiano, mshikamano, amani, kufanya kazi kwa pamoja na bidii ili waweze kujitegemea, na watu wasiokuwa na kazi kuwasihi warudi vijijini kufanya kazi ya kilimo. Vilevile wahusika hawa ujumbe unaoibuliwa unahusu masuala ya usawa wa binadamu kwa wote, umuhimu wa vijiji, mahusiano mazuri baina ya wanandoa na kupinga unyonyaji baina ya mtu na mtu na hata jamii na jamii ama taifa na taifa.

Wahusika wengine waliotumika ni “Mwanasiasa na Bepari” katika ngonjera ya “Azimio Lakomesha Mirija” (uk. 47-48). Wahusika hawa wanazungumzia namna ya kuondoa unyonyaji, kutochagua viongozi fisadi na kuchagua viongozi wenye uadilifu na wenye kujali demokrasia na usawa wa binadamu. Mnyampala (1970) anaeleza kuwa:

111. Ngonjera hii ni ya mazungumzo baina ya Watanzania wawili, mmoja ni Bepari mnyonyaji na wa pili ni Mwanasiasa. Bepari ana moyo wa kisebusebu, anapenda awe kiongozi wa chama huku anawanyonya watu na kulichukia Azimio la Arusha (uk. 47).

Katika nukuu hii tunaona jinsi ngonjera inavyohusiana na drama. Mazungumzo yanayofanyika baina ya Watanzania wawili ni suala linalojitokeza katika drama. Haya ni mambo yanayotokana na mwingilianomatini katika kazi za fasihi. Katika ngonjera hiyo mwandishi anatoa ujumbe kuwa wananchi wanapaswa kuwakwepa wanyonyaji ambao wanataka wawe viongozi wa chama huku wakinyonya nchi na kulichukia Azimio. Hivyo anatoa mafunzo ya kupambana na wanyonyaji katika ngazi zote za uongozi na kupinga watu wanaojilimbikizia mali na kunyonya taifa. Katika mazungumzo yaliyopo katika ngonjera hiyo wanaibuliwa wahusika wengine kama vile: Kabaila na Mabwanyenye. Swali linaloibuliwa ni kwamba “Hawa ni watu gani?” (uk. 48-49). Katika kujibu swali hilo, mwandishi amewatumia wahusika hao kwa kuwaunda katika mchezo wa kuigiza. Kama asemavyo Mnyampala (1970):

112. Katika jitihada ya kutekeleza Azimio, Watanzania wengine waliposikia majina ya Mapepari, Makabaila na Mabwanyenye walishangaa maana hawakujua tafsiri yake ni nini? ...Ngonjera hii ina mchezo wake wa kuigiza ambapo watu hao watatu huvaa mavazi yanayoonyesha tofauti zao (uk.48-49).

Dondoo hili linatudhihirishia kuwa ngonjera huweza kuigizika kama inavyofanyika katika drama. Katika maelezo hayo kuna vipengele vya drama kama vile wahusika, maleba na jukwaa. Aidha, katika ngonjera hiyo ya “Hawa ni watu gani?” wahusika wengine waliotumika ni “Hojaji na Mwanasiasa,” ambapo Hojaji anauliza na kutaka kufahamishwa kuhusu Bepari, Kabaila na Bwanyenye. Mwanasiasa anamjibu na kumwelezea maana ya majina hayo na mbinu ya drama inajibainisha vizuri katika (uk. 50-51). Kama asemavyo mwandishi (uk. 50):

113. *Pazia limefungwa, Bepari, Kabaila na Bwanyenye wanakwenda kukaa jukwaani na mavazi yao rasmi. Halafu pazia linafunguliwa, hapo ngonjera inaendelea kwa kuonyesha waziwazi hali wamekaa vitini, kama hivi:*

Mwanasiasa

Huyo bepari ni huyu, hebu mwone machoni  
Mnene kama mbuyu, mwenye raha maishani  
Hunywa maziwa kibuyu, na kazi havikutani  
Nguvu zetu tumaini, yeye hafanyizi kazi

Huyo naye kabaila, ametakata usoni  
Ardhi kila mahala, na majumba ya mijini  
Kazi yake yeye kula, hana kazi asilani  
Daima yu furahani, maisha yake kunyonya

Na huyu ndiye bwanyenye, ajitaye Sultani  
Hutumwa atukusanye, muungwana namba wani  
Kwa shirika watunyonye, watutie utumwani  
Leo wote wabaini, watunyonyao nchini

Nukuu hii inaonyesha mbinu ya drama (kama vile maelezo ya jukwaa na kadhalika) iliyotumiwa katika kitabu hiki ili kuibua maudhui ya unyonyaji, ubinafsi na ugandamizaji wa baadhi ya watu wenye uchumi wa juu. Kipengele cha wahusika katika mbinu hii ya ushairi drama kimetumiwa pia na washairi wengine mfano Kezilahabi (rejea *Kichomi*, 1974: 51-58). Hapa kuna mwingilianomatini baina ya watunzi wa ushairi wa Kiswahili. Vilevile inaonyesha mwingilianomatini baina ya utanzu wa ushairi na utanzu wa drama.

Kadhalika, mambo yote huonyeshwa katika matendo yanayohusiana na hisia zilizopo. Wahusika wengine waliotumika ni “Mwanafunzi na Mwalimu” katika ngonjera ya “Elimu na Utamaduni” sehemu ya “Elimu ya Kujitegemea” (uk. 56-58). Mwandishi ametumia wahusika hawa ili waweze kutekeleza kwa vitendo elimu ya kujitegemea mashuleni kwa kuwa elimu hiyo ilikuwa ikifundishwa mashuleni ili baada ya kuhitimu wanafunzi hao waweze kujajiri wenyewe. Hivyo kupitia wahusika hao tunapata dhamira ya elimu ya kujitegemea na manufaa yake kwa jamii nzima. Wahusika hao wamejengwa kwa kuhusianisha na jambo linalozungumzwa. Ujumbe

utolewao hapa ni elimu ya kujitegemea ni msingi wa maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

Wahusika wengine waliotumika ni “Hojaji na Mwanasiasa” (uk. 65-66). Hawa wametumika kuzungumzia Sikukuu ya Jamhuri ya Tanzania (bara). Kadhalika mhusika Mwananchi na Mwanasisa wametumika kuelezea Sikukuu ya Muungano (uk. 66-67). Kadhalika, mhusika “Hojaji na Jawabu” wametumika kuelezea Sikukuu ya Vijana (uk. 67-68). Kwa ujumla wahusika hao wanatumika kuibua sikukuu za taifa katika nchi ya Tanzania na umuhimu wake kwa Taifa.

Katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* wahusika wametumika kwa kujirudiarudia. Kitendo cha kujirudiarudia kwa wahusika ni mwingilianomatini wa mwandishi mwenyewe. Mwingilianomatini huweza kujitokeza ndani ya kazi ya mwandishi, kutoka kwa waandishi wengine na kutoka katika muktadha uliomzaa na kumkuza msanii. Mwandishi anatumia dhana yake ya mwanzo na kuitumia kufafanua maudhui mbalimbali yaliyokusudia kuwasilisha kwa jamii husika.

Kadhalika katika *Mahadhi ya Kiswahili* kuna wahusika “mpenziwe na bwana” katika nyimbo zilizokusanywa na Mnyampala na nyingine alizoandika Mnyampala. Kama tuonavyo katika ukurasa wa 10:

114. Laliyowe, milele lisokomeka,  
 Kapumuwe, name nenda pumzika,  
 Kwako wewe, ni lipi la kukumbuka?  
 (Mpenziwe alijibu)  
 Twalisote tukisema na kuteta,  
 Vizioni na mafuta hikupaka,  
 Kwani kwangu kukosa la kukumbuka?...  
 (majibu tena ya bwana)  
 Ajabu ya punda kupanza bambea  
 Kapewa mahaba akayatezea!...

Katika nukuu hiyo, tunaona kuna wahusika wawili wanajibizana, wahusika hao ni bwana (mume) na mpenziwe (mke). Katika majibizano hayo tunapata dhamira ya mapenzi na mahusiano mazuri baina ya wapenzi ama wanandoa. Matumizi ya wahusika katika mbinu ya ushairi-drama yanaleta usikivu, hamasa na hisia kwa hadhira au wasomaji wa kazi husika. Ujumbe ni kuwa mahusiano mema katika ndoa ni msingi wa maendeleo katika familia na jamii kwa ujumla. Mbinu hii imemwezesha mtunzi kufikisha maudhui yaliyokusudiwa kwa hadhira lengwa ama kwa wasomaji wa kazi husika.

#### **4.1.4.2 Hadhira**

Hadhira ni kipengele kimojawapo kinachotumika katika drama (Hussein, 1983 na Muhando, 1983). Aidha, kazi yoyote ya sanaa ya utendaji imeundwa ili kuigizwa ama kuoneshwa mbele za watu. Wamitila (2003) anafafanua kuwa hadhira hurejelea washiriki, watazamaji ama wasikilizaji wa kazi ya fasihi na pia hadhira hutumiwa kuelezea wasomaji wa kazi ya sanaa au walengwa wa kazi ya kifasihi. Aidha, utafiti huu tumebaini kuwa hadhira imejumuisha wasomaji wa kazi ya sanaa ama walengwa wa kazi ya fasihi husika. Katika ngonjera za Mnyampala kuna matumizi ya hadhira kama mojawapo ya kipengele cha ushairi-drama.

Katika kitabu cha *Ngonjera za UKUTA Na 1* kuna matumizi ya hadhira katika ngonjera zilizomo ndani ya kitabu hicho. Aidha, Mnyampala (1970) katika dibaji yake anafafanua kuwa ngonjera ni kusoma mashairi kwa ghibu bila ya kutazamia katika kitabu au karatasi yoyote. Hivyo basi ngonjera hizi zimeandaliwa kisanaa ili ziweze kukaririwa kwa ghibu mbele za watu ama hadhira. Lengo kuu la michezo ya mashairi haya ni kuwasilisha mafunzo kwa hadhira kuhusiana na jambo linalolengwa pia hufurahisha hadhira. Hadhira kama kipengele mojawapo cha drama kimejitokeza katika ngonjera hizi hasa pale ambapo mhusika mmoja anauliza swali na kutaka

kujibiwa. Mwandishi ameonyesha kuwepo kwa hadhira katika “Ngonjera ni Kitu Gani?” mfano katika (uk. 5):

115. Mdadisi  
 Ngonjera kitu gani, nasikia kila mara  
 Yatamkwa midomoni, tena mbele ya *hadhara*  
 Je ma’na yake nini, name nipate busara  
 Maana yake ngonjera, niambie nami nijue

Hapa imetumika neno hadhara ikimaanishwa hadhira, ambapo mwandishi anamaanisha watazamaji ama wasikilizaji wa kazi ya fasihi. Kwa kuwa ngonjera yenyewe ni mchezo unaotarajiwa kuigizwa na watu wawili ama zaidi (Kawawa, 1970). Naye, Mulokozi (2017) anaeleza kuwa ngonjera huwa na pande mbili zinazojibizana kuhusu jambo fulani. Upane mmoja huwa sahihi na upande wa pili huwa umepotoka, lengo la mabishano huwa ni kuushawishi upande uliopotoka ukubaliane na upande wenye msimamo sahihi baada ya kuelimishwa. Hili linapotoka ngonjera huwa imefikia kilele chake na ujumbe hudhahirika kwa hadhira bila matatizo. Kutokana na mawazo ya Kawawa na Mulokozi, utendaji wa sanaa ya ngonjera unahitaji kuwepo kwa hadhira ili iweze kuona na kupata mafunzo kwa kile kinachofanyika. Hivyo katika sanaa hii mwandishi alitunga ngonjera zake ili ziweze kuigizwa mbele ya hadhira kama alivyoeleza mwenyewe katika dibaji yake. Kwa ujumla mtunzi wa ngonjera hizi alitunga ngonjera hizi kwa kulenga hadhira ya vijana kwa kiasi kikubwa ambao walikuwa wanachipukia na kujifunza siasa ya nchi yao. Haya tunayaona katika dibaji yake Mnyampala (1970:3) anaposema:

116. Kusudi la kutunga kitabu hiki ni kutaka kuwatia moyo na hima vijana wetu wanaosoma mashuleni ili wapate kujifunza mtindo huu wa mashairi ya ngonjera, kama yalivyo, na taaluma yake.

Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa hadhira kubwa iliyokusudiwa ilikuwa ni vijana, kwa kuwa wao ndio walikuwa na uwezo wa kukariri mashairi na kuweza kuyaonyesha vyema kwa watazamaji ama wasikilizaji. Kupitia hadhira mwandishi ameweza kutoa dhamira na mafunzo mbalimbali yanayohusu maana ya ngonjera, utamaduni wa taifa na mazingira ya nchi yao, upendo, lugha fasaha, kujua siasa za Azimio la Arusha pamoja na faida yake na miiko yake na kuwa wazalendo kwa nchi yao.

Kwa ujumla hadhira ni kipengele kinachotumika sana katika fasihi simulizi. Kwa sababu hii, waandishi huchota kipengele hiki na kukiweka katika maandishi ili kuweza kuwashirikisha wasomaji katika kazi ya fasihi andishi husika. Kwa hiyo, mwandishi anaweza kushirikisha jamii kwa kuuliza maswali, kutegua vitendawili, matumizi ya methali, kiitikio au mkarara na matumizi ya nyimbo ndani ya kazi yake husika. Hivyo, mwandishi huchota vipengele vya fasihi simulizi na kuvichopeka katika kazi za fasihi andishi. Kitendo cha kuchukua na kuchopeka vipengele vya fasihi simulizi kwenye fasihi andishi ni suala la mwingilianomatini. Hii inatuashiria kuwa hakuna kazi ya fasihi inayoweza kusimama peke yake bila kutegemea kazi nyingine ya fasihi. Kazi yoyote ya fasihi sharti iingiliane na kutegemeana na kazi zingine. Naye Wamitila (2008) anaeleza kuwa mwingilianomatini hauna kikomo, kwani matini yoyote inaweza kuingiliana na matini nyingine. Kwa hiyo mwingiliano wa matini husababisha kuibuka kwa matini nyingine yenye kusawiri baadhi ya vipengele kutoka katika matini tangulizi. Hali hii imejitokeza katika tungo za Mnyampala hususani katika ngonjera. Ngonjera zilikuwepo katika fasihi simulizi za kijamii, Mnyampala amechukua majibizano yaliyokuwepo katika jamii hizo na kuyaboresha kwa kuchota baadhi ya vipengele kutoka katika fasihi za kigeni na kuunda mashairi ya ngonjera yenye ubunifu zaidi na yenye kutumia hadhira.

#### 4.1.4.3 Jukwaa

Jukwaa ni mahali ambapo matendo ya waigizaji hutendeka ili waweze kuonekana na hadhira husika. Murusuri (2011) anafafanua kuwa jukwaa ni mahali ambapo kazi ya sanaa au igizo hufanyika. Jukwaa huweza kuwa nje au ndani ya jengo kubwa linaloweza kuchukua idadi kubwa ya watazamaji. Kadhalika jukwaa huweza kuwa halisi au la kufikirika. Katika uchambuzi huu tumebaini kuwa jukwaa halisi limetumika katika ngonjera hizi kama mojawapo ya vipengele vya drama. Ngonjera hizi ziliigizwa na makundi mbalimbali ya watu ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa shule za msingi, sekondari, Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na watu waliokuwa tayari kuimba ngonjera hizo. Vilevile ngonjera hizo zilikuwa zikitendwa jukwaani katika maeneo mbalimbali kama vile mashuleni, katika mikutano mbalimbali ya kisiasa na sehemu nyinginezo<sup>43</sup>.

Mulokozi (2017) anaeleza kuwa ngonjera ni aina ya propaganda inayoigizwa jukwaani. Anaongezea kuwa mifano ya ngonjera inapatikana katika Mnyampala *Ngonjera za UKUTA Na. 1 na 2*. Kutokana na ufafanuzi wa Mulokozi, tunakubaliana naye kuwa ngonjera za Mnyampala zote zinaweza kuigizwa jukwaani, kwa kuwa ngonjera hizo zina pande mbili zinazojibizana kuhusu jambo fulani. Upande mmoja huwa sahihi na upande wa pili unakuwa umepotoka. Katika mabishano hayo hushawishi upande uliopotoka ukubaliane na upande ulio sahihi. Aidha, ngonjera nyingi zimetumia majukwaa ya asili ambayo yanaweza kupatikana mahali popote kulingana na mahitaji ya jamii. Vilevile majukwaa yaliyotumika katika ngonjera hizi ni yale yanayotegemea shughuli inayofanyika. Mfano katika ngonjera ya “Mke Kuomba Ruhusa kwa Mume” (uk. 40), yaelekea kuna jukwaa lenye vifaa vya

---

<sup>43</sup> Maelezo haya tuliyapata katika mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na Prof. Madumulla pamoja na Bi Mary Mangwela.



shambani. Kwa sababu baada ya malumbano Mke aliendelea kulima shamba la ujamaa vijijini.

Vilevile, katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* jukwaa maalumu linaonekana katika ngonjera ya “Hawa ni Watu Gani?” (uk.50). Mwandishi anaeleza:

117. Pazia linafunguliwa Bepari, Kabaila na Bwanyenye wanakwenda kukaa jukwaani na mavazi yao rasmi.

Jukwaa lililotumika hapo ni lile linaloelezwa na mwandishi kabla ya ngonjera. Jukwaa hilo ni la kudumu na la kisasa ambalo haliwezi kuhamishika kwa urahisi. Mara nyingi jukwaa la namna hii hujengwa ndani ya jengo halisi na la kudumu na hutumia pazia au taa ili kubadilisha matukio mbalimbali. Jukwaa hili ni lile lililozungumziwa na Aristotle katika tamthilia (Wamitila, 2003). Matumizi hayo ya jukwaa yameambatana na matumizi ya maleba. Pale ambapo mwandishi anazungumzia masuala ya uvaaji wa Bepari, Kabaila na Bwanyenye, hali ya uvaaji huleta udrama katika ngonjera na mavazi hayo ndio maleba yenyewe. Katika ngonjera hiyo ya “Hawa Ndio Watu Gani?” (uk. 48-51), wahusika hao wanatambuliwa kutokana na mavazi yao. Kwa ujumla mwandishi amechota vipengele vya drama ama tamthilia na kuvitumia katika uandishi wa ngonjera hizo.

Jukwaa alilotumia Mnyampala ni la kimwingiliano zaidi baina ya sanaa za maonyesho za kigeni na za kijadi. Katika sanaa za maonyesho za kigeni Aristotle alitumia jukwaa la ndani ya jengo likiongozwa na taa. Taa hizo zilikuwa zikiwashwa mara igizo lilipokuwa linaanza na kuzimwa mara onyesho linapokwisha au waigizaji wanapobadilishana sehemu za onyesho hilo. Kwa upande wa sanaa za maonyesho za kijadi, waandishi wa Kiafrika kama vile Ebrahim Hussein na Penina Mhando wanaeleza kwamba jukwaa la Kiafrika linaweza kupatikana mahali popote ambapo

igizo linafanyika kama vile shuleni, uwanjani na kadhalika. Jukwaa hili ndilo limetumika katika *Ngonjera za UKUTANA 1* ili kutangaza siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Kwa ujumla watu waliokuwa wakitamba ngonjera hizo walitumia majukwaa ya kawaida hasa palipokuwa na mkusanyiko wa watu.

Katika mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na Balozi Jobu Lusinde alieleza kuwa ngonjera hizo zilitambwa mahali popote palipokuwa pamechaguliwa na wananchi. Aliongezea kuwa ngonjera hizo zilikuwa na mchango mkubwa kwa wananchi kuijua siasa ya nchi yao. Mwandishi amechukua mtazamo wa jukwaa la sanaa za maonyesho za kijadi na za Ki-Aristotle na kutumia majukwaa hayo katika ngonjera zake. Ili kuibua ujumbe na dhamira ya ufisadi, ukandamizaji na unyonyaji wa watu na raslimali za nchi na ujenzi wa jamii mpya.

#### **4.1.4.4 Majibizano**

Majibizano ni mbinu inayotumika mara nyingi katika utanzu wa tamthilia. Majibizano hutumika katika fasihi simulizi kama vile utanzu wa ushairi simulizi na masimulizi na hata fasihi andishi. Omari (2011) anasema kuwa majibizano ni mbinu mojawapo ya ushairi iliyokuwepo tangu kale na ilitumika kwa namna mbalimbali, lakini majibizano yanayojulikana zaidi ni yale ya ngonjera na ushairi wa majibizano. Anaongezea kuwa ngonjera zinatumia majibizano ambayo yanahusisha upinzani wa pande mbili ambao unaleta mjadala. Majibizano hayo huweza kujitokeza ndani ya shairi husika au baina ya washairi. Wamitila (2008) anaeleza kuwa usemezano katika ushairi huweza kujitokeza pale ambapo mtunzi mmoja anatunga shairi kuhusu suala la mjadala ambalo linaendelezwa na washairi wengine katika tungo zao. Mulokozi (2017) anaeleza kuwa kabla ya Mnyampala, ushairi wa majibizano ulikuwepo. Hata hivyo, haukuwa wa kimaigizo kwa namna ya ngonjera. Ulikuwa unatambwa, kama vile katika ngoma au shughuli za arusi. Maelezo ya Mulokozi

yanatudhihirishia kuwa majibizano yalikuwepo katika fasihi simulizi za kijadi. Kwa upande wa fasihi andishi majibizano yalikuwepo kabla ya Mnyampala, kama vile katika jamii za Wagogo, Uswahilini na katika makabila mengine.

Naye Biersteker (1996) anaeleza kuwa matumizi ya mbinu au sanaa ya ushairi wa majibizano, mathalani yalifanywa baina ya Nyerere na Kandoro kati ya mwaka 1965 na 1969 wakati wa kipindi cha mjadala mkali wa misingi ya Azimio la Arusha (1967) na Ujamaa na Kujitegemea nchini Tanzania. Majibizano hayo yalifanywa mbele ya hadhira na watu waliohusika walialikwa. Hata hivyo, majibizano katika ngonjera za Mnyampala ni tofauti na majibizano yaliyofanywa na Nyerere na Kandoro. Mfano Nyerere na Kandoro walifanya majibizano ambayo kila mmoja alijibu kulingana na uelewa wake kutokana na ujumbe uliotoka kwa mwenzake. Mnyampala katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, aliyafanya majibizano ya kishairi kuwa ya kimaigizo zaidi kwa kutumia wahusika ambao wanapokezana kauli za shairi hilo hilo moja. Hivyo kuanzia mwanzo wa *Ngonjera za UKUTA Na. 1* hadi mwisho kuna majibizano ya kimaigizo ndani ya shairi husika.

Aidha, majibizano ya ushairi wa ngonjera ni ya kimaigizo, na utambaji wa ngonjera hufanywa katika maeneo maalumu ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira mahsus. Kama asemavyo Komba (1969:18) kuwa katika ngonjera kuna michezo, ubeti wa 174 katika utenzi wa Mtumishi Wetu Mnyampala, unasema:

118. Huwa pamo na michezo  
Kuongeza vidokezo  
Hiyo hutia mkazo  
Ngonjera zikavutia

Kupitia dondoo hilo tunakubaliana na Komba kuwa katika ngonjera kuna michezo na ngonjera huweza kuigizwa jukwaani. Michezo hiyo ndiyo drama yenyewe ambayo

lazima kuwepo na majibizano ndani yake. Naye Mihale (2011) anafafanua kuwa ngonjera ni miongoni mwa vitabu maarufu vya ushairi vilivyoandikwa na Mnyampala katika muundo wa ushairi wa majibizano ambao yeye aliuita ngonjera. Tunakubaliana na mawazo ya Mihale kuwa ngonjera zimeandikwa kwa mtindo wa majibizano, lakini si majibizano tu bali majibizano ya kimaigizo.

Katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, Mnyampala ametumia mbinu ya ushairi wa maigizo kwa kuufanya ushairi kuwa wa majibizano na wa kimaigizo zaidi. Amefanya hivi kwa kuweka pande mbili zinazojibizana kuhusu jambo fulani linazozungumziwa. Katika pande hizo kunakuwa na upande mmoja ulio sahihi au kuwa na ujuzi wa kile kinachozungumzwa kwa mujibu wa mtunzi na mwingine unakuwa umepotoka ama kutokuwa na uelewa juu ya jambo linalozungumzwa. Lengo kuu la majibizano hayo ni kutaka kuushawishi upande uliopotoka ama ambao hauna ujuzi ukubaliane na upande ulio sahihi. Mbinu ya majibizano ama dialogia imetumika kuibua ujumbe na dhamira za kisiasa hususani siasa za Ujamaa na Kujitegemea.

Naye Mnyampala (1970) anaeleza kuwa majibizano katika mashairi ya ngonjera ni lazima yawe na mafunzo ndani yake na kama hayana mafunzo ama vidokezo vya kufurahisha na kuchangamsha basi hayawezi kuitwa ngonjera. Kwa ujumla, Mnyampala anakiri kuwa ngonjera ni michezo na lazima kuwa na hali ya kuchangamsha na kuburudisha ambapo hali hizo hujidhihirisha zaidi kupitia vitendo. Ngonjera hizo huweza kuigizika na kuonyesha vitendo kwa hadhira na kusababisha vipengele mbalimbali vya drama kujitokeza.

Kitabu cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* na mswada wa *Hazina ya Washairi* vinahusu mashairi ya waandishi mbalimbali ambao walikuwa wanajibizana, hivyo kuna mtindo wa majibizano baina ya washairi. Katika *Mashairi ya Hekima na*

*Malumbano ya Ushairi* majibizano yaliyopo ni tofauti na majibizano yaliyotumika katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*. Majibizano katika kitabu cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* yamejitokeza baada ya Amri Abedi kuandika shairi la “Raha” (uk. 8) na kuzua malumbano ya ushairi. Katika kitabu hiki majibizano yaliyojitokeza ni yale ambayo mshairi anaandika shairi na wengine wanaibuka kuzungumzia shairi hilo na kusababisha malumbano. Wamitila (2008) anafafanua kuwa usemezano wa kishairi huweza kujitokeza pia pale ambapo mshairi mmoja anazungumzia jambo kwa njia inayojenga uhusiano wa shairi lake na utungo wa mshairi mwingine hata kama mtunzi wa kwanza hakuzungumzia suala la mjadala.

Katika kitabu cha *Mashairi Hekima na Maumbano ya Ushairi* majibizano hayo yamejitokeza vyema hasa katika upande wa *Malumbano ya Ushairi*. Mnyampala (1968) katika dibaji yake anaeleza kuwa malumbano hayo yalifanya kuwepo kwa waandishi waliokuwa upande wa Amri Abedi na wengine upande wa kumtetea yule mtu waliosadiki kuwa Amri Abedi alimtungia shairi hilo. Mbinu hii ya majibizano imetumika kimwingiliano matini hasa katika uundaji wa mashairi na kuibua dhamira ya fitina, upendo, ushirikiano na utu miongoni mwa washairi. Katika malumbano hayo hata Mnyampala alikuwemo na alikuwa katika upande wa kumtetea Amri Abedi.

Majibizano hayo yalitokana na shairi hili la “Raha” (uk. 8) lililoandikwa na Kaluta Amri Abedi, lenye maudhui ya maisha, yaani namna ya kuishi vizuri na walimwengu, kutenda mema katika jamii, kuheshimu watu, kupata mali na vitu vya halali. Aidha, Kaluta Amri Abedi alitaka jamii itambue kuwa si mara zote kuwa na mali nyingi huleta furaha na raha kamili. Pia mwandishi alikuwa anaelimisha jamii kwamba mtu mwenye nacho anaweza kupoteza mali zote kutokana na mabadiliko yanayojitokeza katika jamii. Vilevile, anatoa ujumbe kuwa raha ikizidi husababisha mauzauza ama

karaha. Katika shairi lingine liitwalo “Mtego” (uk. 14) ambalo lilijibu shairi la “Raha,” Khamis Amani Khamis anatoa ujumbe kuwa tusipende kucheka wenzetu wanavyoingia katika maovu bali tunatakiwa kuona aibu kwa ajili ya makosa wanayofanya.

Pia lilifuatia shairi la Mahmoud Hamdouniy ambaye alitunga shairi la “Dunia Duara” (uk. 10), “Dunia Nyama ya Tembo” (uk. 11) na “Mizani” (uk. 12). Hamdouniy anamaanisha kuwa usicheke mambo yanayomtokea mwenzako leo, kwa kuwa dunia ni duara, kesho yanaweza kukutokea wewe. Shairi hili lilikuwa linamwonya Amri Abedi kutofurahia maovu. Pia ujumbe huu unawahusu washairi wote na wasomaji wa mashairi haya kuwa ukiona mwenzako anafikwa na shida ama tatizo unapaswa kumuonea huruma na kujitahadhari ili shida hizo zisije zikakukumba. Tatizo la mwenzako ni lako pia. Mtunzi anawasilisha dhamira ya mapenzi na upendo kwa watu wote na kuwaombea watu wote wanaopata shida ama matatizo mbalimbali. Mwandishi anasisitiza kwamba kabla ya kutoa hukumu kwa mtu ni lazima kufanya uchunguzi kwanza. Vilevile, kuna dhamira ya dini, mwandishi anaitaka jamii kumtanguliza Mungu katika yote na kuwa na upendo kwa watu wote.

Aidha, Mahmoud alitoa shairi lililoitwa “Hujuvywa Asiyejua” (uk. 12-13). Mwandishi wa shairi hili alikuwa anamjibu Kaluta Amri Abedi kutumia msemu “hujuvywa asiyejua ama hutanabahishwa.” Anatoa mafunzo kuwa mtu yeyote asiyejua ni muhimu kuelimishwa ama kutahadharishwa kuliko kumlaumu. Aidha, anasisitiza kuwa watu wanatakiwa kujishusha katika jamii, na majigambo si kitu chema kwani Mungu ndiye anayepanga na kupangua, hivyo mtu yeyote anatakiwa kuwa makini na asemacho ama aandikacho, kwa kuwa kesho hatujui itakuwaje. Dhamira zinazojitokeza katika shairi hili ni dini, madaraka, kuchukua maovu na kutochekelea ubaya.

Shairi la “Ni Waadhi Ushairi” (uk. 13) lililoandikwa na Mathias Mnyampala baadaye lilifuata kuwajibu waliokuwa wanamtuhumu Amri Abedi kwa shairi lake la “Raha.” Mnyampala anaeleza kuwa shairi hilo lilihusu mawaidha ya namna ya kuishi ulimwenguni, wala halikumlenga kumsema mtu. Anaeleza kuwa ushairi uliotungwa na Amri Abedi ulikuwa unahusu mawaidha kwa jamii, watu kutenda mema na namna ya kuishi katika jamii. Anaeleza kuwa ushairi wa kusemana haufai na wala hauna utu kwa binadamu na ni dhambi mbele ya Mungu. Ujumbe anaotoa hapa ni kwamba ushairi si kitu cha kuchekana dosari zetu au kusemana kwani tukifanya hivyo tunamchukiza Mungu.

Mnyampala katika shairi hilo anakemea tabia ya washairi kusemana. Kwa maoni yake, tabia hiyo haipendezi na ni tabia isiyofaa katika jamii. Shairi hili lina dhamira ya dini na upendo, yaani washairi wapendane na wasichekelee mabaya ya wenzao. Aidha, Amri Abedi alitunga shairi la “Dhana” (uk. 15) kuwajibu wale waliokuwa wakimtuhumu. Anaeleza kuwa watu wanapindisha mambo kutokana na kutoelewa maana ya jambo linalozungumzwa. Majibizano haya yaliendelea na mwisho wakamaliza kwa kuombana msamaha. Majibizano haya yanaibua dhamira mbalimbali kama vile maadili, dini, upendo, umoja, ushirikiano na mshikamano miongoni mwa washairi. Ujumbe tunaopata hapa ni kwamba kabla ya kuhukumu jambo au mtu fulani ni lazima kufanya uchunguzi ama utafiti wa jambo na sio kudhania. Vilevile, hakuna mkamilifu hivyo mtu yeyote katika jamii anafaa kuwa mtu anayejikosa na kujirekebisha.

Hapa tunajifunza kuwa binadamu hatujakamilika na tunahitaji kuwa na tahadhari katika maisha tuishio. Ujumbe mwingine ni kwamba washairi wanapaswa kufuata kanuni za ushairi kwa kutunga mashairi yenye mafunzo sio mashairi ya kusemana.

Kwa ujumla katika mashairi hayo kuna mwingiliano wa matini mbalimbali na hata maudhui. Majibizano hayo yaliyojitokeza katika diwani hiyo yamejikita katika mbinu ya ushairi-drama na mbinu hii imesaidia kuibua maudhui mbalimbali ndani ya diwani hiyo.

Kipengele hiki cha majibizano kimetumika pia katika mswada wa *Hazina ya Washairi*. Mnyampala (1966:i) katika dibaji yake anaeleza kuwa “mashairi yaliyomo katika kitabu hiki yanahusu mjadala, mawaidha na ngonjera.” Hivyo, katika mijadala, mawaidha na ngonjera, udruma unajidhihirisha. Katika mswada wa *Hazina ya Washairi* mbinu ya ushairi-drama imejitokeza kupitia kipengele cha majibizano yaliyokuwa yanatolewa kwa njia ya washairi ambapo mshairi mmoja alitunga shairi la kimjadala na wengine kujibu shairi hilo. Katika mbinu hii Nadharia ya Mwingilianomatini imesawiriwa vyema kwani hoja na utunzi wa mashairi yaliyomo katika mswada huu unaingiliana, unategemeana na kukamilishana. Kwa sababu mshairi mmoja anaandika shairi na mwingine baada ya kusoma shairi hilo hulijibu, hivyo mawazo yao yanatokana na shairi lililoanza na kuibua shairi jipya.

Katika mswada huu kuna majibizano tangu mwanzo hadi mwisho wa mswada, lakini katika tasnifu hii tumejadili majibizano yaliyomhusisha Mnyampala. Kwa hiyo katika *Hazina ya Washairi* majibizano yaliyomhusisha Mnyampala ni yale yaliyohusu haki ya mtoto wa kike kuchagua mwenzi wa kuishi naye. Katika majibizano hayo watunzi mbalimbali waliandika mashairi yao yakitoa ufafanuzi juu ya suala hilo na wakitetea haki za watoto wa kike katika kuchagua mwenzi wa kuishi naye. Baadhi ya mashairi hayo ni “Ndoa ya Shuruti Mbaya” (uk. 34) lililoandikwa na Ramadhani Mwaruka, “Ndoa Aridhi Nani” (uk.35) alilotunga Amri Abedi, na “Mzazi Kuridhi Ndoa” (uk. 35) lililoandikwa na Mathias Mnyampala. Katika majibizano hayo kuna dhamira ya



mapenzi, ndoa, usawa wa kijinsia na haki ya mtoto wa kike katika kuchagua mwenzi wa kuishi naye.

Kwa upande wa *Diwani ya Mnyampala* kuna majibizano baina ya Akilimali Snow White na Mnyampala. Mnyampala alipoandika shairi la “Usitukane Wakunga” (uk. 17), Snow White alipinga shairi hilo kwa shairi la “Kuzaa si Kazi Kubwa, Kazi Kubwa ni Kulea.” Kama asemavyo Mnyampala (1965: 18) kuwa “mshairi mmoja wa Kigoma aitwaye Snow-White alipinga shairi hili lilipotoka, naye alisema hivi, *Kuzaa si kazi kubwa, kazi kubwa ni kulea.*” Mnyampala anaendelea kueleza kuwa nami nilimjibu kwamba “Tutalea Mwana Gani?” (uk. 18). Katika mashairi hayo kuna dhamira ya uzazi na malezi. Pia kuna mwingilianomatini na majibizano baina ya mawazo ya Mnyampala na Snow White katika diwani hiyo.

Kadhalika katika *Mahadhi ya Kiswahili*, kipengele cha majibizano kimejitokeza kwa kiasi kidogo tukilinganisha na kazi teule zingine tulizoziorodhesha hapo juu. Majibizano yamejitokeza baina ya wapenzi katika nyimbo zilizokusanywa na Mnyampala mwenyewe mwaka 1943 hadi 1953 na zile zilizotungwa na Mathias Mnyampala, Mbabe Athumani na wengineo. Majibizano hayo tunayapata katika (uk. 10) kama tuonavyo hapa:

119. Laliyowe, milele lisokomeka,  
 Kapumuwe, nami nenda pumzika,  
 Kwako wewe, ni lipi la kukumbuka?  
 (Mpenziwe anajibu)  
 Twalisote tukisema na kuteka,  
 Vizioni na mafuta hikupaka  
 Kwani kwangu kukosa la kukumbuka?
- Kheri kunitinda kwa kisu Kikali,  
 Kama kunikera kwa hili na hili,  
 Nambiwa napendwa sioni dalili.  
 (Majibu tena ya Bwana) ...

Katika nukuu hizo kuna majibizano ya kidrama ambapo kuna mabishano baina ya watu wawili na kuna kubadilishana kwa nafasi. Kupitia majibizano hayo tunapata dhamira ya mapenzi, huhusani kuonyesha upendo kwa mwenzi wa ndoa ama baina ya wachumba. Majibizano mengine yanajitokeza katika nyimbo (uk. 13) zilizoandikwa na kukusanywa na Mnyampala na watunzi wengineo. Kuna majibizano baina ya wapenzi wawili, kama ionekanavyo hapa:

120. Barua yangu ikifika, soma ukitulizana,  
 Majibu yangu nataka, nijibu yenye maana,  
 Roho yangu ikitoka, tahamala sina tena,  
 (Mpenziwe alijibu hivi)  
 Ulipoleta barua, mimi nilikuwa sipo  
 Laiti ningalikua, ningajibu papo hapo,  
 Hana rai hana rua, mwanamume apendapo  
 (Mwandika barua alisema)  
 Waninyang'anya kikombe, sijaisha hamu yangu,...

Katika madondoo haya kuna majibizano baina ya mwanamume na mwanamke, mwanamume anamwandikia barua mwanamke ya kumtaka kimapenzi na mwanamke anamjibu. Majibizano haya yanahusu mahusiano baina ya mke na mume. Kwa ujumla majibizano yaliyokuwemo katika *Mahadhi ya Kiswahili* yanahusu dhamira ya mapenzi, ndoa na mahusiano katika maisha ya mwanadamu.

Tunaweza kuhitimisha kuwa mbinu ya majibizano mara nyingi hujitokeza katika drama. Lakini kwa kuwa kazi za fasihi hazina mipaka na huingiliana na kukamilishana hivyo mbinu hii huweza kutumika pia katika ushairi kama tulivyoona hapa. Mbinu hii imetumika katika kuibua maudhui ndani ya kazi teule za Mnyampala. Irwin (2004) anashadidia hali hii kwa kueleza kuwa, uandishi, usomaji na uhakiki wa matini husika unajumuisha uhusianishaji na utambuzi awali wa matini zingine zilizosomwa kabla. Hii ina maana kuwa matini hutokana na unukuzi ama mahusiano

na matini tangulizi na hakuna matini inayoweza kujitosheleza pasipo utegemezi wa matini nyingine zilizotangulia.

#### 4.1.5 Nyimbo

Wataalamu wengi huainisha nyimbo kuwa ni kipera cha ushairi. Mbinu ya nyimbo inatumiwa sana na watunzi wa kazi mbalimbali za fasihi andishi kama vile riwaya, hadithi fupi na tamthilia. Hata hivyo haina maana kuwa mbinu ya nyimbo haipo katika ushairi, licha ya wataalamu wengine kusema ushairi ni wimbo, kama asemavyo Robert (1958:37) kuwa: “ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi.” Naye Mnyampala (1965: iv) anaeleza kuwa “mashairi si kitu kingine ni nyimbo.” Wataalamu hawa wanaona nyimbo na ushairi ni kitu kimoja, wakati wimbo ni aina mojawapo ya ushairi. Ukweli ni kwamba ushairi na wimbo vina uhusiano wa karibu, na ushairi wa kijadi ulijibainisha katika nyimbo na nyimbo ni mojawapo ya bahari za ushairi wa kijadi (Mulokozi, 2017). Kadhalika Mulokozi (2017:117) anasema kuwa:

121. Nyimbo na ushairi ni ndugu. Undugu huo unatokana na vigezo fulani vinavyobainisha fani hizo: kwa mfano nudhumu (utunzi wa kufuata kanuni fulani za urari, uzito wa hisia, muktadha wa kisanii wa uwasilishaji kwa hadhira, mathalan kwa kutumia ala za muziki, na matini yaliyosukwa kibunifu ili kumathilisha badala ya kuelezea tu...Yatosha kusema kuwa kuna ukaribu kati ya nyimbo na ushairi, lakini si kila wimbo ni shairi, na si kila shairi ni wimbo.

Vilevile, Mulokozi (2017:118) anafafanua kuwa “wimbo ni utungo wa kisanaa unaowasilishwa kimuziki kwa kutumia sauti iliyo katika mpangilio fulani wa mahadhi na melodia, na yenye mapigo ya kiurari.” Anaongezea kuwa nyimbo ni bahari mojawapo ya ushairi wa kimapokeo. Hivyo basi tunakubaliana na Mulokozi kuwa nyimbo ni bahari mojawapo ya ushairi wa kijadi. Kadhalika, nyimbo ni kipengele mojawapo cha fasihi ya Kiswahili ya kimajaribio. Katika mashairi ya Mnyampala

bahari hii imejdhahirisha katika mashairi yake yote kwa kuwa mashairi yake yanafuata kanuni za urari wa vina na mizani na yanaimbika. Vilevile, katika mashairi ya Mnyampala kuna mwingiliano tanzu ama matini unaosababisha kuibuka kwa maudhui ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika kazi hizo. Kutumika kwa nyimbo za namna mbalimbali kunaonyesha kuwa kazi za Mnyampala zimeathiriwa na fasihi simulizi za Kiafrika. Matumizi ya mashairi yanayoimbika katika kazi za Mnyampala yanadhahirisha mwingilianomatini wa tungo zake na tanzu za fasihi simulizi katika jamii. Kama asemavyo Wamitila (2008) fasihi haitoki katika ombwe bali inatokana na fasihi tangulizi aliyowahi kuisoma au kuisikia. Kazi yoyote ya fasihi sharti itokane na fasihi tangulizi.

Nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa katika jamii. Nyimbo ni kila kinachoweza kuimbwa. Hivyo mashairi yote ya kimapokeo yana nyimbo ndani yake kwa kuwa huweza kuimbika. Hivyo basi nyimbo zimejitokeza kwa njia moja ama nyingine katika kazi teule. *Diwani ya Mnyampala, Mashairi ya Vidato, Ngonjera za UKUTANA. 1 na Mahadhi ya Kiswahili* zimetumia mbinu hii ili kuibua maudhui yake. Hivyo, nyimbo hutumika kuwaburudisha wasikilizaji na kuvuta usikivu kwa hadhira na kuwafanya wakumbuke matukio yaliyotungiwa nyimbo. Pia nyimbo hutia hamasa katika vita, kubembeleza watoto ili walale, kuchapuzi kazi, kuleta mahusiano mema, kutumbuiza na hata kunogesa masimulizi. Nyimbo ni fani ya fasihi simulizi na ni mojawapo ya bahari ya ushairi.

Katika *Diwani ya Mnyampala*, licha ya kwamba mashairi yote yanaweza kuimbika, tumetumia mashairi machache ambayo nyimbo zinajitokeza zaidi. Tumefanya hivyo ili kukwepa urudiaji wa maudhui unaoweza kujitokeza katika kazi hii. Mwandishi amechukua masimulizi yanayohusu kuzaliwa kwa Yesu na kuyawakilisha katika

mfumo wa ushairi, ambapo shairi hili lilivyotungwa huwezwa kuimbika vizuri. Hii inaonekana katika shairi la “Rabbi Yesu Kazaliwa” (uk. 39):

122. Leo ni siku Tukufu, ya mwokozi kuzaliwa,  
 Ndio siku takatifu, nayo ilobarikiwa,  
 Baba Mungu tumsifu, ahadi kutimiza,  
 Siku ya kushangiliwa, ndio hii takatifu.

Katika shairi hili Mnyampala anaeleza kisa cha kuzaliwa kwa Yesu, jinsi alivyojaliwa huko Bethlehemu na wazazi wake. Hili ni simulizi ama hadithi ya Yesu ambayo imewekwa katika masimulizi. Hapa mwandishi anaitaka hadhira imsifu na kumtukua Mungu kwa kuwa ametimiza ahadi. Katika wimbo huo kuna maudhui ya dini ya Kikristo. Aidha, katika shairi hili kuna matumizi ya nyimbo kama utanzu mojawapo wa fasihi simulizi. Wimbo huo umejitokeza katika ubeti wa kumi na moja, ambao ni:

123. Bada ya kuwaarifu, na nyimbo zikasikiwa,  
 “Mtukufu Mtukufu, Mtukufu Msifiwa,  
 Wa amani kamilifu, wokovu mumeletewa”  
 Siku ya kushangilia, ndio hii takatifu. (uk. 40)

Hapa kuna matumizi ya nyimbo kama mojawapo ya kipera cha ushairi simulizi (Mulokozi, 1996). Abedi (1964) katika utangulizi ya *Waadhi wa Ushairi* anasema kuwa kabla ya watu hawajajua kuandika mashairi yalikuwa yametungwa na kuimbwa katika ngoma, jando na unyago. Anaeleza kuwa mashairi si kitu kingine bali ni nyimbo na waliokuwa wakizitunga na kuziimba ni “manju” au malenga. Anaongezea kuwa mabadiliko katika utaratibu huu yalitokana na kuja kwa Waarabu ambao walileta ujuzi wa kusoma na kuandika na kuweka ushairi katika maandishi. Kutokana na maelezo ya Abedi ushairi andishi umetokana na ushairi simulizi uliokuwa unajidhihirisha zaidi katika nyimbo.

Kwa hiyo, ushairi unahusiana na nyimbo kwa kiasi kikubwa ijapokuwa ushairi si nyimbo ila nyimbo ni kipengele mojawapo katika ushairi simulizi. Hivyo, mwandishi amechukua nyimbo na hadithi za kuzaliwa kwa Yesu na kuziweka katika ushairi andishi. Wimbo huu wa “Mtukufu Mtukufu, Mtukufu msifiwa, wa amani kamilifu, wokovu mumeletewa” umetokana na wimbo ulioimbwa katika Luka 2: 14, unaosema kuwa “Atukuzwe Mungu juu Mbinguni na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia.” Mwandishi alichukua mawazo ya wimbo huo na kufanya mabadiliko kidogo kulingana na muktadha uliokuwepo ili uwe kisanaa zaidi kwa kufuata urari wa vina na mizani. Suala hili linaonyesha kiwango kikubwa cha mwingiliano tanzu. Mwingiliano tanzu katika kazi za fasihi ni mojawapo ya muhimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini.

Kadhalika, nyimbo zimejitokeza katika shairi la “Amezaliwa Mwokozi” (uk. 130) katika *Diwani ya Mnyampala*. Shairi hili limetokana na maneno yaliyomo katika *Biblia Takatifu* kama ilivyo katika shairi la “Rabbi Kazaliwa Mwokozi” (uk. 39). Shairi la “Amezaliwa Mwokozi” (uk. 130) lina matumizi ya nyimbo katika ubeti wa nne usemao:

124. Haya twimbeni Hossana, kwa sauti waziwazi,  
Sauti za kupatana, ya vinanda na miluzi,  
Tusali bila ajizi,  
Ajizi si muawana, huleta maangamizi,  
Haina jema kufana, mbele huna mtetezi,  
Amezaliwa mwokozi, waumini farahini.

Hapa mwandishi anaposema tuimbe Hossana anaibua dhamira ya dini ya Kikristo hasa katika kuzaliwa kwa Yesu ambaye ndiye chimbuko la dini hiyo. Tunaweza kusema kuna mwingiliano wa hadithi za visasili vya dini ya Kikristo. Pia matumizi ya nyimbo yametumika katika shairi la “Kiongozi Mtukufu” (uk. 26-27), shairi hilo

linazungumzia sikukuu ya Pasaka ambayo inaadhimishwa na waumini wa dini ya Kikristo, ubeti wa saba unasema:

125. Aprili tufikie, na Pasaka takatifu,  
Pasaka tushangilie, na Tujipange kwa safu,  
Tuimbe atusikie, Alleluya suluhifu,  
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee. (uk. 27)

Nukuu inaonyesha mwingiliano wa matini ya sikukuu ya Pasaka inayohusu kufufuka kwa Yesu Kristo, na inayoadhimishwa mara nyingi mwezi wa Aprili kila mwaka. Katika sikukuu hiyo kanisa Katoliki lazima waimbe wimbo wa ‘Alleluya’ na kushangilia ufufuko wa Yesu Kristo, wimbo huo unaibua maudhui ya dini.

Kwa ujumla katika diwani hii mwandishi ametumia mashairi yanayoweza kuimbika na mashairi mengi yana kituo bahari kinachojirudia kila ubeti. Hii inatudhihirishia kuwa mashairi yaliyomo ndani ya diwani hii yanaimbika. Kwa ujumla, mbinu ya nyimbo katika diwani hii imetumika kuibua maudhui ya kisiasa, kijamii, kidini, kiuchumi na kiutamaduni.

Katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, mbinu ya nyimbo inajitokeza vyema kwa kuwa ngonjera ni aina ya mashairi na mashairi haya yanakaririwa kichwani na kughanwa mbele ya hadhira hivyo basi ngonjera hizi zinaweza kuimbika kama wimbo wa kawaida. Komba (1969: 18) anasema kuwa kwenye ngonjera kuna nyimbo. Ubeti wa 175 (uk.18), katika utenzi wa “Mtumishi Wetu Mnyampala” Komba anaeleza kuwa:

126. Pia humo kuna nyimbo,  
Hizo kuvumisha mambo,  
Na kutongoa mafumbo,  
Siasa kuisifia.

Kupitia nukuu hiyo, tunapata ithibati kuwa katika ngonjera kuna nyimbo na ngonjera zote huimbika. Hivyo basi ngonjera za UKUTA zote huimbika na zina mbinu ya

nyimbo ndani yake. Aidha, uimbaji wa ngonjera huibua maudhui mbalimbali kama vile lugha ya Kiswahili na utamaduni wa taifa, ambapo wanajamii hususani wanafunzi, wanajifunza namna ya kutamka maneno fasaha ya Kiswahili. Aidha, uimbikaji wa ngonjera hizi huibua maudhui yanayonata akilini mwa wasikilizaji, kwa mfano “Ngonjera ni Kitu Gani?” (uk. 5-6) ina maudhui ya maana ya ngonjera. Ngonjera hii inapoimbika huwafanya watu washike haraka maana ya ngonjera na kukumbuka kwa urahisi zaidi kuliko isipoimbwa. Kwa ujumla ngonjera zote zinainbika kwa kuwa zimetungwa kwa urari wa vina na mizani hivyo ngonjera zote zilizomo kwenye *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, zina mbinu ya nyimbo. Ngonjera hizo zimetumika kuibua dhamira ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na ujenzi wa jamii mpya.

Mswada wa *Mahadhi ya Kiswahili* unahusu nyimbo za aina mabalimbali. Mnyampala (1967) katika dibaji yake anaeleza kuwa mahadhi ya nyimbo ni moja ya utamaduni maarufu wa taifa la Tanzania; mahadhi ni namna mbalimbali za uimbaji wa nyimbo tamu. Hivyo mbinu hii ya nyimbo imesawiriwa vyema katika mswada huu. Katika mswada huu nyimbo nyingi hazina majina na wala maelezo yanayojitosheleza. Mswada huu una nyimbo zinazohusu kuposa mchumba na hata kufikia kuo (uk. 1). Wimbo huo unaitwa “Habari ya Kutazamia Nyumba” ambao unahusu maudhui ya uchumba na ndoa, uzazi, mapenzi na ukarimu kwa mwenza na kuombeana mema kwa Mungu. Pia kuna nyimbo za arusi zinazohusu bwana arusi anapochoka na kutaka kulala. Wimbo huo upo (uk.2) kama tuonavyo hapa:

127. “Nina usingizi wanienga mato,  
Kanitandikie kitanda na mto,  
Tusowere macho cha feruzi kito.



Katika wimbo huo una dhamira ya mapenzi na ndoa. Aidha, mke baada ya kubeba mimba na kupata mtoto, mwandishi anaeleza kuwa Waswahili huwa na wimbo wa mawaidha kwa mtoto wakati wa kumtoa nje. Wimbo huo ni kama ufuatao:

128. Lifaalo kueleza lieleze,  
Lisilofaa lazima ulimeze,  
Kusudi kwa watu lisiwachukize. (uk. 2)

Wimbo huu unatoa mafunzo kwa mtoto na hata kwa jamii kuwa waangalifu na maneno yatolewayo mbele za watu. Kila utakalo kulisema mbele ya watu ni lazima ulichunguze kwanza. Hapa tunajifunza kuwa ni vizuri kuongea maneno yenye ujumbe na mafunzo mazuri kwa jamii. Vilevile, kuna nyimbo za kubembeleza mtoto akiwa analia ili mtoto aweze kutulia, ni wimbo unaoimbwa na mama wa mtoto ama mlezi wa mtoto. Mfano wa wimbo huu ni:

129. “Mwana nionee uchungu,  
Ni peke yangu na Mungu,  
Mimi naye mkunga wangu,  
Usilielie mtoto.”

Silie mama silie,  
Ukalia waniliza,  
Wanikumbusha makiwa,  
Makiwa ya baba na mama,  
Baba na mama watende,  
Wanioza dumu kongwe,  
Halisafiri halendi,  
Kazi kumega matonge. (uk.2)

Wimbo wa kubembelezea mtoto ulionukuliwa hapo juu unaibua maudhui mbalimbali yahusuyo jamii. Wimbo umetumika kuibua dhamira ya dini, mila na desturi ya kumtafutia mwanamke mchumba na kumwozesha kwa nguvu bila ya ridhaa yake. Hivyo wimbo huu umeweza kuibua hisia mbalimbali alizonazo mwanamke akieleza jamii kuhusu haki ya mwanamke katika kuchagua mwenzi wa kuishi naye. Katika ukurasa huo wa pili kuna wimbo wa watoto unaombembeleza mtoto alale. Wimbo

huo una mistari saba katika ubeti wa kwanza na wa saba, ubeti wa pili, tano, sita, kumi, kumi na moja, kumi na nne na kumi na tano zina mistari minne, ubeti wa tatu, nne, tisa, kumi na tatu zina mistari mitano na ubeti wa nane na wa kumi na mbili, zina mistari sita. Hivyo kutokana na nyimbo hizi tunatambua kuwa wimbo si lazima kuwa na mistari mitatu, bali wimbo huweza kuwa na mistari zaidi ya mitatu (Mulokozi, 2017). Nyimbo hizo zimezungumzia masuala ya uzazi na malezi kwa mtoto pamoja na umuhimu wa dini. Mfano ubeti wa pili unasema:

130. Mama aliponizaa, kanita mwanangu kua,  
 Umati wa Muhamadi, hapana asiyejua,  
 Asoweza kuniumba, hawezi kuniumbua  
 Ooooh - mtoto- Ooooh mtoto (uk. 2)

Hapo mwimbaji anatoa ujumbe kuwa kinachoumbwa na Mungu hakuna ambaye anaweza kukikosoa kwa kuwa haiwezekani kukibadilisha. Hivyo hapa anasisitiza kuwa uumbaji wa Mungu kwa binadamu hauna makosa, endapo umeumbwa una haki zote za kuishi na kuheshimiwa na jamii. Kama tulivyosema hapo juu nyimbo hizi za kubembeleza hubeba hisia na mafunzo ya mama juu ya ndoa yake na hata kwa jamii inayomzunguka. Pia kuna nyimbo zinazohusu masuala ya kifo na mapenzi (uk. 4).

Kadhalika, kuna nyimbo zinazoimbwa na watoto wadogo. Nyimbo hizo mara nyingi zinahusu michezo yao na maudhui yake mara nyingi huwa ya kitoto. Michezo hiyo huhusisha watoto wa kike na wa kiume kwa pamoja, na mara nyingine hushikana mikono kuonyesha umoja na mshikamao baina yao. Hata hivyo katika mswada huu kuna nyimbo za bembea, Mnara wa njia na Kibuzi (uk. 4). Katika nyimbo hizo kuna dhamira ya upendo, ubunifu na umoja miongoni mwa watoto. Hivyo, nyimbo hizo huwasaidia watoto kuwa na umoja, ubunifu, na upendo baina yao. Nyimbo nyingine za watoto zina mafunzo yanayohusu maisha. Mfano katika wimbo wa Kibuzi ubeti wa pili (uk. 5):

131. Simba kalogea, kalogea kongwe,  
Kongwe la mwana mzee, tate haligonile,  
Ligona kwa mke mbuya, na matikiti na matango,  
Jumla kumi na mbili.

Ubeti huu unahusu usaliti wa wanandoa hususani mwanamume kwenda kulala na mwanamke mwingine na kumpatia vitu. Ujumbe unaotolewa hapa ni kwamba usaliti katika ndoa husababisha uvunjifu wa amani katika ndoa na pengine kuchangia kuvunjika kwa ndoa. Pia kuna wimbo mwingine wa watoto uitwao Kinyuri, nao ni wa kuwafurahisha watoto na kuwapa burudani wachezapo.

Katika kitabu hiki pia kuna nyimbo za jando. Nyimbo hizi zimejitokeza katika beti nne na kwa muundo wa tenzi. Wimbo huu una beti zenye mistari miwili, mitatu na mitano. Wimbo huu wa jando (uk. 5) una dhamira zinazohusu maisha kama vile kazi za shamba ama kilimo. Pia wimbo huo umetumika kutoa mafunzo ya maisha kwa vijana. Ubeti wa pili unaeleza kuwa:

132. Nenda na mwanu, shamba kulima,  
Shamba kulima? Namba tashinda. (uk. 5)

Katika dondoo hilo mwimbaji anawahamasisha vijana walioenda jandoni kufanya kazi za shambani kwa bidii ili kufanikiwa katika maisha yao. Aidha, nyimbo hizi za jando zina dhamira zinazohusu ujasiri kwa vijana, kumtegemea Mungu, kutotenda maovu, ndoa na kulipa mahari, upendo kwa watu wote, mapenzi na mahusiano mema ndani ya ndoa.

Kadhalika, kuna nyimbo za mapenzi na wivu katika mahusiano ya kimapenzi. Ubeti wa pili na wa sita, unasema:

133. Kijaluba changu kimenipotea,  
Na nyumbani mwako sina mazoea,  
Ukilia wivu utanikondea. (ubeti wa pili, uk. 6)

Chura mbumbavu alinda kisima,  
Kajiweka kando na amesimama,  
Yanatekwa maji yeye kaasama. (ubeti wa sita, uk. 6)

Beti hizo mbili na zinginezo ndani ya wimbo huu zinaeleza kuhusu usaliti wa mapenzi unavyouma na kuleta wivu. Katika wimbo huo pia kuna maudhui yanayohusu migonganao baina ya wapenzi, majuto kutokana na matatizo yatokanayo na usaliti wa mapenzi, uchonganishi baina ya wapenzi na mawaidha mengineyo yahasuyo mapenzi.

Nyimbo nyingine ni zile zilizokusanywa na Mnyampala mwaka 1943-1953 alipokuwa fundi wa kutribu wa vinanda – Tashkota na Harmonia, nyingine alitunga mwenyewe, nyingine zilitungwa na Mbabe Athumani na wengine (uk. 10-14). Nyimbo hizo zinahusu mawaidha ya mapenzi baina ya wanandoa kuanzia kutafuta mwenzi hadi kuoana. Katika nyimbo hizo, waandishi wanaeleza masuala ya kuachana baina ya wanandoa na majuto yanayotokana na kosa hilo. Vilevile kuna dhamira inayohusu mwanamke mwenye tabia mbaya ambaye ni mlaghai wa mapenzi, na upande mwingine waandishi hawa wamezungumzia mapenzi ya dhati. Isitoshe, kuna dhamira ya dini ambapo mwimbaji anamwomba Mungu awape mapenzi ya dhati yeye na mwenzi wake (uk. 12):

134. Ya Illahi muweke mpenzi wangu,  
Na mahaba yajaze kwake na kwangu,  
Tuwe sawa tuwaudhi walimwengu.

Hapa mwimbaji anazungumzia mapenzi ya dhati kwa wanandoa ama wapenzi wanaotaka kuoana. Mtunzi anasisitiza wanandoa au wapenzi wawe na upendo wa kweli. Watu wakipendana mara nyingi walimwengu huwaonea wivu na chuki. Kutokana na hali hiyo, mwimbaji anamsihi mpenzi wake, wawe na mapenzi ya dhati ili ulimwengu uchukie wakati wao wakiwa na furaha. Mashairi ama nyimbo hizi

zimezungumzia dhamira ya mapenzi, ndoa, umalaya, usaliti. Ujumbe anaotoa ni kuwa, unafiki katika mapenzi si kitu kizuri na huweza kusababisha baadhi yao kupata matatizo na hata kupoteza maisha.

Mbinu ya nyimbo pia imetumika katika *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*. Mnyampala aliandika “Ni Waadhi Ushairi” (uk. 13) na “Johari ya Tanganyika” (uk. 25). Mashairi haya yanaimbika. Shairi la “Ni Waadhi Ushairi” linahusu dhamira ya upendo, dini na maadili ya utunzi wa mashairi. Na shairi la “Johari ya Tanganyika” lina dhamira zinazohusu lugha ya taifa ambayo ni Kiswahili, kukuza lugha ya Kiswahili, kuwaombea washairi baraka ili waendeleo kukuza lugha ya taifa na kusesitiza matumizi ya sheria za kutunga mashairi. Pia katika shairi hili mwandishi anawasifu watunzi wa Tanganyika, Zanzibar na Pwani ya Kenya na wengineo kwa kutumia lugha ya Kiswahili katika utungaji wa mashairi yao. Amezungumzia pia dhamira ya dini.

Mnyampala ametumia mbinu ya nyimbo katika mswada wa *Hazina ya Washairi na Mashairi ya Vidato*. Mashairi ya kimapokeo yana matumizi ya vina na mizani na mashairi yaliyomo katika miswada hiyo yameandikwa kwa mtindo wa kimapokeo. Mbinu ya nyimbo imetumika pia katika mswada hiyo kuibua maudhui mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa upande wa *Hazina ya Washairi* kuna shairi moja tu lililoandikwa na Mnyampala na limekwisha kujadiliwa katika mbinu nyingine. Vilevile katika *Mashairi ya Vidato* maudhui yaliyomo yamejadiliwa pia katika mbinu nyingine katika sura hii, hivyo tukijadili hapa shairi mojamoya tutakuwa tunafanya urudiaji. Kwa hiyo tunachoweza kusema hapa ni kwamba mtindo wa nyimbo umejitokeza pia katika miswada hii na mbinu hiyo imeibua maudhui yanayogusa nyanja zote za kisiasa, kijamii, kiutamaduni na kiuchumi.

Kutokana na mjadala hapo juu, tumebaini kuwa mbinu ya nyimbo imetumika katika kutolea ujumbe na dhamira mbalimbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi kama vile mapenzi na ndoa, malezi, dini, umoja, siasa, elimu, kazi, unyonyaji, ushirikiano na ujasiri. Kadhalika mbinu hii imedhihirika zaidi katika mswada wa *Mahadhi ya Kiswahili* kuliko diwani nyingine, kwa kuwa mswada huo unahusu nyimbo. Nyimbo zimetumika kimwingilianomatini, mtunzi mmoja amehusiana na mtunzi mwingine licha ya kuwa na tamaduni tofauti. Hii inamaanisha kuwa hakuna kitu kipya, kila kitu hutegemeana na kuhusiana kwa watunzi na mambo yaliyopo katika jamii.

#### **4.2 Hitimisho**

Sura hii imejadili na kuchambua data kutokana na kazi teule za Mnyampala kwa kuzingatia lengo la pili pamoja na swali la pili la utafiti. Lengo hili lilihusu kuhakiki mbinu za kifani zilivyotumika kuibua maudhui katika kazi teule za ushairi wa Mathias Mnyampala. Katika kufanya hivyo, sura hii imeshughulikia mambo mawili kwa pamoja, yaani tumezungumzia fani na maudhui (dhamira na ujumbe) kwa pamoja, kwa kuwa hushirikiana, hukamilishana na hutegemeana katika kazi za fasihi. Hivyo maudhui hutegemea mbinu za kifani na fani hutegemea maudhui yanayokusudiwa kutolewa katika kazi ya fasihi husika. Kwa ujumla tumebaini kuwa Mnyampala ni mwandishi mahiri aliyetumia mbinu za kifani katika kuibua maudhui mbalimbali yahasuyo nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mnyampala ametumia mbinu anuwai zenye ubunifu wa kiwango cha juu katika uwasilishaji wa maudhui yake ndani ya kazi husika. Suala la mwingilianomatini limejitokeza vyema katika mbinu zake hasa namna alivyotumia matini simulizi na za tamaduni za kisasa na zilivyoingiliana na kukamilishana katika mashairi yake. Kadhalika kuna mwingilianomatini wa kazi zake na waandishi wengine waliotangulia

na mwingilianomatini wa kazi zake mwenyewe. Pia, kuna mwingilianomatini wa kazi zake na vitabu vitakatifu mfano *Biblia Takatifu* na *Kurani Tukufu*. Kwa ujumla katika kazi za kishairi za Mnyampala tumebaini kwamba mbinu za kifani na maudhui yanayoibuliwa yamefungamana na muktadha wa jamii za Kiafrika. Mwingiliano huo umesababisha kuibua maudhui yaliyokusudiwa kwa jamii na taifa lake. Sura ya tano inashughulikia mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

## SURA YA TANO

### MCHANGO WA MATHIAS MNYAMPALA KATIKA MAENDELEO YA

### USHAIRI WA KISWAHILI

#### 5.0 Utangulizi

Sura hii imejikita katika kushughulikia lengo la tatu la utafiti huu, ambalo ni mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Katika kutathmini mchango wa Mnyampala tumezingatia vipengele mahususi vya fani katika ushairi wa Kiswahili ambavyo ni mtindo, muundo na matumizi ya lugha. Kadhalika tumeangazia mchango wake katika ukusanyaji wa mashairi ya waandishi mbalimbali, kukuza nadharia ya ushairi wa Kiswahili na kuingiza maudhui ya kidini katika ushairi wa Kiswahili.

#### 5.1 Mtindo

Mtindo katika ushairi wa Kiswahili umefafanuliwa na watafiti mbalimbali. Baadhi ya watafiti hao ni Mulokozi (1996), Njogu na Chimera (1999), Wamitila (2004) na Samwel na wenzake (2013). Mulokozi (2017) na Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa mtindo wa mashairi hujidhihirisha katika matumizi yake ya lugha, kama vile uteuzi na upangaji wa maneno, mpangilio wa sauti za lugha ili kuleta athari fulani, matumizi ya tamathali za semi kama vile tashbiha, sitiari, mafumbo tasfida na nyinginezo. Naye Wamitila (2004) anaeleza kuwa mtindo ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji ama wasikilizaji wa kazi husika. Kwa upande wa Samwel na wenzake (2013) mtindo ni upangaji wa fani na maudhui kwa namna ambayo inampambanua mashairi mmoja na mwingine. Wanaongezea kuwa mtindo huchunguza endapo shairi ni la tathlitha, tarbia, takhmisa, sudusia na mitindo mingineyo.



Samwel na wenzake wanafafanua zaidi kuwa mtindo huhusisha maneno aliyoteua mtunzi endapo ni magumu au rahisi, kama ni ya kilahaja au yanatumia lahaja sanifu ama endapo lugha inayotumika ni fasaha na sanifu au ya mtaani. Pia, mtindo unaangalia matumizi ya lugha ya picha, ishara na taswira. Kutokana na mawazo ya Mulokozi (1996), Njogu na Chimerah (1999), Wamitila (2004) na Samwel na wenzake (2013), tunaweza kusema kuwa mtindo ni ufundi anaotumia mwandishi katika kuiumba kazi yake ili iweze kueleweka na walengwa wa kazi hiyo. Hivyo basi, mtindo hujumuisha mbinu za kiuandishi, matumizi ya lugha, tamathali za semi na mbinu nyingine za uandishi. Aidha, mtindo huu huingiliana na kukamilishana na washairi watangulizi. Kama asemavyo Eliot (1988) kuwa mshairi anaendeleza uhusiano wa washairi kwa kuchukua mbinu ama matini mbalimbali kutoka kwa washairi tangulizi na kuziumba upya kulingana na vionjo vya wakati uliopo. Kwa ujumla, Mnyampala kama mmoja wa waandishi wa kazi za fasihi, hususani katika ushairi wa Kiswahili, hakuwa nyuma katika kukikabili na kukimudu kipengele hiki cha mtindo katika kazi zake za ushairi. Katika kipengele hiki cha mtindo, mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili umejitokeza kama ifuatavyo:

### **5.1.1 Mtindo wa Mtiririko**

Mnyampala alibuni mitindo mbalimbali ya uandishi wa ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu umebaini kuwa Mnyampala ni mwasisi wa mtindo wa mtiririko. Mbinu hii hubainisha mashairi ambayo vina vyote vya kati vya mistari mitatu ya kila ubeti hufanana kutoka mwanzo hadi mwisho na vile vya mwisho vya mistari mitatu ya mwanzo navyo hufanana kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Na katika kibwagizo hubadilishana vina<sup>44</sup>. Madumulla (2011) anaeleza kuwa Mnyampala ndiye aliyeanzisha mtindo wa mtiririko na msisitizo. Naye Charles Mnyampala (2014)

---

<sup>44</sup>Mfano wa mashairi ya mtindo huu wa mtiririko umeambatishwa kwenye tasnifu hii.

anaeleza kuwa mtindo wa mtiririko humtaka mshairi ambaye ni tajiri wa msamiati wa Kiswahili asitindikiwe na urari wa vina. Katika *Diwani ya Mnyampala* alitunga shairi lenye kichwa “Tungeni Mtiririko” (uk. 5), anasema:

135. Mhariri mahabubu, pokea wangu mwandiko,  
Napenda kuwa hotubu, washairi walioko,  
Si kama nawaghilibu, na kujitia vituko,  
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Katika shairi hili mwandishi alikuwa anahimiza watunzi wenzake watunge kwa kutumia mtindo wa mtiririko. Katika ushairi huu toka ubeti wa kwanza hadi mwisho, vina vya katikati ni “bu” na vina vya mwisho ni “ko” lakini katika kibwagizo kina cha mwisho kimekuja kati na cha kati kimeenda mwisho. Hivyo katika kibwagizo kina cha kati ni “ko” na mwisho ni “bu.” Kwa kawaida utunzi wa namna hii unahitaji mtu ambaye ni mbobevu katika lugha, vinginevyo kutakuwa na utungaji wa kikasuku ambapo vina vya ushairi kuibua wazo badala ya wazo kuibua vina. Mnyampala anasisitiza kwamba washairi wenzake watumie mtindo huu ili waibue msamiati mbalimbali unaoweza kutumika kukuza Kiswahili.

Mbinu hii imejitokeza katika mashairi mbalimbali yaliyomo katika diwani hiyo. Baadhi ya mashairi hayo ni “Hima Hima Islamu” (uk. 6), “Mali Pepo Dunia” ( uk. 7), “Fadhili Zao Tulipe”(uk. 7), “Heri Mwenye Sura Mbaya” (uk.8), “Wastara Hazumbuki” (uk. 9), “Urafiki Tufanane” (uk. 11) na “Simbiko Haisimbiki” (uk. 13). Mbinu hii ya kiuandishi imejitokeza pia katika baadhi ya beti zilizomo katika mswada wa *Mashairi ya Vidato*. Mfano katika shairi la Saba-Saba, ubeti wa pili unasema:

136. Sabasaba yetu saba, saba ya kila Julai,  
Saba kwa Tanu ni Baba, Baba apigiwe Nai,  
Lazima ije jadhira, jadhira iso kinai,  
Saba ya saba tumai, tumai la sabasaba. (uk. 3)

Katika dondoo hilo vina vya katikati ni “ba” na vina vya mwisho ni “i” lakini katika kibwagizo kina cha mwisho kimekuja kati (i) na cha kati kimeenda mwisho (ba). Vilevile, mbinu hii imejitokeza pia katika shairi la “Kitung’ati” (uk. 7), ambapo mishororo mitatu ya mwanzo katika ubeti wa pili kina cha kati ni “ti” na kina cha mwisho ni “zi.” Katika mshororo wa mwisho kina cha mwisho kimekuja kati “zi” na cha kati kimeenda mwisho “ti.”

Mbinu hii pia imejitokeza katika *Waadhi wa Ushairi* katika shairi la “Mtambuzi” (uk. 20) na “Chambo” (uk. 32). Aidha, mtindo huu bado unatumiwa na baadhi ya waandishi wa ushairi wa Kiswahili katika karne ya 21, mfano mzuri ni mashairi ya Asha S. K. Kunemah (2008). Baadhi ya mashairi yake yanatumia mbinu hii katika utangulizi wake (rejea kitabu chake cha *Misemo na Methali katika Ushairi*, uk. 1, ubeti wa pili na 3 na uk. 45). Hivyo inaonyesha kuwa hadi sasa mtindo huu bado unatumiwa na baadhi ya watunzi ambao wanatunga kazi zao kwa kutumia mtindo wa kimapokeo. Katika kipindi cha mgogoro wa ushairi, istilahi ya mtiririko ilitumiwa kurejelea mashairi huru ama mashairi ya kisasa. Aidha, mtiririko uliokuwa katika mashairi ya Mnyampala ni tofauti na mtiririko unaozungumziwa katika mgogoro wa ushairi. Mulokozi na Kahigi (1979:15) wanaeleza kuwa katika mgogoro wa ushairi ilitokea rai kuwa mashairi “mapya” ya mtiririko ni mashairi guni. Kwa mujibu wa wanamapokeo ni mashairi yasiyofuata kanuni za kimapokeo yaani urari wa vina na mizani (Abedi, 1954, Topan, 1974, Chiraghdin, 1970 na Mayoka, 1977).

### **5.1.2 Mtindo wa Msisitizo**

Mtindo mwingine ambao uliibuliwa na Mnyampala ni mashairi ya msisitizo. Huu ni mtindo wa utunzi ambao aliuanzia miaka ya 1960 na kuutumia kwa mara ya kwanza katika *Diwani ya Mnyampala* na *Waadhi wa Ushairi* zilizoandikwa mwaka

1965. Katika mtindo huu kila ubeti ulikuwa na kipande cha kusesitiza maudhui yaliyotengwa katika ubeti huo<sup>45</sup>. Mbinu hii ilitumiwa katika *Diwani ya Mnyampala* (uk. 121-130). Mfano shairi la “Natunga Msisitizo” (uk. 121) ubeti wa kwanza unasema hivi:

137. Nawapangia maneno, ya sifa na walekezo,  
Na kuzitoa mifano, zinase nyoyo mawazo,  
Usemi wa sisitizo;  
Sisitizo mlingano, usioleta mivizo,  
Maagizo yawe **manono**, nayatilia mkazo,  
Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Dondoo hilo linadhihirisha kuwa ubeti huu ulikuwa na mistari mitano na nusu. Kipande cha mstari kwa kila ubeti kilitumika kusesitiza maudhui ya ubeti husika. Mfano katika ubeti huo maudhui kuhusu mtindo wa msisitizo yanapatikana katika kipande kisemacho ‘usemi wa sisitizo.’ Vilevile, Mnyampala alitumia mtindo huu katika *Waadhi wa Ushairi*, katika shairi la “Mambo Yanazidiana” (uk. 77). Licha ya mtindo huu kuwa mpya lakini ulifuata kaida za wanamapokeo ambazo ni matumizi ya urari wa vina na mizani kama uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili. Kwa kufanya hivyo kuna dhana ya mwingilianomatini imesawiriwa kupitia mtindo huu. Mtindo mpya umechukua baadhi ya kaida zilizopo katika ushairi na kuzitumia kuibua mtindo mpya, hivyo huu ni mwingilianomatini unaojitokeza katika kazi za fasihi. Matini zote zilizoandikwa na kusimuliwa hurejelea matini nyingine na matini yenye mingiliano matini huwa na tabia zenye sifa zinazovuka mipaka yake (Wolfreys, 2004). Kwa kawaida mwandishi wa matini ni msomaji wa matini nyingine. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa kazi zake zimebeba athari za kila aina ambazo huweza kuibua mtindo mpya.

---

<sup>45</sup> Maelezo haya nimeyatoa katika dibaji ya *Maisha ni Kugharimia* iliyoandikwa na Charles Mnyampala (mtoto wa Mathias Mnyampala). Kadhalika mfano wa mtindo wa mashairi haya umeambatishwa kwenye tasnifu hii.

Mtindo wa msisitizo kwa bahati mbaya haukupata kuenea na kutumiwa na watunzi wengine. Huenda haukuenea kwa kuwa watunzi na waimbaji wengi wa mashairi ya Kiswahili kwa wakati huo walikuwa wamezoea mtindo uliokuwepo wa mashairi ya kimapokeo yenye mistari minne (tarbia). Pia mtindo huu unahitaji mtu ambaye ni mahiri katika uteuzi wa maneno na mwenye ubunifu wa kiwango cha juu katika sanaa ya ushairi wa Kiswahili. Isitoshe kutotumika kwa mtindo huu huenda kumesababishwa na kukosekana kwa utafiti wa kina wa Mathias Mnyampala na kusababisha kutofahamika kwa mtindo huo kwa waandishi chipukizi. Hivyo, kupitia utafiti huu mtindo huu unaweza kupata watumiaji katika utunzi wa kazi za ushairi.

Kwa ujumla, mtindo huu ni muafaka na unafaa kutumika katika ushairi wa Kiswahili. Mtindo huu unaleta mvuto katika sanaa ya ushairi na kumfanya msomaji kuwa na hamu ya kujua maudhui yaliyokuwemo katika ushairi husika. Kadhalika mtindo huu ulisaidia kuleta upya katika sanaa ya ushairi wa Kiswahili. Mtindo huu licha ya kuasiliwa kwa ulifuata urari wa vina na mizani kwa namna fulani ulileta mabadiliko katika umbo la sanaa ya ushairi kwa kuwa umbo lililokuwa limezoeleka wakati huo ilikuwa ni la ubeti wenye mistari minne au mitano. Kama asemavyo Eliot (1988) kuwa mshairi huathiriwa na watunzi wengine kiutunzi na kuibuka na kitu kipya ambacho kinatosheleza wakati huo. Hivyo, Mnyampala aliibuka na umbo lenye mistari mitano na nusu. Hii inaonyesha kuwa Mnyampala alikuwa mbunifu alipenda mabadiliko katika sanaa ya ushairi wa Kiswahili.

### **5.1.3 Mtindo wa Majibizano**

Mnyampala alifufua mtindo wa majibizano baina ya wahusika wawili au zaidi katika mashairi yajulikanao kama ngonjera. Mmbaga (2004) anaeleza kuwa ngonjera zimetungwa kwa kutumia mtindo wa tarbia ambao kihistoria ulikuwepo nyakati za

Muyaka katika karne ya 18, kabla hata ya Mnyampala kuanza kuzitunga. Ngonjera zilikuwepo tangu mwanzo lakini ngonjera hizo hazikuwa na sura ama mtindo huu tunaouona katika ngonjera za Mnyampala ambazo zinapatikana katika vitabu vyake *Ngonjera za UKUTA Na. 1 na 2* (Mmbaga, 2004 na Mulokozi, 2017). Mulokozi (2017) anaeleza kuwa kabla ya Mnyampala, ulikuwepo ushairi wa majibizano, lakini ushairi huo haukuwa wa maigizo kwa namna ya kingonjera, bali ulikuwa unatambwa tu kwa kujibizana kati ya wahusika au watu wawili au pande mbili zenye kushindana mfano katika ngoma na shughuli za arusi. Anafafanua zaidi kuwa wahusika waliokuwa wanajibizana walikuwa wanajitungia maneno yao wenyewe, walikuwa hawapokezani kama shairi au wimbo uleule na majibizano hayo yalikuwapo na bado yapo Ugogoni, Uswahilini na katika makabila mengineyo.

Hivyo kutokana na maelezo ya Mulokozi ni dhahiri kuwa Mnyampala aliathiriwa na fasihi simulizi ya kabila lake la Kigogo. Hivyo alichukua majibizano yaliyokuwepo katika fasihi simulizi ya kabila lake na ubunifu alioupata kutoka katika maandishi ya watu wengine na kuunda ushairi wa majibizano (ngonjera) wenye kuigizika. Hapa mwingilianomatini baina ya fasihi simulizi za kijadi, watunzi tangulizi na ngonjera hizo unaojitokeza bayana. Kama afafanuavyo Bakhtin (1981) kuwa Mwingilianomatini hurejelea namna matini au kazi za fasihi huhusiana na kazi nyingine zilizotangulia kwa kiasi kikubwa. Kazi teule za Mnyampala zina majibizano ya aina mbili; majibizano ya papo kwa papo ndani ya shairi moja na majibizano kati ya mshairi mmoja na mshairi mwingine. Mfano wa majibizano ya papo kwa hapo yapo katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1 na 2*.

Majibizano ya mshairi na mshairi yanapatikana pia katika *Diwani ya Mnyampala* (uk. 17-18), majibizano hayo ni baina ya Mnyampala na Snow White. Kadhalika,

majibizano yamejitokeza katika mswada wa *Hazina ya Washairi* ambapo kuna majibizano ya aina mbili yaani mshairi na mshairi (mshairi mmoja anaanzisha mada wengine wanajibu kwa kuunga au kupinga). Vilevile majibizano ya papo kwa hapo yamejitokeza baina ya wahusika wawili (rejea shairi la “Mgonjwa na Daktari” uk. 5 lililoandikwa na Bwana Kihere).

Majibizano yaliyotumika katika shairi la Kihere ni tofauti na yale yaliyomo katika ngonjera za Mnyampala kitabu cha *Ngonjera za UKUTA Na. 1*. Majibizano baina ya Mgonjwa na Daktari hayakutaka kufikia mwafaka bali ni mjadala ambao mgonjwa hakutaka kurekebishwa kwa kile alichokiamini. Majibizano haya ni tofauti na majibizano yaliyo katika kitabu cha *Ngonjera za UKUTA Na. 1* ambapo mmoja anakuwa hajui na mwingine anamwelimisha na mwisho wanafikia suluhu ya kuelewana.

Utafiti huu umegundua kuwa Mnyampala ndiye aliyefufua na kuendeleza kwa kuweka mtindo huu kibunifu zaidi kiasi cha kuwafanya watafiti na wahakiki wengine kama vile Komba (1969) na Mwangomango (1971) wahisi kwamba ndiye aliyeanzisha ngonjera. Mnyampala aliweza kuchukua mtindo uliokuwepo na kuuboresha zaidi kulingana na muktadha wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea uliokuwepo wakati huo. Hivyo mchango wake ni kuyafanya mashairi ya majibizano yawe ya kimaigizo pamoja na kuyatafutia mashairi hayo kisawe chake (yaani akayapa jina la ngonjera). Ngonjera ni neno la asili ya Kigogo lenye maana kwenda pamoja, ni mashairi yaliyovuma sana wakati wa siasa za Ujamaa na yalianzishwa kwa lengo la kueneza siasa ya Ujamaa. Katika kipindi hiki watu walitakiwa kuishi pamoja na kwa ushirikiano katika vijiji vya ujamaa ili waweze kujenga nchi na kufaidi matunda yake kwa pamoja. Majibizano yaliyokuwemo katika ngonjera hizo kwa kiasi kikubwa

yamejengwa katika mfumo wa maswali na majibu. Mfano mzuri ni *Ngonjera za UKUTA Na. 1* ngonjera ya “Utukufu wa Taifa” (uk. 12) inayosema:

138. **Raia**

Bwana ninayo mashaka, makubwa yananitiza  
Nami sinayo hakika, lipi la kutanguliza  
Jambo ninalolitaka, ni ninyi kunieleza  
Lipi la kutanguliza, kwa taifa kulifanya?

**Mwanasiasa**

Maswali nimepulika, hayo uliyoniuliza  
Kauli hajatamka, mbinu zake kueleza  
Ni yapi unayotaka, pengine kutanguliza  
Fumbua na kufumbuza, kwa taifa kulifanya

Kupitia majibizano hayo, Raia anamuuliza swali Mwanasiasa na Mwanasiasa anajibu. Katika majibizano hayo mwanasiasa ndiye aliyepewa hadhi ya juu. Hapa inaonyesha kuwa mwanasiasa ndiye anajua kila kitu na ndiye wa kuelimisha jamii. Wahusika hao wanaendelea na majibizano na mwishowe Raia anaonekana kuelewa maana ya kitu kinachozungumzwa. Raia alikuwa anaelezwa kuhusu na utukufu wa taifa. Mwanasiasa anasisitiza kuwa kitu cha kutanguliza mbele ni kulijenga taifa na kuondokana na ukabila na udini na kutanguliza maslahi ya taifa. Utanzu huu wa ngonjera ulifufuliwa kwa kufanywa upya zaidi kimwingilianomatini na kutumiwa sana wakati wa siasa za Ujamaa na Kujitegemea. Hivyo, watunzi wengi walihusisha ngonjera na masuala ya siasa yaliyokuwa yakiendelea nchini Tanzania katika kipindi hicho.

Utanzu huu ulitumiwa na baadhi ya watunzi wa mashairi waliotunga mashairi yao miaka ya 1970. Mfano Kezilahabi (1974) katika diwani ya *Kichomi* (rejea uk. 51-58). Kezilahabi aliutumia mtindo huo kwa kutumia mashairi ya kisasa yasiyozingatia kanuni za ushairi wa kimapokeo. Hata hivyo utanzu huu bado unatumika na wanafunzi wa shule za msingi (awali) na sekondari (upili) nchini Tanzania.



Kadhalika, mtindo wa majibizano unaendelea kutumiwa na washairi wa kimapokeo na kisasa wa karne ya 21 kama vile Kunemah (2008) katika diwani yake ya *Misemo na Methali katika Ushairi* (uk. 1). Majibizano yaliyotumika ni sawa na yale aliyokuwa anatumia Mnyampala katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*.

Kithaka wa Mberia naye anatumia majibizano katika diwani zake za ushairi, ijapokuwa Mberia hazingatii arudhi za ushairi wa kimapokeo (rejea Mberia katika diwani ya *Mchezo wa Karata* 1997, katika shairi la “Kiwambo cha Televisheni” uk. 37-39 na *Radio na Mwezi*, 2005:61-63). Hata hivyo, Kithaka wa Mberia akiwa mtaalamu wa drama ameandika mtindo huo kwa kuzingatia mabadiliko yanayojitokeza katika jamii kwa kuboresha zaidi na kuuweka zaidi katika drama. Mtindo huo ni wa kimwingilianomatini, kwamba kazi moja inahusiana na kazi nyingine tangulizi. Hii inatokana na ukweli kwamba hakuna kazi ya kifasihi inayoweza kusimama peke yake pasipo kutegemea kazi zingine, kwa kuwa matini za fasihi huhusiana na kukamilishana (Barthes, 1979).

Kutumika kwa mtindo wa majibizano katika kazi za kifasihi kunatokana na mwingiliano wa matini na mbinu mbalimbali za uandishi wa tanzu za fasihi. Kama asemavyo Senkoro (2011) kuwa mwingiliano tanzu ni mbinu ambayo huonyesha kutumiwa kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kutolea au kuwasilisha utanzu mwingine. Hivyo si jambo geni kuona utanzu wa fasihi simulizi ndani ya ushairi andishi. Hii ni kusema kuwa mbinu za utunzi zinaingiliana na kukamilishana. Sambamba na hilo, mbinu hii imekuwa na upya zaidi kutokana na mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa ujumla ngonjera zinatumiwa hadi katika karne tuliyonayo leo. Kwa mfano ngonjera mara nyingi zinatumiwa na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika maadhimisho ya sherehe mbalimbali nchini Tanzania. Istitoshe ngonjera hadi sasa bado zinaonyeshwa katika baadhi ya vyombo vya habari,

mfano katika Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) mchezo au onyesho la “Fataki la Wiki” kipindi kinachorushwa siku ya Jumatatu saa 9:30 jioni na kurudiwa siku ya Alhamisi saa 8:30 alasiri. Katika mchezo huo kuna mbinu ya ushairi-drama. Mchezo huo ni aina mojawapo ya ngonjera na unapendwa na watu wengi kwa kuwa watazamaji wengi hujifunza mambo mengi kuhusu maisha ya kila siku.

Murusuri (2011) anaeleza kuwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Shule ya Sanaa na Lugha walieleza kuwa “Fataki la Wiki” ni ngonjera zinazopendwa na watazamaji wengi wa kipindi hicho. Kazi hiyo ya kifasihi imebeba dhima kubwa ya kuelimisha, kuipa jamii mwelekeo, kutoa hamasa kwa jamii, kukosoa, kuwakumbusha watu wajibu wao katika jamii na kuburudisha jamii.

Kutokana na maelezo hayo, tunaweza kusema kuwa mbinu ya majibizano katika ushairi ni muhimu katika kuelimisha na kutolea mafunzo kwa jamii. Hivyo basi ni muhimu kwa jamii kutambua kuwa ngonjera hazikufufuliwa kwa ajili ya siasa tu bali huweza kutumiwa kuelezea nyanja mbalimbali za maisha iwe masuala ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na mengineyo yahasuyo maisha ya mwanadamu. Pia ngonjera ni muhimu na zinafaa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika.

#### **5.1.4 Mtindo wa Vidato**

Mtindo wa vidato ni ule ambao kuna kubadilishana kwa vina hatua kwa hatua ndani ya shairi moja. Katika mtindo huu vina vya mwisho vya mistari mitatu ya ubeti wa kwanza ndivyo vinakuwa vina vya kati vya mistari mitatu ya ubeti unaofuata na vina vya mwisho hutafutwa vingine. Hivyo ubeti unaofuata unategemea vina vya kati kutoka katika ubeti uliotangulia<sup>46</sup>. Mbinu hii inajidhihirisha vyema katika mswada wa

---

<sup>46</sup>Mfano wa mashairi ya mtindo wa vidato umeambatishwa kwenye tasnifu hii.

*Mashairi ya Vidato*. Mnyampala (1966) anaeleza kuwa mtindo huu wa vidato ni aina fulani ya mashairi makuu kama yale mengine yaliyowahi kusifiwa ulimwenguni humu katika lugha mbalimbali za ulimwenguni, kama vile mashairi ya akina Shakespeare wa Uingereza, Mahabharata na Hamayana wa Bara Hindi ya Kale, Illiad na Odyssey. Aidha, Mnyampala (1967) katika mswada wa *Hazina ya Washairi* anasema kuwa mtindo huu ulianzishwa katika mwaka wa 1966 na unafanana kidogo na ule uitwao “msisitizo” ambao unatokana na mawazo mazito na yenye hekima.

Naye Charles Mnyampala (2014) anaeleza kuwa Mnyampala ndiye aliyeanzisha mtindo wa mashairi ya vidato. Aidha, katika mahojiano yetu na Madumulla anafafanua kuwa mtindo wa mashairi ya vidato haukuanzishwa na Mnyampala bali aliundeleva kutoka kwa washairi waliotangulia kama vile Muyaka bin Haji ambaye aliishi kati ya mwaka 1776 na 1840 na wengineo<sup>47</sup>. Tumepitia *Diwani ya Muyaka* na kubaini kuwa ni kweli mtindo huo ulikuwepo tangu enzi za Muyaka bin Haji (Rejea *Diwani ya Muyaka* uk. 1 na shairi la “Umwongo” (uk. 92). Hivyo mtindo huu umetumiwa na Mnyampala katika kutunga mashairi yote yaliyomo katika mswada wa *Mashairi ya Vidato*. Mfano shairi la “Uaminifu” (uk. 1) ubeti wa pili na wa tatu unasema:

139. Simama kadamnasi, ubaya ujitakase,  
Ujitape ufarisi, wasikizi uwanase,  
Kama mtu Ibilisi, watu budi wakususe,  
Japo tusi usiguse, haja kubwa waminifu.

Mke mwema usikose, mtii mwenye hekima,  
Na amri afuase, akulee kama mama,  
Kama macho asepese, huko afanye dhuluma,  
Japo unatunzwa vema, haja kubwa waminifu.

---

<sup>47</sup> Maelezo haya yalitolewa na Profesa Joshua Madumulla katika Chuo Kikuu cha Iringa tarehe 14/10/2016.

Katika beti hizo vina vya mwisho ubeti wa pili vya mistari mitatu ya mwanzo ambavyo ni “se” vimekuwa vina vya kati vya ubeti wa tatu katika mistari mitatu ya mwanzo. Kadhalika ubeti wa nne, vina vya mwisho vya mistari mitatu ya mwanzo vya ubeti wa tatu “ma” ndivyo vimetumika kuwa vina vya kati vya ubeti wa nne. Hivyo kila ubeti unaofuata unachukua vina kutoka ubeti tangulizi. Katika mbinu hii ya vidato kuna mwingiliano wa vina kama tulivyoonyesha hapo juu. Kadhalika si mwingiliano wa vina tu pia kuna mwingiliano wa maudhui yaliyomo ndani ya shairi husika. Vilevile, kuna mwingiliano wa mbinu hiyo kutoka kwa watunzi watangulizi kama tulivyoeleza hapo awali.

Makaka (2012) anaeleza kuwa mnamo mwaka wa 1966 Mnyampala alikuwa mhadhiri wa muda mfupi wa fasihi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mojawapo ya kozi zilizofundishwa wakati huo ilikuwa ni Mashairi ya Kiswahili, ambapo walijifunza na kujadili mashairi ya Sayyid Abdala bin Ali Nassir, Muyaka bin Haji na ya Sheikh Amri Abedi<sup>48</sup>. Ni dhahiri kwamba Mnyampala aliyajua vizuri mashairi ya watangulizi wake kama ilivyoelezwa hapo awali, ufahamu wake ulimfanya afufue na kuendeleza mbinu hiyo na kuutafutia kisawe chake. Kwa upande mwingine inawezekana kwamba Mnyampala aliandika pasipo na kufahamu kuwa Muyaka naye alitumia mtindo huu. Hata hivyo Mnyampala alikuwa mdadisi na mtu ambaye alipenda kujifunza na kuona wengine wanafanyaje ili kuweza kuibua mitindo mipya ama kuiendeleza mitindo ambayo ilionekana ni mizuri lakini imeanza kutoweka katika jamii. Kwa kufanya hivyo, Mnyampala alijitahidi katika kuleta mabadiliko katika ushairi wa Kiswahili na kuyafanya mashairi yake kuwa na upekee wa namna yake.

Aidha, Mnyampala alijitahidi kutunga mashairi yake kwa kuteua maneno mazuri na yenye maana kulingana na ujumbe anaotaka kuwasilisha katika jamii. Pia alikuwa na

<sup>48</sup>Taarifa hizi pia tulizipata katika mahojiano na nyaraka zake zilizohifadhiwa nyumbani kwake. Baadhi ya nyaraka zinazothibitisha hilo tumeziambatanisha kwenye tasnifu hii.

ufanisi mkubwa wa kupanga vituo na vina vinavyowiana vizuri ili mashairi yake yakiimbwa yapendeze masikioni mwa wasikilizaji. Kwa ujumla Mnyampala alikuwa mshairi mwenye ujuzi wa lugha na mwenye kupenda mabadiliko katika ushairi wa Kiswahili. Hamu yake ni kutaka sanaa ya ushairi iendelee mbele, ndio maana alijitahidi kuibua mitindo mipya na kufufua mitindo mbalimbali katika utanzu huu.

Naye Williams (1974) anaeleza kuwa mtindo wa mashairi mengi ya Mnyampala ni wa kimapinduzi, unaobadilikabadilika na unaoleta mabadiliko makubwa katika ushairi wa Kiswahili kutokana na mashairi ya kimapokeo ya akina Akilimali na wenzake. Tunaweza kusema kuwa Mnyampala alithubutu kuleta mabadiliko katika ushairi wa Kiswahili kwa kubuni mitindo mipya ya uandishi na kufufua mitindo iliyoonekana kusahaulika kwa kuweka ubunifu zaidi na kuzifanya kama tungo mpya.

Kwa ujumla, Mnyampala ni mwandishi aliyependa mabadiliko katika ushairi wa Kiswahili japokuwa alikuwa mfuasi wa mashairi yanayozingatia arudhi ya ushairi wa kimapokeo wenye kuzingatia urari wa vina na mizani. Aidha, mbinu zake mpya za ushairi ziliufanya ushairi uonekane kama ni sanaa inayozingatia mabadiliko yanayotokea katika jamii. Bila shaka mtazamo huu wa Mnyampala ndio uliosababisha hata watunzi wengine kufikiria kuleta mabadiliko katika tasnia ya ushairi wa Kiswahili na fasihi kwa ujumla. Hivyo, kutokana na mabadiliko aliyochangia katika ushairi, Mnyampala ni mfano mzuri Nadharia ya Urasmi Mpya katika fasihi ya Kiswahili.

## **5.2 Muundo**

Dhana ya muundo imezungumziwa na watu mbalimbali. Miongoni mwa waliojadili muundo ni Mulokozi (2017) anayefafanua kuwa miundo ya ushairi wa Kiswahili ni mingi. Mulokozi anabainisha baadhi ya vipengele vinavyotumika zaidi katika muundo

wa ushairi kuwa ni mistari, beti, mizani na vina. Mashairi yana miundo mbalimbali kutegemea ufundi wa mshairi mwenyewe. Ijapokuwa katika muundo kuna muundo ndani na muundo nje lakini katika muundo wa shairi tunaangalia zaidi kile kinachoonekana kwa nje. Kwa mfano tunaangalia mgawo wa vipande, idadi ya mistari katika kila ubeti, kiitikio au mkarara au kibwagizo na idadi ya beti katika shairi (Nyangwine na Masebo, 2002; Njogu na Chimerah, 1999; Samwel na wenzake, 2013).

Mnyampala ametumia miundo mbalimbali katika uandishi wa kazi zake za ushairi. Mashairi yaliyotamalaki katika kazi zake ni ya muundo wa tarbia (mistari minne kila ubeti). Kadhalika yapo mashairi yenye ubeti mmoja tu (taz. *Waadhi wa Ushairi* uk. 1-6) na (uk. 7-11) na kuna mashairi yenye beti mbili (taz. *Waadhi wa Ushairi* uk. 7-11). Vilevile katika *Waadhi wa Ushairi* kuna mashairi yenye muundo wa beti tatu (uk. 11-16), na kuna mashairi yenye beti nne, tano, sita, saba, nane hadi beti kumi na mbili. Mashairi hayo ameyapanga kwa mpangilio akianza na yenye beti chache na kuelekea yenye beti nyingi. Pia muundo wa Mnyampala hubadilika badilika kwa mfano katika dibaji ya *Waadhi wa Ushairi* ametumia mashairi yenye mistari mitatu (tathilitha) (taz. uk. x-xi), mfano wa shairi mojawapo ni hili:

140. Chungu cha Johari kito, Kinivemeto na moyo!  
Shirabu yako ya mato, inisayo wayo wayo,  
Laiti nisiwe mto, hakinga matozi hayo? (uk. x-xi)

Mashairi mengi zaidi katika kazi zake ni yale yenye mistari minne. Vilevile, ushairi wa Mnyampala una muundo wa mashairi yenye mistari sita ama mitano na nusu, ambayo ameyaita mashairi ya msisitizo na yanapatikana katika *Waadhi wa Ushairi* na *Diwani ya Mnyampala*. Katika *Diwani ya Mnyampala*, mashairi haya yanapatikana kuanzia shairi la “Natunga Msisitizo” (uk. 121-130). Muundo huu wa msisitizo pia

umo katika *Waadhi wa Ushairi*, shairi la “Mambo Yanazidiana” (uk. 77-78). Kwa ujumla Mnyampala katika mashairi yake hayo ya tathlitha na tarbia huwa mistari yake imegawanyika katika vipande viwili ambavyo huwa na mizani kumi na sita, kila kipande huwa na mizani nane. Aidha, shairi la “Kifo cha Mama” na “Mawaidha” (uk. 78-79), ametumia muundo wa tenzi, ambao ubeti huwa na mistari minne yenye mizani nane kwa kila mstari. Shairi hilo la “Kifo cha Mama” (uk. 78) linaonekana hivi:

141. Kifo kwetu ni faradhi,  
Kuletwako na maradhi,  
Japo kifo chatuudhi,  
Wapi tutakimbilia?

Kweli dunia ni pana,  
Viumbe twazaliana,  
Sivyo tungekanyagana  
Twazaliwa twapungua.

Nukuu hapo juu inaonyesha kuwa kila ubeti una kibwagizo chake. Pia kuna mashairi mengine ambayo kibwagizo hubadilishwa katika kila kipande cha mstari, mfano shairi la “Uaminifu” (uk. 1) na “Kiasi” (uk. 4) katika *Mashairi ya Vidato*. Hivyo Mnyampala aliweza kutumia miundo inayobadilikabadilika katika kazi zake za ushairi. Tunaweza kusema kuwa mabadiliko katika umbo la ushairi yalianza taratibu na baadhi ya wataalamu wa ushairi wa kimapokeo, akiwemo Mnyampala, alikuwa mstari wa mbele katika kubadili miundo ya mashairi yake na kuleta upya katika sanaa ya ushairi wa Kiswahili.

Kwa ujumla, miundo aliyotumia Mnyampala ina mchango katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili na inatumika hadi sasa na baadhi ya waandishi wa karne ya ishirini na moja, kwa mfano, mashairi ya Kunemah (2008) na Walibora (2007). Kwa hiyo, miundo ya wanamapokeo inaendelea kutumiwa hadi sasa na washairi

mbalimbali, wakiwemo wanausasa. Usasa unatokana na umapokeo na upya. Hivyo ni dhahiri kuwa mchango wa washairi wa kimapokeo ni muhimu katika kuendeleza ushairi wa kisasa. Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kuwa muundo wa shairi lazima uamuliwe na kufungamana na mawazo, mtiririko wa hisia na makusudio ya mtunzi. Hivyo, mtunzi yeyote ni lazima aongozwe na maudhui, hisia na makusudio ya utunzi. Kutokana na ukweli huo, tunaona mwingilianomatini wa miundo ya wanamapokeo na wanausasa katika ushairi wa kisasa. Mfano katika diwani ya *Msimu wa Tisa* ya Kithaka wa Mberia, baadhi ya mashairi yake yamepangwa kwa muundo unaoelekeana na wa kimapokeo wa mistari minne, tofauti ni kwamba ushairi wake haufuati vipengele vya kiarudhi<sup>49</sup> vinavyozingatiwa na wanamapokeo.

Kutokana na maelezo hayo tunaweza kusema kuwa waandishi wa ushairi wa kimapokeo wana mchango pia katika waandishi wa ushairi wa kisasa. Maathiriano hayo yametokana na mwingilianomatini uliopo katika kazi za fasihi. Kwa kuwa waandishi wa matini ni wasomaji wa matini nyingine za fasihi, ni dhahiri kuwa kazi zao zinabeba athari za kila aina za waandishi wengine watangulizi wa fasihi. Hivyo basi ni muhimu kufahamu miundo waliyotumia washairi wakongwe na kuona jinsi ilivyochangia maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Kwa kuwa kazi za fasihi huingiliana, hutegemea na kuathiriana na matini nyingine. Mnyampala alikuwa mbunifu na mahiri katika kutumia miundo mbalimbali. Aliweza kutumia muundo wa kipande, msitari na ubeti mmoja kuwasilisha ujumbe unaojitosheleza kwa walengwa. Miundo ya Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili inaonyesha ukomavu katika mbinu za utunzi na ujuzi wa lugha ya Kiswahili. Kupitia miundo yake aliweza kuibua misamiati na kukuza lugha ya Kiswahili. Mchango wa Mnyampala katika muundo wa shairi wa Kiswahili hauna kifani.

---

<sup>49</sup>Vipengele vya kiarudhi ni vile vinavyofuata urari wa vina na mizani.



### 5.3 Matumizi ya Lugha

Matumizi ya lugha katika ushairi wa Kiswahili ni mojawapo ya vipengele muhimu sana katika kukuza ushairi wa Kiswahili. Baadhi ya waandishi huweka lugha kama kipengele kimojawapo cha mtindo. Katika utafiti huu tumekijadili kipengele hiki kama kipengele kinachojitegemea licha ya kuwa kinaweza kujadiliwa katika mtindo. Mchango katika matumizi ya lugha unajitokeza namna ambavyo Mnyampala anateua maneno yanayoeleweka kwa wasomaji kwa kutumia picha na ishara katika kazi zake za ushairi wa Kiswahili. Uteuzi huo ulitokana na ujuzi wa lugha ya Kiswahili aliokuwa nao pamoja na mwingilianomatini wa tungo mbalimbali zilizokuwepo wakati huo. Nabhany (1990) anafafanua kuwa licha ya mtunzi kuchagua na kupanga kwa uangalifu kazi yake, ni lazima awe mjuzi wa lugha ya Kiswahili na kunga za ushairi mfano bahari za ushairi kwa kuwa zina msamiati wake maalum. Hivyo, tunakubaliana na Nabhany kuwa lugha ina nafasi na umuhimu mkubwa sana katika ushairi wa Kiswahili. Mnyampala aliweza kutumia mpangilio mzuri wa maneno mateule kutokana na ujuzi wake katika lugha, mtindo huu uliathiri watunzi wengine.

Vilevile mwandishi huyu alipobaini kuwa huenda maneno aliyotumia hayataeleweka sana na jamii anayoandikia aliweka faharasa au kamusi ndogo ya maneno magumu mwishoni mwa kitabu husika ili wasomaji waweze kuelewa maana ya maneno hayo. Mfano mwishoni mwa *Waadhi wa Ushairi* ameweka orodha ya maneno magumu iliyoitwa “Kamusi ndogo ya maneno yasiyojulikana vyema” (uk. 84-87). Pia mwishoni mwa mswada *Mahadhi ya Kiswahili* ameweka orodha ya maneno magumu yaliyotumika ndani ya mswada huo akiyaita “Kamusi ndogo ya maneno magumu” (uk. 17).

Mnyampala aliweza kutumia lugha mbalimbali katika kazi zake kwa mfano lugha za Kibantu, Kiingereza, Kiarabu na nyinginezo. Naye Williams (1974) anaeleza kuwa

lugha ya ushairi ya Mnyampala ni ya mchanganyiko; kuna mahali alipotumia Kiswahili sanifu na kuna wakati mwingine amechanganya lugha ya kawaida na Kiswahili cha zamani, kitarafa ama kilugha. Ngugi (1998) anaeleza kuwa Mnyampala alitumia misamiati migumu katika shairi lake la “Siraji Ng’aza Sirati.” Hivyo kutokana na mawazo hayo tunatambua kuwa Mnyampala alikuwa bingwa wa kuteua maneno kutoka katika lugha mbalimbali alizokuwa anazifahamu na kuyatumia katika ushairi wake na kuyatolea ufafanuzi. Katika *Diwani ya Mnyampala*, mshairi huyu ameonyesha ukomavu katika matumizi ya lugha kupitia mashairi ya “Tungeni Mtiririko” (uk. 5), “Njozi ya Mawe Matatu” (uk. 33), “Mimi siye Mzoevu,” “Watungaji wa Unguja” (uk. 114), “Msaka Thani Rubiya” (uk. 133), “Siraji Ng’aza Sirati” (uk. 135), “Natunga Msisitizo” (uk. 121), “Shairi Johari Shwari” (uk. 79), “Lugha Yetu Kiswahili” (uk. 123), “Niache Vivyo Nilivyo” (uk.126), “Rada ya Mwana Ufito” (uk. 141) na mengineyo. Katika mashairi haya tunaona ufundi wa Mnyampala katika uteuzi wa maneno na ameweza kutumia lugha ipasavyo katika kukuza lugha ya Kiswahili.

Mfano mwingine wa matumizi ya lugha unapatikana katika *Diwani ya Mnyampala* katika shairi la “Yapi Yawele 1959” (uk. 90) ubeti wa kwanza na wa pili, lisemalo:

142. Kwa heri na muagano, ruhusa tuone ule,  
Tuchungulie makano, yaliyo baki yakele,  
Ulivyotoa mfano, kuahidia wavyele,  
Yaliyopita si ndwele, tugange yanayokuja.

...Bali tulipewa watano, mawaziri watoshile?  
Yaliyopita si ndwele, tugange yanayokuja.

Katika shairi hili kuna maneno yanayotokana na Kiswahili cha kale na ya kikabila ama kilugha. Neno ‘yawele’ ni la Kiswahili cha kale, lenye maana *yaliyotokea*, ‘wavyele’ ni Kigogo maana yake ni *kayemba* (wanavyoitana wazazi wa mume na mke) na ‘watoshile’ ni Kiswahili cha kale linalomaanisha *wanatosha*. Naye, Williams

anaeleza kuwa Kiswahili kilichojitokeza katika shairi la “Yapi Yawele 1959?” kinaonekana ni cha kale. Aidha, kutokana na utafiti huu tumebaini kuwa si Kiswahili cha kale tu kilichotumika. Pia kuna mchanganyiko na maneno ya kilugha kama vile Kigogo. Neno lingine lenye asili ya Kigogo katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1 na 2* ni ‘ngonjera’ likimaanisha kuambatana au kwenda pamoja ama kwenda sambamba.

Vilevile, Mnyampala katika *Diwani ya Mnyampala* ametumia maneno ya lugha nyingine kama vile Kiebrania, Kigriki, Kilatini, Kiarabu na Kiingereza. Mfano neno ‘Pasaka’ lina asili ya Kiebrania, lenye kumaanisha kuvuka au kupita. Neno hili linapatikana katika shairi la “Kiongozi Mtukufu” (uk. 26-27) ubeti wa saba usemao:

143. Aprili tufikie, na Pasaka takatifu,  
Na Pasaka isogee, kwa siku zake tawafu,  
Ni karibu tutegee, na tuyaache machafu....

Pia kuna neno “toharani” katika shairi la “Ya Watenzi Wote” (uk. 133) ubeti wa tano, usemao:

144. Siku ya pili msibani,, kukumbuka wafu wote,,  
Waliokufa vitani, tunakuiteni sote,  
Ye yote wa toharani, tusali watakate,...

Neno ‘toharani’ asili yake ni Kilatini, lenye kumaanisha mahali pa kutakaswa ama kusafishwa. Kadhalika katika shairi hilo (uk. 133), kuna neno ‘Krismas’ linalotokana na neno Chrismass ambalo asili yake ni Kilatini. Neno hili limeundwa na maneno mawili Christ na Mass ikimaanisha Kristo wa watu wote ama misa ya Kristo. Neno hili linapatikana pia katika shairi la “Rabbi Yesu Kazaliwa” (uk. 39) ubeti wa sita, usemao:

145. Noeli ni takatifu, ndio siku mbarikiwa,  
Krismas muarifu, ndio yenye kusifiwa,  
Kuondoa maumbufu, kwake tulikochukizwa,...

Kwa upande wa lugha ya Kiarabu, ametumia maneno yafuatayo: ‘Manani’ lenye maana ya Mungu katika shairi la “Mali pepo Dunia” (uk. 7), na ‘Inshallah’ katika shairi la “Chama na Kibarikiwe” (uk. 94) ubeti wa tatu. Neno Inshallah humaanisha Mungu akipenda. Pia neno ‘Mdalasini’ likimaanisha mti unaotumika kama kiungo kwenye vyakula, limejitokeza katika shairi la “Ua Hili Ua Gani?” (uk. 85). Katika shairi la “Ni Madaraka Kamili” (uk. 139), ubeti wa saba, kuna neno ‘Qudusi’ lenye maana Mungu Mtakatifu. Maneno mengine mengi yametumika katika mashairi yake.

Pia kuna maneno ya Kiingereza ambayo yametumika kama maneno ya kawaida ambayo ni ‘nambariwani’ lenye maana ya nambari moja, ‘taiti’ maana yake bana na kuwini lenye maana kufanikiwa, maneno hayo yamejitokeza katika *Waadhi wa Ushairi*. Licha ya maneno hayo pia kuna mchanganyiko wa Kiingereza na Kiswahili katika mashairi yake mfano mzuri ni katika *Diwani ya Mnyampala* shairi la “Msaka Thani Rubiya” (uk. 133) ubeti wa kwanza na pili unasema:

146. A nice melody is wine, when touches an ear,  
As entered in mine, eyes affected to tear,  
I tasted the vine, thank you my dear,  
Mthaka than Rubiya, kama hada mahuzeni.

Sauti nzuri ni divai, inayogusa masikio,  
Na inavyoniingia, macho yatoka machozi,  
Nimejaribu mzabibu, nashukuru ndugu wangu,  
Mthaka than Rubiya, kama hada mauzeni. (tafsiri yetu)

Hapo tunaona Mnyampala ametumia lugha ya Kiingereza na kukimudu vizuri katika utunzi wake. Hivyo Mnyampala aliweza kutumia lugha mbalimbali kutokana na mwingiliano wa jamii hasa katika kipengele cha dini na elimu pamoja na kazi alizoweza kufanya katika jamii mbalimbali ndani na nje ya mkoa wa Dodoma. Vilevile kuwepo kwa wageni, hasa Waarabu, kulifanya mashairi mengi ya kimapokeo

kutumia maneno mengi ya lugha ya kigeni hasa Kiarabu. Vilevile Mnyampala ametumia pia taswira, methali na takriri kama tuonavyo hapa chini.

### 5.3.1 Matumizi ya Taswira

Mnyampala ametumia aina mbalimbali za taswira katika ushairi wake. Taswira zilizotumika zina mchango katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Kipengele cha taswira kimejadiliwa katika sura ya nne (taz. 4.1.1). Mnyampala ameonyesha ubunifu wa hali ya juu katika uumbaji wa taswira zake. Baadhi ya taswira zake aliziumba kwa kutumia tamathali za semi ambazo pia zilitumika na waandishi wengine kama vile Shaaban Robert na wengineo. Kwa hiyo, mchango wake kwa upande wa taswira ni namna alivyotumia vizuri taswira zake kwa kuchota mambo mbalimbali yaliyomzunguka yeye na jamii yake na kuyaweka katika kazi zake. Vilevile katika baadhi ya taswira, amechota baadhi ya vipengele kutoka katika historia na sehemu nyingine ya maisha yake mfano shairi la “Njozi ya Mawe Matatu” (uk. 34) na “Nchi Gani Ilotoweka” (uk. 55) katika *Diwani ya Mnyampala*.

Mnyampala ametumia taswira za kugusa, kuonja, kuona, kufikirika na zinginezo. Aidha kupitia taswira hizo tunapata maudhui mbalimbali za kisiasa, kijamii na kiuchumi. Taswira hizo zimekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili, kwa kuwa aina za taswira alizozitumia zinatumiwa hadi sasa na waandishi wa karne ya ishirini na moja katika uandishi wa kazi zao za ushairi (rejea mashairi ya Kithaka wa Mberia *Msimu wa Tisa*).

Kwa ujumla watunzi wa ushairi walitunga na wanaendelea kutunga tungo zenye maudhui ya kisiasa, kijamii na kiuchumi ili kuonyesha mambo yaliyopo katika jamii na kuyaweka katika maandishi kwa lengo la kuelimisha jamii. Hivyo basi ni dhahiri kuwa watunzi wa ushairi wataendelea kutumia taswira mbalimbali ambazo pia

zilitumiwa na waandishi wakongwe akiwemo Mnyampala, kwa kuwa ushairi hautoki katika ombwe bali unatokana na fasihi yenyewe pamoja na mazingira yaliyomlea na kumkuza mshairi. Hivyo waandishi wa kimapokeo akiwemo Mnyampala wana mchango mkubwa katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Hii inatokana na kwamba hakuna matini inayoweza kujitegemea bila ya kuhusisha matini tangulizi kwa namna fulani.

### 5.3.2 Matumizi ya Methali

Methali mara nyingi hutumika katika mazungumzo ya kawaida ya kila siku na katika kazi mbalimbali za fasihi ikiwemo ushairi wa Kiswahili. Kwa kawaida matumizi ya methali yana lengo la kumfanya msikilizaji ama msomaji kupata ujumbe fulani uliokusudiwa na mwandishi kwa uzito wake kamili. Katika sura ya nne (taz. 4.1.2) tumejadili jinsi methali kama mbinu ya kifani zinavyosaidia kuibua maudhui mbalimbali katika kazi teule za Mnyampala. Tumbaini kuwa matumizi ya methali katika kazi za Mnyampala yana mchango mkubwa katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Katika kazi za ushairi wake, kuna methali zenye kutoa mafunzo kwa jamii na kuwafanya wanajamii kubadili mienendo yao. Mfano katika shairi la “Muenda Omo na Tezi,” Mnyampala ametumia methali ya “muenda omo na tezi, marejeo ni ngamani” (uk. 20-21). Katika methali hiyo, kuna mafunzo kuhusiana na maadili na uvumilivu katika maisha.

Vilevile, Mnyampala alimudu matumizi ya methali zilizojaa mafunzo kwa rika zote na kugusa nyanja zote za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Methali ni kipera cha fasihi simulizi na zilikuwepo tangu zamani. Asemavyo Knappert (1979), labda kilichowapa washairi wa Kiswahili ilhamu kubwa zaidi ni kuwepo kwa methali nyingi katika lugha ya Kiswahili ambazo zilikuwa hazina ya fasihi simulizi iliyofichwa katika nyoyo za wazee waliokuwepo tangu kale. Anaongezea kuwa

inawezekana kuwa ushairi wa Kiswahili kabla haujawekwa katika maandishi, wasanii au manju wa fasihi simulizi waliunda methali kwa namna ya kishairi yaani zenye urari wa vina na mizani. Kutokana na maelezo ya Knappert ni bayana kwamba methali ni kipera cha fasihi simulizi ndani ya utanzu wa semi.

Hivyo basi, methali zimeendelea kutumiwa na watunzi wengine wa kazi za sanaa ya ushairi wa Kiswahili. Washairi hao wameweza kutumia methali katika kazi zao kama mojawapo ya nguzo muhimu ya kutolea mafunzo na maonyo kwa jamii husika. Mfano mzuri unajitokeza katika mashairi ya Kunemah (2008) mfano shairi la “Kipya Kinyemi Japo Donda” (uk. 2) na “tamaa mbele mauti nyuma” katika shairi la “Tamaa Mbele Mauti Nyuma” (uk. 3).

Kutokana na mjadala huo ni dhahiri kuwa mbinu ya methali ni muhimu katika sanaa ya ushairi wa Kiswahili. Kwa kutafiti kazi za Mnyampala tumebaini kuwa methali mbalimbali ambazo alizitumia ni zile ambazo zinaendelea kutumika hadi sasa. Kadhalika, methali bado zinatumika katika kazi mbalimbali za kifasihi na waandishi wa ushairi wa karne ya 21, kwa kuwa zimejaa hekima na mafunzo ya kidunia. Aidha, Mulokozi (2017) anaeleza kuwa methali nyingine huwa na muundo wa kishairi (yaani kila kipande huwa na urari wa vina na mizani) mfano ‘Haraka haraka, haina baraka’ kuna kina cha “ka.” Kwa upande wa Mnyampala ametumia methali zenye vina vinavyolingana katika *Mashairi ya vidato*, shairi la “Mtaka Nyingi Nasaba” (uk. 8), isemayo ‘mtaka nyingi nasaba, hupata mingi misiba’. Katika methali hiyo kuna kina cha kati “ba” na mwisho “ba.” Vilevile Mnyampala alitumia methalizenye vina tofauti (rejea, 4.1.2) na nyingi kazitumia kwenye kibwagizo kusisitiza maudhui yaliyomo ndani ya shairi na kipande cha methali kimetumika kama kichwa cha shairi. Hivyo methali ni kipera cha fasihi simulizi kisichopitwa na wakati. Kwa hiyo ni muhimu

kwa waandishi chipukizi kuzijua methali mbalimbali na kuzitumia katika utunzi wa kazi zao ili kuleta mvuto wa kazi zao.

### 5.3.3 Mbinu ya Takriri

Mnyampala ametumia pia takriri katika utunzi wa kazi zake kama mojawapo ya vipengele vya lugha, na kama mojawapo ya mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kuwa takriri ni marudiorudio ya sauti, silabi, neno, sentensi, wazo au ridhimu fulani ili kuleta athari na maana maalum kwa msikilizaji au msomaji wa shairi hilo. Wanaongezea kuwa takriri ni njia ya kishairi ya kuonyesha uzito wa hisia, kusesitiza wazo au dhamira fulani au kutia muziki katika shairi ili liweze kuimbika. Hivyo basi takriri ni mpangilio wa lugha na ridhimu katika shairi ambapo silabi, neno au msitari hurudiwa rudiwa kila mara katika tungo husika ili kuleta uzuri wa sanaa na kuongeza hisia za kishairi katika maudhui ya shairi husika. Kwa ujumla takriri hulifanya shairi kuwa zuri kisanaa na kimuziki ama linaloimbika. Mnyampala ametumia takriri nyingi katika mashairi yake, mathalani takriri silabi zimejitokeza toka mwanzo hadi mwisho wa mashairi yaliyomo ndani ya kazi teule na nyinginezo ambazo mashairi huyu amezitunga. Pia Mnyampala ametumia takriri neno na takriri msitari katika kazi zake za ushairi. Kwa mfano, neno ‘guoguo’ katika shairi la “Taabu kwa ‘Guoguo’ (uk2-3), ubeti wa pili usemao:

147. Wamepangwa jina lao guoguo mitaani,  
Na nguo wazibebao, hodi hodi majumbani,  
Je huko kwenu mnao, wakopeshao mijini?  
Heri nishone dukani, taabu kwa Guoguo.

Neno guoguo, katika shairi hilo limejitokeza tangu mwanzo wa shairi hadi mwisho wa shairi kwa lengo la kusesitiza maudhui ya biashara ya mitumba kuwa haifai ni bora



kushona nguo mpya kuliko kununua mitumba. Kadhalika, katika diwani hii kuna takriri neno chungu katika shairi la ‘Mchungu Chungu Kiungu’ (uk. 74), mfano:

148. Chungu nasokota uzi, niupitie ushanga,  
Chungu kutunga ni kazi, na kazi kubwa kupanda,  
Chungu na zake saizi, asilete kuvungavunga,  
Chungu mchungaji chungu, kwa mtima wa mbawazi.

Katika shairi hilo, neno ‘chungu’ limejirudia katika beti zote 12 na kuleta mvuto wa shairi husika. Neno ‘chungu’ limetumika kuelezea maudhui yahasuyo dini, kuwaheshimu na kuwatunza wazazi, malezi kwa watoto, kazi, maadili, usiri katika nyumba, mapenzi na ndoa. Takriri neno nyingine katika diwani hiyo inapatikana katika shairi la “Tenda Tendo la Kulinda” (uk. 75). Katika ubeti wa kwanza kuna neno ‘tendo’ linalojirudia kila ubeti ili kusisitiza maudhui ya upendo, amani, matendo mema, kuachana na uovu na maadili katika jamii. Kwa ufupi tunaweza kueleza kuwa kuanzia shairi namba 88 hadi 95, msanii ametumia mbinu ya takriri ambapo kuna takriri neno ‘tamaa’ katika shairi la “Tamaa Huzaa Baa” (uk. 76-77). Vilevile ametumia takriri ya ‘fahamu’ katika shairi la “Fahamu Hatamu Ngumu” (uk. 77-78), ‘wakati’ katika shairi la “Wakati Titi la Nyati” (uk.78-79), ‘shairi’ katika “Shairi Johari Shwari” (uk.79-80), ‘chama’ katika “Chama na Kibarikiwe” (uk. 80-81) na ‘taa’ katika shairi la “Taa Mitaa Hung’aa.” Aidha, katika *Diwani ya Mnyampala* kuna matumizi ya takriri silabi, neno na ridhimu ili kusaidia kufikisha maudhui husika kwa jamii husika katika hali ya hisia na msisitizo unaofaa. Kadhalika katika diwani hiyo kila shairi kuna kibwagizo kinachofanana toka mwanzo wa shairi hadi mwisho.

Vilevile, takriri mstari ama kibwagizo imejitokeza katika mashairi karibia yote yaliyomo ndani ya *Diwani ya Mnyampala*, na kazi zake nyingine. Takriri ni muhimu katika ushairi wa Kiswahili kwa kuwa huwafanya wasomaji kupata wazo alilokusudia mwandishi. Mbinu hii imeweza kutumika hata kwa washairi wa kisasa katika kazi zao

za ushairi, kwa lengo la kuibua maudhui mbalimbali katika kazi husika ama kusesitiza ujumbe ulioko katika kazi zao. Walibora (2007) anaeleza kuwa mshairi anayetumia barabara mbinu ya takriri yaani urudiaji wa silabi, maneno au miundo anafanya hivyo ili kusesitiza ujumbe na kuleta uzuri wa kisanaa. Anafafanua zaidi kuwa, takriri ni mojawapo ya sifa muhimu sana katika ushairi na hujipambanua kwa njia mbalimbali katika mashairi ya arudhi na huru katika tamaduni zote ulimwenguni. Hivyo kutokana na mawazo hayo Mnyampala ameipamba kazi yake kwa takriri na ameonyesha ubunifu katika matumizi ya mbinu ya takriri na kuzifanya kazi zake zivutie. Aidha, kutokana na matumizi mazuri ya takriri ameweza kuibua hata mitindo mipya ya ushairi kwa mfano mtindo wa mtiririko.

Mbinu ya takriri ilikuwepo kabla ya Mnyampala mfano katika *Diwani ya Muyaka bin Haji*, na hadi sasa (rejea kazi za ushairi za Kezilahabi, Kithaka wa Mberia na nyinginezo) inaendelea kutumika katika utunzi wa kazi mbalimbali za ushairi wa Kiswahili. Hii inatokana na kwamba hakuna kazi ya fasihi ambayo haina uhusiano na kazi nyingine kwa namna moja au nyingine. Kwa ujumla waandishi wa kimapokeo (1950 na kuendelea) na wanausasa wa miaka ya 1970 wana mchango mkubwa sana katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kwa kuwa takriri mbalimbali walizotumia ni zile zilizonufaisha shairi, zenye uasili, zilizofungamana na muundo asilia wa lugha inayohusika na iliyojitokeza katika sanaa bila kulazimisha na inayoendana na maudhui ya shairi husika. Pia takriri zao zilikuwa zinavuta hisia za mashairi na kuleta mtiririko na msisitizo wa maudhui ya shairi husika. Hivyo kupitia kazi za Mnyampala waandishi chipukizi huweza kujifunza takriri na ridhimu zinazofaa kupitia mtunzi huyu ili kuweza kutunga mashairi yenye ubunifu wa kiwango cha juu katika sanaa ya ushairi.

Kwa ujumla katika matumizi ya lugha, Mnyampala alikuwa mstari wa mbele katika kuibua misamiati mbalimbali katika ushairi wa Kiswahili kutokana na uteuzi wake wa maneno, matumizi ya taswira mbalimbali, misemo, methali, takriri na mbinu nyingine za kisanaa. Mnyampala amejitahidi kutumia maneno yanayoeleweka na pale alipotumia neno lisiloeleweka na jamii alitoa orodha ya kamusi ya maneno magumu mwishoni mwa kitabu chake. Kwa ujumla maneno yanayopatikana katika kamusi yake ni mchango kwa waandishi wengine na kutoa mwanga hata kwa watunzi wa kamusi mbalimbali za kitaaluma na nyanja nyingine kwa ujumla. Hivyo maneno hayo yanaweza kutumiwa na mtu yeyote bila ya kuhitaji idhini kutoka kwa mwandishi ama mmiliki wa kazi husika.

#### **5.4 Kukusanya Mashairi ya Waandishi Mbalimbali**

Mnyampala aliweza kukusanya mashairi ya waandishi mbalimbali kwa lengo la kuyahifadhi kwa manufaa ya kizazi kijacho. Baadhi ya kazi alizokusanya na kuzihariri ni kitabu cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*, mswada wa *Hazina ya Washairi* na mswada wa *Mahadhi ya Kiswahili*. Kukusanya mashairi mbalimbali na kuyaweka katika diwani moja kuliendeleza ushairi wa Kiswahili. Mashairi hayo aliyatoa magazeti mbalimbali mfano gazeti la *Mapenzi ya Mungu*, *Ngurumo* na *Mambo Leo* (Mnyampala, 1966 katika Dibaji yake). Mnyampala anaeleza kuwa kazi hiyo ya ukusanyaji wa mashairi mwanzoni ilifanywa na wageni, kama asemavyo mwenyewe katika dibaji yake ya mswada wa *Hazina ya Washairi* kuwa:

149. Ukusanyaji wa mashairi ya washairi ilishughulikiwa hasa na wageni ambao hawakuwa wenyeji wa nchi hii-kama vile mashairi ya Fumo Liongo, mashairi ya Muyaka bin Haji Al-Ghassaniy, Utenzi wa Al-Akida, Utenzi wa Barasisi, Utenzi wa Mkonumbi na nyinginezo nyingi zilizokusanywa na wageni. (uk. i)

Kutokana na nukuu hiyo tunabaini kuwa Mnyampala alipata wazo la kukusanya mashairi ya washairi wenzake kupitia washairi waliotangulia kama ionekanavyo katika dondoo hilo. Kwa hiyo, Mnyampala aliweza kunakiri mashairi ya washairi mabingwa na kuyaweka katika miswada kwa manufaa ya vizazi vijavyo na kujenga lugha ya taifa ambayo ni Kiswahili. Mashairi yaliyomo katika mswada wa *Hazina ya Washairi* yalianza kukusanywa mwaka 1965 (Mnyampala, 1966). Ukusanyaji wa mashairi hayo ulitokana na wito aliutoa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika utangulizi wa *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* kuwa waandishi wanatakiwa kuandika kitabu kingine kikubwa kuliko hicho. Kama asemavyo Mnyampala katika dibaji yake kuwa:

150. Mawazo haya ya kukusanya mashairi yalikuja? Nilikumbushwa na Mtukufu Raisi wetu Mwalimu Julius K. Nyerere wakati alipoandika utangulizi wa kitabu cha “Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi” kwa ajili ya toleo la pili, alisema: “Nawashukuru pia jamaa wa chama cha washairi kwa kukitoa kijitabu hiki. – Ninalowaomba zaidi ni kwamba wajitayarisha kututolea kijitabu kikubwa zaidi kuliko hiki” (*Hazina ya Ushairi*, uk. i).

Maneno hayo yalimpa Mnyampala hamasa ya kukusanya mashairi mengi zaidi tangu mwaka 1935 hadi 1965, ambapo alifanikiwa kwa kiasi kikubwa. Ukusanyaji huo uliofanywa na Mnyampala una mchango mkubwa kwa maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kwa kuwa tunapata kufahamu waandishi wengine walioandika kazi za ushairi wa Kiswahili. Pia tunapata maudhui mbalimbali ya kisiasa, kijamii na kiuchumi yaliyoibuliwa na waandishi hao.

Baadaye Saadan Kandoro naye aliandika kitabu cha *Mashairi ya Kandoro* (1972) chenye mashairi yake na mkusanyiko wa mashairi ya watunzi mbalimbali wa ushairi kama vile Julius Nyerere, Amri Abedi, Akilimali Snow White na wengineo. Vilevile,

katika karne ya ishirini na moja tunaona waandishi kama vile Ken Walibora ambao wameweza kukusanya mashairi mbalimbali na kuhariri diwani yake iitwayo *Diwani ya Karne Mpya* (2007). Katika diwani hiyo mna mashairi themanini yaliyotungwa na watunzi kumi na nane tofautitofauti wenye asili ya Kenya na Tanzania na wenye tajriba ya maisha tofautitofauti ya ndani na nje ya Afrika Mashariki. Hivyo katika mashairi hayo kuna mseto wa tajriba, mikabala na mikondo mbalimbali. Mchanganyiko huo unachangia kuleta uhalisia pamoja na mwingiliano wa mambo katika nyanja mbalimbali za kisiasa, kijamii na hata kiuchumi.

Aidha, *Diwani ya Karne Mpya* imekusanya tungo za washairi wakongwe na wapya. Umuhimu wa diwani hii unadhihirika katika maudhui, mikabala ya kifalsafa, maumbo na miundo, pamoja na misisitizo ya washairi waliochangia diwani hii. Haya yote yametokana na mchango wa waandishi waliotangulia akiwemo Mathias Mnyampala aliyewahi kukusanya mashairi ya washairi wengine na kuyahifadhi kwa manufaa ya taifa. Kama asemavyo Kezilahabi (1976) hamu ya kurejelea mbinu mbalimbali zilizotumika na washairi wa zamani zilichangia kuzua ushairi mpya. Hivyo basi, hakuna kitu ambacho kinaibuka bila ya kutegemea mawazo ama matini zilizotangulia, katika kazi za sanaa lazima ziwe na mwingiliano wa matini mbalimbali zinazoibua matini mpya inayoendana na muktadha husika.

Vilevile, Mnyampala aliweza kukusanya nyimbo mbalimbali maarufu kwa manufaa ya jamii na taifa kwa ujumla. Nyimbo hizo aliziita *Mahadhi ya Kiswahili*, nyimbo hizo zilikusanywa katika sehemu mbalimbali za Tanzania na pwani ya Kenya. Nyimbo hizo zilihusu kubembeleza watoto, jando, kutafuta mchumba na mahaba na mapenzi. Hata hivyo *Mahadhi ya Kiswahili* ni mswada ambao haujachapishwa hadi sasa. Aidha, maudhui yaliyomo katika mswada huu yanajitokeza pia katika nyimbo

zinazotungwa katika karne hii. Hii inatuthibitishia kuwa fasihi inatokana na fasihi yenyewe na hakuna matini inayoibuka bila ya kutegemea matini tangulizi.

Sambamba na hilo, tumebaini kuwa baadhi ya nyimbo hizi zilikuwa hazizingatii arudhi na idadi ya mistari hutofautiana kwa kila ubeti. Mtindo huo unajibainisha waziwazi katika nukuu hapa chini:

151. Owani baba owani, kitunguu na ubani,  
Nyoka kalala njiani, tumkanyage kichwani;  
Usiache wenda kuni, na wenda kisimani,  
Nitakupiga ukuni, uangukie majini,  
Makosa niliyokosa, sina maombezi kwani?  
Muombezi wangu nyota, na mwana wa Sultani,  
Oooh, mtoto, Oooo mtoto. (*Mahadhi ya Kiswahili*, uk. 2)

Katika nukuu hiyo, tumebaini kuwa wimbo si lazima uwe na mistari mitatu. Kwa mfano wimbo huu una mistari saba na bado ni wimbo. Kadhalika wimbo huu hauna urari wa vina katika vipande; mistari wa kwanza hadi wa nne vina vya kati ni 'ni' na mistari wa tano ni 'sa', ubeti wa sita ni 'ta' na ubeti wa saba ni 'to'. Pia katika ukurasa huohuo, kuna wimbo mwingine ambao hauzingatii urari wa vina, wimbo huo unasema:

152. Silie mama silie,  
Ukilia waniliza, wanikumbusha makiwa,  
Makiwa ya baba na mama,  
Baba na mama watende,  
Wanioza dume kongwe,  
Halisafiri halendi,  
Kazi kumega matonge. (uk. 2)

Wimbo huu haufuati kanuni za arudhi za ushairi wa kimapokeo. Mkusanyiko wa nyimbo hizi za Mnyampala unathibitisha kuwa ushairi wa mwanzo (wimbo) ulikuwa hauzingatii arudhi ya ushairi na nyimbo hizo zilikuwepo kabla ya ujio wa wakoloni. Mbega (1995) anaeleza kuwa kadri watu walivyojinyakulia mambo mapya ya kigeni

ndivyo baadhi ya tamaduni zilivyopotea na kuwa haba ama kumalizika. Hivyo basi, utamaduni wa kigeni au mambo mapya yalisababisha baadhi ya vipengele vya utamaduni kupotea na kuingiza vipengele vya kigeni katika ushairi wa Kiswahili. Vipengele hivyo vilichangia kuleta mabadiliko katika utamaduni wa wenyeji ili kuchukuana na utamaduni huo wa kigeni. Mabadiliko hayo yalisababisha kupoteza mtindo na muundo wa asili wa ushairi wa Kiswahili. Kwa hiyo, arudhi ya ushairi kama vile urari wa vina ilitokana na maingiliano ya tamaduni mbalimbali hususani ujio wa Waarabu na hati ya Kiarabu.

### **5.5 Kukuza Nadharia ya Ushairi wa Kiswahili**

Wafula na Njogu (2007) wanaifasili nadharia kama miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya kifasihi kuifahamu kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Fasili hii, zaidi ya ubora wake, ina udhaifu mkuu mmoja wa kuchukulia kwamba kazi ya fasihi lazima iwe andishi, kazi ya fasihi inaweza pia kuwa simulizi. Wamitila (2003) anasema kwamba nadharia ni sayansi au sanaa inayohusika na kanuni za kijumla na mikabala au hata kanuni fulani zinazotumika katika uchanganuzi wa suala fulani. Aidha, tunaweza kusema kuwa nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo, imani au mkabala fulani wa mawazo ya watu fulani juu ya jambo fulani. Kadhalika, nadharia inaweza kutokana na mawazo yaliyoundwa kitambo na jopo la wataalamu au inaweza kutokana na usomaji au usikilizaji makini wa kazi ya fasihi ya mtu binafsi. Kwa ujumla maisha ya mwanadamu yanaongozwa na nadharia kadha wa kadha.

Kutokana na maana zinazohusu nadharia, katika utafiti huu tumebaini kuwa Mnyampala alikuwa na mwongozo aliokuwa anafuata katika utunzi wa mashairi yake. Kwa ujumla mtunzi huyu alikuwa anafuata kaida za kimapokeo. Hivyo alikuwa na

nadharia yake ya kimapokeo iliyokuwa ikimwongoza katika utunzi wa kazi zake. Hili linajibainisha kwa kuangalia kazi zake kuhusu ushairi wa Kiswahili. Aidha, Mnyampala ni miongoni mwa wataalamu waliotoa maana ya ushairi pamoja na aina zake. Maana hiyo pamoja na aina za mashairi zinapatikana katika Dibaji<sup>50</sup> yake ya *Diwani ya Mnyampala*, Mnyampala anaeleza kuwa:

153. Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Ndicho kitu kilicho bora sana katika maongozi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalumu kwa shairi. Shairi laweza kumliza mtu akatokwa na machozi kwa ajili ya mchomo wa hanjari la kuukata moyo na maini kwa ule mchomo na mguso wa maneno ya shairi la mshairi bora. Vile vile, shairi jingine laweza kuuburudisha moyo mtu akafurahi akthari ya furaha na kujiona kuwa nayo heri mithili ya mtu aliye peponi. Shairi lina usemi ulio mtamu sana. Kwa maoni yanayopenya moyo yaliyo bora sana. Hivyo ushairi una sifa iliyo bora sana ulimwenguni na mafunzo yenye uadilifu na mazingira ya dunia yalivyo (Mnyampala, 1965)

Kutokana na dondoo hili, tunapata wazo kuwa kwa mujibu wa Mathias Mnyampala miongoni mwa sifa za ushairi wa Kiswahili ni kutumia lugha ya kishairi isiyokuwa na maneno ya kashfa wala matusi. Pia, ushairi unapaswa kuwa na urari wa vina na mizani kamili zinazotakiwa katika ushairi wa Kiswahili. Sifa nyingine za ushairi wa Kiswahili anazobainisha mtunzi huyu ni kuwa shairi linapaswa liwe na vina vinavyopatana au vinavyolingana, hususani mwishoni mwa kila msitari kwa ubeti mzima, ingawa vina vya kati vinaweza kukosekana. Katika dibaji hiyo, Mnyampala anasisitiza juu ya sanaa ya shairi kwa kusema kuwa shairi la Kiswahili lihusu mwendo wa mashairi bora yaani linatakiwa lisizidi mno maneno ya kurudiarudia, lisitungwe namna ya kulinganisha matuta, lisiwe pyororo (lisiloeleweka) bali liwe shairi kamili kama mashairi ya watu mahiri, werevu na wenye hekima. Mnyampala

<sup>50</sup>Kitabu nilichotumia Dibaji haikupewa ukurasa, ila katika toleo 2014 ni (uk. vii).



alichangia katika kutoa maana ya ushairi kwa kuegemea katika mkondo wa wanamapokeo. Kwa kufanya hivyo amechangia kukua kwa nadharia ya ushairi wa kimapokeo.

Mnyampala alikuwa miongoni mwa wataalamu wa mwanzo kutoa aina za ushairi. Mnyampala aliweza kutoa aina tano za ushairi: “mashairi ya kawaida, mashairi ya furaha, mashairi ya huzuni, mashairi mazito na mashairi ya kuadibu” (taz. *Diwani ya Mnyampala*, 2014: (vii-viii). Kila aina ya ushairi ina vipera vyake vifuatavyo:

154. 1. MASHAIRI YA KAWAIDA

- (1) Mawaidha ya dunia
- (2) Visa na mikasa kwa kawaida
- (3) Wasifu wa kila kitu kwa ujumla
- (4) Furaha au huzuni na
- (5) Shairi maalum, n.k

2. MASHAIRI YA FURAHA

- (1) Kushangilia tamasha
- (2) Kutakia kheri na mafanikio
- (3) Wasifu wa Furaha hiyo ilivyo
- (4) Ombi la kudumisha furaha hiyi, na
- (5) Waadhi kwa ajili ya tafrija hiyo

3. MASHAIRI YA HUZUNI

- (a) (1) Shairi la rambirambi (kama ni kifo)
- (2) Maombezi kwa Mungu kwa ajili ya marehemu
- (3) Maombezi kwa wale waliobaki wanaomhusu
- (4) Historia marehemu (kama inajulikana)
- (5) Kumbukumbu itakiwayo
- (b) (1) Shairi la Tanibihi na stighifari
- (2) Shairi la manusurina
- (3) Shairi la pole yenyewe iliyomfika mtu
- (4) Kumtahadharisha ya mbele, na
- (5) Uzindushi wa jumla

4. MASHAIRI MAZITO

- (1) Shairi la kuzama (kufumba)
- (2) Shairi la tambo (kutega fumbo)
- (3) Pigo kuu la ushairi na taaluma zake, na
- (4) Fahari ya ushairi na taaluma zake, na
- (5) Kuonyesha mbinu za Lugha ya mshairi yule

### 5. MASHAIRI YA KUADIBU

- (1) Kumuonya mtu kinaganaga bila kutumia utusi
- (2) Kumtanabahisha ya hatima
- (3) Ni nini hasara ya upujufu
- (4) Ungwana ni nini, na
- (5) Maandiko matakatifu

Aina hizi za ushairi zilizoainishwa na Mnyampala ni mchango wake mmojawapo katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Mbali na aina hizi za ushairi, mtunzi huyu amependekeza sifa za ushairi ambazo hazifai tu kwa ushairi wa kimapokeo bali pia hata katika ushairi wa kisasa kama alivyofanya Amri Abedi (1954). Tunazipata sheria hizi katika dibaji ya *Diwani ya Mnyampala*, Mnyampala anaeleza kuwa washairi hodari hutunga mashairi yao kwa nadhari<sup>51</sup> za aina tano (uk. viii-x), ambazo ni:

155. (1) Shairi liwe na *Poetical Swahili*, yaani Kiswahili kinachohusu mwenendo wa mashairi bora.
- (2) Shairi liwe na urari wa mizani kamili zinazohusika na ushairi wa kawaida kwa lugha ya Kiswahili kisichokuwa na kashifa ya utusi ndani yake.
- (3) Shairi liwe na vina vinavyopatana, hususani mwishoni mwa kila ubeti kwa shairi lote zima ingawa vina vya katikati vikosane kwa utenzi wake.
- (4) Shairi kama halikulingana vina vyake yaani, mtiririko, lakini liwe na muwala. Yaani liwe na maana iliyo bora sana yenye ufundisho ndani mwake, furahisho, mvuto wa maarifa ama kasida za kumsifu Mungu pengine watu maarufu na vitu vinginevyo vistahilio kusifiwa.
- (5) Lisizidi mno maneno ya kurudiarudia. Lisitungwe namna ya kulinganisha matuta. Lisiwe pyororo la mashairi, bali wenye hekima.

Kyamba (2016) anaeleza kuwa nadharia ya Mnyampala ya ushairi inahusu mashairi ya kijadi na maneno ya hekima. Pia anasisitiza kuwa hata kama shairi halina vina basi liwe na mtiririko na muwala, pia kuwe na maana bora sana yenye mafundisho ndani mwake, ufurahisho, mvuto wa maarifa ama kasida za kumsifu Mungu, watu maarufu

---

<sup>51</sup> Ni kanuni au mashariti au sheria.

au vitu vinginevyo vinavyostahili kusifiwa. Kwa ujumla nadharia ya Mnyampala ya ushairi wa Kiswahili ni muhimu sana katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kwa sababu Mnyampala ni miongoni mwa washairi wa kimapokeo waliosaidia kutoa maana ya ushairi, aina za ushairi, uundaji wa kanuni za ushairi wa kimapokeo pamoja na uundaji wa istilahi na msamiati mbalimbali ya ushairi na Kiswahili.

### **5.6 Kuingiza Maudhui ya Dini katika Ushairi wa Kiswahili**

Mnyampala ambaye alikuwa mkristo wa kwanza kutunga na kuandika mashairi ya Kiswahili, alisaidia kuelimisha jamii kuwa ushairi wa Kiswahili si kwa ajili ya Waislamu tu. Hivyo alisaidia kutoa mwelekeo mpya kwa kuonyesha kuwa ushairi pia huweza kutungwa kwa kuhusisha maudhui ya Kikristo kupitia kazi zake na kuchangia kukuza taaluma ya ushairi. Hivyo, Mnyampala alisaidia kusawiri Ukristo katika kazi za ushairi kupitia kazi zake za *Utenzi wa Injili* na *Utenzi wa Zaburi*. Vilevile katika *Diwani ya Mnyampala* kuna shairi la “Kiongozi Mtukufu” (uk. 26), “Rabbi Yesu Kazaliwa” (uk. 39), “Amezaliwa Mwokozi” (uk. 130).

Kadhalika, Mnyampala katika kazi zingine za ushairi aliingiza maudhui ya dini zote mbili ya Kikristo na Kiislamu (taz. 3.2.1.4). Hii inaonyesha kuwa Mnyampala hakuwa mbaguzi wa dini. Hata hivyo, huenda mawazo ya Mnyampala ya kuweka maudhui yahasuyo Ukristo katika ushairi, yalitokana na waandishi wa karne ya kumi na nane na kumi na tisa. Tungo zinazohusu maudhui ya dini ya Kiislamu kama vile *Utenzi wa Al-Inkishafi* uliotungwa na Sayyid Abdallah Bin Ali (1810), *Utenzi wa Hamziya* uliotungwa na Seyyid Aidamis bin Athuman (1749) na *Diwani ya Muyaka* bin Haji Al-Ghassaniy ambaye inasadikika aliishi miaka ya 1776-1840 (Bhalo, 1977 na Shitemi, 2010) na nyinginezo zilizohusu maudhui ya Kiislamu, zilimsaidia Mnyampala kuandika kazi zake kwa kuhusisha maudhui ya Kikristo.

Aidha, waandishi wengine mashuhuri wa karne ya ishirini kama vile Shaaban Robert, Amri Abedi, Saadani Kandoro, Mahmoud Hamdouniy, Akilimali Snow White walitumia sanaa ya ushairi kutoa mawaidha ya dini ya Kiislamu katika baadhi ya beti za mashairi yao. Kwa mujibu wa Ponera (2010), Shaaban Robert ni mshairi aliyetumia sanaa ya ushairi kutoa maadili ya kidini, mfano *Utenzi wa Hati* (uk. 8-22) na *Utenzi wa Adili* (uk. 23-40) ambazo zinapatikana katika kitabu cha *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1991). Katika tenzi hizo aliwataka wanawe Mwanjaa na Selemani wafuate maadili na kushika dini, kuwa wasafi kiroho na kuachana na anasa za dunia. Shaaban Robert aliwauka wanawe wamtangulize Mungu katika yote na kushika dini, hususani dini ya Kiislamu. Hapa tunaweza kusema kuwa Shaaban Robert katika utunzi wake alitunga akiegemea zaidi katika dini ya Kiislamu. Kwa upande wa Muyaka, baadhi ya mashairi yake yalihusu dini ya Kiislamu, lakini Mnyampala alitunga mashairi yake kwa kuunganisha dini zote mbili, Ukristo na Uislamu. Hivyo, tunaweza kusema Mnyampala alikwenda mbele zaidi kwa kuchanganya dini zote mbili katika utunzi wake. Vilevile, Mnyampala (2011:9) anamwelezea Amri Abedi kuwa ni “mshairi aliyetumia sanaa yake kutoa mawaidha kuhusu dini ya Kiislamu,” mfano katika ubeti wa kumi na kumi na mbili anasema.

156. Dini hukuipokea, ninashukuru Mola,  
Kamilisha dini pia, kwa kutabii Rasula,  
Mshenga kutufikia, hazitatufaa hila,  
Dawa mziwanda kula, kula upate afia.

Rahimu Mola Jalia, ninashukuru Allah,  
Mara kwa mara jalia, nandika hizi risala,  
Mshairi aje jua, Mjumbeo wa fadhila,  
Dawa mziwanda kula, kula upate afia.

Mnyampala anaeleza kuwa shairi hilo lilitungwa kwa ajili ya kumhubiria dini mpwawe bwana Saadani Abdu Kandoro ili afuate madhehebu ya Ahmadiyya. Shairi

hili linapatikana pia katika kitabu cha *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954). Naye Kandoro alimjibu akisema “Sili Nisichotamani, Sili Ingawa ni Dawa” (uk. 9) katika *Historia ya Hayati Sheikh Kaluta Amri Abedi: 1924-1964* (2011). Kwa ujumla mashairi hayo yalikuwa yanahusu maudhui ya dini ya Kiislamu. Kutokana na mwelekeo huo katika utafiti huu tumebaini kwamba Mnyampala naye aliona kuna umuhimu wa kutumia sanaa ya ushairi kutoa mawaidha ya dini ya Kikristo. Mnyampala alikuwa Mkristo wa kwanza katika uandishi wa ushairi na aliyeathiriwa kwa kiasi kikubwa na mafundisho ya Kikristo na mwalimu wake Damiani (taz. 1.1.1.2). Hivyo basi, Mnyampala alijitahidi kuonyesha kuwa ushairi si kwa ajili ya Waislamu tu bali unafaa pia kupitisha maudhui ya Kikristo na kipindi hicho washairi Wakristo walikuwa Mnyampala na Nyerere. Vilevile, kuna mashairi ya Mnyampala yanayohusu dini ya Kikristo na Kiislamu yanajitokeza vyema katika *Diwani ya Mnyampala* (taz. 3.2.1.4). Pia uhusiano wa Mnyampala na dini nyingine unaelezwa vyema katika historia ya maisha ya mwandishi (taz. 1.1.1.3).

Aidha, katika mswada wa *Fasili Johari ya Kiswahili*, Mnyampala (1959) anatoa maelezo yanayohusiana na matumizi ya ushairi katika maandishi matakatifu. Hii inatuthibitishia kuwa Mnyampala alisoma na kuelewa vizuri maandishi matakatifu, aliweza kugundua sehemu mbalimbali za *Biblia Takatifu* na *Kurani Tukufu* zinazozingatia kanuni ya arudhi ya ushairi. Kwa ujumla Mnyampala alikuwa mshairi mdadisi ndio maana aliweza kutambua jinsi ushairi ulivyotumika katika *Biblia Takatifu* na *Kurani Tukufu*. Mfano, katika (uk. 3) wa mswada wa *Fasili Johari ya Kiswahili*, anaeleza kuwa:

157. Yumkini hapana cha kupungua juu ya kusudi la kuheshimu kazi ya mashairi na watunzi wenyewe. Utunzi au wimbaji wake haukuachwa, na matumizi ya mashairi yaliendelea kukua zaidi na zaidi kwa kufuata

ushairi kuwa ni zana za shughuli za mahubiri ya dini. Hivyo mashairi yalitumiwa pia katika enzi za maagano mapya.

Kutokana na maelezo hayo Mnyampala alikuwa akizungumzia mahubiri na mafunzo ya dini zote katika ushairi wa Kiswahili, bila kujali tofauti za dini.

Aidha, umoja wa watunzi unajibainisha hata katika kitabu cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* ambapo waandishi wa dini mbalimbali walionyesha kushirikiana bila hata ya kuzingatia tofauti zao za kidini. Hivyo Mnyampala na watunzi wengine walikuwa na umoja bila kujali tofauti za kidini zao; walizingatia usawa wa binadamu na kuheshimu dini ya kila mmoja. Mashairi ya Mnyampala yalihubiri upendo wa Mungu kwa watu wote.

Washairi wengine Wakristo waliotunga mashairi yenye maudhui ya dini ya Kikristo ni Nyerere. Nyerere ni mshairi Mkristo aliyetunga tenzi tano, ambazo ni *Injili ya Matayo* (1996), *Injili ya Yohana* (1996), *Injili ya Marko* (1996), *Injili ya Luka* (1996) na *Utenzi wa Matendo ya Mitume* (1996) (taz. Samandito, 2012). Kwa ujumla tungo hizo zilieleza maisha ya Yesu na mafundisho yake hapa duniani kama ilivyokuwa katika tungo za Mnyampala hususani *Utenzi wa Injili* (1966). Washairi wengine ambao ni Wakristo katika ushairi wa Kiswahili walioibuka baadaye, hususani wanausasa, ni Euphrase Kezilahabi, Ken Walibora na Kithaka wa Mberia.

## 5.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia lengo la tatu ambalo linahusu mchango wa Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Mchango wake unapatikana katika mtindo, muundo, matumizi ya lugha na ukusanyaji wa mashairi mbalimbali ya waandishi wengine. Kadhalika, Mnyampala alikuza nadharia ya ushairi wa Kiswahili na kuingiza maudhui ya dini ya Kikristo katika ushairi huo. Vipengele hivyo vyote vina

mchango mkubwa katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Mnyampala alikuwa anapenda mabadiliko katika sanaa ya ushairi na hii ndiyo maana alikuwa anajaribu kuibua mitindo na miundo mipya ya utunzi wa ushairi wakati wa uhai wake. Japo Mnyampala alithamini matumizi ya arudhi katika utunzi wa mashairi, alitambua umuhimu wa mabadiliko katika sanaa hii. Hivyo, mbinu zilizotumiwa na Mnyampala katika utunzi wake zinatumiwa hadi sasa. Ijapokuwa kwa sasa zinatumiwa katika mtindo mpya kutokana na mabadiliko ya jamii ili kuendana na mabadiliko yaliyoko katika jamii. Hivyo, mchango wake katika ushairi wa Kiswahili hauna kifani. Sura inayofuata inahusu matokeo, mahitimisho na mapendekezo.

## SURA YA SITA

### MATOKEO, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 6.0 Utangulizi

Sura hii ni hitimisho ya utafiti huu uliochunguza mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Katika sura hii kuna muhtasari wa tasnifu kwa kurejelea kila sura, matokeo ya utafiti na mahitimisho ya utafiti huu. Imejadili pia mapendekezo ya utafiti yanayotokana na malengo yaliyoshughulikiwa.

#### 6.1 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu umechunguza mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Katika kutimiza azma hiyo, tumechunguza kazi sita za ushairi, zilizochapishwa na zisizochapishwa. Kazi hizo ni *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965), *Ngonjera za UKUTA Na. 1* (1970), *Hazina ya Washairi, Mashairi ya Vidato na Mahadhi ya Kiswahili*. Aidha, *Ngonjera za UKUTA Na. 2* na vitabu vingine vya ushairi wa Mnyampala vimetumika pale ilipobidi kusherehesha hoja husika.

Sura ya kwanza inaangazia misingi ya utafiti huu. Katika sura hii mambo yaliyojadiliwa ni pamoja na usuli wa suala la utafiti. Katika usuli huo tumeeleza historia ya mwandishi kutokana na data tulizokusanya nyanjani na maktabani. Vilevile, tumeeleza suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti. Masuala mengine yaliyojadiliwa katika sura hii ya kwanza ni mbinu za utafiti, vifaa vya utafiti na hatimaye uchanganuzi wa data.

Sura ya pili inahusu mapitio ya maandishi na misingi ya nadharia. Katika sura hii tumepitia baadhi ya maandishi yanayoeleza ushairi wa Kiswahili na historia yake.



Kadhalika, kuna maandishi yanayohusu muktadha katika ushairi na yaliyoandikwa kuhusu tungo za Mathias Mnyampala. Katika kufanya hivyo nilibaini pengo la utafiti ambalo halikushughulikiwa na tafiti zilizotangulia. Pengo hilo ni kuwa mchango wa Mathias Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili haukushughulikiwa kikamilifu na tafiti tangulizi. Katika sehemu ya mwisho ya sura hiyo ya pili, nimejadili misingi ya Nadharia ya Mwingilianomatini, nadharia ambayo iliniongoza katika kufikia malengo na maswali ya utafiti huu. Katika sura ya tatu, nne na ya tano nilijikita katika uchanganuzi wa data.

Sura ya tatu imejadili lengo la kwanza ambalo linahusu muktadha uliomsukuma Mnyampala kutunga kazi zake za ushairi wa Kiswahili. Katika sura hii, tumefafanua miktadha ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kimwingilianomatini ilivyoathiri utunzi wa kazi za Mathias Mnyampala. Sura ya nne, imeshughulikia mbinu za kifani zilizotumika kuibua maudhui mbalimbali katika kazi teule za ushairi wa Mathias Mnyampala. Katika sura hii kwa upande wa maudhui tulijikita katika kuangazia dhamira na ujumbe.

Sura ya tano, imejadili mchango wa Mathias Mnyampala katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili. Mambo yaliyozingatiwa katika kuleta mchango huo ni mitindo, muundo, matumizi ya lugha, ukusanyaji mashairi mbalimbali, kukuza nadharia ya ushairi na kuingiza maudhui ya dini katika ushairi wa Kiswahili. Hivyo, katika sura hii tumeweza kujenga mjadala kuhusu mchango wa kazi za ushairi wa Mathias Mnyampala katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili kwa kuhusisha na kazi nyingine za karne ya ishirini na za ishirini na moja. Sura ya sita ndiyo mwisho wa tasnifu hii na imeshughulikia muhtasari, matokeo, mahitimisho na mapendekezo.

## 6.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu uliohusu mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili ulikuwa na matokeo kadha wa kadha. Mathalani, kuhusu muktadha uliomsukuma Mnyampala kuandika tungo zake, utafiti huu ulibaini kwamba, ni vigumu kumtenga Mnyampala na muktadha wake wa uandishi pamoja na mazingira yaliyomlea na kumkuza mtunzi huyo. Ni wazi kuwa kazi ya fasihi inatokana na fasihi yenyewe pamoja na mazingira yaliyomlea na kumkuza. Utafiti huu ulibaini kuwa kupitia muktadha wa kijamii, kisiasa, kiuchumi na kimwingilianomatini ndimo kazi za Mathias Mnyampala zimeibuliwa.

Kuhusu mbinu zilizotumika kuibua maudhui katika kazi teule za Mnyampala imebainika kwamba, Mnyampala alikuwa na uwezo mkubwa wa kutumia maneno ya lugha ya Kiswahili na mbinu mbalimbali za utunzi ili kuboresha na kupamba ushairi wa Kiswahili. Pia, alikuwa mdadisi na mbunifu, aliyependa taaluma ya ushairi iendeleo mbele zaidi. Jitihada za makusudi alizifanya Mathias Mnyampala kuhakikisha kuwa taaluma hii inaendelea. Isitoshe, utafiti huu uligundua kuwa mbinu za kifani zilizotumika katika kuibua maudhui ya kazi teule zinaingiliana, zinategemeana na kukamilishana. Vilevile katika baadhi ya mashairi, mwandishi ametumia mbinu zaidi ya moja kuibua maudhui yaliyomo ndani ya shairi husika. Kwa mfano katika *Diwani ya Mnyampala*, shairi la ‘Taa Mitaa Hung’aa’ (uk. 81) ubeti wa kwanza mwandishi ametumia mbinu mbili kwa wakati mmoja, yaani taswira ya taa, na takriri neno “taa” kuisitiza maudhui yaliyomo ndani ya shairi husika. Pia shairi la ‘Wakati Titi la Nyati’ (uk.78), kibwagizo cha shairi hilo kisemacho ‘wakati titi la nyati hukamuliwa kwa shaka’ imetumika kama methali na taswira kwa wakati mmoja. Kwa ujumla, mbinu za taswira, methali, misemo, ushairi-drama na nyimbo zimetumiwa na mwandishi huyu kuibua maudhui mbalimbali katika kazi zake teule za ushairi wa

Kiswahili na nyinginezo. Kwa njia hii, tungo zake zimekuwa ghala ya tanzu hizo za kifasihi simulizi.

Kwa upande wa maudhui, imebainika kuwa Mnyampala aliangazia ujumbe na dhamira kadha wa kadha katika mashairi yake. Baadhi ya dhamira hizo ni uzalendo, mapenzi na ndoa, malezi, uzazi, haki ya mwanamke, utunzi, umuhimu wa Kiswahili, masuala ya utamaduni wa Kiafrika na umuhimu wake, masuala ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea pamoja na Azimio la Arusha. Maudhui hayo ni dhahiri kwamba yamesadifu na kuakisi hali halisi ya mazingira yaliyokuwepo kabla na wakati wa miaka 1960 katika jamii zetu, pia kwa kiasi fulani yameweza kuakisi hali halisi iliyopo sasa. Mnyampala anatoa ujumbe kwa kuiasa na kuionya jamii yake kufanya kazi kwa bidii, kuwa waangalifu katika maisha na kuishi maisha ya upendo, ushirikiano, umoja na usawa katika jamii ili kuweza kuistawisha jamii na kujenga taifa lao. Aidha, kupitia kazi za Mnyampala tunajifunza historia ya taifa la Tanzania na jamii yake kwa ujumla.

Katika kutathimini mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili, tumebaini kwamba, kazi za ushairi za Mathias Mnyampala zina mchango mkubwa katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Kwa mfano katika kipengele cha mtindo, Mnyampala aliibua mitindo mbalimbali kama vile msisitizo na mtiririko. Mtindo wa mtiririko umeendelea kutumiwa na waandishi wengine waliofuata mfano Asha Kunemah (2008). Vilevile, mwandishi huyu aliweza kufufua na kuhisha baadhi ya mbinu ambazo zilitumika hapo awali na kuzifanya mpya. Mbinu hizo ni ngonjera na mashairi ya vidato. Aidha, mchango wake katika mashairi ya ngonjera hautasahaulika katika tasnia hii. Kupitia kwa utafiti huu tumebaini kuwa Mathias Mnyampala ni mwanzilishi wa neno ngonjera. Ijapokuwa utungo wa namna hiyo

ulikuwepo tangu zamani, Mnyampala ndiye aliyehuisa utungo huo uliokuwepo katika jamii mbalimbali za Kiafrika na kuufanya kuwa wa kimaigizo. Kwa ujumla, Mnyampala alieneza ngonjera na alizitumia katika muundo mpya zaidi unaoweza kuigizika.

Hivyo, madai kwamba Mnyampala ni mwanzilishi wa ngonjera si ya kweli. Ila ifahamike kuwa Mnyampala aliutumia utungo huu miaka ya 1960 ili kueneza siasa za Ujamaa na Kujitegemea ambayo misingi yake ilikuwa kwenye siasa za Azimio la Arusha. Kadhalika utungo huu uliendelea kutumika miaka ya 1970, kwa lengo la kuwasifu viongozi wa siasa na kutolea mafunzo mbalimbali katika jamii. Ngonjera zilitumika kama burudani zenye ujumbe ndani yake katika sikukuu mbalimbali za kitaifa kama vile sikukuu za uhuru, muungano, wafanyakazi, wakulima na katika shughuli nyinginezo za kijamii na kisiasa.

Zaidi ya hayo, kupitia kwa utafiti huu tumeweza kubaini kuwa Mnyampala si mwasisi wa mashairi ya vidato kama mwanawe Charles Mnyampala alivyoeleza katika kitabu cha *Maisha ni Kugharimia* (2014). Katika utafiti huu tumeweza kugundua kuwa mtindo wa mashairi ya vidato ulikuwepo na ulitumiwa na washairi wengine wa mwanzo ambapo mfano mzuri ni katika *Diwani ya Muyaka*. Hivyo basi mchango wa Mnyampala ni katika kutoa kisawe (jina la vidato) cha mashairi hayo. Hivyo, Mnyampala alikuwa wa kwanza kutumia istilahi ya “mashairi ya vidato” ambapo watunzi wa awali hawakutambulisha mtindo huo kwa istilahi maalum. Aidha, waandishi waliotangulia walitumia mbinu hiyo bila ya kuweka kisawe chochote. Mnyampala aliweza kutumia mtindo wa mashairi hayo na kuyabatiza kwa jina la ‘vidato’.

Sambamba na hilo, katika utafiti huu tumebaini kuwa Mnyampala amechangia sana katika kukuza nadharia ya kimapokeo kwa kuitumia katika utunzi wa mashairi yake, ambapo alikuwa anasisitiza upekee wa shairi la Kiswahili kimtindo na kimuundo hasa urari wa vina na mizani. Katika kufanya hivyo aliweza kutoa maana ya ushairi, aina za ushairi, kanuni za utunzi wa mashairi ambazo zinaingiliana kwa namna fulani na sheria za ushairi za Amri Abedi, katika diwani yake ya *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Mnyampala pia alikuwa msitari wa mbele katika kukuza sana ya ushairi wa Kiswahili kwa kuibua msamiati mbalimbali kutoka katika Kiswahili cha kale na lugha za Kibantu mfano ‘ngonjera’, wavyele, kitung’ati, vidato na mengineyo yaliyoibuliwa naye. Kadhalika, mtaalam huyu aliweza kukusanya mashairi mbalimbali kutoka katika magazeti mbalimbali na kuyaweka katika kitabu kimoja kilichoitwa *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi na Hazina ya Washairi* kwa lengo la kuhifadhi na kutunza mashairi kwa manufaa ya vizazi vijavyo. Vilevile aliweza kukusanya nyimbo za watoto, vijana, kubembeleza watoto, mapenzi na ndoa, harusini na kuziweka katika andiko moja aliloliita *Mahadhi ya Kiswahili*.

Mnyampala akiwa mshairi Mkristo wa kwanza katika taaluma ya ushairi wa Kiswahili aliuthibitishia umma kuwa ushairi wa Kiswahili si kwa ajili ya washairi Waislamu tu, bali ni kwa kila mtu. Hivyo, alibainisha hayo kwa kutunga mashairi na tenzi zilizohusu dini ya Kikristo ili kuthibitisha hoja hiyo. Mfano mzuri ni *Utenzi wa Injili* na *Utenzi wa Zaburi* pamoja na mashairi mengine mbalimbali yaliyoandikwa kwenye vitabu vyake vya ushairi wa Kiswahili yaliyohusu dini ya Kikristo (rejea 3.2.1.4 na 5.6).

Hivyo basi, matokeo yaliyojadiliwa hapa yanadhihirisha kwamba Mathias Mnyampala ni miongoni mwa waandishi mashuhuri katika uga wa ushairi na fasihi ya Kiswahili. Mnyampala alitunga mashairi mbalimbali kwa kutumia mitindo na miundo

mbalimbali ya ushairi wa Kiswahili kama tulivyoeleza awali. Hivyo, anajipambanua kama gwiji katika ushairi wa Kiswahili na jabali lililopaswa kuzingatiwa katika kutathmini maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

### **6.3 Mahitimisho**

Mintaarafu ya mijadala na uchanganuzi ulioendelezwa katika tasnifu hii, imebainika kwamba mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kwa kujikita katika kazi teule sita zilizochapishwa na zisizochapishwa hauna kifani. Ni dhahiri kuwa Mathias Mnyampala amechangia pakubwa katika kutoa maana ya ushairi, aina zake na sifa za ushairi wa Kiswahili.

Kadhalika ilibainika kuwa Mnyampala alisaidia katika kukuza lugha na ushairi wa Kiswahili kwa kuibua msamiati mbalimbali pamoja na kufufua na kubuni mbinu mbalimbali za utunzi wa mashairi yake. Kwa upande wa mbinu za utunzi wa mashairi ilibainika kuwa, Mnyampala alianzisha utunzi wa mashairi ya msisitizo na mtiririko. Pia alifufua mitindo na miundo mbalimbali katika ushairi wa Kiswahili kama vile mashairi ya vidato na ngonjera. Kwa upande wa ngonjera aliufanya ushairi wa majibizano (ngonjera) kuwa wa kimaigizo unaoweza kutendeka jukwaani ambapo wahusika hupokezana kauli za shairi hilohilo moja mbele ya hadhira. Hii inatoa changamoto kwa waandishi kuandika kazi zenye kulenga kukuza na kuendeleza ushairi, fasihi na Kiswahili kwa kuwa wabunifu na kuibua misamiati pamoja na mitindo mbalimbali inayoweza kutumika katika Kiswahili.

Kupitia utafiti huu, tulibaini miswada, barua na nyaraka mbalimbali ambazo aliziandika Mnyampala enzi za uhai wake. Kwa hakika, miswada hiyo ni malighafi ya tafiti za kifasihi na machapisho ya kitaaluma. Aidha, utafiti huu ulidhihirisha kuwa Mnyampala hakuandika mashairi tu, bali aliandika pia nathari, hadithi fupi na kazi

nyingine zilizohusu mila na desturi za Wagogo. Kupitia utafiti huu ni matumaini yetu kuwa wasomaji wa tasnifu hii wataanza kumtazama Mnyampala kwa mapana zaidi ya vile walivyokuwa wakimwona hapo mwanzo na kwamba kumbe yeye si mshairi tu, bali ni mwananathari na mtamaduni pia.

Utafiti huu ulibainisha matumizi ya mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini. Mihimili inayosisitiza kwamba hakuna kazi ya fasihi inayoweza kujitegemea pasipo na kutegemea matini nyingine tangulizi ili kuibua maana ya matini husika. Kupitia kwa nadharia hii imebainika kuwa muktadha wa utunzi wa kazi za ushairi za Mnyampala unaingiliana na muktadha uliokuwepo kabla ya uhuru, kipindi cha uhuru na sera zilizokuwepo baada ya uhuru zilizochangia kazi husika kuibuka. Pia, imedhihirika kuwa kuna mwingiliano wa tanzu za fasihi simulizi na mbinu za kifani zilizotumia. Kadhalika, kuna mwingiliano wa maudhui pamoja na mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

Kwa ujumla, mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili ni mkubwa na mchango huo umejidhihirisha kwa namna ya pekee kupitia mbinu za kifani, dhamira, ujumbe na muktadha. Katika utafiti huu, yapo mambo mengi ya msingi ambayo yameibuliwa wakati wa mchakato mzima wa ukamilishaji wa utafiti huu. Mambo haya yanahusu kazi za Mnyampala na uhifadhi wake.

### 6.3.1 Uhifadhi wa Kazi na Nyaraka za Mnyampala

Utafiti huu umebaini kuwa uhifadhi wa kazi za Mnyampala pamoja na nyaraka zake hauridhishi. Kwa kawaida kazi za kisanaa ikiwemo fasihi, ili ziweze kudumu kwa muda mrefu ni lazima kutunzwa vizuri. Kazi hizo zinaweza kutunzwa katika maktaba au kanzi maalum inayoweza kukusanya kazi mbalimbali za wasanii au watunzi na kuzihifadhi ili zitumike pale zitakapohitajika. Kazi za Mnyampala zimehifadhiwa

katika mazingira yasiyoridhisha. Jambo la kusikitisha ni kwamba, kuna baadhi ya nyaraka zilizotoweka na zingine zimeliwa na panya kutokana na mazingira duni ya uhifadhi wake. Ifuatayo ni picha inayoonyesha namna kazi zake zilivyohifadhiwa.



**Picha namba 5: Vifaa vinavyotumika kuhifadhi nyaraka za Mathias Mnyampala (tarehe 3/11/2016).**

#### **6.4 Mapendekezo ya Mtafiti**

Mtafiti anapendekeza kuwa wanataaluma pamoja na wadau mbalimbali wa elimu wawe na mikakati ya makusudi ya kuwaenzi na kuwakumbuka wataalamu mbalimbali waliosaidia kukuza na kueneza fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu umebaini kuwa Mathias Mnyampala aliandika kazi nyingi za Kiswahili na kati ya hizo nyingi bado hazijachapishwa<sup>52</sup>.

Kutokana na umuhimu wa kazi zilizoandikwa na Mathias Mnyampala, mtafiti anapendekeza viongozi wa mkoa wa Dodoma, wakishirikiana na jamaa wa karibu wa

<sup>52</sup> Katika mahojiano ya tarehe 27/11/2016 na mtafiti, familia ya Mnyampala ilikiri waziwazi kuwepo kwa kazi nyingi zisizochapishwa zinazotunzwa nyumbani kwa marehemu mwanaye Charles Mnyampala. Majina ya kazi ambazo hazijachapishwa zimeambatishwa kwenye tasnifu hii.



Mnyampala wachapishe kazi zake ambazo hazijachapishwa ili kuwezesha watafiti kuzifanyia utafiti na kubaini mchango wake katika tanzu nyingine za fasihi na taaluma ya Kiswahili. Pia, Uongozi wa mkoa wa Dodoma utenge sehemu (chumba) maalum katika maktaba ya mkoa ili kuhifadhi kazi za Mathias Mnyampala. Kufanya hivi kutatoa nafasi kwa watu kuzisoma na kuongeza maarifa yatokanayo na kazi hizo. Uongozi wa mkoa unahusika kwa sababu Mnyampala alikuwa mzaliwa wa mkoa huo na alikuwa mstari wa mbele kuandika kazi za kitaaluma na zile zilizohusu jamii na utamaduni wa Kigogo.

Vilevile, kuwepo na mikakati ya kimakusudi ya kutambua waasisi na mashujaa waliosaidia kuinua taaluma ya Kiswahili na ushairi kitaifa, kama kilivyofanya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa kuanzisha kozi inayohusu wataalamu walioandika ushairi wa Kiswahili. Aidha, kuwepo na uhamasishwaji wa wanataaluma kufanya tafiti mbalimbali zinazohusu mashujaa wa lugha adhimu ya Kiswahili, kwa fursa hiyo mambo mbalimbali yaliyofanywa na mabingwa hao ambayo hayajulikani yanaweza yakaibuliwa na kuchangia maendeleo na kukuza taaluma ya fasihi na Kiswahili kwa ujumla. Asasi za kitaaluma ziwe na mipango na mikakati mahususi ya kufanya utafiti ili kuibaini endapo kuna miswada ya wataalamu wakongwe walioaga dunia ili ichapishwe kwa manufaa ya kitaaluma.

Asasi hizo zifanye juhudi ya kuichapisha miswada ya wataalamu hao kwa manufaa ya kizazi kilichopo, kijacho pamoja na kuzipatia familia zao kipato. Kwa hiyo, ili kuwaenzi wataalamu hawa ni vyema mitaala ya elimu kuweka kipengele kinachohusu wataalamu waliochangia kukuza lugha ya Kiswahili kupitia utunzi wa kazi zao mbalimbali. Hii itasaidia wanafunzi kuwajua wataalamu mbalimbali na kujenga uzalendo wa kukuza lugha ya Kiswahili na kuipenda lugha yao. Vilevile, serikali

inatakiwa kuweka siku maalum kitaifa ya kuwaenzi wataalamu wa Kiswahili waliosaidia kukuza lugha ya Kiswahili na fasihi kwa ujumla.

### **6.5 Mapendekezo kuhusu Tafiti za Baadaye**

Utafiti huu ulilenga zaidi kuchunguza na kuchambua mwingilianomatini wa ushairi wa Mnyampala kwa kujikita zaidi katika mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Na kupambanua muktadha wa utunzi na mbinu tano za kifani ambazo ni taswira, methali, misemo, ushairi-drama na nyimbo zilivyochangia kuibua maudhui katika kazi teule za ushairi za Mathias Mnyampala. Bila shaka uchambuzi huu umekuza ufahamu na uelewa kuhusu Mnyampala na kazi zake na kuleta mwanga mzuri wa kuwaangazia wataalam wengine. Hata hivyo tasnifu hii imejadili mwingilianomatini na mchango wa ushairi wa Mathias Mnyampala katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili kupitia kazi zake teule. Kwa ujumla kazi hii ni ya kwanza ambayo imeweza kuchunguza mwingilianomatini wa ushairi wa Mathias Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili.

Aidha, ni bayana katika kazi za ushairi za Mathias Mnyampala kuna mbinu nyingi zilizotumika kuibua maudhui mbalimbali katika kazi zake. Hivyo basi kuna haja ya kuendeleza utafiti zaidi katika maeneo mengine ambayo hayakuangaziwa katika utafiti huu, kama vile mbinu nyingine ambazo hazikuchunguzwa katika utafiti huu kwa mfano tamathali za semi, jazanda, vitendawili, mbinu za uandishi, kimuundo na nyinginezo. Aidha, katika utafiti huu tumejikita zaidi kuangazia kazi za ushairi zilizoandikwa na Mnyampala hivyo hatukujikita katika kuangazia kazi zingine kama vile nathari na hadithi fupi. Hivyo, watafiti wanaweza kufanya utafiti kuhusiana na kazi zake nyingine za kinathari na hadithi fupi ili kubaini mchango wake katika tungo hizo na fasihi kwa ujumla. Pia wanaweza kuangalia masuala yahasuyo falsafa na

itikadi za mwandishi katika kazi zake. Vilevile, kuna nyaraka mbalimbali kama vile barua na vitabu vinavyohusu simulizi mbalimbali, watafiti wajaribu kufuatilia nyaraka hizo ili kuchunguza endapo zina mchango katika taaluma ya Kiswahili.

## MAREJELEO

- Abedi, A. (1983). (toleo la kwanza 1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Abdulaziz, M. H. (1969). "Maisha ya Mathias Mnyampala" *Swahili*. Vol. 39/1- 2: 1-9. Dar es Salaam: TUKI.
- \_\_\_\_\_(1979). *Muyaka: 19<sup>th</sup> Century Popular Swahili Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Alfaro, M. J. M. (1996). "Intertextuality: origin and development of the concept." Katika *Atlantis AEDEAN*: 268-285
- Ali, A. E. (2014). "[Kutathmini Nafasi ya Mwanamke Katika Mashairi ya Kiswahili: Uchunguzi wa Mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala.](#)" Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu Huria Tanzania (Haijachapishwa).
- Allen, G. (2000). *Intertextuality*. London: Fontana.
- Amuka, P. S. (1992). "The Place of Deconstruction in the Speech of Africa: The Role of *Pakrouk* and *Ngero* in Telling Culture of Dholuo." Katika *Reflections on Theories and Methods in Oral Literature*. Nairobi: KOLA.
- Babbie, E. (1992). *The Practice of Social Research*. California: Wadsworth Publishing Company.
- Bakhtin, M. M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Ed. Michael Holquist Trens. Garyl Emerson and Michael Holquist. Austin and London: University of Texas Press.
- \_\_\_\_\_(1986). *Speech Genres and Other Late Essays*. Austin: University of Texas Press.
- Barmford, S. (2011). "Only Connect?: Aspects of Intertextuality in Zadie Smith's on Beauty." Tasnifu ya uzamili. University of Helsinki. (Haijachapishwa).
- Barthes, R. (1977). *Image Music Text*. London: Fontana.
- Bauman, R. (2004). *Cross-Cultural Perspectives on Intertextuality*. Oxford: Blackwell Publishing Ltd.
- Biersteker, A. (1996). *Kujibizana: Questions of Language and Power in Nineteenth and Twentieth-Century in Kiswahili*. Michigan: Michigan State University Press.
- Chiraghadin, S. (1970). "Utangulizi wa Mhariri" *Malenga wa Mvita*. Nairobi: Oxford University Press.

- Chiraghdin, S., Nabhany, S.A., na Baruwa, A. (1975). "Tarehe ya Ushairi wa Kiswahili." Wah. A. Abdala na T.S.Y. Sengo katika *Mulika Na. 7*: 59-67. Dar es Salaam: TUKI.
- Chiraghdin, S., na Mnyampala, M. E. (1974). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.
- Clayton, J., na Rothstein, E. (1991). *The Influence of Intertextuality in Literary History*. Wisconsin: The University of Wisconsin Press.
- Cohen, L., na Lawrence, M. (2000). *Research Methods in Education*. London: Routledge Press.
- De Saussure, F. (1916). *A Course for General Linguistics*. New York: Mc Graw Hill.
- Eliot, T. S. (1988). "Tradition and the Individual Talent" (1919). Katika *The Theory of Criticism: From Plato to the Present*: 408-410. Mhariri Raman Selden. Longman Group UK Limited: England.
- Friedrich, P. (1986). *The Princes of Naranja: An Essay in Anthrohistorical Method*. Austin: University of Texas Press.
- Frolova, N. (2008). "Mazungumuzo ya Washairi wa Kimapokeo na wa Kisasa: Mabishano au Majadiliano? Katika, *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.
- Gay, L. R., na Wenzake (2006). *Education Research: Competencies for Analysis and Application*. New Jersey: Person Merrill Prentise Hall.
- Gibbe, A. G. (1978). "Mathias Mnyampala: Mshairi Maarufu." *Mulika Na. 13*. Dar es Salaam: TUKI.
- \_\_\_\_\_ (1994). "Inkishafi: Uhakiki wa Kidayakronia." Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Idara ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Moi. (Haijchapishwa).
- Genette, G. (1997). *Palimpsests: Literature in the Second Degree*. University of Nebraska Press: Lincoln & London.
- Harries, L. (1962). *Swahili Poetry*. London: Oxford University Press.
- \_\_\_\_\_ (1972). "Poetry and Political in Tanzania." Katika *Ba Shiru 4*: 52-54.
- Hichens, W. (Mh.) (1940). *Diwani ya Muyaka*. Johannesburg: University of Witwatersand.
- Hirsch, E. D. Jr (1960). *Objective Interpretation*. USA: PMLA. (1976). *The Aims of Interpretation*. Chicago: Chicago University Press.
- Holman, H., na Harmon, W. (1986). *A Handbook to Literature* (5<sup>th</sup> Edition). New York: Macmillan

- Hussein, E. (1983). "Hatua mbalimbali za Kubuni na Kutunga Tamthilia Kufuatana na Misingi ya Ki-Aristotle." Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Indede, F. N. (2008). "Mabadiliko katika Umbo la Ushairi na Athari zake katika Ushairi wa Kiswahili. Katika, *Swahili Forum*, Na 15: 73-94.
- Irwin, W. (2004). "Against Intertextuality." Katika *Philosophy and literature*. Vol. 28: 227-242.
- Issa, I. (2013). "Usawiri wa Mhusika Mwanamke katika Ushairi wa Mathias Mnyampala: Mifano kutoka *Diwani ya Mnyampala (1965) na Waadhi wa Ushairi (1965)*." Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Jonker, J., na Pennink, B. (2010). *The Essence of Research Methodology*. Berlin: Heidelberg Springer-Verlag Publishers.
- Kawawa, R. M. (1970). "Utangulizi" wa *Ngonjera za UKUTA Na. 1*. Dar es Salaam. Oxford University Press.
- Kehinde, A. (2003). "Intertextuality and Contemporary African Novel." *Nordic Journal of African Studies*. Juzuu la 12: 372-386.
- Kernell, S., Jacobson, G. C., Kousser, T., na Vavreck, L. (2014). *The Logic of American Politics*, 6th edition. Sage Publications, CQ Press. p.3. katika "What Is Politics?" <http://collegeamericangovernment.org/What%20Is%20Politics.pdf> 19/05/2018
- Kezilahabi, E. (1973). "The Development of Swahili Poetry, 18<sup>th</sup> -20<sup>th</sup> C." Katika *Swahili Vol. 42/2*. Dar es Salaam: TUKI.
- \_\_\_\_\_ (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
- \_\_\_\_\_ (1983). "Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili." Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Khatib, M. S. (2011). "Chanjo za Matakwa ya Mwanamume katika Mwili wa Mwanamke: Ulinganisho wa Mashairi ya Muyaka bin Haji na Shaaban Robert." Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Kihore, M. Y. (1978). "Waadhi wa Ushairi." Wah. L. N. Honero na T. S. Y. Sengo katika *Mulika Na. 12*: 54-59. Dar es Salaam: TUKI.
- Kijumwa, M. (1913). *Utenzi wa Fumo Liyongo katika Tenzi Tatu za Kale* (mh. M. M. Mulokozi). Dar es Salaam: TUKI.
- Kimani, R. (1983). "Suala la Ushairi wa Kiswahili." Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

- King'ei, K. (1987). "Usanifu wa Lugha katika Maandishi ya E. Hussein." Katika *Mulika Na. 19*: 19-35. Dar es Salaam: TUKI.
- King'ei, K., na Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
- King'ei, K., na Ndalau, A. (2008). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: East African Education Publishers.
- Kitogo, S. A. (2002). "The Poet's Contribution to Political Development: A Case study of Abdu Kandoro." Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Knappert, I. J. (1974). "The Appreciation of Swahili Poetry." Katika Swahili Vol. 44/2. Dar es Salaam: TUKI.
- \_\_\_\_\_ (1979). *Four Centuries of Swahili Verse*. London: Heinemann.
- Komba, J. J. (1969). "Mtumishi Wetu Mnyampala" *Jarida la Kiswahili* Vol. 39/1 na 2. Dar es Salaam: TUKI.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishers.
- Koul, L. (2006). *Methodology of Educational Research*. New Delhi: VEKAS Publishing House.
- Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art*. New York: Columbia Press.
- Kristeva, J. (1986). 'Word, Dialogue and Novel'. In: Toril Moi, ed. *The Kristeva Reader*. Oxford: Blackwell, 35–61.
- Kunemah, A. S. (2008). *Misemo na Methali katika Ushairi*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kyamba, A.N. (2016). "Muundo wa Diwani ya Mnyampala (1965) Na Nafasi Yake Katika Kuibua Maudhui." Katika *Kioo cha Lugha, Juz. 14*. Dar es Salaam: TUKI.
- Lambert, E. H. (1966). "Waadhi wa Ushairi." *Swahili* Vol. 36/2: 190-191. Dar es Salaam: TUKI.
- Lasswell, H. 1936/1951. "Politics: Who Gets What, When, and How." *Meridian Books*. p.13. <http://collegeamericangovernment.org/What%20Is%20Politics.pdf> 19/05/2018.
- Ligami, P., na Busara, S. (2001). "Tahakiki ya Methali za Kiswahili." Katika Njogu, K., Momanyi, C., na Mathooko, M. (wah.) *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communication.
- Mberia, K. (2005). *Radio na Mwezi*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

- \_\_\_\_\_ (2007). *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.
- \_\_\_\_\_ (2007). *Msimu wa Tisa*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.
- Madumulla, J. S. (1988). "Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka." Katika *Kiswahili* 55/1 & 55/2: 182-195. Dar es Salaam: TUKI.
- \_\_\_\_\_ (1995). *Proverbs and Sayings: Theory and Practice*. Dar es Salaam: TUKI.
- \_\_\_\_\_ (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Historia, Nadharia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd na Nairobi Phoenix Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2011). "Mathias Mnyampala: Jabali Lililosahaulika." Makala iliyowasiliswa katika kumbukizi ya Amri Abedi na Mathias Mnyampala (Karimjee, Dar es Salaam). Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Maitaria, J. N. (2011). "Methali kama Fomula katika Utunzi na Uwasilishaji wa Ushairi wa Kiswahili. Mfano wa Mashairi ya Abdilatif Abdalla. Makala ya Semina katika Idara ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- \_\_\_\_\_ (2017). "Ushairi kama Chombo cha Kuhifadhi na Kuelimisha Jamii kuhusu Utamaduni: Mfano wa Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali. Katika *Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja*: 131-146. Eldoret: Moi University Press
- Makaka, E. E. (2012). "Mathias Mnyampala: A Multifaceted Personality." Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Massamba, D. P. B. (1983). "Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili." *Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili: Fasihi Na. III*: 55-95. Dar es Salaam: TUKI.
- Masungwa, S. T. (2012). "Taswira na Ishara katika Ushairi wa Mathias E. Mnyampala." Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Mayoka, J. M. (1977). "Vina na Mizani ni Uti wa Mgongo wa Ushairi wa Kiswahili." Katika *Mulika Na. 9*: 3-12. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbogo, E. (2011). *Sundiata*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Mbiti, J. (1969). *African Religion and Philosophy*. New York: Praeger Publishers.
- Mbogo, E. (2009). *Fumo Liyongo*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.



- Mgute, W. (2012). Mchango wa Mathias Mnyampala katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Mihale, K. P. (2011). "Ujumi katika Ushairi wa Mnyampala." Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Mlacha, S. A. K. (1981). "Methali kama Chombo Muhimu katika Jamii." Katika *Makala za Semina ya Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam:TUKI.
- \_\_\_\_\_ (1985). "Dhima ya Methali katika Malezi." Katika Jarida la *Kiswahili Vol. 52/1 & 52/2*: 175-186. Dar es Salaam: TUKI
- Mlama (Muhando), P. O. (1983). "Hali ya Sanaa za Maonyesho Tanzania." Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mligo, E. S. (2012) *Jifunze Utafiti: Mwongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenyeMantiki*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGYS).
- Mmbaga, N. O. (1981). "Ngonjera za Kiswahili." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).
- Mnyampala, M. (1954). *Historia, Mila na Desturi za Wagogo*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Mnyampala, M. (1959). *Fasili Johari ya Mashairi*. Dar es Salaam: East African Swahili Committee.
- \_\_\_\_\_ (1961). *Kisa cha Mrina Asali na Wenzake Wawili*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- \_\_\_\_\_ (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- \_\_\_\_\_ (1965). *Waadhi wa Ushairi*. Dar es Salaam. Oxford University Press.
- \_\_\_\_\_ (1966). *Utenzi wa Injili*. Tanzania: Ndanda Mission Press.
- \_\_\_\_\_ (1966). *Utenzi wa Zaburi*. Tanzania: Ndanda Mission Press.
- \_\_\_\_\_ (1966). *Taaluma ya Kiswahili*. Dar es Salaam: UKUTA.
- \_\_\_\_\_ (1967). *Kisa cha Bahati na Wazazi Wake*. Tanzania: Ndanda Mission Press.
- \_\_\_\_\_ (1967). *Sikilizeni Hekima: Methali na Mawaidha*. Tanzania: Ndanda Mission Press.
- \_\_\_\_\_ (1968). *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*. Dar es Salaam: UKUTA.

- \_\_\_\_\_ (1968). *Mbinu za Ujamaa*. Tanzania: Ndanda Mission Press.
- \_\_\_\_\_ (1970). *Ngonjera za UKUTA Na. 1*. Dar es Salaam. Oxford University Press.
- \_\_\_\_\_ (1971). *Diwani ya Lambert*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.
- \_\_\_\_\_ (1971). *Ngonjera za UKUTA Na. 2*. Dar es Salaam. Oxford University Press.
- Mnyampala, M. (2011). *Historia ya Hayati Sheikh Amri Abedi Kaluta: 1924-1964*. Dar es Salaam: Ahamadiya Printing Press.
- \_\_\_\_\_ (2014). *Maisha ni Kugharamia*. Paris: DL<sub>2</sub>A-Buluu Publishing.
- \_\_\_\_\_ (2014). *Ugogo na Ardhi Yake*. Paris: DL<sub>2</sub>A-Buluu Publishing.
- Msabila, D. T., na S. G. Nalail. (2013). *Research Proposal and Dissertation Writing: Principle and Practice*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Mugenda, A. G. (2013). *Qualitative Research Methods: Introduction*. Nairobi: ACTS Press.
- Mulokozi, M. M. (1975). "Revolution and Reaction in Swahili Poetry" in *Kiswahili Vol. 45/2*: 46-65. Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, M. M., na Kahigi, K.K. (1976). *Malenga wa Bara*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.
- \_\_\_\_\_ (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mulokozi, M. M. (1989). "Uchambuzi wa Mashairi." Katika *Mulika Na 29*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.
- \_\_\_\_\_ (Mh) (1999). *Tenzi Tatu za Kale (Fumo Liyongo, Al-Inkshafi na Mwana Kuponu)*. Dar es Salaam: TUKI.
- \_\_\_\_\_ (2017). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU Dar es Salaam.
- Mulokozi, M. M., na Sengo, T.S.Y. (2005). *History of Kiswahili Poetry A.D. 1000-2000*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, M. M. (2008). "Nadharia ya Jadi ya Ushairi wa Kiswahili: Je Upo?" Katika, *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.
- Mumbo, C. K., na Indede, F. N. (2004). *Johari ya Kiswahili: Kidato cha Tatu*. Nairobi: Acme Press Ltd.

- Murusuri, R. S. (2011). "Utamthiliya katika Ngonjera: Mifano kutoka Ngonjera za UKUTA." *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Mutembei, A. K. (2012). *Korasi katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uhakiki*. Dar es Salaam: TATAKI.
- Mwangomango, J. (1971). "Ngonjera za Ushairi." *Kiswahili Vol 41/2*, uk. 67-71. Dar es Salaam. TUKI.
- Nassir, S. A. (1810). *Al-Inkshafi* (Mh. W. Hichens, 1972). Oxford University Press.
- Ndulute, C. L. (1985). Politics in a Poetic Garb: The Literary Fortunes of Mathias Mnyampala. Mulokozi, M.M. na Massamba, D.P.B. (1985) (whr). *Jarida la TUKI*, Juzuu Na. 52/1&2.Uk. 143-160. Dar es Salaam: TUKI.
- Ngure, A. (2004). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishing House.
- Nicholaus, A. (2011). "Falsafa ya Ubuntu Iliyosawiriwa katika Tamthilia Teule za Penina Muhando," *Tasnifu ya Uzamili katika Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Ngesa, A., Matundura, E., na Kobia, J. (2015). "Mwingilianomatini katika Tamthilia za Kiswahili: Mashetani na Kijiba cha Moyo." *Katika Swahili Forum 22 (2015): 42-71*.
- Nyangwine, N., na Masebo, J. (2002). *Uhakiki Katika Fasihi*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangine Publishers
- Nyerere, J. K. (1966). *Julius Kaizari*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- \_\_\_\_\_ (1966). *Mabepari wa Venisi*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- \_\_\_\_\_ (1967). *The President Explains the Arusha Declaration*. Dar es Salaam: National Printing Co.
- \_\_\_\_\_ (1968). (toleo la 2) Katika utangulizi wa *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*. Dar es Salaam: UKUTA.
- \_\_\_\_\_ (1996a). *Utenzi wa Enjili: Kadri ya Utongo wa Luka*. Ndanda: Benedictine Publications.
- \_\_\_\_\_ (1996b). *Utenzi wa Enjili: Kadri ya Utongo wa Marko*. Ndanda: Benedictine Publications.
- \_\_\_\_\_ (1996c). *Utenzi wa Enjili: Kadri ya Utongo wa Matayo*. Ndanda: Benedictine Publications.

- \_\_\_\_\_ (1996d). *Utenzi wa Enjili: Kadri ya Utongo wa Yohana*. Ndanda: Benedictine Publications.
- \_\_\_\_\_ (1996e). *Utenzi wa Matendo ya Mitume*. Ndanda: Benedictine Publications.
- Niane, D. T. (mh) (1965). *Sundiata: An Epic of Old Mali* (Tr. G. D. Pickett). London: Longman.
- Ohly, R. (1977). "Problems of Literary Genres in Swahili. Swahili Studies: Supplement to Kiswahili 47/1: 68-79. Dar es Salaam: TUKI.
- Olson, S. H. (1975). "Philosophical Implications of some Swahili Idioms." In Swahili Vol. 45/2, Dar es Salaam: IKR: 32-37.
- Omari, S. (2011). "Poetics of 'Daladala': The Case of HIV/AIDS Dialogue in 'Daladala' Ticket Slogan." In <http://www.academia.edu>. Tarehe 2/6/2018.
- Omary, M. (2011). "Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008)." M.A Kiswahili: Dar es Salaam. (Haijachapishwa).
- Omwega, S.O. (2016). "Mtunzi na muktadha wa lugha yake." *International Journal of African Literature and Cultural Studies*, vol 1 (1): 35-38. Katika: <http://www.onlinesciencejournals.com/index.php/ijalcs>
- Orr, M. (2008). *Intertextuality: Debates and Contexts*. Cambridge: Polity Press.
- Ponera, A. S. (2014). "Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi." Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Ponera, D. L. (2015). "Nafasi ya Ukristo katika Ushairi wa Manyampala." Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Ramadhani, A. J. (1974). "Ushairi" Wah. A. Abdala na R.L. Jaka katika *Mulika Na. 3*: 1-8 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Printpak Tanzania Ltd.
- Robert, S. (1958). "Hotuba Juu ya Ushairi." *Journal of the East African Swahili Committee, Na. 28/1:37-41*. Dar es Salaam.
- \_\_\_\_\_ (1959). *Kielelezo cha Fasihi*. Nairobi: Nelson.
- \_\_\_\_\_ (1974). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Nairobi: Nelson.
- Roy, M. (2013). Mathias E. Mnyampala (1917-1969): Poésie D'expression Swahilie et Construction Nationale Tanzanienne. Litt\_eratures. Institut Na-tional des Langues et Civilisations Orientales. Inalco Paris. Fran\_cais. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa).

- Samwel, M., Seleman, A.J., na Kabiero, A.J. (2013). *Ushairi wa Kiswahili: Nadharia, Maendeleo, Mwongozo kwa Walimu wa Kiswahili na Diwani ya Mea*. Dar es Salaam: MEVELI Publishers.
- Sanka, S.M. (1994). "Semantic Deviation in Iraqw Oral Poetry." Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa).
- Samandito, J. (2011). Mathias Mnyampala kama Muumini. Katika <http://www.academia.edu/6304971/4>. Tarehe 15/7/2018.
- Senkoro, F. M. E. K. (1988). *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: DUP.
- \_\_\_\_\_ (1976). "Mwamko wa Kisiasa katika Ushairi wa Shaaban Robert." Katika *Mulika Na. 8*: 30-41. Dar es Salaam: TUKI.
- \_\_\_\_\_ (1995). "E. Kezilahabi: Shaaban Robert wa Pili," katika *Kioo cha Lugha, Na. 1*: 61-69. Dar es Salaam: TUKI.
- \_\_\_\_\_ (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Shitemi, L. N. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini*. Eldoret: Moi University Press.
- Simala, K. I. (2000). "Ukakiki wa Sitiari za Uana katika Ushairi wa Kiswahili." Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Idara ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Moi. (haijachapishwa).
- Sunkuli, L. O., na Miruka, O. S. (1990). *A Dictionary of Oral Literature*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Topan, F., na Grant, K. (1971). *Mashairi ya Azimio la Arusha*. Dar es Salaam: Longman.
- Topan, F. (1974). *Utangulizi wa Kichomi*. Nairobi: Heinemann.
- Wafula, R. M., na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Walibora, K. (2007). *Diwani ya Karne Mpya*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wanjala, W. F. (2015). *Mwingiliano Tanzania Katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kongwa*. Tasnifu ya uzamifu (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.
- Wamitila, K. W. (2001). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.
- \_\_\_\_\_ (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers Limited.
- \_\_\_\_\_ (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.
- Widawsky, R. (2014). "Julia Kristeva's Psychoanalytic Work" Katika *Journal of American Psychoanalytic Association*. Juz. 62. Na. 2 (60-67). <http://journals.sagepub.com/doi/full/10.1177>. Tarehe 17/6/2017.
- Williams, J. C. (1974). "Diwani ya Mnyampala." Wah. A. Abdala na R.L. Jaka katika *Mulika Na. 3*: 15-23. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Printpak Tanzania Ltd.
- Wolfreys, J. (2004). *Critical Keyword in Literature and Cultural Theory*. Landon: Palgrave.

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho A: Mwongozo wa Mahojiano kwa Wahadhiri na Wanafunzi

Jina langu ni Anna Nicholas Kyamba kutoka Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Moi. Ninafanya utafiti kuhusu Mathias Mnyampala na Ushairi wa Kiswahili. Madhumuni ya utafiti ni kuchunguza mchango wa Mathias Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili. Kazi za ushairi zitakazochambuliwa ni *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965), *Ngonjera za UKUTA Na. 1* (1970), *Hazina ya Washairi, Mahadhi ya Kiswahili* na *Mashairi ya Vidato*. Tafadhali naomba ushirikiano wako katika kujibu maswali yafuatayo:

1. Je, unamfahamu Mathias Mnyampala?
2. Je, unafahamu kazi zozote alizoandika Mathias Mnyampala? Zitaje.
3. Mathias Mnyampala ameandika kazi ngapi za ushairi na za nathari?
4. Je umewahi kusoma na kuhakiki kazi za ushairi za Mathias Mnyampala?
5. Kama umewahi kusoma au kuhakiki ni mambo gani yalikuwutia kusoma na kuhakiki kazi hizi?
6. Ulikutana na changamoto gani wakati wa kusoma na kuhakiki kazi hizo?
7. Kwa maoni yako, hali ya usomaji wa kazi za ushairi za Mathias Mnyampala ipoje?
8. Katika kazi alizoandika Mathias Mnyampala ni kazi zipi zimechapishwa na zipi hazijachapishwa?
9. Unafikiri ni kwa nini baadhi ya kazi za Mathias Mnyampala hadi leo hazijachapishwa?
10. Je, unaweza kuelezea fani na maudhui ya kazi za ushairi za Mathias Mnyampala?
11. Unafikiri ni sababu zipi zimepelekea kutofanyika utafiti wa kina kuhusu Mathias Mnyampala na utunzi wake?
12. Je, ni muktadha upi uliomsukuma Mathias Mnyampala kuandika kazi zake?
13. Unaweza kutaja mchango wa Mathias Mnyampala katika taaluma ya Kiswahili na jamii kwa ujumla?
14. Je, kazi za ushairi za Mathias Mnyampala zina mchango gani kifani na kimaudhui katika ushairi wa Kiswahili?

## **Kiambatisho B: Mwongozo wa Mahojiano kwa Familia ya Mathias Mnyampala**

Jina langu ni Anna Nicholas Kyamba kutoka Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Moi nchini Kenya. Ninafanya utafiti kuhusu Mathias Mnyampala na Ushairi wa Kiswahili. Madhumuni ya utafiti ni kuchunguza mchango wa Mathias Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili. Kazi za ushairi zitakazochambuliwa ni *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965) *Ngonjera za UKUTA Na. 1* (1970), *Hazina ya Washairi*, *Mahadhi ya Kiswahili* na *Mashairi ya Vidato*. Utafiti huu unafanywa kwa madhumuni niliyobainisha na si kwa matumizi mengine. Tafadhali naomba ushirikiano wako katika kujibu maswali yafuatayo:

1. Mathias Mnyampala alizaliwa mwaka gani? Wapi? Na ni wa jamii gani?
2. Yeye ni mzaliwa wa ngapi?
3. Je, katika familia yao walizaliwa watoto wangapi, kati yao wa kiume walikuwa wangapi na wa kike walikuwa wangapi?
4. Wazazi wake waliitwa nani?
5. Mathias Mnyampala alikuwa na kiwango gani cha elimu?
6. Mnyampala alioa wanawake wangapi?
7. Je, Mnyampala alifanikiwa kupata watoto wangapi, kati ya watoto hao wa kiume ni wangapi na wa kike ni wangapi?
8. Wadhifa wake katika serikali ulikuwa ni upi?
9. Alianza kujishughulisha na uandishi wa kazi za ushairi mwaka gani?
10. Kazi alizowahi kutunga na kuandika wakati wa uhai wake ni zipi?
11. Mbali na ushairi, ni kazi zipi za fasihi au nyinginezo alizoandika?
12. Je umewahi kusoma kazi za fasihi za Mathias Mnyampala?
13. Ikiwa umewahi kusoma kazi zake za ushairi, ni kazi zipi ulizisoma? Zitaje.
14. Katika kazi ulizosoma unafikiri ni muktadha gani uliompelekea Mathias Mnyampala kuandika kazi za ushairi?
15. Unafikiri kazi za Mnyampala zina mchango gani katika fasihi na jamii?



**Kiambatisho C. Kazi za Mathias Mnyampala ambazo Hazijachapishwa**

1. *Azimio la Arusha na Maandiko Matakatiifu*
2. *Furaha ya Kiswahili cha Mapinduzi na Kiswahili Chororo.*
3. *Hadithi za Wahenga Wetu: Kitabu cha Kwanza*
4. *Hadithi za Wahenga Wetu: Kitabu cha Pili*
5. *Hadithi za Wahenga Wetu: Kitabu cha Tatu*
6. *Hadithi za Wahenga Wetu: Kitabu cha Nne*
7. *Hazina ya Washairi*
8. *Kisa cha Dume la Nyani na Hadithi Nyingine*
9. *Kisa cha Kazimba na Msichana*
10. *Kisa cha Msichana na Dume la Nyani*
11. *Kisa cha Ndezi na Binadamu: Kitabu cha Kwanza*
12. *Kisa cha Ndezi na Binadamu: Kitabu cha Pili*
13. *Kisa cha Ndezi na Binadamu: Kitabu cha Tatu*
14. *Kisa cha Ndezi na Binadamu: Kitabu cha Nne*
15. *Kisa cha Tandala na Bibi Mtekamaji*
16. *Mahadhi ya Kiswahili*
17. *Mashairi ya Vidato*
18. *Methali za Kiswahili na Maneno yenye Hekima: Kitabu cha Kwanza*
19. *Methali za Kiswahili na Maneno yenye Hekima: Kitabu cha Pili*
20. *Ufasaha wa Kiswahili*
21. *Umoja ni Ngome Yetu*

Kiambatisho D: Mtindo wa Mashairi ya Mtiririko (uk. 5) katika Diwani Ya Mnyampala

**8. TUNGENI MTIRIRIKO**

Mhariri mahabubu, pokea wangu mwandiko,  
Nakupenda kuwahutubu, wahariri walioko,  
Si kama nawaghilibu, na kujitia vituko,  
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Msichukue ghadhabu, kwa mabavu na vituko,  
Lichungulie taratibu, usanifu beti zako,  
Kama wajibu jawabu, ukae kwanza kitako,  
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Nisikie Masharubu, wape habari wa Keko,  
Mwingine sikughilibu, na vingine lisiweko,  
Sitoke kwenye kilabu, ukajidai mwandiko,  
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Uliza kwanza swahibu, umwende kwa kicheko,  
Mwingine sikughilibu, na vingine lisiweko,  
Sitoke kwenye kilabu, ukajidai mwandiko,  
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Kisa kilichokusibu, kipate nacho mwandiko,  
Maanaye na sababu, mwanzo ni chokocho,  
Ni kipawa cha Wahabu, usipate masumbuko,  
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Mwendo huo siharibu, vinginevyo lisiweko,  
Ukianza na Hatibu, simwite tena Maiko,  
Na uzuri wa dhahabu, usipate masumbuko,  
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Tungozo ziwe dhahabu, zambatane na mwitiko,  
Wengi wasitaajabu, jinsi ya mtiririko  
Liimbwapo ni taibu, lipendeze walioko,  
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Asiliye ughaibu, moyoni ndilo chimbuko,  
Yaliimbwa na mababu, hao waliokuweko,  
Hawakulewa sharabu, waliotunza tambiko,  
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Walotunga ya thawabu, na matusi yasiweko,  
Watunzaji wa madhehebu, na dini na zilizoko,  
Kumtukuza Wahabu, Majambo mtakasiko,  
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Beti kumi kwa hesabu, hazina mchanganyiko,  
Nimemuweka Katibu, hap kaka a kitako,  
Kati 'bu' imeratibu, mwisho 'ko' imekuwepo,  
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

**Kiambatisho E: Mtindo wa Mashairi ya Msisitizo (uk. 121) katika Diwani Ya  
Mnyampala**

**139. NATUNGA MSISITIZO**

Nawapangia maneno, ya sifa na mwelekezo,  
Na kuzitoa mifano, zinase nyoyo mawazo,  
Usemi wa sisitizo;  
Sisitizo mlingano, usioleta mvizo,  
Maagizo yawe **manono**, nayatilia mkazo,  
Natunga masisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Tutunge ya tangamano, wana wapewe agizo,  
Tuwafunze maagano, yasiyoleta chagizo,  
Maovu kuwa katazo;  
Katazo la matukano, yanayoleta mzozo,  
Zogo halina **patano**, mbele lina maapizo,  
Natunga masisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Utungo una mkono, wa kheri na matulizo,  
Matulizo ya mtuno, usioleta vikwazo,  
Ni mema mataulizo;  
Tangulizo la maono, kwani una bembelezo,  
Watu waache **kinzano**, kwani huleta tatizo,  
Natunga masisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Tungo hizi kama ngano, kwa mkulima pendezo,  
Hung'aa katika chano, makapi hata masozo,  
Katu hazina chukizo;  
Chukizo la baya pano, unaoleta ufyozo,  
Bali ni **maridhiano**, ubani lete chetezo,  
Natunga masisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Shikamaneni mikono, epukeni angamizo,  
Tuepuke mapambano, maneno ya kwaruzo,  
Si maungwana utwezo;  
Utwezo na maumano, uadui pandikizo,  
Cheka muonyeshe **meno**, siwe kama hatunazo,  
Natunga masisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Zifanyeni mikutono, machungu mtie pozo,  
Mema yale mashindano, kati hayana katazo,  
Bali neno la umizo;  
Umizo kenye mibano, kudhan kama mchezo,  
Akheri **uhusiano**, tuepuke magombezo,  
Natunga masisitizo, tungo zenye mwendo mpya.


Tafuteni mapendano, kuepuka ubwakizo,  
Si vibaya makunyano, kwa wale wenye puuzo,  
Tusilete magombezo;  
Magombezo yele mno, na matusi mzo mzo,  
Huvunja **shirikiano**, bagukano na utwezo,  
Natunga masisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Viteni sikilizano, ziada yenu ni tuzo,  
 Tunzo la ujulikano, mwororo uso vikwazo,  
     Muepuke ambukizo;  
 Ambukizo la mang'ano, magomvi na mapaazo,  
 Tungeacha **matetano**, tutunge tungo zijazo  
 Natunga masisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Nashona mpya mshono, gazetini ni pambizo,  
 Tungo za uwezekano, kama wa nyumba na nguzo,  
     Kwa wagonjwa ni nguzo;  
 Uguzo dawa ya mboni, isiyokuwa na tozo,  
 Tungo mistari **tano**, wa sita ni mwishilizo,  
 Natunga masisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Si tungo za msumeno, kukwaruza kwa kerezo,  
 Khamis kasifu mno, mng'ao wa suko kwazo,  
     Zinacho kielelezo;  
 Kielelezo fatano, wa kupata elekezo,  
 Kisoma watoa **jino**, acha zipate enezo,  
 Natunga masisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Kiambatisho F: Mtindo wa Mashairi ya Vidato "Uaminifu" (uk. 1) katika  
Mswada wa Mashairi Ya Vidato



## Kiambatisho G: Vibali vya Utafiti



CHUO KIKUU CHA MOI

KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA

Tarehe: Juni 9, 2016

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA

**YAH: MAENDELEO YA MASOMO YA ANNA NICHOLAUS KYAMBA (NAMBARI YA USAJILI-SASS/DPHIL/KIS/01/15)-SHAHADA YA UZAMIFU**

Anna Nicholas Kyamba ni Mzanifu anayeingia mwaka wa pili katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Moi, Kenya. Kyamba amekamilisha kozi zote za kiwango cha uzamifu. Aidha ametetea pendekezo lake la utafiti na kupita vizuri. Mada ya utafiti wake ni: **"Mchango wa Mathias Mnyampala katika Ushairi wa Kiswahili"**

Kwa waraka huu, Anna Kyamba, ameruhusiwa kwenda nyanjani (uwandani) ili kukusanya data na baadaye kuanza shughuli ya uchanganuzi wa data.

Ni maombi yangu kwamba atapata msaada anaouhitaji katika harakati za kukusanya data. Kwa niaba ya Idara ya Kiswahili namtakia utulivu na kila la heri katika shughuli hii muhimu ya kitaaluma.



**Dkt. Mosol Kandagor,**  
**Mkuu wa Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika.**

**Nakala kwa:** Naibu Makamu wa Chansela, Akademia, Utafiti na Uendelezaji (DVC- Academics Research and Extension)  
Mkuu wa Kitivo (Dean, SASS)

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
President's Office  
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

DAR ES SALAAM REGION  
Phone Number: 2203158  
Fax number: 2203158  
email: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)  
website: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)



REGIONAL COMMISSIONER'S OFFICE,  
3 RASHID KAWAWA ROAD,  
P.O. BOX 5429,  
12880 DAR ES SALAAM

In reply please quote:  
Ref. No. ....

25<sup>th</sup> JUNE ..... 2016

District Administrative Secretary,

KINDOMONI .....

P. O. Box .....

DAR ES SALAAM.

**RE: RESEARCH PERMIT**

Prof/Dr/Mrs./Ms/Miss ANNA NICHOLAUS KYAMBA ..... is  
student/Research from MOI UNIVERSITY ..... has been  
permitted to undertake research on MCHAMGO WA MATIARA  
MNYAMPALA KATIKA MAONDJELO YA USHAKI  
WA KISWAHILI .....

From JULY ..... 2016 to AUGUST ..... 2016.

I kindly request your good assistance to enable her/his research.

For; REGIONAL ADMINISTRATION SECRETARY  
DAR ES SALAAM

Copy: Municipal Director,  
KINDOMONI .....  
DAR ES SALAAM.

" Principal/Vice Chancellor  
MOI UNIVERSITY .....

# KINONDONI MUNICIPAL COUNCIL

ALL CORRESPONDENCES TO BE ADDRESSED TO THE MUNICIPAL DIRECTOR

Tel: 2170173  
Fax: 2172606

In reply please quote:

Ref. KMC/T.20/81



MUNICIPAL DIRECTOR  
KINONDONI MUNICIPAL  
COUNCIL  
P. O. BOX 31902  
2MOROGORO ROAD  
14883 DAR ES SALAAM

Date 27 /06/2016.

**MS. Amina Nicholaus Kyamba,**  
**DAR ES SALAAM.**

## RE: RESEARCH PERMIT

Refer to the above heading.

I am pleased to inform you that your above request has been considered by the Municipal Director, and has offered you a place to Collect data for **one month.**

Upon receipt of this letter, please report to the **Ward Executive Officer -- Mzimuni** for commencement of your research.

During the period of field, you are required to obey the rules and regulations of the Institution as they will be defined by the supervisor of the research.

.....  
M. Masimbusi  
For: **THE MUNICIPAL DIRECTOR**  
**KINONDONI**

**Copy:** District Administrative Secretary,  
P. O. Box 9583,  
**DAR ES SALAAM.**

*Imppo heleno*  
*Heleno*  
*25/6/2016*



Imppo helena  
H. Helena  
25/6/2016

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
PRESIDENT OFFICE  
MINISTRY OF REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT  
KINONDONI DISTRICT

Telephone No. 2170169 / 2170183

To reply please quote:

Ref. No. AB.320/378/01B



THE DISTRICT COMMISSIONER'S OFFICE  
P.O. BOX 9583,  
KINONDONI,  
DAR ES SALAAM,  
TANZANIA.

25<sup>th</sup> JUNE 2016

MUNICIPAL DIRECTOR  
KINONDONI  
DAR - ES - SALAAM

RE: RESEARCH PERMIT

ANNA NICHOLAUS KYAMBA is a Student/researcher from MOI UNIVERSITY (MAIN CAMPUS) He/She has been permitted to undertake field work research on "MCHANGO WA MATHIAS MNYAMPALA KATIKA MAENDELEO YA USHAKI WA KISWAHILI" From JULY TO AUGUST 2016

I kindly request your good assistance to enable him/her to complete his/her research.

For: - District Administrative Secretary  
KINONDONI

PS / Katar Mbi muni  
27/6/2016

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**  
**President's Office**  
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**DAR ES SALAAM REGION**

Phone Number: 2203158

Fax number: 2203158

email: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)website: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)**REGIONAL COMMISSIONER'S OFFICE,**

3 RASHID KAWAWA ROAD,

P.O. BOX 5429,

12880 DAR ES SALAAM

In reply please quote:

Ref. No. ....

25<sup>th</sup> JUNE  
 ..... 2017

District Administrative Secretary,

... UBUNGO .....

P. O. Box .....

**DAR ES SALAAM.****RE: RESEARCH PERMIT**

Prof/Dr/Mrs./Ms/Miss ANNA NICHOLAUS KYAMBA is  
 student/**Research** from MOI UNIVERSITY has been  
 permitted to undertake research on MCHANGO WA MATIAS  
MNYAMPALA KATIKA MAENDELEO YA USHAIRI  
WA KISWAHILI

From JULY 2017 to AUGUST 2017.

I kindly request your good assistance to enable her/his research.

For; **REGIONAL ADMINISTRATION SECRETARY**  
**DAR ES SALAAM**

Copy: Municipal Director,

... UBUNGO .....**DAR ES SALAAM.**

“ Principal/Vice Chancellor

... MOI UNIVERSITY .....

# UBUNGO MUNICIPAL COUNCIL

ALL CORRESPONDENCES TO BE ADDRESSED TO THE MUNICIPAL DIRECTOR

Tel: 0222-926341  
Fax: 0222-926342



**MUNICIPAL DIRECTOR UBUNGO  
MUNICIPAL COUNCIL,  
P. O. BOX 55068  
DAR ES SALAAM.**

In reply please quote: ✓

DATE: 28/06/2016.

Ref. AB.27/333/01

Anna Nicholaus Kyamba,  
Moi University,  
**KENYA.**

RE: **FIELD ATTACHMENT**

Refer to the above heading.

I am pleased to inform you that your above request has been considered by the Municipal Director, and has offered you a place to conduct field attachment from **June, 2016 to August, 2016**

Upon receipt of this letter, please report to the **Ward Executive Officer – Ubungo** commencement of your field attachment.

During the period of field attachment you are required to obey the rules and regulations of the institution as they will be defined by the supervisor of the field.

Hoping to see you soon.

*E. F. Kisenha*  
E. F. Kisenha  
For: **THE MUNICIPAL DIRECTOR  
UBUNGO**  
Kny: MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO  
DAR-ES-SALAAM

Copy: Principal,  
Moi University,  
**KENYA.**

OFISI YA MKURUGENZI  
MANISPAA YA UBUNGO

26 JUN 2016

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
PRESIDENT'S OFFICE  
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

Telephone No.  
**022 -2926340/5**  
Please reply quote



The DISTRICT COMMISSIONER'S OFFICE,  
**S.L.P 55064,**  
**UBUNGO- DAR ES SALAAM.**

Ref. N:AB.66/213/01B/97

26<sup>th</sup> June, 2016

Municipal Director,  
S. L. P. 55068,  
**DAR ES SALAAM.**

**RE: FIELD PERMIT**

Ms. **Anna Nicholaus Kyamba** is student/researcher from **Moi University** has been permitted to undertake field work research on "**Mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya Ushauri wa Kiswahili**" From July, 2016 to August, 2016.

I kindly request your good assistance to enable him to complete his research.

Diana K. Nkarage

**For: DISTRICT ADMINISTRATIVE SECRETARY  
UBUNGO**

Kiny: **KATIBU TAWALA WA WILAYA**  
**S. L. P. 55064**  
**UBUNGO**

Copy to: Researcher.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**Mkoa wa Dodoma**  
 Anwani ya Simu REGCOM  
 Simu Nambari: 2324343/2324384  
 E-Mail No. ras@dodoma.go.tz  
 Fax No. 255 026 2320046  
 Unapojibu tafadhali taja  
**Kumb DB.357/369/01C/131**



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa  
 S.L.P 914,  
 Dodoma.

**24 Oktoba, 2016**

Katibu Tawala Wilaya,  
 Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,  
**DODOMA.**

**YAH: KIBALI CHA UTAFITI**


Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Napenda kuchukua nafasi kumtambulisha kwako Anna Nicholas Kyamba mwanachuo wa shahada ya Uzamifu katika Chuo Kikuu cha Moi. Kwa sasa anafanya utafiti katika Mkoa wa Dodoma.

Utafiti wake unahusu **"Mchango wa Mathias Mnyampala katika Ushairi wa Kiswahili"** na Wilaya yako itahusika.

Kibali cha utafiti kimetolewa kuanzia **24 Oktoba, 2016 hadi Disemba, 2016**. Tafadhali wapatiwe ushirikiano ili kukamilisha lengo lao.

Nawashukuru kwa ushirikiano Wako.

  
 Paul K. Masanja

**Kny. KATIBU TAWALA MKOA**  
**DODOMA.**

**Nakala:** Mkuu wa Idara,  
 Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,  
 Chuo Kikuu cha Moi,  
 S.L.P. 3900,  
**KENYA.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**HALMASHAURI YA MANISPAA DODOMA**  
*(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)*

**MKOA WA DODOMA**

Tel.: 2354817/2321550  
 Fax: 2321550



Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa  
 S.L.P.1249  
**Dodoma**  
 E-mail: Md@dodomamc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HMD/PF.

Tarehe: 25 Oktoba, 2016

Watendaji wa Kata,  
 Majengo, Kilimani na Dodoma Makulu,  
 S.L.P 1249,  
**DODOMA.**


**YAH: KIBALI CHA UTAFITI**

Tafadhali husikeni na somo tajwa hapo juu.

Namtambulisha kwenu B. Anna Nicholaus Kyamba ambaye ni Mwanachuo wa Shahada ya Uzamivu, kutoka Chuo Kikuu cha Moi Kenya, ambaye anataka kufanya utafiti katika Kata zenu kuhusu **"Mchango wa Mathias Mnyampala katika Ushairi wa Kiswahili"**

Kwa barua hii kibali cha kufanya Utafiti kimetolewa kuanzia tarehe 24 Oktoba, 2016 hadi Disemba 2016. Tafadhali apewe ushirikiano utakaomwezesha kufanikisha utafiti wake.

Nashukuru kwa ushirikiano wenu.

  
**Agatha Kalesu**  
**Kny: MKURUGENZI WA MANISPAA**  
**DODOMA**

MKURUGENZI WA  
 MANISPAA DODOMA

CHUO KIKUU CHA DAR-ES-SALAAM,

S.L.P 35091,

DAR-ES-SALAAM

08/11/2016

Mkuu wa KITIVO

KITIVO CHA SAYANSI YA JAMII

CHUO KIKUU CHA DODOMA

S.L.P 428

DODOMA

NDUGU,

YAH! MAOMBI YA KUSOMA KATIKA

MAKTABA YA KITIVO CHAKO

Kichwa cha barua hii chahusika.

Mimi Anna Nicholas Kyamba ni  
mfanyakazi wa chuo kikuu cha Dar-es-Salaam. Kwa sasa ninasoma masomo ya uzamitwa na nipo katika hatua ya ukusanyaji wa data. Minaomba kuingia katika maktaba ya kitivo cha sayansi ya Jamii ili kuweza kusoma matini mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti wangu. Mada ya utafiti huo ni  
"MCHANGO WA MATHIAS MNYAMPARA KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI".

Minaambatanisha risiti ya banki inayoonyesha malipo ya siku nne.


Natangulisa shukrani zangu za dhafi

Anna N. Kyamba

~~Anna~~ - -

MHAJIRI MSAIBIRI (UOASM)

UNIVERSITY OF DODOMA  
 P.O. BOX 259 DODOMA  
 T/N: 005-566-557



**RECEIPT**

No. **436444** Date: **04 Nov 2016**

RECEIVED FROM: **ANNA NICHOLAUS KYAMBA**

The Sum of **TZS Two thousand only**

Being payment in respect of: **Sundry Income**

**LIBRARY SERVICE FOR 4 DAYS ONLY**

Cash/Cheque No.: **Credit Advice**

TZS **2,000.00**

STUD GRDD

Codes: **16080**

**8148-1682-9833-4052-9830-8**

WITH THANKS  
 Imrma



HATI YA KUKABIDHI MAANDISHI NA PICHA ZA HAYATI MATHIAS  
EUGEN MNYAMPALA WA MCHICHIMI

MIMI STANLEY CHARLES MACHICHIMI NI MJKUU WA MWARDISHI WA VITABU VYA KISWALI VYA HAYATI MATHIAS E MNYAMPALA WA MACHICHIMI. LEO NI TAREHE 27/10/2016, NIMEMKABIDHI MAANDISHI NA PICHA ZA HISTORIA YA MAISHA YA HAYATI MATHIAS E MNYAMPALA WA MACHICHIMI KWA ANNA NICHOLAUS KYAMBA MTAFIGI WA MCHANGO WA MATHIAS MNYAMPALA KATIKA MAENDELEO YA USTAIRI WA KISWALI KWA AJILI YA MANDISHI NA TASNIFI YAKE INAYOMUHUSU HAYATI MATHIAS E MNYAMPALA. ANAFUMIA KWA AJILI YA UTAFIGI TU NA SI KWA AJILI YA BIASHARA.

SAINI YANGU: *Stanley Charles*

SAINI YA MTAFIGI: *Anna* --

TAREHE: 27/10/2016

**Kiambatisho H: Picha Mbalimbali Zilizopigwa Nyanjani**



**Picha namba 6: Mathias Mnyampala wakati wa uhai wake (1917-1969).  
(tarehe 3/11/2016)**




**Picha namba 7: Mzee Mnyampala Machichimi (Baba yake Mathias Mnyampala). (tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 8: Mama yake Mathias Mnyampala na Mjukuu wake Charles Mnyampala. (tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 9: Mke wa Marehemu Mathias Mnyampala akiwa na watoto wake Charles upande wa kulia na Edward upande wa kushoto miaka ya sitini, Dar es Salaam. (tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 10: Mathias Mnyampala akiwa katika jengo la Chuo Kikuu cha Lumumba, alikuwa Mwalimu wa kufunza Kiswahili na Mashairi, Dar es Salaam. (tarehe 3/11/2016)**

# THE INSTITUTE OF ADULT EDUCATION UNIVERSITY COLLEGE, DAR ES SALAAM

Director - Paul H. Bertelsen, M.A., cand. polit.

P.O. Box 9184. - Telephone 20377

27th October, 1966.

To whom it may concern

Mr. M. E. Mnyampala has been a part-time tutor in Mashairi ya Kiswahili for the Institute of Adult Education, University College, Dar es Salaam, for five 10-week terms.

Mr. Mnyampala has been an efficient teacher. The syllabus, which he himself drew up, included the art of writing poems and the study of rhythms and measures. The different types of Swahili poems were studied, together with the works of famous Swahili poets. In particular, such writers as Al-Inkishafi, Muyaka and Sheik Amri Abedi were discussed. Mr. Mnyampala encouraged the students to write poems at home, and these were then discussed in class.

I am very grateful for the valuable services Mr. Mnyampala has rendered to the Institute of Adult Education.



P. H. Bertelsen  
Director

**Picha namba 11: Barua inayodhibitisha kuwa Mathias Mnyampala aliwahi kuwa mwalimu wa muda mfupi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (tarehe 3/11/2016)**

TANGANYIKA TERRITORY

**Local**  
**████████ Civil Service — CERTIFICATE OF SERVICE**

Name of Officer..... Mathias Mnyampara

Position held and Department { Tax Clerk, Provincial Administration.

Period of service: From 1/1/1942 to 31/7/1945.

Cause of termination of engagement { Retrenchment.

Efficiency Fair. 502/5/140  
3-10-56

General conduct..... Good.

J. E. S. GRIFFITHS, D.C.  
*Head of Department*

Date 1st August, 19 45.

Right thumbprint of bearer.  
or signature

Efficiency and General Conduct are assessed as "Very Good," "Good," "Fair" or "Indifferent."

G P Dsm 47312/12-41/2m

\* Previously worked for Native Authority as from 23/12/37 to 31/12/41.

27th February, 1947.

CERTIFIED TRUE COPY. T. Griffiths  
DISTRICT COMMISSIONER,  
DODOMA.

**Picha namba 12: Cheti cha Ukarani, Dodoma. (tarehe 3/11/2016)**

TANGANYIKA TERRITORY.

*Local*  
African Civil Service.

DOD/51140  
3-10-56

CERTIFICATE OF SERVICE

Name of Officer ..... *M. MATHIAS* / *M. NYAMPALA* .....

Position held ) ..... (1) ..... *FAMINE STORE CLERK* ..... *NT.*  
and Department) ..... (2) ..... *CLERK TSETSE CAMP* ..... *NT.*

Period of Service. From ..... (1) ..... *25.8.46* ..... - ..... *30.4.47* .....  
..... (2) ..... *1.5.47* ..... - ..... *31.10.47* .....

Cause of Termination ) ..... *Tsetse camp closed down during*  
of engagement ) ..... *the planting season* .....

Efficiency ..... *Very Good* ..... *Educated intelligent* .....  
..... *capable initiative* .....

General conduct ..... *Excellent* .....

*Mathias*  
No. 10

DISTRICT OFFICE  
Date *31.10.47* head of Department.  
Date ..... *31.10.1947* .....

*Mathias Nyampala*  
Right thumb print of bearer.

LABOUR EXCHANGE  
KILOSA  
15-6-50

Efficiency and General Conduct are assessed as "Very Good," "Good,"  
"Fair," or "Indifferent."

G.P. Dsm. - 14  
185

Picha namba 13: Cheti cha kazi ya utunza store na ukarani wa ndorobo, Shinyanga. (tarehe 3/11/2016)



TANGANYIKA TERRITORY

## Certificate of Service

Name of Officer MATHIAS E. MNYAPALA

Position held and Department TAX CLERK, PROVINCIAL ADMINISTRATION.  
DODOMA DISTRICT.

Period of Service: From 1/2/1948 to 31/3/1951.

Cause of termination of engagement Resigned at own request.

Efficiency Very Good DOD/S/140  
3-10-56

General conduct Very Good.

**LABOUR EXCHANGE**  
*KLE/S/107*  
**KILOSA**  
*15-6-54.*

*[Signature]*  
Head of Department


*[Signature]*  
Chief Secretary

12/4/ 1957


Efficiency and General Conduct are assessed as "Very Good," "Good," "Fair" or "Indifferent"

G.P.Dam. S 59246 548 5m

**Picha namba 14: Cheti cha ukarani wa kodi mkoa wa Dodoma.  
(tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 15: Cheti cha mafunzo ya Biblia. (tarehe 3/11/2016)**



Picha namba 16: Cheti cha upigaji chapa. (tarehe 3/11/2016)



Picha namba 17: Mashine aliyokuwa anatumia kuchapia kazi zake za ushairi na nyinginezo (tarehe 3/11/2016)

**ANTONIOU SISAL ESTATES LTD.**  
**KIMAMBA**  
 TANGANYIKA TERRITORY.


N<sup>o</sup> 444  
 Kimamba, 23<sup>rd</sup> November 1956

**CERTIFICATE OF SERVICE**

This is to certify that MATHIAS MNYAMPALA  
 has completed four cards in our service as a Byelist - class  
 He leaves today on collection  
 His work has been good

207/S/140  
3-10-56

For and on behalf of  
**ANTONIOU SISAL ESTATE LTD.**  
 Manager/Field Ast.



**Picha namba 18: Cheti cha Mathias Mnyampala katika mashamba ya mikonge Kimamba, Morogoro. (tarehe 3/11/2016)**

Telegraphic Address:  
 "Tributary" Dodoma  
 Telephone Nos.: 53 and 54  
 In reply please quote

DEPARTMENT OF WATER DEVELOPMENT  
 AND IRRIGATION,  
 DIVISIONAL ENGINEER,  
 DODOMA

Ref. No. 2/27/17. 20th September, 1956.

TANGANYIKA TERRITORY DOD/S/140  
 - CERTIFICATE OF SERVICE - 3-10-56

Name of Officer: MATHIAS E. MNYAMPALA  
 Position held ) TYPIST  
 and Department ) WATER DEVELOPMENT & IRRIGATION DEPT. DODOMA.

Period of Service. From: 1/1/1956 to 20/9/1956

Cause of Termination ) RESIGNED AT OWN REQUEST  
 of Engagement )

Efficiency: GOOD

General conduct: GOOD

DESIGNATION.

*O. F. M. M.*  
 Divisional Engineer  
 Water Development  
 DODOMA

Right thumb of bearer or signature.

Efficiency and General Conduct assessed are "Very Good", "Good",  
 "Fair", or "Indifferent"

**Picha namba 19: Cheti cha upigaji chapa katika Idara ya Maji na Umwagiliaji, Dodoma. (tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 20: Picha ya pamoja wakiwemo Rashid M. Kawawa, Mathias Mnyampala na Charles Mathias Mnyampala (tarehe 3/11/2016)**




**Picha namba 21: Mathias Mnyampala akiwa na washairi maarufu nchini Tanzania. (tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 22: Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa na Washairi maarufu Tanzania akiwemo Mathias Mnyampala. (tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 23: Mathias Mnyampala akisindikizwa na makamanda wa Jeshi la Kujenga Taifa, mara baada ya kufundisha ngonjera katika kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa Mgulani, Jijini Dar es Salaam mwaka 1967. (tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 24: Barua ya uthibitisho wa ujuzi wa upigaji chapa.  
(tarehe 3/11/2016)**



TANGANYIKA

**LETTER OF APPOINTMENT TO THE SUBORDINATE SERVICE**  
APPENDIX A/7 (See General Order 40)

Ref. No. PAF/MEM Station : DODOMA  
Date : 16th February 1957

To : Mr. Mathias Emnzehe Mnyampala,  
Dodoma.

I am authorized to inform you that you are appointed to the Subordinate Service in Group  
S2-1  
as a Clerk

in this Department/Province with effect from 5th November, 1956,  
at a salary of Shs. 176/- per month in the scale Shs. 176/- x 12/-  
by Shs. 188/- x 10/- to Shs. 228/-

2. Your appointment is subject to the relevant provisions of the General Orders and other instructions applicable to the Subordinate Service, provided that, in the case of employees who do not contribute to the Government Employees Provident Fund, appointments may be terminated by either party at the end of any month without notice.

*K. Johnson*  
Head of Department/Provincial Commissioner  
PROVINCIAL AGRICULTURAL OFFICER,  
CENTRAL Province.

I agree to accept the appointment.  
Date : 16/2/57  
*Mnyampala*  
Employee

Copy to : The Chief Secretary. \*  
Copy to : The Accountant-General.  
Copy to : The Director of Audit.  
" " : The Director of Agriculture.  
\*Only in the case of clerks.

G P Dam 79595/3-56/10m/F3-2u1

**Picha namba 25: Barua ya ajira ya ukarani, Dodoma. (tarehe 3/11/2016)**

Kwa Registrar  
 CONFIDENTIAL C/COM

Kwa Registra,  
 D'salaam.

KUMZISHWA KAZI

AHSANTE SANA KWA BARUA YAKO  
 TELEGRAMS: "REGISTRAR". TEL. REF:  
 NO C/COM/6/11/279. YA TAREHE  
~~29th~~ 29th April 1969. BWANA MGANGA  
 KUPENDEKEZA NI PUMZIKE KAZI  
 MARA MOJA NIMEKUBALI.

WASALAM  
 NAKUBALIANA NA YOJE MKIOYA -  
 ZUNGU MUZA

Mimi  
 M. E. MNYAMPALA.

Picha namba 26: Barua ya kupumzishwa kazi kwa sababu ya kuugua.  
 (tarehe 3/11/2016)




**Picha namba 27: Wananchi wakiwa wamebeba mwili wa marehemu Mathias Mnyampala. (tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 28: Mheshimiwa Rashidi M. Kawawa akiongoza mazishi ya Mathias Mnyapala katika makaburi ya Bahi, kata ya Majengo. (tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 29: Charles Mathias Mnyampala akiangalia tamasha la maandishi wa vitabu ikiwa ni pamoja na vitabu vya baba yake. Wakati huo Charles alikuwa kidato cha pili, mwaka 1969, katika sekondari ya Dodoma. (tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 30: Cheti cha tuzo cha mtunzi maarufu wa Kiswahili.  
(tarehe 3/11/2016)**



**Picha namba 31: Mtafiti akiwa kwenye nyumba aliyoishi Mathias Mnyampala, Dodoma.(tarehe, 26/10/2016)**



**Picha namba 32: Mtafiti (kulia) na Mke wa Mathias Mnyampala, Bibi Mary Mangwela (kushoto), nyumbani kwa Mnyampala, Dodoma. (tarehe, 26/10/2016)**



**Picha namba 33: Mtafiti akiwa na mke wa Charles Mnyampala (Beatrice Laban Mhogolo), ndiye anayehifadhi kazi za Mathias Mnyampala, Dodoma.(tarehe, 28/10/2016)**



**Picha namba 34: Picha iliyopo sasa Ihumwa, mahali alipozaliwa Mathias Mnyampala. (tarehe, 18/11/2016)**



**Picha namba 35: Mtafiti akiwa na Bi Katarina (mdogo wake Mathias Mnyampala) na Stephano Sosteness (Mtoto wa mdogo wake), Dodoma. (tarehe, 30/10/2016)**



**Picha namba 36: Mahojiano baina ya mtafiti (kulia) na Mh. Jobu Lusinde (jamaa na rafiki wa karibu wa Mnyampala) nyumbani kwake Kilimani, Dodoma. (tarehe, 21/11/2016)**





**Picha namba 37: Mahojiano baina ya mtafiti (kushoto) na Profesa Joshua Madumulla (kulia) katika Chuo Kikuu cha Iringa, Iringa, Tanzania. (tarehe 14/10/2016)**



**Picha namba 38: picha iliyopigwa baada ya Mahojiano baina ya Mtafiti na Prof. Mughabuso M. Mulokozi ofisini kwake, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (tarehe 8/07/2016)**



**Picha namba 39: Picha iliyopigwa baada ya mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti (kulia) na Amiri Kaluta Amri Abedi (kulia) katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Kaluta, Magomeni, Dar es Salaam (tarehe 11/07/2016)**



**Picha namba 40: Picha iliopigwa baada ya mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti (kulia) na Mzee Hatibu Khamsini Mubiru (kulia) ofisini mwake katika Msikiti wa Hamadiyya, Mnazi Mmoja, Dar es Salaam (tarehe 14/07/2016)**



**Picha namba 41: Mahojiano baina ya mtafiti (kushoto) na Mzee Saidi Manoro (kulia) nyumbani kwake Magomeni, Dar es Salaam (tarehe 18/07/2016)**

